

MASWALI 40

MAJIBU 40

**Mazungumzo na January Makamba
Kuhusu Tanzania Mpya**

**na Padre
Privatus Karugendo**

**Dibaji na
Mzee Ali Hassan Mwinyi
Rais Mstaafu, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

Yaliyomo

Dibaji vii

Utangulizi ix

- 1** Kabla hatujaanza, na kabla sijasahau, nimekuwa na hamu kubwa ya kusikia kauli yako mwenyewe kuhusu hili suala la Urais. Mjadala wa Urais, hasa ndani ya Chama chenu, umekuwa mkali sana. Majina mengi yametajwa, ikiwemo lako. Je, ni kweli unaingia? Nimekusikia ukisema umefikia uamuzi wa kugombea kwa asilimia 90. Hiyo asilimia 10 bado tu? **1**
- 2** Naamini watu wengi watapenda kujua January Makamba ni nani haswa. Hebu tuelezee kwa kifupi historia yako; ulizaliwa wapi, umekulia wapi, umepitia wapi, umefikaje hapa ulipo leo? Jina la baba yako limekubeba? **13**
- 3** Je umeshapata watoto? Kama ni ndiyo ni wangapi? Je, mtazamo wako kuhusu familia na malezi ya watoto ni upi? Watu wanasema maji hufuata mkondo, je, ungependa watoto wako wawe wanasiasa kama wewe? **19**
- 4** Umesema kwamba ulisomea Chuo Kikuu cha Kikatoliki Marekani. Kama ujuavyo, mimi ni Padre. Napenda kusikia kidogo kuhusu suala hili. Ulifunza nini pale. **21**
- 5** Umenukuliwa na baadhi ya vyombo vya habari ukisema kwamba sasa ni wakati wa viongozi vijana kujitokeza na kuchukua nafasi kubwa za uongozi kama Urais wa nchi. Kwa nini mjadala huu ni muhimu wakati huu na vitu gani vipya vya kuibadilisha Tanzania vinavyoweza kufanywa na vijana na si wazee? Kwanini vijana waaminiwe kwenye nafasi kubwa wakati hawana uzoefu wa kuongoza? **23**
- 6** Je, umekomaa vya kutosha kushika nafasi ya Urais? Umefanya nini kwenye wizara yako, kiasi kwamba watu waweze kuamini kwamba unastahili nafasi ya juu zaidi ya hiyo uliyo nayo kwa sasa? Ulipochaguliwa kuwa Mbunge ulianzisha Shirika la Maendeleo Bumbuli. Nini kilikusukuma? Shirika linafanya nini na limewasaidia vipi watu wa Bumbuli. Je, kama jimbo bado lina changamoto unastahili kuomba nafasi ya juu? **28**
- 7** Ni changamoto gani kubwa zinawakabili vijana wa Tanzania? Wanasiasa wengi wamekuwa wakisema watamaliza tatizo la ajira nchini. Kuna

mawazo gani mapya kutoka kwa viongozi wa kizazi kipya ya kumaliza tatizo hili?..... **37**

- 8** Kuna wazo kwamba nchi tukiigawa katika majimbo ya kiutawala, itapiga hatua za kimaendeleo kwa haraka. Kuna siku nilikusikia ukipinga wazo hili na ukasema kwamba badala ya majimbo ya kiutawala tuigawe nchi kwenye majimbo ya kiuchumi. Je, unaweza kufafanua fikra hizi? **45**
- 9** Baada ya kuingia Bungeni, ulipewa nafasi ya kuwa Mwenyekiti wa Kamati nyeti ya Nishati na Madini. Kwanza, tuambie uliwezaje kupata Uenyekiti wa Kamati nyeti katika wiki chache tu baada ya kuingia Bungeni. Tuelezee baadhi ya changamoto kwenye nafasi hii, lakini pia mlichukua hatua gani kulisaidia taifa kwenye sekta hizi nyeti? Ilikuwaje Kamati hii ikavunjwa mara tu baada ya wewe kuachia Uenyekiti? Nini kifanyike kumaliza tatizo la mgao wa umeme na bei kubwa za umeme? **57**
- 10** Umeeleza kwamba ulikuwa sehemu ya kampeni ya Urais ya CCM mwaka 2005 na kwamba ulipata nafasi ya kuzunguka na Mheshimiwa Kikwete akiwa mgombea wa Urais wa CCM kwenye uchaguzi huo. Ulikuwa unafanya shughuli gani na ulijifunza nini katika shughuli ile? **62**
- 11** Kwa miaka mitano na zaidi, ulipata nafasi ya pekee ya kuwa karibu na Rais wakati wote. Kutokana na nafasi hiyo ni mambo gani ya msingi uliyojifunza na yakakujenga kuwa kama ulivyo leo hii? Kwa nini uliamua kuacha kazi nzuri ya Ikulu na kwenda kugombea ubunge? Je, ilikuwa rahisi Rais kukuachia? **65**
- 12** Hivi karibuni wananchi wengi hasa wa kipato cha chini na cha kati wamekuwa wakilalamika kwamba maisha yamekuwa makali, na gharama za maisha zimekuwa zikipanda kila kukicha. Maarifa gani yanahitajika ili kuweza kupunguza ukali wa maisha kwa Watanzania? **70**
- 13** Watanzania wengi wanajishughulisha na kilimo, ufugaji na uvuvi lakini wamekuwa hawanufaiki na shughuli hizi licha ya mipango mingi tangu wakati wa uhuru hadi sasa. Je, kizazi kipya cha uongozi wa nchi kinapaswa kuwa na maarifa gani mapya kuhusu mapinduzi ya kilimo na maendeleo ya uvuvi na ufugaji? **73**
- 14** Tanzania imekuwa ikisifika kwamba uchumi wake unakua kwa kasi kwa miaka kadhaa sasa. Lakini wananchi wengi bado hawajaona hayo manufaa. Nini kifanyike wananchi nao waone na wanufaike na uchumi kukua? Unauelezeaje uchumi wetu kwa ujumla? **79**
- 15** Mwaka jana nilisoma kwenye vyombo vya habari kwamba ulipata tuzo ya taasisi ya National Democratic Institute ya Marekani, unaweza kutueleza ni tuzo ya nini na kwa nini ulipata? Pili, tulisoma kwamba uliteuliwa

na taasisi ya *World Economic Forum* kuwa mmoja wa viongozi vijana mashuhuri duniani (*Young Global Leaders*). Pia tena majuzi tukasoma kwamba jarida mashuhuri duniani la *Forbes* limekutaja kuwa mmoja wa watu kumi wenye ushawishi Afrika kwa mwaka 2014. Ni kwanini unadhani wanakupa hizi tuzo? Na je, tuzo hizi zina maana gani kwa wapiga kura wako?..... **89**

16 Kama kiongozi kijana uliyepata kufanya kazi katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ikulu, unazungumziaje nafasi ya Tanzania katika siasa za kimataifa?..... **92**

17 Tunaona jinsi nchi jirani zetu wanavyopata changamoto za usalama. Je, sisi tufanyaje kuepokana nazo? **94**

18 Kiwango cha elimu katika taifa letu kimeporomoka, ni kwa nini na unafikiri ni kitu gani kifanyike kuinua hali ya elimu katika taifa letu?..... **97**

19 Walimu ni sehemu kubwa ya watumishi wa umma. Je, wewe unayajua matatizo yao? Una fikra na mawazo gani ya kuyashughulikia? Vipi kuhusu wahadhiri wa vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu?..... **102**

20 Kumekuwa na malalamiko kuhusu utendaji Serikalini, hasa juu ya urasimu; kwamba maamuzi hayafanyiki kwa wakati, lakini pia hakuna uwajibikaji. Je, nini kifanyike kurekebisha hali hii? **105**

21 Mfumo mpya wa Matokeo Makubwa Sasa, BRN, ni mwanzo mzuri lakini lazima uende sambamba na uwezo wa kufanya maamuzi na kuchukua hatua za uwajibikaji pale matokeo makubwa yanapokuwa hayajapatikana. Wananchi wanalalamikia sana ufisadi. Mikakati ya sasa inaelekea haijafanikiwa kiasi cha kuridhisha wananchi. Je, wewe una mbinu zozote mpya za kupambana na tatizo hili? Je, unaongeleaje ufisadi wa Richmond, EPA na IPTL. **108**

22 Kumekuwa na hii dhana ya kufanya maamuzi magumu kama sifa ya uongozi. Je, unalisemeaje hili? Je, wewe umeshawahi kufanya maamuzi yoyote magumu kwenye uongozi wako? **111**

23 Hapa tupo Dar es Salaam. Inaelekea karibu kila mtu anataka kuhamia na kuishi Dar es Salaam. Una maoni gani kuhusu nafasi ya Jiji la Dar es Salaam katika maendeleo ya nchi yetu? Nini changamoto za jiji hili na nini kifanyike kuzirekebisha?..... **116**

24 Mwaka 2012 ulipeleka Bungeni Muswada Binafsi wa Sheria ya Kudhibiti shughuli za Upangishaji Nyumba. Tuelezee maudhui yake, nini kilikusukuma na muswada huo umefikia wapi?..... **122**

- 25** Inaelekea siku hizi kila mwanasiasa anajikita katika kundi la vijana na kuzungumzia masuala yanayowavutia vijana. Hakuna makundi mengine ya kuyasemea? Ni makundi gani na mahitaji yao ni yapi na ufumbuzi wa changamoto zao ni upi? **125**
- 26** Umekuwa mmoja ya viongozi ambao wanaliongelea sana suala la mabadiliko ya kasi ya kuongezeka kwa idadi ya watu nchini na taifa kuwa changa kiumri. Unaweza kutuelezea kwa upana nini maana ya mabadiliko haya kwenye mustakabali wa taifa letu la leo na la kesho? **129**
- 27** Miaka ya hivi karibuni imejitokeza dalili kwamba mahusiano ya watanzania wenye dini tofauti si mazuri na kuna dalili kwamba hali hii inaweza kuleta kutoelewana siku za usoni. Wewe unalisemeaje suala hili? Nini nafasi ya imani ya kiroho katika kumwongoza Kiongozi wa nchi? **132**
- 28** Wewe kama kiongozi kijana, umewasaidiaje hawa vijana wenzenu wa *Bongo Movies* na vijana wa muziki wa kizazi kipya maana yake kila siku wanalamika. Pia inaelekea tumetelekeza maendeleo ya sanaa kwa ujumla. Tufanyeje? **137**
- 29** Tanzania imekuwa ikijulikana kama kichwa cha mwendawazimu kwenye medani ya michezo ya kimataifa. Ni muda mrefu sasa tumeshindwa kupata medali zozote kwenye michezo ya Jumuiya ya Madola au Olimpiki. Mara ya mwisho kwa Taifa Stars kushiriki fainali za kombe la Mataifa ya Afrika ilikuwa ni miaka 36 iliyopita. Una fikra gani mpya katika kulirekebisha hili na kuwafanya Watanzania kujisikia fahari kutokana na mafanikio ya wanamichezo wake? **142**
- 30** Watu wengi wamekuwa wanalamikia bandari na reli. Wengine wanasema kwamba kwa takribani miaka kumi sasa bandari na reli ziko vilevile, hakuna upanuzi wala ujenzi mpya. Una maoni gani kuhusu miundombinu ya usafirishaji? Nini kipya kinaweza kufanyika? **145**
- 31** Nimetembea sana vijijini na nimeona kuwa vijiji vingi havina huduma yoyote ya afya. Hata kule ambapo zipo watumishi hawatoshi, vifaa hakuna, hakuna umeme, na wakati wote hakuna dawa. Ukienda hospitali, iwe ndogo au kubwa, una hatari ya kupata ugonjwa kuliko nyumbani. Haya matatizo wewe unayaonaje? Kwa kweli watu hawamudu gharama za matibabu na wanakufa bila sababu za msingi. Nini kifanyike? ... **151**
- 32** Umesema kwamba Rais Kikwete amejitahidi kuboresha huduma. Unadhani ni huduma gani ya jamii bado ni kero kwa Watanzania na unadhani kuna maarifa gani mapya ya kuitatua? **156**

- 33** Ukiwa kama kiongozi kijana wa CCM, uliyepata fursa ya kuwa kiongozi wa juu wa Chama chenu, huoni kama Chama chenu kimepoteza mwelekeo na kinapata ushindani mkubwa sasa? Kuna sababu za Chama chenu kuendelea kuaminiwa na Watanzania? Ukichaguliwa Rais, pia unakuwa Mwenyekiti wa CCM, je kijana anaweza kukiongoza Chama kikongwe kama CCM?**159**
- 34** Hapa Tanzania karibu kila mtu, hata ambao ni watumishi wa Serikali na hata wananchi wa vijijini ni wajasiriamali. Lakini ujasiriamali unakwamishwa na ukosefu wa mikopo. Benki ziko nyingi lakini hazikopeshi watu maskini ambao hawana dhamana. Taasisi za ukopeshaji, *microfinance*, zimejaa lakini riba ni kubwa na watu wanashindwa. Kulikuwa na Mabilioni ya JK lakini hayakufika mbali. Kuna jambo gani kubwa na jipya la kumaliza tatizo hili?**167**
- 35** Nini nafasi ya uhuru wa vyombo vya habari katika kuchochea maendeleo ya taifa letu. Unaongeleaje suala la kuwa na vyombo vya habari vingi ambavyo vinaandika habari za uchochezi.....**169**
- 36** Baada ya uvumbuzi wa gesi nchini, kumekuwa na mjadala kuhusu Watanzania kunufaika na rasilimali za taifa hili. Una maoni gani kuhusu huu mjadala? Nini kifanyike ili watu wa hali ya chini wanufaika? Kama kiongozi umeshiriki vipi kuhakikisha Watanzania wananufaika na rasilimali zao?**172**
- 37** Wakati wa Bajeti, kila tunapozungumzia kutotekelezwa kwa miradi ya maendeleo, kutolipwa kwa wazabuni, kutolipwa kwa walimu na askari, tunasikia sana msemo wa “kasungura kadogo”. Je, kutokana na hali hii, kuna matumaini ya kupata maendeleo kama kila wakati Serikali inasema haina fedha ya kutekeleza majukumu yake ya msingi? Je, kuna maarifa gani mapya, ambayo wewe kama kiongozi wa kizazi kipya, ambayo unayo kuhusu namna ya kupata fedha za maendeleo?.....**175**
- 38** Mwaka jana niliona picha yako kwenye gazeti ukiwa Butiama na Mama Maria Nyerere mkiomba pembeni ya kaburi la Mwalimu Nyerere. Ulifikaje huko? Mama Maria alikupa usia gani? Unazungumziaje nafasi ya Mwalimu Nyerere kwenye siasa za sasa za nchi yetu?**186**
- 39** Je, kati ya marais wanne waliowahi kuliongoza taifa letu, unafikiri ni rais gani ameacha historia kubwa kama Rais aliyefanya mambo makubwa kuliko wote katika taifa letu?**188**
- 40** Kuna mambo yoyote unayodhani hatukuyazungumzia ambayo unadhani yana umuhimu katika ustawi wa nchi yetu?.....**193**



Dibaji

Nimefarijika kuyasoma mazungumzo baina ya Padri Privatus Karugendo na Ndugu January Makamba, mmoja wa viongozi mahiri wa zama za sasa. Nawapongeza kwa kuamua kuyaweka mazungumzo yao katika rekodi ya maandishi. Hakika tumejifunza mengi kuhusu na kutokana na historia na falsafa ya maisha ya Ndugu Makamba pamoja na fikra zake kuhusu Tanzania ijayo.

Jamii inanufaika tunapowafahamu kwa kina viongozi wetu. Utaratibu huu wa Padri Karugendo ni jambo jema na inabidi uendelezwe. Binafsi nilikuwa namfahamu Ndugu Makamba kama kiongozi ndani ya Chama chetu na kwenye Serikali. Fursa ya kusoma mazungumzo yake imenisaidia kumfahamu zaidi kama mtu lakini pia kufahamu fikra zake. Nimefarijika kwamba nchi yetu na Rais wetu Kikwete ameendeleza utamaduni aliouanzisha Mwalimu Nyerere na kuendelezwa nami wa kuwaamini vijana na kuwapa fursa za uongozi ili kuwaandaa kuiongoza nchi yetu. Nilimteua Ndugu Jakaya Mrisho Kikwete

kuwa Mbunge na Naibu Waziri akiwa na umri wa miaka 38 tu na baadaye Waziri wa Wizara muhimu ya Maji, Nishati na Madini akiwa na umri wa miaka 40 na baadaye Waziri wa Fedha. Sikufanya hivyo kwasababu tu ya umri wake bali kutokana na kuamini katika msingi wa kuandaa viongozi wa vizazi vijavyo kwa kuwapa majukumu katika Chama na ndani ya Serikali. Kwa kusoma mazungumzo ya Padri Karugendo na Ndugu Makamba ni dhahiri kabisa kwamba Ndugu Makamba aidha ameandaliwa au amejiandaa vizuri kuwa kiongozi mkubwa. Kazi hii ya kuandaa viongozi lazima iendelee kufanywa. Kiongozi mzuri ni yule anayetengeneza viongozi wengine wapya.

Kila zama na kitabu chake, kila zama na changamoto zake na kila zama na mitume wake. Wenye zama zao wanakitendea haki kizazi chao na vizazi vijavyo wanaporekodi masaibu na matumaini ya zama husika. Nimejifunza kupitia mazungumzo haya kuhusu aina ya Tanzania ambayo Ndugu Makamba anaitaka. Imani yangu ni kwamba mazungumzo haya, pamoja na mengine ambayo wengine watayafanya, yataleta mjadala wenye afya kuhusu Tanzania tuitakayo.



Ali Hassan Mwinyi

Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Dar es Salaam

22/12/2014

Utangulizi

Kitabu hiki ni matokeo ya mahojiano yetu na Mheshimiwa January Makamba. Hatukuwa kabisa na lengo la kuandika kitabu, bali ilikuwa ni kiu ya kutaka kumfahamu huyu kijana, Mbunge na Naibu Waziri ni nani, ana fikra na ndoto gani kuhusu Tanzania tuitakayo? Huu ni mradi tulioubuni, ili kutaka kuwafahamu vijana wetu, hasa wale waliochomoza kwenye medani za siasa na kushika nafasi za juu za uongozi serikalini wakiwa na umri mdogo na kiu ya kuleta mabadiliko katika nchi yetu.

Tarehe 28/1/2014, January Makamba alitimiza miaka 40 ya kuzaliwa, na siku hiyo ndiyo tuliyoanza naye mahojiano ya maswali 40 juu ya masuala mbali mbali ndani ya jamii yetu ya Tanzania; siasa, uchumi, dini, elimu, afya na maisha yake binafsi na yeye akatupatia majibu 40! Dhamira yangu ilikuwa ni kuandika makala na uchambuzi wangu kuhusu majibu yake kabla sijaendelea kuwahoji wengine. Kishawishi cha kuandika kitabu hiki, kilitokana na umahiri wa kijana huyu kuyajibu maswali yetu kwa ufasaha na kwa kina pamoja na uelewa wake mkubwa wa karibu nyanja na sekta zote zinazoihusu nchi yetu. Ukimsikiliza January Makamba unabaini na unamuona kijana ambaye anajua anachokizungumza. Nilifaidi mazungumzo yetu na nikaona makala peke yake haitatenda haki juu ya kina na mapana ya mazungumzo yetu. Nilipenda watu wayapate kama nilivyoyapata mimi bila ya kupunguza au kuhariri chochote. Nikaamua nichukue muda, kwa kushirikiana naye, kutafuta uwezo wa kuchapisha hiki kitabu. Katika kunakili rekodi za mazungumzo yetu kwenye maandishi nililazimika kumrudia na kuendelea kuzungumza naye tena mara kadhaa kwa kuwa matukio mapya yaliendelea kutokea kwenye jamii ikiwemo yeye mwenyewe kuweka wazi azma yake ya kugombea. Bahati njema sasa tunakitoa kitabu hiki akiwa anatimiza miaka 41.

Mradi huu wa kuwahoji vijana wetu kwa lengo la kutaka kuwafahamu vizuri, nategemea kuendelea nao kwa vijana wengine na wala hatutaachia kwa January Makamba. Tutakuwa tunauliza idadi ya maswali kulingana na umri wa kijana, kama atakuwa na miaka 35, tutauliza maswali 35. Kama ni kijana mkubwa wa miaka 55, tutauliza maswali 55!

Tunataka mabadiliko katika taifa letu la Tanzania. Hakuna shaka juu ya hili. Maswali muhimu ya kujiuliza ni: Mabadiliko haya tuyatakayo yana sura

ipi? Yaletwe na nani na kwa wakati gani? Wengine wanasema mabadiliko yataletwa na vijana. Na vijana wenyewe wanalishikia bango pendekezo hili maana wanasema Mwalimu Nyerere, alianza mchakato wa kuleta mbadiliko akiwa na umri wa miaka wa chini ya miaka 30 ndani ya Chama cha TAA, na baadaye alipochaguliwa kuwa Rais wa TANU akiwa na miaka 32, na baadaye kuwa kiongozi wa taifa letu jipya akiwa na umri wa miaka 39. Mwanamapinduzi wa Cuba Fidel Castro, alianza mapambano akiwa kijana mdogo, rafiki yake Che, alikufa akiwa na umri wa miaka 39, hata Yesu wa Nazareti alikufa akiwa na umri wa miaka 33 akiwa katika harakati ya kuleta mabadiliko makubwa katika Jamii yake ya Israeli. Hivyo vijana ni muhimu sana katika kuleta mabadiliko; Mataifa yaliyo makini hayachezi na vijana, yanawaandaa na kuwaonyesha njia ya kupita ili walete mabadiliko yaliyo chanya; maana mabadiliko katika jamii yoyote ile ni lazima. Mataifa, yanayochelewa kuandaa mfumo mzuri wa kuwafundisha vijana ili washike madaraka, wazalishe mali na kuendeleza uchumi wa nchi yao; yameshuhudia vijana wakijichukulia madaraka kwa nguvu. Nchi nyingi za Afrika zilizoonja adha ya mapinduzi ni zile zilizowapuuza vijana wake. Na mara nyingi mapinduzi yameongozwa na vijana.

Tanzania tuna vijana wengi na wamegawanyika kwenye makundi mbali mbali yasiyoshirikiana. Tuna vijana wa mitaani, hawa wanaendelea kuwa wengi. Vijana hawa kwao kuishi na kufa ni mapacha, hivyo ni bomu ambalo linaweza kulipuka saa yoyote ile. Hili ni kundi ambalo kama likiongozwa vizuri linaweza kuleta mabadiliko chanya, lakini likipuuza linaweza kutupeleka tusikopenda; na ni kwa vile tunaamini kuhubiri na kukemea tu inatosha! Tuna kundi la machinga, hawa ni tofauti kidogo na wale wa mitaani. Wanajitahidi kufanya biashara ndogo ngogo kwa mtaji mdogo. Kwa vile shilingi inaendelea kuzama na dola inaelea juu ya maji, kiwango cha vijana hawa kutunza amani na kuwa na mwelekeo wa kujenga taifa lenye maendeleo ni finyu. Kundi la kati ni la wasomi, wale waliopata elimu ya zaidi ya Sekondari, digrii na kuendelea. Hawa wanapata kazi na kufanya kwenye mazingira ya chukua chako mapema. Badala ya kufanya kazi na kuwa wabunifu wanatengeneza mikakati ya kukwapua, kuingia kwenye mikataba mibovu yenye kuzalisha asilimia kumi za kuweka mfukoni.

Mbali na kwamba vijana wetu wametengwa kwenye matabaka ya wasomi na wasiokuwa na kisomo, wanaosoma shule za kimataifa na wale wanaosoma shule za kata; bado wako kwenye makundi ya dini, siasa na itikadi mbali mbali. Vijana wetu wamegawanyika. Hawana sauti moja; pamoja na tofauti ambazo haziepukiki, bado hawana kitu cha kuwaunganisha kama vijana wa Tanzania. Na kama hawana umoja, ni vigumu kushiriki kikamilifu na kwa uaminifu katika mchakato mzima wa kuleta mabadiliko.

Mwandishi mashuhuri wa taaluma za maendeleo Thomas Alan, katika makala yake: “Development as practice in a liberal capitalist world” iliyochapishwa mwaka 2000 kwenye jarida la “Journal of International Development (2000) ukurasa wa 73-87, anajenga hoja kwamba mabadiliko katika jamii yoyote ile yanajikita katika misingi mikuu mitatu: 1. Vision; taswira/ ndoto au picha ya mabadiliko ambayo jamii inataka kuwa nayo. 2. Historia ya mabadiliko katika jamii husika na 3. Bidii, juhudi na msukumo miongoni mwa makundi ya kijamii wa kutaka mabadiliko. Kwa maoni yake ni kwamba utata mkubwa wa misingi hii ni kama ule wa yai na kifaranga. Ni kipi kitangulie kingine? Unaanza na vision na kufuatisha historia, au unaanza na historia na kufuatisha vision na bidii? Jibu la utata huu ni kwamba misingi yote mitatu ni lazima iende kwa pamoja. Kinyume na hapo ni vigumu kuleta mabadiliko ya kweli na yenye manufaa kwa watu.

Ukiwa na taswira muafaka na bayana juu ya jamii bila kuzingatia historia ya mabadiliko katika jamii hiyo, huwezi kuleta mabadiliko ya kweli. Matokeo yake ni vurugu kama tunavyoshuhudia kwenye jamii nyingi za bara la Afrika na kama ilivyo hapa ndani ya taifa letu. Hakuna vision, lakini tuna bidii ya kutaka kuleta mabadiliko. Na jinsi mambo yanavyokwenda hata historia ya jamii yetu tunaiweka pembeni. Ujamaa tunaupiga teke na kujidanganya kwamba si sehemu ya historia yetu. Tunajitahidi kwa bidii ile ile ya kutaka kuleta mabadiliko kwa kuukumbatia ubepari na ujinga wa utandawazi. Matokeo yake ni ufisadi wa kutisha kiasi cha kuliiza taifa letu.

Pia ukizingatia historia peke yake, bila kuwa na taswira muafaka na bayana pamoja na bidii ya kuleta mabadiliko, huwezi kufanikiwa kuleta mabadiliko endelevu. Unaweza kufanikiwa kuzalisha kitu kingine kama udikiteta, uporaji wa mali, matabaka na mambo mengine mabaya yasiyopendeza mbele za mwanadamu na mwenyezi Mungu.

Je, January Makamba, anafahamu kwamba vijana wa taifa hili wamegawanyika kwenye makundi matatu niliyoyataja hapo juu na wanahitaji kitu cha kuwaunganisha? Je ana taswira na kufahamu kwa kina historia ya mabadiliko katika taifa letu?: historia ya utemi, utumwa, ukoloni, uhuru, ujamaa, Azimio la Arusha, Azimio la Zanzibar, utandawazi, ubinafsishaji, mchanganyiko wa ubepari na ujamaa. Anafahamu tulikotoka, tuliko na tunakokwenda? Je ana bidii yakuleta mabadiliko? Je anafahamu kwamba taswira ya kitaifa si kazi ya mtu mmoja na wala si kazi ya chama kimoja cha siasa. Kama nilivyodokeza hapo juu ni kwamba mabadiliko ni mradi wa pamoja, hivyo na uundaji wa taswira ya kitaifa ni mradi wa pamoja. Ni lazima sisi kama Watanzania kuamua kwa pamoja taswira muafaka ya taifa letu.

Je, January Makamba, anafahamu kwamba kazi kubwa inayohitajika ili mabadiliko ya kweli yatokee ni kubadilisha mitizamo, au “mental frame”, hasa za wanasiasa”. Na hili ni swala zima la historia ya mabadiliko katika taifa letu. Awamu ya kwanza ya uongozi wa taifa letu ilijitahidi sana kubomoa mfumo wa elimu na siasa ambapo “mental frame” ya watawala ilikuwa kusimamia maslahi ya wakoloni na vibaraka wao. Siasa ya ujamaa na kujitegemea ilikuwa ikilenga kuondoa “mental frame” ya utumwa na ukoloni. Bahati mbaya mbegu za “mental frame” ya utumwa na ukoloni zimeendelea kuota na kustawi hadi leo. Tukitaka kumsikiliza bwana Thomas Alan, na hoja yake ya misingi mitatu ya mabadiliko, ni lazima tukubali kwamba wakati wa mchakato wa kujenga ujamaa na kujitegemea misingi hiyo mitatu haikufuatwa vilivyo.

Na tumeendelea kutaka kuleta mabadiliko bila kuwa na jitihada za kutosha kubadili “mental frame” ya watanzania. Na matokeo yake ni kwamba siasa zetu zimetufikisha mahala ambapo jamii yetu imegawanyika sana katika matabaka ya walalahoi na wanyonyaji. Kwa ufupi jamii yetu imepoteza mwelekeo. Kazi ya kujenga jamii ya Watanzania wenye ujuzi na maarifa yanayoongozwa na falsafa ya kujitawala na kujitegemea imetushinda. Kinachohitajika ni ujenzi wa mfumo wa kisiasa utakaowawezesha watanzania kujiamini na kuendesha maisha yao bila kutegemea misaada ya fedha na mawazo kutoka nje.

Kama utakavyobaini wakati unasoma kitabu hiki, maswali haya 40 niliyomuuliza January yalikuwa na maswali mengine ya mfuatilizio, yaani follow-up questions, kwa ajili ya ufafanuzi zaidi. Mfumo wetu wa mahojiano ulikuwa ni wa mazungumzo. Hata hivyo, kwenye kurekodi mazungumzo haya katika maandishi, niliamua kuyaunganisha maswali ya mfuatilizio pamoja na maswali ya msingi ili kuweza kupata mtiririko mzuri katika usomaji.

Kwa kukisoma kitabu hiki, utapata majibu ya maswali tuliyoyauliza hapo juu, majibu ya maswali yetu 40 na kumfahamu kwa undani kijana huyu aitwaye January Makamba.

Karibuni!

Padre Privatus Karugendo

Dar es Salaam

17/12/2014

1

Kabla hatujaanza, na kabla sijasahau, nimekuwa na hamu kubwa ya kusikia kauli yako mwenyewe kuhusu hili suala la Urais. Mjadala wa Urais, hasa ndani ya Chama chenu, umekuwa mkali sana. Majina mengi yametajwa, ikiwemo lako. Je, ni kweli unaingia? Nimekusikia ukisema umefikia uamuzi wa kugombea kwa asilimia 90. Hiyo asilimia 10 bado tu?

Uamuzi wa kugombea uongozi wa juu wa nchi sio uamuzi mdogo. Ni uamuzi unaohitaji tafakuri ya kina. Binafsi sipendezwi na mjadala wa majina. Tungeanza kwanza kujadili changamoto za sasa na zijazo za nchi yetu na aina ya uongozi na vigezo vinavyohitajika ili kukabiliana na changamoto hizo.

Ni kweli kumekuwa na ushawishi mkubwa – hasa kutoka kwa vijana – kwamba na mimi niingize jina langu. Mwanzoni sikuwa naamini kwamba ushawishi huu ni wa dhati. Lakini kwa kadri siku zinavyoenda wanaotoa ushawishi huu wamekuwa wanaongezeka – na sasa sio vijana pekee, bali watu wa makundi na rika mbalimbali kutoka kila kona ya Tanzania. Kwa ajili hiyo, imenilazimu nichukue muda kutafakari kwa kina.

Bado nazungumza na watu mbalimbali kwenye jamii yetu, ikiwemo wazee ndani ya Chama chetu waliowahi kushika uongozi katika nchi hii, kuhusu changamoto za nchi yetu na aina ya uongozi tunaohitaji.

Mwelekeo wa mazungumzo na tafakuri yangu kuhusu changamoto za nchi yetu na aina ya uongozi tunaohitaji, unaidhihirishia kwamba uwezo wa kushika nafasi hii ninao, nimekomaa vya kutosha, ninayo maarifa na uzoefu wa kutosha, na ninayo dhamira ya kuongoza mabadiliko makubwa ambayo vijana na Watanzania wote wana kiu nayo, na ninao uwezo wa kuipeperusha vizuri bendara ya Chama cha Mapinduzi na kukiwezesha Chama chetu kushinda kwa kishindo.



January Makamba akizungumzia jambo na wananchi, October 2014.

Kuomba uongozi wa nchi sio harakati binafsi na wafuasi wako kupata vyeo. Ni dhamana kubwa ya kujenga mustakabali wa nchi na kuwaunganisha Watanzania wote. Kwa hiyo uamuzi wa kugombea lazima uupe heshima na nafasi inayolingana na dhamana yenyewe.

Tafakuri yangu imejikita katika kuiangalia hali ya nchi kwa sasa na changamoto zilizopo na majukumu ya Rais ajaye. Naomba nizungumzie yaliyopo akili mwangu katika kipindi chote ambacho nimekuwa nafanya tafakari hii.

Nchi yetu iko katika njia panda. Katika miaka 10 ijayo, Tanzania inaweza kuchukua njia mojawapo kati ya hizi mbili: inaweza kupiga hatua kubwa ya maendeleo na hali ya maisha ya wananchi wote kuboreka – kutokana na ugunduzi wa gesi asilia, kuendelea kupanuka na kuboreka kwa huduma za kijamii, kupanuka kwa sekta binafsi na fursa nyingi za biashara, jitihada kubwa za ujenzi wa miundombinu na mambo mengine mazuri yaliyofanywa na Serikali za awamu zote. Lakini vilevile, ipo hatari ya ya taifa letu kupasuka - kutokana na dalili za mpasuko wa kidini, mmomonyoko wa maadili kwenye jamii, kuporomoka kwa imani ya wananchi kwa Dola, ufa katika Muungano na umasikini na tofauti kubwa ya kipato baina ya watu na hali ya kukata tamaa miongoni mwa wananchi.

Ni lazima sote tuhakikishe hatuchukui njia hii ya pili. Hapa, uongozi madhubuti, uongozi wa zama za sasa, unahitajika. Nchi yetu leo hii iko moja na ina amani na utulivu kutokana na kazi iliyofanywa na umadhubuti wa viongozi waliopita kuanzia awamu ya kwanza hadi awamu ya nne.

Rais ajaye ana kazi kubwa zaidi ya kusimamia umoja wa nchi yetu na usalama, amani na utulivu kuliko viongozi waliopita. Huu ni msitu mpya kabisa. Lazima kiongozi ajaye ayajue kwa kina mazingira ya sasa, awe ameyaishi, na kutambua mahitaji yake.

Nchi yetu kijiografia na kimaumbile ina changamoto kubwa za kiusalama. Nchi yetu ina mipaka 8 mirefu; majirani wenye changamoto za usalama; ina makabila 120 makubwa na madogo, ina ukubwa wa ardhi wa kilomita za mraba laki tisa na nusu, ni Muungano wa nchi mbili; nusu ya wananchi wake wakiwa wamezaliwa ndani ya uongozi wa Rais Mkapa na Kikwete na vijana chini ya miaka 35 ni asilimia karibu 80, na wengi wao wakiwa hawana ajira. Kuna viashiria vya nyufa kati ya wakulima na wafugaji, wachimba madini wadogo na wawekezaji wakubwa, Wakristo na Waislamu, Wabara na Wazanzibari, matajiri na maskini wa kutupwa. Nchi hii pia ina rasilimali na maliasili nyingi zinazotolewa jicho na mataifa na makampuni ya nje ambayo yako tayari kutumia njia zozote kuzipata ikiwepo kuligawanya taifa.

Vilevile, hivi karibu tumeshuhudia tishio la mpasuko wa taifa katika misingi ya dini na ukanda miongoni mwa wananchi. Tumeshuhudia nyumba za dini zikichomwa moto, viongozi kupigwa risasi na kumwagiwa tindikali, wananchi wa upande mmoja wa nchi wakidai rasilimali zilizopo eneo lao ni zao peke yao, na baadhi ya wanasiasa wakipanga kete zao za kuwania uongozi kwa misingi ya kikanda na kidini. Matukio yote haya yanaonyesha kutokuaminiana miongoni mwa makundi jamii, na baina ya makundi hayo na uongozi na serikali hali inayofanya kila kundi kutafuta kujihami lenyewe.

Ukweli huu unatoa jukumu na changamoto kwa Rais ajaye kuiunganisha na kuilinda nchi yetu dhidi ya matishio yote ya migawanyiko.

Katika tafakuri yangu nimejiridhisha kwamba lazima Rais wa Awamu ya Tano awe ni mtu mwenye kuzitambua changamoto hizo na kuwa na mkakati wa kuzitatua. Changamoto hizi ni za kiuongozi na utatuzi wake utategemea tu kiongozi mwenyewe, hulka yake, mtazamo wake na usahihi wa maamuzi yake. Na yote hii inategemea wajihi, yaani *character*, wa kiongozi mwenyewe. Hivyo, wajihi wa mgombea unapaswa kujibu maswali yanayoletwa na changamoto hizi.



January Makamba akimkaribisha Mzee Yusuf, mwimbaji maarufu wa Taarab nchini, katika moja ya mikutano ya CCM.

Katika kujitafakari kwangu, nimejiridhisha kwamba changamoto au wajibu wa pili wa Rais ajaye ni kuongeza kasi ya kuondoa umaskini. Serikali za awamu zote zimefanya jitihada kubwa sana za kuondoa umasikini. Ni dhahiri kuwa tumepata matokeo mchanganyiko. Yako matokeo mazuri na yasiyoridhisha. Tunaweza kujivunia kupanuka kwa tabaka la kati na kuinuka kwa wazawa katika sekta binafsi. Hata hivyo hatuwezi kufumbia macho pia kuwa wako masikini ambao wametumbukia kwenye ufukara. Wapo watu wamejikomboa na umasikini lakini bado masikini ni wengi. Tumeshuhudia miji ikikua kwa kasi kubwa na umasikini ukiongezeka mijini hali iliyozaa uhalifu na uvunjifu wa amani. Huwezi kutaka kuomba nafasi ya uongozi wa juu bila kuwa umeyatafakari haya na kutengeneza fikra za kukabiliana nayo.

Ni dhahiri kwamba tofauti ya kipato baina ya walionacho na wasionacho imeongezeka. Ni lazima kuchukua hatua za kupunguza tofauti hiyo. Umasikini wa mijini unakabili zaidi vijana ambao ndio wengi. Katika kukabiliana na

changamoto hii, pamoja na kufanya juhudi za kuongeza uzalishaji na kutengeneza fursa za wananchi kupata ajira na kujiajiri, uongozi wa awamu ijayo unayo changamoto ya kuongeza ajira, kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za afya, elimu, maji na ustawi wa jamii kwa wananchi wasiojiweza na wenye kipato duni.

Katika kutafakari, nimebaini kwamba tuna tatizo kubwa zaidi la kuzimika kwa matumaini ya masikini juu ya uwepo wa fursa ya kuondokana na hali yao ya umasikini. Kukithiri kwa mfumo wa kujipatia kipato kwa njia zilizo kinyume na sheria, ukwepaji wa kodi, biashara ya madawa ya kulevywa, rushwa, ubadhirifu na maisha ya kifahari ya viongozi na serikali kumefifisha matumaini na imani kwa wananchi kuwa uongozi unajali na unahangaika kuwakwamua kutoka kwenye hali yao. Hali inayofanya masikini wajione wamekosa mtetezi

Rais ajaye asiwe na chembe hata kidogo ya kuhisiwa kunufaika na fursa ya muda mrefu wa uongozi katika Serikali.

Ni dhahiri kwamba Rais ajaye atapokea nchi huku imani ya wananchi kwa Serikali, vyombo vya dola na Mahakama ikiwa imeporomoka. Hali hii ni kichocheo cha uvunjifu wa amani. Katika kutafakari, nimebaini kwamba Rais ajaye ana mtihamu mkubwa wa kurejesha imani haswa ya wananchi wengi masikini kuwa anaguswa na hali yao, na kuwa anachukua jitihada za kuwakwamua kutoka katika hali yao. Hayo yatadhihirika si tu kwa maneno bali hatua atakazochukua dhidi ya viongozi wabadhirifu, wala rushwa na matumizi ya serikali yake. Hapaswi kuhisiwa wala kutuhumiwa kwamba yeye ni miongoni mwa hao.

Mtu yoyote anayetaka kuingoza nchi yetu lazima aamini moja ya sifa kubwa na tunu za nchi yetu ni Muungano wetu.

Muungano wetu umetikiswa. Nimejiridhisha kwamba kiongozi ajaye lazima ahakikishe Muungano wetu unajibu changamoto za umasikini na changamoto za kimuundo, mambo ambayo yamezaa hoja na kelele za kuuvunja. Uhai wa Muungano utategemea sana ni kwa jinsi gani unawasaidia Watanzania wa pande zote kwa kuwapa fursa ya kuendeleza ndoto zao za kiuchumi na kijamii. Kinyume na hapo, Muungano utakuwa mali ya viongozi na wanasiasa na hautadumu. Changamoto ya Rais ajaye ni kufufua ndoto na dhamira ya Muungano kwa kuupatia sababu mpya. Ubunifu unahitajika katika kuweka taasisi na miundo itakayotoa fursa zaidi kwa wananchi wa Tanzania na haswa Wazanzibari kuondokana na umasikini, na kuondoa mpasuko miongoni mwa jamii ya Wazanzibari.

Rais ajaye afanikiwe kuwashawishi Watanzania kuhusu azma yake ya kusimamia Muungano usivunjike kutokana na mashinikizo ya viongozi wachache wenye ajenda binafsi na uchu wa madaraka.

Katika kipindi chote ambacho nimekuwa kiongozi, nimekuwa naamini kwamba elimu haina itikadi, inagusa maslahi ya kaya moja moja na maslahi ya taifa.



January Makamba akiwa na rafiki yake Mzee John Momose Cheyo, Mwenyekiti wa UDP, Bungeni Dodoma.

Kama alivyowahi kusema Mzee Mandela, elimu ndio ufunguo pekee wa mlango unaowezesha masikini kupenya kuingia kwenye maisha mazuri. Hivi sasa, kuna kilio kikubwa sana kwa wananchi wote wa vyama vyote, wazazi kwa walimu, na pia wanafunzi. Elimu yetu yapaswa kuakisi jitihada zetu za kujenga uchumi imara miaka zaidi ya kumi ijayo, na kuweza kunyakua fursa zitakazoletwa na ukuaji wa uchumi wetu, ikiwemo uchumi mpya wa gesi.

Ni vigumu leo hii, kwa vigezo vyovyote vya kitakwimu au kinadharia, kushawishi umma kuwa elimu yetu iko imara. Ushahidi wa wazi ni pale ambapo viongozi na

Watanzania wenye uwezo wanapokwepa kupeleka watoto wao kwenye shule za Serikali hapa nchini. Elimu sasa imekuwa ni sababu nyingine ya kutengeneza mpasuko. Kumekuwepo na kigugumizi kuhusu mitaala, falsafa ya elimu yenyewe, ubora wa waalimu, vifaa vya kufundishia na ubora wa majengo. Aidha, suala la mikopo kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu lina matatizo makubwa.

Pamoja na uwekezaji mkubwa wa Serikali ya Awamu ya Nne katika elimu, bado elimu imekuwa ikionekana kuporomoka. Elimu haijachochea vijana kujiajiri wala kuajirika, haichochei udadisi wala ubunifu, uthubutu wala nidhamu, weledi wala uzalendo. Hakuna shaka yoyote kuwa mfumo wa elimu unahitaji mageuzi makubwa na machungu. Huwezi kutafakari kuomba uongozi wa nchi bila ya kuyatafakari yote haya – na kuukubali ukweli huu mchungu.

Rais Ajaye anatakiwa aje na majawabu kuhusu namna gani ataendesha mageuzi makubwa na machungu katika sekta ya Elimu. Kauli za juu juu tu za kuboresha elimu tunazosikia kutoka kwa baadhi ya watarajiwa hazitoshi. Lazima kwenda kwa kina zaidi. Binafsi nimefanya hivyo. Lazima kurudisha matumaini ya kila kaya kuwa nao watakuwa na fursa ya kuwa na maisha bora na kufaidi keki ya taifa. Katika awamu zijazo, elimu itakuwa ndio siasa.

Vilevile, huwezi kutafakari kuomba uongozi wa nchi bila kukubali kwamba kuna kilio cha wananchi kumiliki na kufaidika na rasilimali za nchi. Uwekezaji wa mabilioni ya dola katika sekta ya madini bado haujawanufaisha wananchi walio wengi hata wale waishio pembezoni mwa migodi mikubwa. Hofu kubwa waliyonayo wananchi kwa sasa ni kujirudia kwa historia hiyo katika uwekezaji kwenye gesi. Matukio ya Mtwara ya wananchi kupinga ujenzi wa bomba la gesi ni kielelezo cha hali hiyo.

Siku za karibuni kumekuwepo na vilio viwili vikubwa. Kwanza, kutaka uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa leseni, uvunaji wa rasilimali na usimamiaji wa mapato yatoanayo na rasilimali za taifa; na pili wananchi haswa wazawa kutaka kumilikishwa, au kunufaika zaidi na, rasilimali hizo.

Rais wa Awamu ya Tano anatarajiwa aje na mikakati ya kuleta uwazi, uwajibikaji kwa upande wa wawekezaji na pia kuwezesha Watanzania kushiriki kikamilifu na kunufaika katika shughuli za uchumi wa gesi.

Katika kutafakari nafasi ya uongozi wa nchi, ni muhimu kutambua kwamba Serikali sio jawabu la kila kitu. Ukuaji wa uchumi wa Tanzania na jitihada za kuondoa umasikini zitegemea sana ukuaji wa sekta binafsi. Sekta binafsi

kwa sasa imegubikwa na changamoto nyingi, ikiwemo za kimfumo. Sekta binafsi inayo malalamiko mengi na ya msingi kuhusu mfumo wa kodi, urasimu, rushwa na kutotabirika kwa maamuzi ya Serikali kuhusu biashara na uwekezaji.



January Makamba akikutana na wananchi mbalimbali katika shughuli zake za uongozi.

Changamoto zote hizi kwa pamoja zimechochea ukwepaji kodi, uvunjaji wa taratibu na “ujanja ujanja” katika sekta binafsi. Serikali imechukuliwa kama adui badala ya kuwa rafiki wa sekta binafsi.



Mazingira yalivyo kwa sasa yanavunja moyo na kuzorotesha jitihada za wajasiriamali wa kati na wadogo. Wengi wa hawa wako katika sekta isiyo rasmi ambayo ndio yenye kuajiri watu wengi na inakadiriwa kuwa na uchumi mkubwa sana. Wajasiriamali wa kati na wadogo ndio waajiri wakubwa katika uchumi kuliko viwanda na biashara kubwa. Juhudi za kurasimisha sekta isiyo rasmi lazima zifanyike kwa kasi mpya na maarifa mapya. Wajasiriamali wadogo bado hawakopesheki, na pale wanapokopesheka, mazingira ya biashara ikiwemo mfumo wa kodi na urasimu unachangia kuua biashara zao.

Rais ajaye lazima awe karibu na aongoze jitihada za dhati za kuwasaidia wafanyabiashara wa kati, wengi wao waliopo huko mikoani, wengi wao wakiwa wasafirishaji, wanunua mazao, wenye viwanda vidogo vidogo, ili nao wawe wafanyabiashara wakubwa.

Kama unatafakari kuomba uongozi wa nchi, basi ni muhimu uwe tayari na uwe na uwezo na ujuzi wa kuwa rafiki wa sekta binafsi. Unatarajiwa uongeze kasi kwenye kazi iliyoanzwa na viongozi waliopita ya kutatua changamoto zinazofanya mazingira ya biashara yawe magumu. Sheria, kanuni na taratibu zipo na ya kufanywa yanajulikana kwani ripoti mbalimbali za kimataifa zimeyabainisha na sekta binafsi kupitia taasisi zao zimeyawasilisha Serikalini kwa miaka mingi sasa. Kinachohitajika ni msukumo thabiti wa kiuongozi wa kuboresha mazingira na utayari wa kukataa matakwa ya warasimu wanaotukuza zaidi taratibu kuliko ufanisi na matokeo.

Viongozi wote waliopita wa nchi hii, wamefanya kazi kubwa ya kuijenga na kuilinda heshima ya nchi yetu kwenye nyanja za kimataifa. Ni muhimu heshima hiyo ikaendelezwa. Rais ndio kielelezo cha taifa duniani kote. Kiongozi ajaye, kwa wajihi wake, maarifa yake na kwa weledi wake, yeye kama mtu binafsi, lazima awe na uwezo na ushawishi wa kuendelea kuipaza diplomasia ya nchi yetu.

Tanzania ina majirani nane, sita kati yao ni nchi zisizopakana na bahari. Hivyo, jiografia ya Tanzania inaleta fursa lukuki kama masoko ya bidhaa zetu na soko la bandari yetu lakini pia na changamoto kama uhamiaji haramu, ujambazi, uharamia, utapakaaji wa silaha ndogondogo, magendo mipakani na matishio mengineyo ikiwemo ugaidi. Katika miaka ijayo changamoto hizi zitakuwa kubwa zaidi. Hili nalo limechukua muda wangu mwingi kwenye kutafakari. Rais ajaye lazima awe na uwezo wa kuendeleza uhusiano mzuri na majirani zetu katika kuhakikisha usalama wa nchi na watu wake unalindwa.

Ni muhimu kuwatoa hofu wananchi waishio mipakani, kuhusu usalama wao na kuhusu uraia wao, na kuwatoa hofu na kuwajengea mazingira mazuri wale wanaofanya biashara kati ya Tanzania na nchi jirani.

Mahusiano ya Tanzania na mataifa tajiri na makubwa duniani ni mazuri na yameendelea kuimarika. Rais Kikwete amefanya kazi nzuri sana kwenye hili. Tanzania bado ni nchi inayotegemea misaada kutoka kwa mataifa haya katika kufidia nakisi ya bajeti yake. Rais ajaye lazima athamini mchango huu lakini pia ajue kwamba nchi wahisani sio wajomba zetu na lazima aongoze mkakati madhubuti wa taifa letu kujitegemea kibajeti na kubadili mahusiano yetu na nchi kubwa kutoka kwenye ufadhili kwenda kwenye ushirika wa kibiashara na uwekezaji.

Haya niliyoyazungumza ni machache tu. Yapo mambo mengi ambayo nimekuwa nikiyatafakari, na naamini mengine yatajitokeza wakati naendelea kutafakari, ambayo kwa kweli kama mtu unataka kuongoza nchi lazima utengeneze fikra kadhaa za namna ya kuyakabili hata kabla hujaanza harakati na kutangaza nia.

Kuomba uongozi hakuanzii na kuishia na kauli-mbiu rahisi za afya bure, elimu bure ambazo hazina ufafanuzi wala maelezo – ambazo ni rahisi kuvutia na kuhadaa watu. Hazishii na kauli za juu juu kwamba tutaongeza ajira au tutaboresha elimu. Kila mtu aweza kusema haya. Swali kubwa ni kiviipi? Kwa maarifa gani mapya?

Nafahamu kwamba ndani ya Chama chetu wagombea wetu wanaongozwa na Ilani ambayo inatengenezwa na Chama. Lakini, pale unapojaza fomu ya kuomba kuteuliwa na Chama chetu kwa nafasi ya Urais, ndio unaomba nafasi ya Urais hivyo.

Kwa hiyo huwezi kuwa unaomba nafasi ya Urais halafu huna fikra zozote au imani yoyote inayokusuma au dhamira ya kufanya lolote na ukasema unasubiri upewe Ilani. Ilani itakuongoza kwa sababu unapeperusha bendera ya Chama lakini haukatazwi kufanya ya zaidi ya Ilani.

Hata Rais Kikwete kuna mambo makubwa na ya msingi ambayo hayamo kwenye Ilani lakini aliyadhamiria kuyafanya kwa manufaa ya taifa na ameyafanya.

Najua nimeongea kwa kirefu sana lakini nadhani swali hili lilikuwa ni la msingi sana. Nimalizie kwa kusema kwamba, katika harakati za kutafuta nafasi hii,

wote wanaoiwania watambue kwamba kuna Rais aliyeko madarakani ambaye anafanya kazi nzuri. Kwa hiyo ni muhimu kuwe na staha katika harakati hizi. Vilevile Chama chetu kinao utaratibu mzuri wa namna ya kuomba nafasi hizi, utaratibu ambao lazima ufuatwe.

Nitakapotangaza rasmi kujitosa katika nafasi hii, na naamini itakuwa muda si mrefu kuanzia sasa, na kuanza kampeni basi haitakuwa kuingia kujaribu tu, au kuingia kwa ajili tu ya kujipanga na uchaguzi wa miaka ya mbele au kwa ajili kuweka mazingira ya kumuunga mkono mtu mwingine ili akupe cheo kizuri. Hapana. Nitakapoamua nitaingia kwa dhamira ya kushinda na kuongoza mabadiliko makubwa ambayo Watanzania wanayatarajia.

2

Naamini watu wengi watapenda kujua January Makamba ni nani haswa. Hebu tuelezee kwa kifupi historia yako; ulizaliwa wapi, umekulia wapi, umepitia wapi, umefikaje hapa ulipo leo? Jina la baba yako limekubeba?



PICHA YA KUSHOTO: Mstari wa mbele kutoka kushoto, Mama January, January Makamba, Mwamvita Makamba, Ali Makamba, Mzee Makamba akiwa amemshika Thuwein Makamba. Mstari wa nyuma ni wadogo zake Mzee Makamba. PICHA YA KULIA: Kutoka kushoto, Ali Makamba, Bhuto Makamba, Dhamana Makamba (Shangazi yake January), Mwamvita Makamba na January Makamba.

Nilizaliwa tarehe 28 Januari 1974 mjini Singida, kwa Bi. Josephine Joseph na Bwana Yusuf Makamba. Mwaka 1978, nilipelekwa kuishi kijijini kwa bibi mzaa mama Kyaka, Kagera wakati mama ameenda kuendelea na masomo ya uuguzi. Kijijini kwetu ilikuwa umbali mfupi kutoka Mutukula, mpakani mwa Tanzania na Uganda. Idi Amini alipovamia Tanzania mwaka huo, kitongoji chetu kinachoitwa Kituntu, sio Kituntu ya Karagwe unayojua wewe Padre, karibu na Kyaka nacho

kilipigwa mabomu. Mimi na bibi yangu tulikimbia makazi yetu na kuhamia kwenye kambi ya wakimbizi eneo linaloitwa Mwisu. Baba yangu wakati huo alikuwa mstari wa mbele kwenye vita dhidi ya Idi Amin. Tulikaa kambini kwa muda baadaye tukafanyiwa utaratibu wa kuondoka kwenda Biharamulo na mama akaja kutuchukua. Sina kumbukumbu kubwa sana ya kipindi hiki kwa kuwa nilikuwa bado mdogo ila nakumbuka mvua nyingi, milio ya ndege na mabomu.

Nimesoma shule nne za msingi katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu kutokana na wazazi kuhamishwa mara kwa mara katika utumishi wa umma. Lakini pia kuanzia darasa la tatu hadi la tano nilirudishwa tena kijijini, Kituntu Kyaka, kukaa na bibi. Maisha ya kijijini siwezi kuyasahau. Enzi hizo, miaka ya mwanzoni mwa 1980, maisha ya kijijini yalikuwa magumu sana, bidhaa muhimu kama sukari, sabuni, dawa za mswaki, chumvi, na nyinginezo, zilikuwa adimu. Kutoka kitongojini Kituntu hadi shuleni ilikuwa mwendo mrefu na baada ya shule nilikuwa na kazi ya kwenda kuchunga mbuzi wa bibi, na baada ya kuchunga mbuzi kila jioni saa moja ilikuwa ni kazi ya kuchota maji mtoni, na baada ya hapo ilikuwa ni kumsaidia bibi kuuza pombe ya lubisi usiku na Jumamosi ilikuwa ni kwenda shamba kupalilia migomba na mikahawa. Maisha yale yalinifundisha mambo mengi. Baada ya miaka mitatu, nilirudi kukaa na wazazi na kumaliza darasa la saba Shule ya Msingi Masiwani, Tanga Mjini.

Nilianza Sekondari katika shule ya Sekondari Handeni, Tanga. Nakumbuka wakati naanza pale shule ile ilikuwa bado inajengwa, sisi tulikuwa Form 1 wa pili – na ilikuwa haina tofauti kabisa na shule ambazo sasa zinaitwa shule za Kata. Kwa kuwa hii ilikuwa shule ya kutwa, mzazi wangu alipohamishwa kikazi kutoka Handeni, nikahamia Shule ya Sekondari Galanos Tanga, ambayo ilikuwa shule ya Serikali ya boarding.

Nilikuwa mwanafunzi mzuri pale Galanos, na, nikiwa kidato cha tatu, nikachaguliwa kuwa Makamu wa Kiranja Mkuu. Nilikuwa nafanya vizuri darasani, nikachagua mchepuo wa sayansi nikiwa na *combination* ya *Chemistry* (Kemia), *Biology* (Baiolojia) na *Agriculture* (Kilimo) (CBA). Nilipata daraja la kwanza kwenye mthani wa kanda wa *mock* wa kidato cha nne, nikiwa na uhakika wa kuendelea na A-Level katika Shule ya Sekondari Kibaha, shule pekee iliyokuwa inafundisha mchepuo wa CBA hapa nchini. Hata hivyo, nilifanyiwa hujuma kubwa kutokana na siasa zinazomhusu Mzee wangu na kufutiwa matokeo ya mthani wa kidato cha nne.

Sikufa moyo, nilirudia mthani kama mtahiniwa binafsi na kufaulu na kuweza kusoma A-Level katika Shule ya Sekondari Forest Hill Morogoro na nikapata

Daraja la Pili kwenye mthani wa Kidato cha Sita. Kabla ya kwenda Chuo Kikuu, niliamua kwenda kufanya kazi kwenye makambi ya wakimbizi kutoka Burundi yaliyokuwa wilaya ya Kasulu, Mkoani Kigoma. Niliipenda sana kazi ile ya kuhudumia wakimbizi na kuifanya kwa bidii kubwa. Nilipewa madaraka zaidi hadi kufikia nafasi ya Meneja wa Kambi Msaidizi wa Kambi ya Mtabila 2 iliyokuwa na wakimbizi zaidi la laki moja. Nilibahatika kuwa na wajibu na dhamana kubwa ya kuongoza kambi kubwa na wafanyakazi wengi nikiwa na umri mdogo tu wa miaka 21. Nilikuwa na wafanyakazi wengi, tena wengine watu wazima, waliokuwa wanaripoti kwangu. Nilikuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba wakimbizi laki moja wanapata viwanja vya kuishi, wanapata vifaa muhimu kama mahema, na wanapata chakula. Kazi ile ilibadilisha kabisa mtazamo wangu juu ya maisha. Baada ya kushuhudia adha wanayopata wanadamu wenzetu kutokana na vita hadi kukimbia makazi yao na nchi yao na kuja kukaa maporini kwenye nchi yetu, na baada ya kutafakari kuhusu udhalilishwaji na mateso yanayotokana na ukimbizi, niliamua kuachana na azma ya kusoma sayansi na uchumi na nikaamua kwamba maisha yangu nitayatoa katika kuchukua masomo kuhusu amani, na namna ya kutafuta amani ili nitoe mchango kwenye kuepusha vita na kupatikana kwa amani duniani. Hivyo, nilianza kutafuta vyuo duniani vinavyofundisha masuala ya amani. Nilipata chuo kimoja cha Wakatoliki Marekani, kinachoitwa St. John's University. Lakini kilikuwa Chuo aghali kidogo, kwa hiyo nikaanza kusoma masomo ya awali kwenye Chuo kingine kidogo katika jiji la Boston kinachoitwa *Quincy College* na baadae nikajiunga na *St. John's University* na kupata shahada ya kwanza ya sayansi ya masomo ya amani (*Bachelor of Science in Peace Studies*). Gharama za masomo zilikuwa kubwa na nilihangaika kufanya kazi mbalimbali, ikiwemo kazi za ulinzi na kuhudumia watu wenye magonjwa ya akili ili kulipia ada ya shule.

Baada ya kumaliza shahada ya kwanza, nilishinda tuzo ya kujiunga na taasisi ya Rais Mstaafu wa Marekani, Jimmy Carter, inayoitwa *Carter Presidential Center* iliyopo Atlanta hukohuko Marekani. Ilikuwa changamoto kubwa na fursa nzuri kwa sababu vijana wote waliojiunga pale walikuwa ni vijana mahiri sana na wenye uwezo mkubwa. Taasisi ile ilinipeleka nchini Sierra Leone kusimamia uchaguzi mkuu na kutekeleza mradi wa kufufua taasisi za haki zilizoporomoka baada ya vita. Nako pia nilijifunza mengi kuhusu ujenzi wa taifa.

Baada ya hapo nikaamua kuchukua shahada ya pili (*Masters degree*) kwenye Chuo Kikuu cha *George Mason* kilichoko Jimbo la Virginia, Marekani. Nilipata wakati mgumu kulipa ada, kiasi cha kukaribia kufukuzwa shule. Niliomba msaada kwa watu mbalimbali akiwemo Rais wa wakati ule Mhe. Benjamin William Mkapa. Bahati nzuri, alikubali kusaidia kwa sharti kwamba nije kutumia

utaalamu wangu Serikalini nitakapomaliza masomo. Na ndivyo nilivyofanya. Baada ya masomo hayo, nikajiunga na Wizara ya Mambo ya Nje.

Mwaka 2005 nilifunga ndoa na mchumba wangu wa miaka minne, Ramona Urasa, na nimekuwa na familia yenye furaha sasa mwaka wa kumi.



January Makamba na mkewe wakipongenzwa na Rais Benjamin Mkapa (kabla hajastaafu) wakati wa harusi yao kwenye viwanja vya Karimjee miaka 10 iliyopita. Nyuma ni Mzee Makamba, Mama Makamba na Mama Anna Mkapa.

Pale Wizarani, nilipata fursa ya kufanya kazi na Waziri wa Mambo ya Nje wakati huo, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete. Nahisi alipenda kazi zangu na mara alipoamua kuwania nafasi ya Urais akanitaka nichukue likizo isiyo na malipo Serikalini ili niwe msaidizi wake kwenye kampeni zile. Siwezi kusahau maishani mwangu ile fursa kubwa kwani niliweza kujua kwa kina nchi yangu na watu wake. Na kwa kuwa kampeni zinahusu ahadi za utatuzi wa kero za watu, nilipata fursa ya kujua kero za Watanzania kwenye kila wilaya ya nchi yetu.

Baada ya Rais Kikwete kushinda aliniteua kuwa Msaidizi wake Ikulu, nikiwa na jukumu la kumsaidia kuandika hotuba zake, pamoja na mambo mengine mengi

ya uendeshaji wa shughuli zake za kila siku. Kazi ile ilikuwa ngumu kwa sababu inakulazimisha kujifunza na kujua karibu kila kitu ndani ya Serikali na duniani kwa ujumla, na kufanya utafiti karibu kila siku kwa sababu Rais anazungumza kila siku kuhusu mambo mbalimbali na kwa makundi mbalimbali. Pia kazi ile inakupa fursa ya kuhudhuria vikao vya Baraza la Mawaziri kama msikilizaji ambapo pia unajifunza mambo mengi ya uendeshaji wa Serikali, ikiwemo maamuzi muhimu ya kisera na kiutendaji yanavyofanywa. Ni nafasi ya heshima sana na sitamsahau Rais Kikwete kwa kunipa fursa ile.

Baba yangu alikuwa mwanasiasa karibu maisha yake yote lakini sikupata kuwaza kuingia kwenye siasa katika maisha yangu hadi nilipofanya kazi na Rais Kikwete. Baada ya kufanya kazi ile Ikulu kwa miaka mitano, nami nikahamasika na kuamua kushiriki katika uongozi wa umma. Niliamua kwenda kwetu Bumbuli kugombea nafasi ya Ubunge mwaka 2010, nikafanikiwa. Baada ya kuingia Bungeni nikapata nafasi ya kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini. Kazi ile tuliifanya vizuri sana na wenzangu kwenye Kamati hasa katika kipindi kile kigumu cha mgao wa umeme na matatizo ya mafuta nchini.



Mzee Yusuf Makamba, Katibu Mkuu Mstaafu wa CCM na baba mzazi wa January Makamba akimuombea kura mgombea pekee wa Uenyekiti wa CCM kwenye Mkutano Mkuu wa Taifa wa CCM Kizota, Novemba 2012.

Baada ya kitambo kidogo, nikateuliwa kwenye Sekretarieti ya Chama nikiwa kama Katibu wa NEC wa Siasa na Mambo ya Nje, na nikawa Mjumbe wa Kamati Kuu na Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM. Nilishika nafasi hizi katika kipindi kigumu sana kisiasa kwa Chama chetu na nilijifunza mambo mengi na kutoa

mchango wangu kwenye kukijenga na kukiimarisha. Baada ya kitambo kingine, nikateuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Kuhusu kubebwa na jina la mzazi, kama nilivyosema hapo awali, pamoja na kwamba mzazi wangu alikuwa kwenye siasa kwa muda mrefu, binafsi, ingawa nilipenda na nilishiriki kuwa kiongozi tangu shuleni, sikuwa na mawazo ya kuingia katika siasa. Nilipokuwa Sekondari nilipenda kuwa mwanasayansi wa kilimo.

Baada ya kuzunguka nchi nzima kwenye kampeni ya 2005 na baada ya kufanya kazi ya kumsaidia Rais Ikulu ndipo nilipobaini kwamba siasa, ukiiendesha vizuri na kwa manufaa ya watu, inayo nafasi ya kubadilisha maisha ya watu. Nilipofanya uamuzi wa kugombea Ubunge, sikutaka ushauri wa baba yangu kwa sababu nilikuwa na uhakika kwamba angenikatalia. Niliamua mwenyewe na nikaanza harakati na ndipo nikamwambia. Kwa hiyo, unaweza kuwa na mzazi mwanasiasa na bado ukaweza kuwa na uhuru wa kujiamulia mwenyewe unataka kufanya nini.

Ni kweli kwamba jina maarufu la mzazi aliye kwenye siasa linasaidia kwa maana tayari kuna watu ambao wanamheshimu na ambao wapo tayari kukusaidia. Lakini pia jina hilo linaweza kukuharibia kwa sababu pia unaweza kurithi maadui zake, ambao wanakuona wewe ni sehemu ya yeye hata kama una mawazo na mtizamo huru. Kwa hiyo, siasa yangu nimejitahidi kuifanya kama mimi binafsi. Mimi na baba yangu tuna staili tofauti za siasa na mimi nina namna yangu ya kufanya mambo ambayo inatofautiana na yake. Lakini pia kuna mambo mengi mazuri ambayo nimejifunza kutoka kwake ikiwemo haja ya kuwa na msimamo usioyumba katika unayoyaamini na haja ya kutokumuogopa mtu yoyote.

3

Je umeshapata watoto? Kama ni ndiyo ni wangapi? Je, mtazamo wako kuhusu familia na malezi ya watoto ni upi? Watu wanasema maji hufuata mkondo, je, ungependa watoto wako wawe wanasiasa kama wewe?

Mwenyezi Mungu ametujalia mimi na mke wangu wa miaka kumi watoto wawili. Naamini familia ndio kitovu kikuu na msingi wa jamii. Mimi naamini kwamba kiongozi mwenye familia ana nafasi ya kuwa kiongozi mzuri zaidi. Kuwa na familia ndio kunakufanya uwe mtu mzima pia kunakufanya uwe responsible na kunakufanya uwe na mtazamo, au kwa kiingereza wanasema *perspective*, chanya na ya kuangalia mbali zaidi. Hata vitabu vya dini zote vinasisitiza umuhimu wa familia kama kitovu cha jamii iliyo bora.

Na hata aina ya taifa tulilionalo inaanzia kwenye aina ya familia tulizonazo na aina ya malezi tunayoyatoa kwa watoto wetu ndani ya familia. Msemu wa mtoto umleavyo ndivyo akuavyo ni wa kweli kabisa. Naamini kwamba ni muhimu wazazi wakawapenda sana watoto wao – na hapa sina maana ya kuwadekeza. Kuwapenda sana watoto kunawafundisha watoto umuhimu wa upendo.

Ni muhimu kuwajenga watoto katika misingi ya kujitegemea tangu wakiwa wadogo. Ni muhimu pia kuwajenga watoto mapema katika misingi ya kuthamini ukweli na kuthamini haki na umuhimu wa kuwajali na kuwaheshimu watu wote. Ni muhimu kuwajenga watoto waweze kujiamini na kujieleza kwa ufasaha. Ni muhimu watoto wakajua tangu mapema kwamba Mungu yupo. Ni muhimu kuwajengea watoto udadisi, ikiwemo kusoma vitabu na kutaka kujua mambo mengi zaidi. Ni muhimu kutenga muda wa kutosha kuzungumza na watoto wetu na kuwadadisi kuhusu mambo mbalimbali.

Si sahihi kujenga mazingira ya watoto kuwaogopa wazazi kiasi cha kushindwa kusema yaliyo moyoni au kukiri pale wanapokosea na kubaki na siri ambazo ni hatari kwa ustawi wao.



January Makamba akiwa na mke na watoto wake nyumbani.

Mimi na mke wangu tunajitahidi kuwalea watoto wetu kwenye misingi hii. Kuna changamoto nyingi za malezi ya watoto katika mazingira ya sasa. Gharama za elimu ziko juu na gharama za matibabu nazo zimepanda. Kama wazazi, moja ya mambo ambayo yanatusumbua kila siku ni kuhakikisha kwamba, wakati wote, tunakuwa na uwezo wa kuwatibu wanapougua na kuwalipia ada ya shule.

Lakini pia kuna changamoto mahsusi za ulimwengu wa sasa wa utandawazi ambapo watoto wanakuwa exposed na mambo mengi wasiyostahili kuyafahamu au kuyafanya katika umri mdogo. Wazazi lazima wawe makini katika kukabiliana na changamoto hii. Watoto lazima walindwe na mambo haya lakini pia lazima walindwe dhidi ya watu wasio wema wanaoweza kuwanyanyasa au kuwaharibu kwa namna moja au nyingine.

Kuhusu watoto wangu kuingia siasa, nisingependa kuwachagulia watoto wangu kazi ya kufanya.

Hata mimi wazazi wangu hawakuniamulia wala kunisukuma kuingia kwenye siasa licha ya kwamba baba yangu alikuwa mwanasiasa.

Ningependa wawe na ndoto njema na malengo makubwa juu ya maisha yao na mchango wao kwenye jamii yetu na mimi wajibu wangu utakuwa kuwapa sapoti watimize ndoto zao hizo.

4

Umesema kwamba ulisomea Chuo Kikuu cha Kikatoliki Marekani. Kama ujuavyo, mimi ni Padre. Napenda kusikia kidogo kuhusu suala hili. Ulijifunza nini pale.

Ni kweli, nilisoma St. John's University, chuo cha Wakatoliki Wabenedictino, kilichopo Minnesota, Marekani. Pale chuoni palikuwa na Seminari na Monasteria ya Watawa. Sehemu kubwa ya walimu wangu walikuwa watawa wa Kibenedicto. Zaidi ya masomo ya darasani, nilijifunza umuhimu wa huduma kwa watu wengine na umuhimu wa kuyapa tafsiri pana zaidi maisha yako kuliko manufaa yako binafsi – kama vile kazi nzuri, nyumba nzuri, gari nzuri na kadhalika.

Kwa hiyo, wakati mwingine napata shida kidogo kutoka kwa ndugu na jamaa na marafiki kwa sababu katika vitu ambavyo binafsi havinisumbui ni haja ya kukusanya mali, majumba, magari ya kifahari na kadhalika. Falsafa yangu ni kwamba hapa duniani tunapita tu kutimiza mapenzi ya Mungu na kwamba hakuna mtu atakayekumbukwa kwa mali zake bali kwa mchango wake kwa jamii pana na labda pia kwa uadilifu wa watoto aliowakuza na kuwalea.

Hii haipaswi kuwa kauli-mbiu tu ya kisiasa kwa ajili ya kufurahisha watu bali inapaswa kuwa imani ya ndani ya moyo kabisa. Na nadhani ni falsafa ya dini zote pia. Falsafa hii ni muhimu sana kwa viongozi kwa sababu inatoa fursa ya kutotumia dhamana uliyopewa kujinufaisha.

Pia pale chuoni nilipata fursa ya kufanya kazi kwenye nyumba ya watawa waliostaafu, ambao ni wazee sana. Kwa utaratibu wa baadhi ya nchi zilizoendelea, mtu akishakuwa mzee sana anapelekwa kwenye nyumba maalum, inaitwa *Nursing Home* ambapo wanaajiriwa watu kuwahudumia hadi mwisho wa uhai wao. Mimi nilipata fursa ya kuhudumia watawa wenye umri wa miaka kati ya 80 hadi 104 ambao wapo katika miaka ya mwisho ya uhai wao – baadhi ambao hawajiwezi kabisa. Kazi yangu ilikuwa ni kuwapa chakula, wengine kuwapa dawa zao, na wengine kuzungumza nao tu, kuwapa kampuni wasiwe wapweke katika vyumba vyao na kuwafariji. Ni kazi inayokupa uthabiti na kukujenga katika moyo wa kuhudumia watu wengine. Lakini pia mazungumzo na watu

ambao wamejitoa maisha yao kwenye imani, na ambao sasa wanajua kabisa wanafikia mwisho wa uhai wao, nayo yalikuwa yanasisimua na kufundisha sana. Kipindi kile cha kuwa pale Chuoni na kutoa huduma na kujifunza masuala mengi kimenijenga kama mtu lakini pia kama kiongozi. Siwezi kusahau.



January Makamba akiwa na Mwalimu Mkuu na Masista wengine wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Kifungilo Lushoto.

5

Umenukuliwa na baadhi ya vyombo vya habari ukisema kwamba sasa ni wakati wa viongozi vijana kujitokeza na kuchukua nafasi kubwa za uongozi kama Urais wa nchi. Kwa nini mjadala huu ni muhimu wakati huu na vitu gani vipya vya kuibadilisha Tanzania vinavyoweza kufanywa na vijana na si wazee? Kwanini vijana waaminiwe kwenye nafasi kubwa wakati hawana uzoefu wa kuongoza?

Nianze kwa kufafanua kwamba siamini kwamba umri pekee ni sifa ya uongozi. Siamini kwenye dhana kwamba ukiwa Mzee unafaa na ukiwa kijana hufai, au ukiwa Mzee hufai na ukiwa kijana unafaa. Ujana sio sifa, uzee sio kashfa. Ujana sio kashfa, uzee sio sifa. Tunapokubaliana kwamba umri sio kigezo maana yake ni kwamba mwenye miaka 40 asionekane hawezi kutokana tu na miaka yake 40. Mimi naamini kwamba uongozi ni suala la marika. Kila rika au kila kizazi kina wakati wake. Kila rika lina wajibu wake. Ndio maana Mwalimu Nyerere aliamua kung'atuka akiwa na miaka 62 tu, sio kwamba alishindwa, sio kwamba hakuwa na nguvu wala uwezo wa kuendelea, bali alifanya hivyo kuachia rika au kizazi kingine kiendeleo.

Kwa hiyo hoja yangu ilikuwa ni kwamba kila kizazi kina changamoto zake na majukumu yake. Nimekuwa nawahimiza vijana wenzangu kwamba sasa ni wajibu wao kujitokeza ili kutimiza wajibu na majukumu ya rika na kizazi chao. Kwamba ni wajibu wao kuitengeneza Tanzania mpya wanayotaka kuiishi kwa miaka 50 ijayo.

Wapo waliofanya kazi na Mwalimu Nyerere, ambaye alistaafu miaka 30 iliyopita na kuwaacha Serikalini, na bado wanataka kuendelea kuomba uongozi. Hiyo ni haki yao ya kidemokrasia na wala wasibezwe.



January Makamba ana ukaribu na urafiki na Rais wa Zamani wa Afrika ya Kusini, Ndugu Thabo Mbeki. Hapa wakisalimiana kwa furaha katika moja ya mikutano ya kimataifa. Mbele ya Waziri Mkuu wa Zamani wa Tanzania, Cleopa Msuya.

Lakini mimi naamini kwamba tunaishi kwenye dunia tofauti sana yenye mahitaji tofauti na changamoto tofauti, dunia inayohitaji uongozi wenye maarifa mapya. Na rika na umri ni vitu tofauti. Mwalimu Nyerere alitaka kung'atuka mwaka 1980, akiwa na miaka 58 tu lakini akang'atuka mwaka 1985 akiwa na miaka 63. Aling'atuka kwa sababu dunia ilikuwa inabadilika haraka sana, kama ilivyo sasa, na busara ikamtuma awaamini na kuwaachia viongozi wa rika jipya ili kukabiliana na changamoto mpya na mahitaji mapya. Na kila mtu anajua kwamba aliwatarajia Marehemu Edward Sokoine na Dr. Salim Ahmed Salim, wakati huo wote walikuwa kwenye miaka ya 40, wamrithi uongozi. Baadaye alichaguliwa Ndugu Ali Hassan Mwinyi ambaye alikuwa na ujasiri wa kufanya mabadiliko makubwa na ya kihistoria na kubadilisha mfumo mzima wa siasa na uchumi wa nchi yetu.

Kuna watu wa rika mbili. Kuna wenye kesho nyingi kuliko jana na kuna wenye jana nyingi kuliko kesho.

Uongozi ni kutengeneza kesho njema. Wenye kesho nyingi hawapaswi kukaa pembeni na kukunja mikono na kuwaachia wenye jana nyingi

kazi ya kujenga kesho njema. Wakifanya hivyo, uhakika wa kesho njema unaweza usiwe mkubwa kwa sababu wenye jana nyingi wanaweza kuhangaika na masaibu ya jana zao kuliko matumaini ya kesho.

Lakini pia siamini katika dhana kwamba vijana waongoze peke yao. Nchi hii sio ya vijana peke yao. Hapana. Wazee ni muhimu sana. Hata wakati wa harakati za kutafuta uhuru, vijana ndio walioongoza harakati hizo. Mwalimu Nyerere alichaguliwa kuwa Rais wa TANU akiwa na miaka 32 tu. Lakini wazee walikuwa nyuma yao, nao walishiriki. Ni muhimu kuwe na mchanganyiko. Ni vyema tukajenga imani na uongozi wa vijana. Sasa hivi kijana yoyote akijitokeza anabazwa na wakati mwingine anatungiwa uongo kwamba ni kibaraka wa Mzee fulani, kwamba haiwezekani kwamba akawa yuko yeye mwenyewe. Inasikitisha. Lakini pia na viongozi vijana wanao wajibu wa kufanya kazi ya ziada ili kuheshimika. Tabia njema na kujiheshimu na kuheshimu wananchi na viongozi wa juu ni suala la msingi sana.


Vilevile kuna aina mbili za viongozi vijana: kuna viongozi vijana ambao wana nafasi za uongozi tu na kuna vijana ambao wameelelewa kiuongozi. Kuna vijana wenye vyeo na kuna ambao wametayarishwa, ambao wamepewa fursa za kuifahamu dunia inavyoendeshwa na kuifahamu nchi, kuifahamu serikali na kutambua uzito wa dhamana ya uongozi. Wapo pia viongozi vijana ambao hawakupata fursa hizo. Kwa hiyo kuna vijana ambao wamekomaa na wapo tayari, na kuna vijana ambao hawapo tayari kama ambavyo wapo pia wazee ambao pia, pamoja na muda mrefu wa uongozi, hawako tayari.

Viongozi vijana ambao wako tayari wanatambua wajibu wa kuutambua, kuuthamini, kuutunza na kuuendeleza urithi na tunu za taifa letu. Wanatambua kwamba hawaanzi upya katika kuijenga nchi hii, kwamba kuna kazi kubwa imefanywa na viongozi waliotangulia, na kwamba wao wanaanzia hapo na wanasisimama katika mabega ya viongozi waliotangulia, na wana wajibu wa kuendeleza yale yaliyo mema na kuilinda misingi muhimu ya Chama na taifa letu.

Kuhusu uzoefu, imedhihirika kwa mifano mingi hapa nchini na kote duniani kwamba uwezo wa uongozi na mafanikio ya kiongozi wa nchi hayatokani na nafasi alizopata kushika huko nyuma. Moja ya mijadala mikubwa kwenye uchaguzi wa Marekani wa mwaka 2008 ilikuwa ni hili la uzoefu. Obama alikuwa Mbunge kwa miaka mitatu tu, basi. Hajawahi kuwa hata Naibu Waziri. Viongozi wenzake na wengine waliompinga wakasema hana uzoefu. Wamarekani wengi wa kawaida wakasema kwamba sifa na ubora wa uongozi haupimwi

kwa miaka mingi na nafasi za ndani ya Serikali. Wakampa kura nyingi kuongoza taifa kubwa duniani.

Majuzi kuna rafiki yangu alitumia nukuu ya Waziri Mkuu Mstaafu wa Uingereza Tony Blair aliyoitoa mara baada ya kuchaguliwa kuongoza Serikali mwaka 1997. Tony Blair, aliyechaguliwa kuongoza Uingereza akiwa na miaka 43 tu, alisema kwamba “wakati nachaguliwa kama Waziri Mkuu, nilikuwa sijawahi kushika nafasi yoyote Serikalini. Sikuwahi kuwa hata Naibu Waziri. Na Uwaziri Mkuu ndio kazi yangu ya kwanza na pekee Serikalini”. Mtu anaweza kujenga hoja kwamba hii ni mifano ya nchi nyingine zilizoendelea haihusiani na Tanzania. Lakini dhana ni ileile ya kwamba baadhi yetu tuko tayari kuchagua wagombea wasiofaa kwa kigezo tu kwamba ni wanasiasa wakongwe.



January akizungumza na Balozi wa China nchini Tanzania Mheshimiwa Lu Youqing kuhusu uhusiano kati ya Tanzania na China juu ya maendeleo ya Tanzania.

Katika nchi yetu hii, viongozi vijana waliaminiwa kwa jukumu kubwa la kuongoza mapambano ya kutafuta uhuru na baadae viongozi hao hao vijana akina Job Lusinde, George Kahama, Oscar Kambona, Pius Msekwa, Salim Ahmed Salim, John Samuel Malecela na wengineo, wengi wakiwa na umri wa chini ya miaka 30, waliaminiwa katika jukumu zito la kuongoza ujenzi wa taifa jipya. Hakuna sababu ya kuacha kuendelea kuamini vijana.

Lakini hata hapa nchini, mwaka 2010, Watanzania asilimia 40 walipiga kura za Urais – dhidi ya Rais aliyekuwa madarakani. Watanzania hawa waliwapigia kura watu ambao hawajawahi kushika hata Ukuu wa Wilaya.

Watanzania wanapochagua Rais, hawaangalii ukubwa wa nafasi alizowahi kushika huko nyuma bali wanatafuta mtu watakayemwamini.

Kwa kifupi, Watanzania wana busara kubwa zaidi kuhusu vigezo na sifa za kiongozi wanayemtaka kuliko sisi wanasiasa tunavyohangaika kuorodhesha miaka tuliyodumu kwenye siasa kama ndio sifa ya uongozi.



January Makamba akisalimiwa na kina mama mara baada ya mkutano wake na wananchi.

6

Je, umekomaa vya kutosha kushika nafasi ya Urais? Umefanya nini kwenye wizara yako, kiasi kwamba watu waweze kuamini kwamba unastahili nafasi ya juu zaidi ya hiyo uliyo nayo kwa sasa? Ulipochaguliwa kuwa Mbunge ulianzisha Shirika la Maendeleo Bumbuli. Nini kilikusukuma? Shirika linafanya nini na limewasaidia vipi watu wa Bumbuli. Je, kama jimbo bado lina changamoto unastahili kuomba nafasi ya juu?

Sina hakika una maana gani kwenye neno kukomaa. Lakini kama una maana ya umri, ndio, nimekomaa. Umri uliowekwa kwenye Katiba ya nchi yetu kwa nafasi ya Urais ni miaka 40 ambao nimeshaupita. Kuna nchi kubwa kama vile Marekani wameweka miaka 35.

Mwaka huu ninafikisha miaka 41, na kwa umri huu, nina umri mkubwa zaidi ya asilimia 85 ya Watanzania. Waasisi wa taifa letu walioweka umri wa miaka 40 kama kigezo cha Urais kwenye Katiba walikuwa na busara ya kuona kwamba umri huo ni umri wa mtu mzima aliyekomaa.

Kama una maana ya kukomaa kwa maana ya kuzifahamu kero za Watanzania na uwezo wa kuzipatia majawabu, jibu pia ni ndio, nimekomaa. Na tena sio kuyafahamu majawabu ya siku zote bali maarifa mapya yanayoendana na karne hii mpya. Kama ni kukomaa kwa maana ya kuwepo kwenye siasa kwa miaka mingi, sina hakika Watanzania wanatafuta kiongozi ambaye kwa miaka 40 ameshiriki kuuweka mfumo tunaoulalamikia.

Watanzania hawatafuti mwanasiasa mkongwe kuwaongoza, wanatafuta kiongozi mahiri na mwadilifu wa zama mpya.

Kama ni kukomaa kwa maana ya nafasi za uongozi nilizoshika, jibu pia ni ndio, nafasi hizo zimenikomaza: nimefanya kazi jikoni kabisa Ikulu, nikimsaidia Rais; nimekuwa Mwenyekiti wa Kamati muhimu ya Bunge ya Nishati na Madini; nimekuwa kwenye Sekretarieti ya Chama chetu kama Mkuu wa Idara ya Siasa na Mambo ya Nje ya CCM; nimekuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM; pia nimekuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa; nimekuwa Mbunge na nimekuwa ndani ya Serikali. Najua Serikali na uendeshaji wake vizuri sana. Nakijua Chama chetu vizuri sana.

Kama ni kukomaa kwa maana ya busara, hekima na uwezo wa kufanya maamuzi sahihi, jibu pia ni ndio, nimekomaa. Sina rekodi ya kuropoka, kutukana, kuhamaki, kushambuliana na watu na kufanya maamuzi ya papara. Najua uzito wa dhamana ya uongozi.



January Makamba akizungumza kuiwakilisha Tanzania katika moja ya Mikutano ya Kimataifa kuhusu Sayansi na Teknolojia.

Watanzania wengi ninaokutana nao wanataka nchi yetu ifungue ukurasa mpya.

Ukomavu wa kiongozi haupo kwenye umri wake bali kwenye maarifa yake na busara zake na malezi yake na uadilifu na uzalendo wake. Historia inaonyesha kwamba uwezo wa uthubutu hautokani na umri mkubwa wala uzoefu mrefu kwenye siasa. Na ukweli ni kwamba kwa kadri unapokuwa kwenye system miaka mingi ndipo mazoea ya kufanya uliyozoea unapunguza uthubutu wa kufanya mambo mapya na hivyo kupunguza uwezekano wa kufanya mabadiliko makubwa. Wakati wazee wanamchagua Mwalimu Julius Nyerere kuwa Rais wa TANU mwaka 1954 ili aongoze harakati za uhuru, ambazo ni ngumu na hatari kuliko hata uongozi wa nchi, ukomavu wake haukutazamwa kwenye umri wake mdogo wa miaka 32. Wakati Tony Blair anachaguliwa kuwa Waziri Mkuu wa taifa kubwa la Uingereza, akiwa na miaka 43 tu, na akiwa hajawahi kushika nafasi yoyote ya uongozi Serikali, hata Unaibu Waziri, ukomavu wake haukutizamwa kutokana na umri wake au uzoefu wake kwenye siasa. Wakati Rais Obama anagombea alikuwa Mbunge kwa miaka mitatu tu na kulikuwa na maneno mengi pia kwamba hajakomaa. Lakini wananchi waliona anatosha. Mifano ipo mingi sana. Cha msingi ni kwamba wenye kuamua kiongozi awe nani ni Watanzania wenyewe – kwa msaada wa Mungu.

Jingine ninaloweza kusema ni kwamba hakuna kazi yoyote inayomuandaa au kumkomaza mtu kuwa Rais wa Tanzania. Kuna watu wanne tu hapa Tanzania ambao tunaweza kusema kuwa wana uzoefu wa Urais: Mwalimu Nyerere, Mzee Ali Hassan Mwinyi, Mzee Benjamin William Mkapa, na Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Kinachomfanya mtu awe tayari ni makuzi yake, maadili yake, busara yake, hekima zake, dira yake pamoja na vipaji na talanta na karama alizojaliwa na Mungu.


Kama nilivyosema, Watanzania wanataka kiongozi mahiri na sio mwanasiasa mkongwe. Wanataka kiongozi atakayefanya maamuzi, lakini atakayefanya maamuzi makini. Wanataka kiongozi mwadilifu.

Unaweza ukawa na umri wa miaka 40 na ukawa na ukomavu na hekima na busara na vipaji vya kufanya maamuzi makini – na unaweza ukawa ndani ya siasa kwa miaka 40 na ukafanya maamuzi ya papara. Ushahidi tunauona kila siku.

Umeuliza pia kuhusu Shirika la Maendeleo Bumbuli au BDC. Moja ya sababu zangu za kuingia kwenye siasa ni kuleta ubunifu katika kutatua kero za wananchi. Kwa mfumo wa utawala na maendeleo wa nchi yetu, Serikali bado ina mkono mkubwa kwenye kuleta maendeleo ya watu. Kwa kutambua kwamba mchango na jitihada za Serikali pekee hazitoshi kusukuma maendeleo kwa kasi ambayo mimi naipenda, niliamua kutengeneza utaratibu wa ziada wa kusukuma maendeleo ya watu wa Bumbuli. Kwanza, nilifanya utafiti wa

kina juu ya changamoto zilizopo na sababu zake, kisha tukafanya uchambuzi wa baadhi ya changamoto ambazo Serikali inaziweza na nyingine ambazo Serikali haina uwezo wa kuzitatua. Tukaanzisha Shirika la Maendeleo Bumbuli kwa ajili ya kusukuma shughuli za maendeleo kwa kasi zaidi. Falsafa yetu ni kuwezesha na kuvutia biashara zitakazoongeza chachu ya uwekezaji na mzunguko wa fedha jimboni, kutoa ushawishi, huduma, ushauri na msaada kwa watu wengine wanaotaka kuwekeza Bumbuli, na kutafuta na kuunganisha wabia wa maendeleo katika jimbo la Bumbuli, na kufanya shughuli nyingine za kijamii.

Shirika hili nililianzisha kwa mtaji wa fedha yangu ya mfukoni ambayo ilikuwa ni mkopo wa magari ya Wabunge. Tumefanikiwa sana kwenye mambo kadhaa lakini pia tumekabiliwa na changamoto nyingi, ikiwemo fedha za uendeshaji wa shughuli zetu. Kwa kiasi kikubwa bado natumia fedha zangu kusaidia shughuli za Shirika. Tulitegemea misaada kadhaa kutoka maeneo mbalimbali lakini imechelewa.



January Makamba akitangaza nia ya kugombea Ubunge wa Jimbo la Bumbuli.

Hata hivyo, nafarijika kwamba program tulizozianzisha zinaenda vizuri.

Program kubwa ni ile ya ukopeshaji, ambapo hadi sasa tumekopesha karibu shilingi milioni 250 kwa vikundi vya wajasiriamali Bumbuli, wengi wao wakiwa kina mama.



January Makamba akisaidiana kuandika hotuba na Rais Kikwete katika Mkutano wa Kimataifa wa Kanda za Kiuchumi uliofanyika Kampala 2008.

Kuna baadhi ya maeneo watu niliowaamini kuendesha shughuli za ukopeshaji wametuangusha na wamewaangusha wananchi kwa hiyo tunalazimika kurekebisha hali hiyo. Tuna mipango mingine mikubwa kwa mwaka wa 2015.

Kwa kuzingatia mazingira magumu ya hali ya hewa ya baridi kali, Shirika hili limeanzisha programu ya kugawa viatu vya shule kwa wanafunzi wote wa Shule za Msingi katika Jimbo la Bumbuli kila mwaka. Tumeanza mwaka huu kwa kugawa pea 45,000 na tutaendelea kufanya hivyo kila mwaka. Pia tumeanzisha programu za kuwaandaa wanafunzi wa kidato cha nne kufanya vyema katika mitihani yao ya taifa. Tunaendelea na jitihada za kwenye kiwanda cha kusindika mboga na matunda. Pia tunatoa ushauri na kushirikiana na Halmashauri ya Bumbuli kuiwezesha kupata mtaji wa shilingi bilioni 5 kwa ajili ya kuwekeza kwenye shughuli za maendeleo.

Umeuliza pia kuhusu mafanikio ambayo tumeyapata Wizarani hadi tuaminiwe kwa nafasi za juu. Labda niseme kwamba Wizarani haiendeshwii na mtu mmoja

au wawili. Kuna timu ya watendaji, wataalam na watumishi wa Wizara pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara. Na pia kuna wenzetu wengine ndani ya Serikali nzima ambao bila wao Wizara moja haiwezi kutimiza majukumu yake. Mara nyingi sijisikii vyema pale Wizara moja au Serikali inapotimiza majukumu yake, basi hujitokeza mtu mmoja kusema yeye kafanya – kwamba ni mafanikio yake. Mafanikio yote ya Serikali huwa ni mafanikio ya timu nzima inayoongozwa na Rais, ambaye ndio kiongozi wa Serikali.

Naamini pia ni muhimu kuondokana na hii dhana kwamba madaraka ya juu ni kama zawadi kwa mtu akitimiza majukumu yake aliyopewa. Hii habari ya kusema kwamba bwana fulani akiwa Waziri wa wizara fulani alitimiza wajibu wake kwa hiyo tumzawadie uongozi wa juu haina maana.

Wakati Mwalimu Nyerere anachaguliwa kuwa Rais wa TANU mwaka 1954, akiwa na miaka 32 tu, ili kuongoza harakati za kutafuta uhuru wa nchi yetu, kama kungekuwa na swali kwamba kwani kafanya nini hadi awe Rais wa TANU, kwamba kuna wanaostahili zaidi Urais wa TANU kwa sababu wamefanya makubwa zaidi hata kabla Mwalimu hajatia mguu Dar es Salaam, basi historia ya nchi yetu ingekuwa tofauti na ilivyo leo.

Hata hivyo, nikisema nikusimulie mafanikio ya Wizara yetu hapa tutakesha. Lakini niseme kwa kifupi tu kwamba Serikali ya Rais Kikwete, na nasisitiza hapa kwamba Serikali ya Rais Kikwete kwa sababu ndio kiongozi wetu, imepata mafanikio makubwa sana katika sekta ya mawasiliano. Ndio sekta inayoongoza kwa kukua kwa kasi na kwa muda mrefu – kwa kiwango cha wastani wa asilimia 20 katika kipindi cha miaka saba. Hakuna sekta yoyote ya uchumi iliyokuwa kwa kasi hiyo na kwa kipindi kirefu kama hicho. Kwamba sasa hivi karibu kila mtu ana simu ya mkononi na anaweza kumudu kuitumia sio jambo lililotokea lenyewe tu kwa ajali – ni matokeo ya uamuzi wa Serikali, ni matokeo ya Sera za Serikali, ni matokeo ya Sheria na Kanuni tulizozindika Serikalini. Maisha ya Watanzania yamebadilika kwa kiwango kikubwa sana kutokana na sera muafaka tulizoweka, zilizowezesha uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya mawasiliano ikiwemo kwenye mitandao ya simu za mikononi. Huduma ya fedha, kutuma na kupokea fedha, sasa inapatikana kwa Watanzania karibu wote – hata wale wasio na akaunti za Benki. Biashara za aina zote zimeshamirishwa kutokana na urahisi wa mawasiliano – jambo lililowezeshwa na uwekezaji wa Serikali kwenye kujenga mkongo wa mawasiliano wa taifa.

Kumekuwepo na mashaka kwamba Serikali haipati mapato stahiki kutoka kwenye makampuni ya simu. Suala la usimamizi wa kodi na mapato ni suala

la Wizara ya Fedha sio la Wizara za kisekta. Hata hivyo, mwezi Oktoba 2013, tumefunga mtambo wa kisasa wa kufuatilia mapato ya makampuni ya simu na sasa mapato ya Serikali yameongezeka kwa kiwango kikubwa. Pia, kutokana na usimamizi mzuri wa sekta hii, ajira zimeongezeka sana – kwanza kwenye makampuni yenyewe lakini pia kwa Watanzania wengi hasa kina mama walioingia kwenye biashara za kuuza vocha na huduma za kuhamisha fedha. Karibu katika kila kona ya nchi yetu wapo watu wanaofanya biashara hizi – na hizi ni ajira nyingi sana zinazowasaidia Watanzania wa kawaida.

Tumejenga Chuo Kikuu kikubwa cha Sayansi na Teknolojia na chenye hadhi ya kimataifa pale Arusha ambacho kinafundisha wanasayansi na watafiti wa



January Makamba akipokelewa mara baada ya kuwasili katika moja ya kampeni za uchaguzi za CCM.

ubora wa juu, waliojikita katika kutumia elimu ya sayansi kutafuta majawabu ya matatizo ya msingi ya Watanzania. Kuanzia mwakani tutakuwa tunatoa wahitimu watafiti wa sayansi, yaani PhDs, 500 kila mwaka na tutaendelea kuongeza. Tumeinua hadhi ya Chuo cha Ufundi Mbeya na sasa ni Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia. Tume ya Sayansi na Teknolojia iliyo chini ya Wizara yetu nayo inafanya kazi nzuri ya kutoa chachu kwenye tasnia za utafiti na uvumbuzi. Hata hivyo, msingi wa maendeleo ya sayansi na teknolojia unaanzia kwenye elimu ya sayansi na hesabu kwenye shule za Sekondari. Na sote tunafahamu kwamba kuna changamoto kubwa kwenye eneo hili. Ndio maana nilisema hapo awali kwamba ili Wizara moja ifanikiwe lazima Serikali nzima ifanye vizuri.



Bado changamoto zipo nyingi ikiwemo ubora wa huduma za mawasiliano, gharama za kupiga simu na kukosekana kwa huduma za mawasiliano vijijini, fedha chache zinazopangwa kwa ajili ya utafiti na kadhalika. Serikali imejipanga vizuri na iko mikakati madhubuti ya kukabiliana na changamoto hizi. Labda moja ya tatizo kwenye Wizara yetu ni kwamba tunafanya kazi kimya kimya.

Kuhusu jimbo, kama nakumbuka nadhani umeuliza iwapo kama mtu jimbo lake bado lina changamoto za maendeleo, kwanini apewe nafasi ya uongozi wa nchi. Kwanza niseme kwamba hakuna jimbo hata moja hapa nchini ambalo halina changamoto – iwe maji, umeme, afya, barabara, au ajira. Hakuna mtu hata mmoja anayeweza kujitokeza na kusema kwamba kamaliza changamoto jimboni kwake na kwa hiyo huo ndio msingi wa kuchaguliwa kwa nafasi ya juu.

Rais wetu mstaafu, Mzee Mkapa, na Rais wetu wa sasa, Mheshimiwa Kikwete, walikuwa Wabunge. Walifanya kazi nzuri sana kwenye majimbo yao lakini hawakumaliza changamoto na hadi leo Masasi na Chalinze kuna changamoto. Tunesema mwaka 1995 kwamba Mheshimiwa Mkapa hafai kuwa Rais kwa sababu Masasi au Nanyumbu kuna wanafunzi wanafeli au kuna barabara hazipitiki, basi nchi yetu ingekosa kiongozi mzuri. Tunesema mwaka 2005, kwamba Mheshimiwa Kikwete hafai kuwa Rais kwa sababu kuna watu katika baadhi ya maeneo ya Chalinze hawana maji au kuna shule watoto wanakaa chini, basi tungekosa Rais mzuri ambaye anaifanyia nchi yetu kazi kubwa. Kwa hiyo hii habari ya kusema huyu bwana au yule bwana hafai uongozi wa nchi kwa sababu mvua ikinyesha jimboni kwake kuna barabara moja magari yanakwama mara nyingi inakuwa ni siasa tu.

Kama ambavyo Rais Mkapa na Rais Kikwete, licha ya kutomaliza changamoto za majimbo waliyoyaongoza, waliweka misingi ya maendeleo tunayoyaona katika majimbo hayo leo, na mimi nimejitahidi kuweka misingi imara kwa ajili ya maendeleo katika jimbo letu. Shirika la Maendeleo la Bumbuli litaendelea kubaki milele na kuwasaidia wananchi. Lakini pia, baada ya miaka mingi ya kunyimwa Halmashauri mpya, binafsi nililisukuma kwa nguvu kubwa na kuhakikisha kwamba tunapata Halmashauri. Sasa hivi kila mwaka tunapata pesa mpya za maendeleo shilingi bilioni 18 ambazo huko nyuma hazijawahi kuwepo. Mji wa Bumbuli umechangamka, mzunguko wa pesa ni mkubwa sasa. Pia, wananchi, hasa wakulima wa chai, sasa wameondokana na dhuluma iliyokuwa inafanywa kwenye zao la chai na sasa tumepata ukombozi baada ya kupata maumivu ya muda mrefu.

7

Ni changamoto gani kubwa zinawakabili vijana wa Tanzania? Wanasiasa wengi wamekuwa wakisema watamaliza tatizo la ajira nchini. Kuna mawazo gani mapya kutoka kwa viongozi wa kizazi kipya ya kumaliza tatizo hili?

Vijana kwa sasa ni kundi kubwa sana katika jamii ya Watanzania. Asilimia 78 ya Watanzania wana umri chini ya miaka 35. Ukiangalia matokeo ya sensa ya watu ya mwaka 2012, utaona kwamba Watanzania walio chini ya miaka 35 ni wengi kuliko idadi ya Watanzania wote waliokuwepo miaka kumi tu iliyopita, yaani 2002. Hili ni kundi muhimu ambalo ustawi wake ndio utakaomua ustawi wa taifa letu. Vijana wana mahitaji matatu: kwanza, wapate elimu iliyo bora, elimu inayoendana na mahitaji ya sasa na yajayo ya uchumi na jamii, na wawezeshwe kumudu kuilipia elimu hiyo bora na elimu hiyo iwasaidie katika kujitambua, kujenga maisha yao na kutoa mchango kwa taifa; pili, vijana wanahitaji fursa za kupata kipato – kwa maana ya nafasi za kuajiriwa na fursa za mikopo na uwezeshaji wa kujiajiri na kufanya biashara zenye tija ili waweze kujenga maisha yao yawe bora; na tatu, vijana wanahitaji wawe na sauti na kauli katika maamuzi yanayohusu mustakabali wa nchi yao. Haya mahitaji mawili ya kwanza nimekwishayaelezea kwa namna moja au nyingine hapo awali.

Sasa nizungumzie suala la ajira na ufumbuzi wake. Lakini kabla ya hapo naomba niseme kwamba kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya ajira na upatikanaji na ubora wa elimu. Kati ya vijana 900,000 wa miaka kati ya 15-24 walioingia kwenye soko la ajira mwaka 2011, asilimia 14 hawakumaliza shule ya msingi, asilimia 44 walimaliza shule ya msingi lakini hawakuenda Sekondari; asilimia 38 walienda Sekondari lakini wakaishia katikati, hawakumaliza kidato cha nne; na asilimia 4 tu ndio walioenda zaidi ya kidato cha sita. Hapa kuna changamoto kubwa, kwa maana kwamba asilimia zaidi ya 90 ya vijana wanaoingia kwenye soko la ajira wanakuwa hawajawezeshwa kwa nyenzo kuu – yaani elimu – ya kupata na kumudu ajira bora au kujiajiri kwa ufanisi.

Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba elimu bora ni sehemu kubwa ya jawabu la ajira hapa nchini.



January Makamba akiwa amezungukwa na vijana wa Bodaboda akiwasikiliza shida zao.

Tatizo la ajira lipo kwa vijana wa mijini na vijijini, vijana waliopata bahati ya kupata elimu ya juu na hata ambao wameishia la saba au kidato cha nne. Ukiwa umesoma, ajira tatizo, ukiwa haujasoma ajira pia tatizo.

Kwa mujibu wa takwimu za Serikali, inakadiriwa kwamba wapo Watanzania milioni 23 kwenye soko la ajira – kwa maana ya watu wenye umri na uwezo wa kufanya kazi. Hawa ni watu wengi sana. Na kila mwaka wanaingia vijana 900,000 kwenye soko la ajira. Hawa ni wengi sana.

Moja ya sera za msingi za CCM ni kuwawezesha wananchi kiuchumi ili waweze kumiliki na kuendesha uchumi wa nchi yao na waweze kunufaika na uchumi unaokua. Katika kufanya hivyo, lazima wawe na maarifa ya kisasa kwa kuwa tupo kwenye mazingira ya uchumi wa kisasa.

Yapo mambo ambayo Serikali imekuwa inafanya kumaliza tatizo la ajira. Mimi nitajaribu kuongelea mambo mapya ya kuongezea zaidi ya yale tunayofanya sasa.

Kwanza kabisa, ni muhimu kubadilisha mtazamo na kuondokana na dhana ya ajira au dhana ya kuajiriwa. Tuchukue dhana mpya ya kipato. Kimsingi watu hawatafuti ajira bali wanatafuta kipato cha kujiendeleza

kimaisha. Kuajiriwa ni moja tu ya njia ya kutafuta kipato. Tukiwa na dhana ya kipato itaweza kutusaidia kupanua wigo wa mawazo na fikra kuhusu mambo tunayoweza kuyafanya.

Sasa, nini tufanye kumaliza hili tatizo?

Kwanza, kupatikana kwa fursa za vipato kwa wananchi kuna uhusiano wa moja kwa moja na kunawiri kwa uchumi wa taifa, kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji mali na uwekezaji wa sekta binafsi katika shughuli zinahusisha watu wengi, uwekezaji wa Serikali kwenye miradi mikubwa, na kuwepo kwa mazingira rahisi na mazuri ya kuanzisha na kufanya biashara. Kwa hiyo haya mambo lazima tuyafanye kwa uthabiti na kwa dhamira ya dhati kabisa.

Pili, Serikali imekuwa na mipango mizuri ya kuwezesha yote haya lakini kumekuwa na nidhamu ndogo katika utekelezaji na ufuatiliaji. Tatizo la kipato kwa wananchi linahitaji mkakati mahsusi, mkakati mkubwa na wa haraka – mkakati ambao utaweka nidhamu na wajibu wa kisheria kwa wahusika kuutekeleza.

Suala la ajira linahitaji msukumo na hatua za kimapinduzi, na sio maneno tu ya kurudia kauli kwamba ni bomu bila kutoa ufumbuzi.

Pamoja na hatua hizi nilizozitaja awali napendekeza hatua nyingine mahsusi za kumaliza tatizo la ajira na kuweka chachu mpya ya ukuaji wa uchumi:

Bunge lipitishe Muswada Maalum, Muswada wa Matumizi kwa Uwezeshaji Kiuchumi kwa Vijana, ambao utakuwa ni sheria maalum ya matumizi ya shilingi trilioni 3.6 kwa ajili ya mkakati wa miaka mitatu wa kupanua ajira kwa kuchochea shughuli za uzalishaji mali na uchumi au Jobs Bill kwa lugha nyingine.

Mwaka 2009, ulipotokea mdororo wa uchumi na wanunuzi wa pamba kukaribia kufilisika Rais Kikwete alionyesha ujasiri na kupeleka Bungeni Mpango Mahsusi wa kiasi cha shilingi trilioni 1.7 kuokoa zao la pamba na mabenki yaliyowakopesha wanunuzi wa pamba. Sasa ni wakati wa kutengeneza Muswada na Mpango Mahsusi na wa hatua kubwa zaidi ya ile ya 2009 kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la ajira.

Kwa kifupi, Muswada huu, utatenga fedha na kuweka utaratibu kwa maeneo muhimu yafuatayo:

Kwanza, kuwezesha kujengwa na kufufuliwa kwa viwanda 11 vya nguo nchini. Huko nyuma tulishawahi kuwa na viwanda vingi vya nguo. Sasa hivi havizidi vitano. Sekta ndogo ya viwanda vya nguo ndio inayoajiri watu wengi zaidi lakini pia ndio itakayotoa soko la uhakika la zao la pamba. Kwa sasa, ni asilimia 30 tu ya pamba yetu ndio inayotumika nchini. Fedha hizi zitatumika kama dhamana kwa makampuni binafsi hapa nchini kukopa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vipya 11. Hatua nyingine ya kuchukua hapa ni hatua ya kikodi na kiushuru ili kuwezesha viwanda hivi kukabiliana na ushindani wa kanga, vitenge, mitumba na vitambaa vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi.

Sera za kukuza viwanda vilivyo na uwezo wa kuajiri watu wengi – kama vya nguo- na vyenye kuzalisha bidhaa za matumizi ya wengi ndani ya nchi na zile za kuuza nje zitawekewa kipaumbele.

Pili, fedha hizi zitatumika kama mkopo na dhamana ya mkopo kwa yoyote anayetaka kuanzisha kiwanda au viwanda vya kusindika au kuongeza thamani ya mazao ya kilimo – ikiwemo zao la korosho ambalo ubanguaji wake unaajiri watu wengi.

Mtu yoyote atakayeamua kuanzisha kiwanda cha kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, kitakachoajiri watu kuanzia kumi, hasa maeneo ya vijijini, atapendelewa na Serikali na kusaidiwa kuharakisha uwekezaji huo na atapewa nafuu ya kodi.



January Makamba, akiwa na Meneja wa Kampuni ya Kilombero Valley Teak Company, Ndugu Hans Lemm, alipotembelea kiwanda cha kuongeza thamani ya mbao zinazozalishwa na mti wa mtiki.

Tatu, shughuli za ujenzi wa nyumba zinaajiri watu wengi. Kwa hiyo sehemu ya fedha hizi zitatumika kuwezesha uanzishwaji wa makampuni madogo na ya kati ya ujenzi wa nyumba lakini pia kuanzisha miradi mingi na mikubwa ya ujenzi wa nyumba bora za makazi na biashara kwa maeneo ya mijini na vijijini. Tuna mahitaji makubwa ya nyumba na tuna mahitaji makubwa ya ajira. Tukijenga nyumba nyingi kila siku kama wendawazimu tutamaliza matatizo mawili kwa mpigo. Sambamba na hili, ujenzi wa viwanda vya vifaa ya ujenzi, kama vile viwanda vya nondo, mabati, simenti, vigae, vioo, ili kupunguza gharama za ujenzi wa nyumba pia ni muhimu.

Lakini sote tunajua kwamba ujenzi wa miundombinu mikubwa, hasa ya usafirishaji ni njia mojawapo ya kuongeza chachu katika uchumi na kuongeza ajira. Kwa hiyo jitihada za makusudi ni muhimu ziwepo kuongeza kasi na ukubwa wa miradi ya miundombinu nchini ambayo itaajiri vijana wengi zaidi na kuingiza fedha nyingi zaidi kwenye mzunguko wa uchumi, hasa pale tutakapohakikisha kwamba wajenzi wa miradi hii ni makampuni ya ndani yatakapohifadhi na kuwekeza fedha hizo hapa ndani.

Nne, kwa kushirikiana na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Muswada huu utaanzisha mfuko mkubwa kwa ajili ya kutoa dhamana na mikopo kwa wajasiriamali wadogo kwa masharti nafuu kuliko mabenki au mifuko mingineyo iliyopo hapa nchini.

Wajasiriamali watakaopewa upendeleo ni wale wanaofanya shughuli za uzalishaji mali hasa kilimo, uvuvi, mifugo na shughuli za biashara zinazotoa ajira kwa watu wengine. Mfuko huu utaendeshwa kwa uwazi na weledi mkubwa, ikiwemo njia ya kutoa mtaji kwa kuchukua hisa kwenye baadhi ya biashara hizi za kati na baadaye kuzirudisha hisa hizo kwa masharti nafuu pale biashara hizi zinapokuwa zimeinuka. Lengo ni kurahisisha na kuharakisha upatikanaji wa mitaji.

Tano, Muswada huu utaweka sharti kwamba asilimia si chini ya 30 ya thamani ya manunuzi Serikalini na kwenye taasisi za umma yatatengewa kwa ajili ya makampuni yanayomilikiwa na vijana wasiozidi umri wa miaka 40 na wanawake – ili mradi makampuni hayo yawe na uhai usiopungua miaka miwili na yawe yameajiri pia watu wengine.

Sita, Muswada huu utarasimisha shughuli za sanaa – ikiwemo sinema, muziki na kazi zote za ubunifu– na kutenga fedha kwa ajili ya maendeleo ya tasnia hii, ikiwemo kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa wazalishaji, waendeshaji

na wasanii wenyewe kwenye kuendeleza ubunifu na kuzalisha, kutangaza na kuuza kazi mpya kwa njia za kisasa.

Saba, kwa wale wanaohitaji kuajiriwa, tutaweka vituo vya kutoa mafunzo ya namna ya kuomba na kufanya usaili wa kazi – lakini pia tunaweza kutumia Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, yaani FDCs, kama vituo vya kupata na kujenga maarifa mapya kwa muda mfupi kuhusu mbinu na ushauri wa kukabiliana na soko la ajira na fursa zilizopo za kujiajiri.

Nane, kwa biashara kubwa na viwanda vilivyopo sasa, Muswada utaweka motisha kwa yoyote ambaye ataweza kuongeza ajira mpya 50 au zaidi kwa mwaka, sio vibarua wa muda mfupi bali ajira kamili, kwa kupunguziwa kodi za mishahara, yaani payroll taxes; na kwa waajiri ambao ni kampuni mpya ndogo, yaani SMEs, motisha wa kupunguziwa kodi hizi kwa kila kazi mpya tano au zaidi kwa mwaka.

Ukweli hapa ni kwamba kunawiri kwa uchumi hakutokani na kodi inayokusanywa na Serikali bali kunatokana na kipato na uwezo wa manunuzi walionao wananchi na kipato cha wafanyabiashara kuweza kukuza biashara zao na kutoa ajira nyingi zaidi.

Tisa, Muswada utatenga fedha za kuweka mazingira ya ujenzi wa vyuo vya ufundi, kwa kushirikiana na sekta binafsi, kwenye kila wilaya hapa nchini ili wanafunzi ambao hawajapata fursa ya kuendelea na kidato cha kwanza au kidato cha sita au vyuo vya ualimu wapate mafunzo mbalimbali mahsusi ya ufundi stadi na taaluma zinazohitajika kwenye soko la ajira na kwenye uchumi kwa ujumla. Takwimu zinaonyesha kwamba asilimia kubwa ya wahitimu wa vyuo vya ufundi hujiajiri.

Tutakapokuwa na Chuo cha Ufundi kikubwa na chenye hadhi katika kila Wilaya tutatengeneza kundi kubwa la vijana ambao watakuwa na maarifa na stadi za kutengeneza maisha yao na watakuwa tayari kujiajiri.

Na utaratibu unaweza kuwekwa kwamba yoyote atakayemaliza Chuo cha Ufundi, kama alisomea ufundi-seremala basi siku ya mahafali anakabidhiwa vifaa vya kuanzia kazi, au mkopo au vocha ya kumuwezesha kununua vifaa hivyo. Uwezo wa kufanya hivi tunao.

Kumi, Muswada huu utatenga fedha kwa ajili ya kuweka katika kila wilaya vituo vya mafunzo ya maarifa mapya katika shughuli zinazoajiri watu wengi – kilimo,

uvuvi na ufugaji – na maarifa ya uendeshaaji biashara ili vijana wanaofanya shughuli hizi waweze kuzifanya kwa tija na wapate manufaa. Kwa kuanzia, tunaweza kuanza kwa kutumia vyuo vilivyopo vya Maendeleo ya Jamii (FDCs) ambavyo havitumiki kama inavyopaswa.

Kumi na moja, Muswada huu utaweka kanuni zitakazoainisha kiwango cha chini cha thamani ya manunuzi yanayofanywa na wawekezaji wakubwa, hasa katika sekta za mawasiliano, madini na mafuta na gesi, kufanywa hapa nchini na kutoka kwa makampuni ya hapa nchini.

Kumi na mbili, Muswada utanzisha Mamlaka ya Ujasiriamali Mdogo na wa Kati (*Small and Medium Enterprises Authority*). Mamlaka hii kubwa, ambayo itaanzishwa kisheria, itachukua na kuunganisha baadhi ya majukumu ya Baraza la Uwezeshaji la Taifa na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO) na itakuwa na jukumu la kusimamia na kuratibu maendeleo ya kampuni changa na biashara ndogo nchini. Kote duniani, biashara za kampuni ndogo na za kati ndio injini ya uchumi wa nchi. Hapa kwetu asilimia karibu 90 ya biashara zote nchini ni biashara ndogo na za kati, ambazo zinaajiri watu wasiozidi wawili. Wajasiriamali Wadogo na wa Kati wana changamoto mahsusi, zikiwemo za masuala ya kodi, urasimishaji, masuala ya vibali, leseni, mitaji, elimu ya biashara, na uelewa wa fursa zilizopo. Changamoto hizi zikitatuliwa basi mchango wa biashara hizi kwa uchumi na utatuzi wa ajira utakuwa mkubwa. Kwa mujibu wa takwimu za Benki ya Dunia, asilimia 20 tu ya biashara na kampuni ndogo zikiongeza mfanyakazi mmoja kwa mwaka, ajira 400,000 zitazalishwa. Je asilimia 80 za biashara hizi zikiongeza watu watatu kwa mwaka? Tutakuwa tumemaliza tatizo la ajira. Lakini, ili hili litokee, lazima tuwe na taasisi madhubuti kama hii Mamlaka ninayopendekeza, ambayo itashughulika na ustawi wa biashara na makampuni madogo na ya kati.

Katika kusaidia biashara na makampuni madogo na ya kati, Mamlaka ya Ujasiriamali Mdogo na wa Kati inaweza kupewa majukumu yafuatayo: kwanza, kusimamia utekelezaji wa sharti jipya la kisheria la asilimia 30 ya manunuzi ya Serikali yapewe kwa kampuni ndogo na za kati zinazomilikiwa na vijana na wanawake wenye uwezo; pili, kuyajengea uwezo wa weledi wa kibiashara makampuni madogo na ya kati kuwania zabuni; tatu, kusimamia uharakishaji wa malipo kutoka Serikalini kwa wazabuni wadogo na wa kati ambao biashara zao hudhoofika na hata kampuni kufa pale Serikali inapochelewa kuwalipa; na, nne, kujenga uwezo wa makampuni na biashara ndogo na za kati kumudu na kuweza kutumia nyenzo za kisasa za biashara ikiwemo mifumo ya kisasa ya mahesabu.

Mwisho, sheria hii itaweka taasisi na mifumo madhubuti ya kuhakikisha kwamba malengo ya fedha hizi yanatimia na kila mtu anatimiza wajibu wake.

Labda nimalizie kwa kusema kwamba katika haya niliyoyasema kuna ambayo yanafanyika kwa kiasi fulani. Msingi wa mapendekezo yangu ni kwamba, kwanza: sasa tuyafanye kwa msukumo mkubwa zaidi na utaratibu wa dharura; pili, tuweke rasilimali-fedha za kutosha kwa ajili ya kufanya kuliko kuwa na mipango mizuri bila kuwa na fedha; tatu, badala ya kuwa na mipango na mikakati tu, basi kuweka sheria itakayolazimisha na kuweka wajibu wa kutekeleza mipango na mikakati hii. Lakini mwisho, kuunganisha yale mazuri ya sasa na haya mapya ili kuwa na mwendelezo utakaowezesha utekelezaji wa haraka bila kufumua kila kitu. Tukifanya haya yote kwa nidhamu kubwa, tutawakomboa watu wengi katika maisha ya mashaka kuhusu kipato na ustawi wao.



January Makamba akisalimiana na wanafunzi wa Sekondari ya Mtakatifu Agnes inayomilikiwa na Kanisa Katoliki Jimbo la Mahenge.

8

Kuna wazo kwamba nchi tukiigawa katika majimbo ya kiutawala, itapiga hatua za kimaendeleo kwa haraka. Kuna siku nilikusikia ukipinga wazo hili na ukasema kwamba badala ya majimbo ya kiutawala tuigawe nchi kwenye majimbo ya kiuchumi. Je, unaweza kufafanua fikra hizi?

Ni kweli nilisema hivyo. Naamini kwamba kwa muda mrefu sasa tumekuwa tukitazama mgawanyo wa maeneo ya nchi yetu katika misingi ya kiutawala au kiuongozi zaidi kuliko kiuchumi.

Nimekwishasikia huko nyuma hata baadhi ya viongozi wanaotafuta uongozi wakizungumza kwa misingi ya ukanda.

Kiongozi makini ni yule anayetoa fikra za kuangalia fursa za kiuchumi zilizopo katika kanda au mkoa au wilaya na kutengeneza fikra za namna ya kuzitumia fursa hizo kuwainua watu kiuchumi.

Kwa hiyo wazo langu ni kuziangalia kanda za nchi yetu na kuzifanya kanda za kiuchumi kwa kuangalia fursa mahsusi za kiuchumi katika kanda hizi na kutoa msukumo mahsusi kwa shughuli mahsusi za kiuchumi. Msingi wa wazo hili ni kutawanya uchumi na manufaa ya uchumi katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, sio kila kitu ni Dar es Salaam peke yake.

Mfumo wa uchumi wa kikoloni ulitazama nchi yetu kama eneo la uzalishaji mali, kama vile shamba tu la Malkia. Wakoloni hawakujali maendeleo ya watu wetu. Ndio maana kuna baadhi ya maeneo ya nchi yetu yalitengwa tu kwa ajili ya kutoa manamba kwenye mashamba, na kuna baadhi ya maeneo yalitoa askari tu katika jeshi la mkoloni. Miundombinu yote iliyojengwa na mkoloni ilikuwa ni kwaajili ya kusafirisha bidhaa ghafi kuja bandarini kwa ajili ya kusafirishwa nje ya nchi.

Pamoja na kwamba nchi yetu imejitawala sasa na kuna maendeleo, bado mfumo huu wa uchumi wa kikoloni haujabadilika sana. Dar es Salaam inachangia asilimia 18 ya Pato la Taifa na asilimia karibu 60 ya mapato ya Serikali ingawa shughuli za uzalishaji mali zinafanyika nchi nzima. Wazo langu ni kwamba lazima tuufumue mfumo huu wa kikoloni ili tujenge uchumi wa kisasa wenye nguvu katika mikoa yetu. Wazo langu ni kwamba tuigawe nchi yetu katika kanda sita za kiuchumi zitakazotoa msukumo mahsusi kwa shughuli mahsusi za kiuchumi.



January Makamba akitoa hoja bungeni.

Tuanze na kanda ya Ziwa yenye mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Kagera, Geita na Mara. Mikoa hii ina rasilimali nyingi, idadi kubwa ya watu, ina dhahabu, ina almasi, ina pamba, ina mifugo mingi, ina vivutio vingi vya utalii, ina ardhi kubwa yenye rutuba, na ina ziwa kubwa linalopakana na nchi mbili. Rasilimali zote hizi zinaweza kutumika kuwainua wananachi wake kiuchumi na kuchangia katika pato la taifa, endapo tutajipanga kimkamkati. Ninazo fikra za kuwezesha kanda hii kuwa na nguvu kubwa ya kiuchumi. Kwa mfano Mwanza ni jiji pekee katika ukanda huu wa Afrika ambapo, ukisafiri, unaweza kufika katika nchi tano ndani ya dakika 90 – yaani Uganda, Kenya, Rwanda, Burundi

na Kongo. Kwa mantiki hii kanda hii inaweza kuwa kitovu kikubwa cha biashara na uwekezaji katika Afrika Mashariki na Kati. Kufanya fikra hizi zifanikiwe ni muhimu kuweka msukumo mkubwa katika sekta ya uchukuzi. Kwa hiyo hakuna budi kuimarisha reli na bandari kadhaa za Ziwa Victoria, kama vile ya Bukoba, Ukerewe, Musoma na Mwanza. Lakini muhimu zaidi kukifanya kiwanja cha ndege cha Mwanza kuwa kiwanja kikubwa na cha kisasa. Tukifanikiwa kuifanya Kanda ya Ziwa kuwa kituo kikubwa cha uchukuzi, yaani *logistics hub*, biashara kubwa za kufungasha mizigo mikubwa, au kwa lugha nyingine *break-bulk* na consolidation, kwa watu wa nchi jirani zinaweza kufanyika Mwanza. Zaidi ya kurahisisha biashara kati ya eneo hili la maziwa makuu na dunia, mfumo huu pia utatoa fursa za ajira na kipato kwa watu wengi wa kanda hii.

Msukumo mwingine wa kiuchumi kwenye Kanda ya Ziwa utakuwa ni wa viwanda vya aina mbalimbali. Kwanza, viwanda vya nguo – kwa sababu asilimia 80 ya pamba inayolimwa Tanzania inalimwa kanda ya ziwa.

Viwanda vya nguo ndio vinavyoongoza kwa kutoa ajira ya viwandani. Kwa sasa asilimia 70 ya pamba yetu inauzwa nje ikiwa ghafi. Tukijenga viwanda sita hadi nane vikubwa vya nguo kwenye eneo hili tutakuwa tumefanya jambo kubwa sana. Pili, viwanda vya kusindika nyama na ngozi na viwanda vya kutengeneza bidhaa za ngozi. Sehemu kubwa ya ng'ombe wa Tanzania wanafugwa katika Kanda ya Ziwa, lakini hakuna kiwanda cha kusindika nyama wala kiwanda cha kutengeneza bidhaa za ngozi. Tukijenga viwanda hivi basi wafugaji wanaweza kupata mafanikio makubwa kutoka katika mifugo yao.

Aina ya nne ya viwanda ni vile vya kuchakata madini, hasa dhahabu na almasi. Kanda ya ziwa ina madini na migodi mikubwa lakini pia lina wachimbaji wadogo wengi. Kiwango cha dhahabu kilichopo kinaruhusu kabisa ujenzi wa kiwanda cha ufuaji wa dhahabu kanda ya ziwa. Hakuna sababu kabisa ya kusafirisha udongo nje ya nchi. Lakini pia wachimbaji wadogo wanapata bei ndogo ya dhahabu na madini yao kwa sababu hakuna pahala wanapoweza kwenda kuuza moja moja zaidi ya kwa wanunuzi wa kati ambao wananufaika zaidi na wanatorosha dhahabu nje bila kulipiwa kodi. Pia napendekeza kuanzisha kituo kikubwa cha biashara ya dhahabu kwenye mji kama Kahama ili kuwezesha wachimbaji wadogo kupata bei nzuri ya dhahabu na kuliko hivi sasa.

Huwezi kuongelea kanda ya ziwa bila kuongelea uvuvi kwa sababu wananchi wengi katika kanda hii wanategemea shughuli za uvuvi katika maisha yao. Katika miaka ya hivi karibuni, biashara ya uvuvi imezorota kutokana na viwanda vingi vilivyokuwa vinatoa soko kwa wavuvi na ajira kwa wakazi wa kanda

ya ziwa vimefungwa au vimepunguza uzalishaji. Na lazima kuweka mikakati madhubuti ya kurudisha uhai katika shughuli za uvuvi. Tutaifanyaje? Kwanza, tutahakikisha kwamba wavuvi wadogo na wakati wanawezeshwa ili kupata mikopo na zana kama vile injini, nyavu, maboti na majokofu ili waweze kwenda mbali zaidi ziwani na kupata samaki walio wengi zaidi. Pili, kuna haja ya kuweka mazingira ya uvuvi endelevu ili kuhakikisha uhakika wa upatikanaji wa samaki wakati wote. Mwisho, tutahakikisha wenye viwanda vitakavyonunua samaki wanasaidiwa kukabiliana na ushindani, lakini pia wanawajibishwa kuwalipa malipo stahiki wavuvi wanaowauzia samaki.

Mwisho ni biashara ya utalii. Kanda ya Ziwa ina vivutio vingi vya utalii, lakini bado hakuna hoteli hata moja ya Kimataifa ya nyota tano ambapo unaweza kuwaleta Marais kadhaa au kufanya mkutano mkubwa wa Kimataifa. Hili linaweza kubadilishwa kwa haraka. Kwenda Serengeti kutokea Arusha ni saa nne. Kwenda Serengeti kutoka Mwanza ni mwendo wa saa moja. Lakini cha ajabu watalii wote wanaotaka kwenda Serengeti wanapitia Arusha. Kwa hiyo, jiji la Arusha limechangamka huku vijana wengi wakiwa na makampuni na biashara za utalii. Mwanza pia inaweza kuwa hivyo hivyo.

Moja ya nyenzo ya kuifanya kanda ya ziwa kuwa kanda ya kiuchumi ni kuwa na nishati ya uhakika. Katika kufanikisha hili napendekeza kwanza tujenge bomba la mafuta na bomba la gesi kutoka Dar es salaam hadi kanda ya ziwa. Hili litahakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa wananchi wa mikoa hii na kuchochea shughuli za uchumi.

Kwa kuzitaja shughuli hizi, sina maana shughuli nyingine za kiuchumi kwenye kanda hii haziwezi kufanyika. Hapana. Zinaweza kufanyika. Hapa nimesema tu ni kuweka vipaumbele na kutoa msukumo kulingana na mazingira mahsusi ya kanda na fursa zilizopo. Nimeingalia Kanda ya Ziwa kimkakati wa kiuchumi.

Kanda nyingine ni Kanda ya Kusini yenye mikoa ya Mtwara, na Lindi. Kwa miaka mingi mikoa hii imeonekana kama imesahauliwa kimaendeleo ingawa inazo fursa nyingi za kiuchumi zinazoweza kutumika kuinua kipato cha watu wake. Kutokana na historia ya mikoa hii Serikali ina wajibu kufanya juhudi za maksudi za kuhakikisha maendeleo ya mikoa hii inapatikana. Mwanga mpya umepatikana kutokana na uvumbuzi wa gesi ambayo inapaswa kuwanufaisha wananchi wa mikoa hii na taifa kwa ujumla.

Huwezi kuongelea maendeleo ya mikoa ya kanda ya kusini bila kuzungumzia kilimo cha korosho. Kwa miaka mingi wakulima wa korosho wamekuwa

wakilalamika kutokana na kutopata bei nzuri ya korosho. Vile vile, viwanda vya kubangua korosho vingi vimekufa na kubaki maghala. Lazima tufufue na kuimarisha kilimo cha korosho. Soko la zao la korosho litahakikishwa kwa kuwepo viwanda vya kubangua korosho. Kwa sasa, asilimia 85 ya korosho tunayouza nje ya nchi haijasindikwa. Tunaowauzia wanatushangaa kwa sababu usindikaji wa korosho hauhitaji miujiza. Tukifufua viwanda hivi kwa wingi tutaongeza ajira, kwa kina mama na vijana, lakini pia pato la wakulima litaongezeka. Hili linahitaji uamuzi madhubuti na mkono mzito wa Serikali kwa sababu wapo wenye maslahi makubwa ya kutokuwepo kwa viwanda hivi.

Msukumo katika kanda hii ya uchumi ni katika viwanda – ambavyo kwa kweli ndio mkombozi wa ajira. Hapa tunaongelea viwanda vya aina mbili.

Aina ya kwanza ni viwanda vya saruji. Tayari kuna kiwanda kikubwa cha saruji kinajengwa Mtwara. Kingine kinatarajiwa kujengwa Lindi. Bado vinahitajika viwanda vingine kadhaa vya saruji kwa sababu kwa sasa Tanzania ni moja ya nchi zinazoongoza duniani kwa bei kubwa na kwa matumizi madogo ya saruji ilhali shughuli za ujenzi zimechachamaa kila kona ya nchi na mahitaji yakiwa bado ni makubwa sana. Bahati nzuri malighafi ya saruji imejaa katika mikoa hiyo. Bahati nzuri gesi ya kutosha kuzalisha umeme wa kutosha kwa ajili ya viwanda hivyo ipo.



Ndugu January Makamba akifurahia jambo na Waziri Mkuu Ndugu Mizengo Pinda na Mbunge wa Singida Mjini Ndugu Mohammed Dewji baada ya kikao cha Bunge Dodoma.

Aina nyingine ya viwanda katika kanda hii ni viwanda vya mazao ya gesi, yaani *petrochemicals*, kama vile viwanda vya mbolea na bidhaa za plastiki. Kuna mahitaji makubwa sana ya mbolea nchini. Tunaagiza mbolea kutoka nje ya nchi kwa gharama kubwa. Wakulima wetu wengi hawana uwezo wa kununua mbolea hiyo na hivyo tija na uzalishaji wa kilimo kuwa mdogo. Viwanda hivi ni muhimu kwa maslahi ya taifa. Napendekeza kanda hii ituzalishie mbolea nyingi kwa wakulima wetu na hata kuuza nje ya nchi.

Pia kuna mahitaji makubwa ya bidhaa za plastiki nchini, ikiwemo mabomba ya kusambaza maji na matenki. Hatuna sababu ya kuagiza bidhaa hizi nje ya nchi. Zinaweza kuzalishwa kabisa nchini. Mikoa ya Lindi na Mtwara sasa inaweza kuzalisha bidhaa hizi kwa matumizi ya ndani na kuuza nje ya nchi.

Msukumo mwingine wa kiuchumi kwenye kanda hii ni shughuli za uchukuzi. Tayari kuna bandari ya Mtwara. Nafarijika hii inaimarishwa ili kukidhi mahitaji ya uchumi wa gesi. Lakini ukiwa na viwanda vya saruji na mbolea unahitaji reli. Ipo fursa ya kujenga reli ya kuiunganisha Kanda hii ya Kusini na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kupitia maeneo ya Liganga na Mchuchuma kwa ajili ya usafirishaji wa chuma, makaa ya mawe, na mazao ya kilimo. Reli hii itasaidia sana kuichangamsha kanda hii kiuchumi.

Mikoa ya Lindi na Mtwara pia sasa imepata fursa mahsusi ya kiuchumi kutokana na upatikanaji wa gesi. Fursa za kuwepo kwa gesi ikiwemo viwanda vya kuchakata gesi kwa ajili ya kuiuza nje ya nchi ni muhimu pia ikatumika kuipa Kanda hii mwamko mahsusi wa kiuchumi wa kuweza kubadilisha maisha ya watu wa kawaida. Ni muhimu kutengeneza maarifa mahsusi ya kuwashirikisha wananchi katika uchumi huu.

Moja ya sehemu zenye fukwe nzuri zaidi katika ufukwe mzima wa Bahari ya Hindi kutoka Djibouti hadi Cape Town ni kipande cha kutoka Kilwa hadi Mtwara. Kipande hiki hakijaendelezwa sana kiutalii. Inawezekana kabisa kujenga mahoteli makubwa ya kitalii na viwanja vya kisasa vya mchezo wa gofu na uvuvi wa kitalii (*sports fishing*) kwenye kipande hiki lakini cha kwanza ni kuboresha miundombinu ya kufika huko, ikiwemo barabara na viwanja vya ndege. Ajira na kodi na manufaa mengine yatakayopatikana kutokana na kufunguka kwa eneo hili kutabadilisha kabisa hali za maisha za watu wa kanda hii.

Mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe, Ruvuma, Rukwa, Morogoro na Katavi nayo pia inaweza kuwa Kanda maalum ya kiuchumi.

Msukumo mkubwa katika kanda hii ni kilimo. Mikoa hii ni ghala la chakula la taifa. Mikoa hii inalima mazao karibu yote ya chakula. Lakini kwanza ni muhimu kukawa na mtandao mkubwa wa maghala makubwa ya kuhifadhi chakula na maghala ya kuhifadhi pembejeo, hasa mbolea, mbegu na madawa.

Kichocheo kikubwa cha maendeleo ya kilimo ni kipato wanachopata wakulima kutokana na shughuli za kilimo. Wakinufaika na kilimo hawahitaji kuhimizwa kulima. Kwa hiyo mfumo wa ununuzi wa mazao katika kanda hii ni muhimu sana. Kupunguza gharama za shughuli za kilimo ni muhimu sana. Kanda hii tunaweza kuifanya ikawa mfano hapa Afrika kwa mfumo mzuri wa kusambaza pembejeo na kununua mazao ya wakulima. Mpango wa *Commodities Exchange*, ambao unalazimisha kuwa na maghala ya mazao yaliyounganishwa kwenye mtandao mmoja wa soko la mazao, utasaidia sana.

Ninapendekeza kujenga mtandao wa maghala madogo ya kisasa kwenye kila tarafa za mikoa hii ambapo wananchi wanaweza kumudu kupeleka mazao yao. Tunaweza pia kuweka mfumo ambapo mkulima anaweza kukodisha hifadhi ya mazao yake kwenye ghala hadi atakapokuwa tayari kuuza.

Msukumo mwingine katika kanda hii ni viwanda vya kusindika mazao ya kilimo. Viwanda hivi vitatoa ajira kwa wananchi, soko la uhakika kwa mazao, na kuongeza thamani ya mazao ya wakulima.

Kanda hii inapakana na nchi za Kongo, Msumbiji, Malawi na Zambia. Nchi hizi zinahitaji chakula kingi kila wakati. Mikoa ya kanda hii inaweza kupiga hatua kubwa ya maendeleo kama tutaweka utaratibu mzuri wa kuuza chakula katika nchi hizi jirani.

Lakini pia Kanda hii ina chuma na makaa ya mawe. Bahati nzuri watu wa kuendeleza chuma na makaa ya mawe ya Liganga na Mchuchuma wamepatikana. Viwanda hivi vitatoa chachu ya maendeleo kwenye kanda hii na taifa kwa ujumla.

Kanda hii pia inapitiwa na reli ya Tazara lakini pia itaunganishwa na reli mpya inayoenda Mtwara. Hii itasaidia kurahisisha biashara, uwekezaji na masoko. Na itakuwa rahisi sasa mbolea inayotoka Mtwara kupelekwa kanda hii kwa kilimo na mazao kutoka kanda hii mpaka bandari ya Mtwara.

Pia kanda hii inatengeneza ukanda wa utalii wa kusini mwa nchi yetu kwa kuwepo kwa hifadhi na mbuga za wanyama za Katavi, Selous na Ruaha pamoja na hifadhi za milima ya Udzungwa na maeneo mengine mazuri. Miundombinu

mahsusi ya utalii katika maeneo haya inahitajika ili utalii ushamiri kama ilivyo kwenye ukanda wa utalii wa kaskazini na kuvutia wageni wengi na kutoa ajira .

Kanda hii tayari ina uwanja wa ndege wa kimataifa wa Songwe. Uwanja huu unaweza kutumika vizuri zaidi kuliko sasa. Hadi sasa, hakuna ndege inayotoka moja kwa moja nje ya Tanzania na kutua Songwe. Hali ya hewa ya Mbeya inaruhusu kilimo cha maua kwa ajili ya kuuza nje ya nchi. Arusha na Moshi wanafanya hivyo. Mbeya na Iringa wanaweza pia kufanya hivyo. Viazi mviringo vya Mbeya vinauzwa nchi nzima, hadi Kenya. Tukiweka miundombinu ya vituo vya kisasa vya kufungasha maua, mazao ya mbogamboga, na matunda (*Packing Houses*) tunaweza kuzalisha na kuuza kwa wingi zaidi na kuinua hali ya maisha ya wananchi wa mikoa hii na taifa kwa ujumla.

Chai pia inalimwa kwa kiwango kikubwa katika mikoa ya kanda hii. Bahati mbaya uzalishaji wa wakulima wadogo umekuwa na manufaa madogo kwa wakulima hao. Inahitajika mipango madhubuti ya kuwawezesha wakulima wadogo kumiliki viwanda vyao vya chai na kupanua mashamba yao. Tunalo eneo kubwa la kulima chai na kahawa na tukiweka mkazo basi eneo hili linaweza kujulikana duniani kama eneo mahsusi la chai na kahawa.

Ranchi ya Kitulo inaweza kupewa jukumu mahsusi la kitaifa kama Ranchi Maalum ya Kitaifa ya kuzalisha mitamba na mbegu bora za ng'ombe kwa ajili ya kusambaza nchi nzima kwa ajili ya maendeleo ya ufugaji wa kisasa.

Mwisho, kanda hii ndio inaongoza kwa kutoa mazao ya misitu kama mbao, nguzo za umeme na karatasi. Tunahitaji kuweka msisitizo kuendeleza biashara endelevu ya mazao ya misitu na uzalishaji wa fenicha. Kuna nchi kama Finland na Canada ambazo zinafaidika kiuchumi kutokana na mazao ya misitu.

Kanda ya Magharibi ya mikoa ya Tabora na Kigoma pia yaweza kuwa kanda ya kiuchumi. Kigoma inaweza kuwa kituo kikubwa cha biashara na uwekezaji kinachohudumia nchi jirani za Burundi na Kongo. Moja ya njia ya kufanya hivyo ni kuipanua Bandari ya Kigoma ili iwe bandari huru na bandari kubwa ya mizigo –na uchukuzi, kwa nchi za Burundi na Kongo, kwa kuwa Kongo ya Mashariki inategemea upande wa Tanzania kwa karibu bidhaa zote. Hili lazima liende sambamba na kuimarisha reli ya kati ili iwe ya kisasa ikiwa na treni ya abiria na mizigo karibu kila siku.

Kwa Tabora, kilimo cha tumbaku kilichokuwa kinatamba huko nyuma kinaweza kurudi katika hadhi yake ya zamani. Kwa miaka kadhaa sasa zao la tumbaku ndilo linaloongoza kwa kutuingizia fedha za kigeni. Hata hivyo, hali ya wakulima

wa tumbaku na hali ya maeneo ambayo tumbaku inalimwa haifanani na sifa hiyo. Hapana budi sasa kuwa na mfumo mpya wa kilimo na ununuzi wa zao la tumbaku.



Zao la misitu ni muhimu katika kutoa ajira na kukuza uchumi wa Taifa na linahitaji kutiliwa mkazo ikiwemo utunzaji wa misitu na uvunaji endelevu.

Ukiondoa mafuta ya magari na mitambo, bidhaa inayoongoza kwa kuagizwa kutoka nje ya nchi ni mafuta ya kula. Mafuta haya tunaweza kuyazalisha hapahapa nchini. Mkoa wa Kigoma pekee unaweza kuzalisha mafuta ya kula ya kutosha ya kulisha nchi nzima kutokana na kilimo cha mawese. Kwa hiyo, lazima kuanzisha kilimo kikubwa cha mawese na viwanda vya kusindika mawese na bidhaa ya nyingine za mawese, ikiwemo sabuni na umeme kutoka katika kanda hii. Kilimo hiki pia kinaweza kumaliza tatizo la ajira katika kanda ya magharibi.

Vilevile, Ziwa Tanganyika ni rasilimali kubwa iliyopo katika kanda hii ambayo haijatumika vizuri, hasa kwa utalii, uvuvi na uchukuzi. Ziwa Tanganyika linaweza kabisa kuubadilisha uchumi wa Kigoma na kubadilisha hali ya maisha ya watu wa Kigoma.

Kanda ya Kati yenye mikoa ya Singida na Dodoma pia inaweza kuwa kanda maalum ya kiuchumi.

Katika aina mbalimbali za mafuta ya kula, mafuta ya alizeti yana thamani kubwa, kama yakikamuliwa na kutengenezwa katika ubora na viwango vya juu. Tunaweza kuitumia mikoa ya Singida na Dodoma, pamoja na baadhi ya maeneo ya mkoa wa jirani wa Manyara, mahsusi kwa kilimo cha ufuta, alizeti na karanga na kuwawezesha wakulima wadogo kuendeleza viwanda vya kuzalisha mafuta ya kula. Kwa sasa viko viwanda vidogo vidogo vya kukamua mafuta lakini wakulima hawa hawapati bei nzuri kwa sababu wauzaji wa mafuta wanaoagiza nje wana mtandao mkubwa wa usambazaji na wakulima hawa hawaongezi thamani ya mafuta yao. Tutawasaidia sana wakulima wa mazao haya, ambayo yana bei nzuri, kupata kipato zaidi na kuzalisha kwa kiwango cha ubora wa kuweza kuyauza nje ya nchi.

Vilevile Dodoma, kwa kuwa ina hadhi maalum ya kuwa makao makuu ya nchi, inahitaji msukumo mpya wa kiuchumi ili iendane na hadhi hiyo. Serikali kuhamia Dodoma kunatoa chachu lakini chachu kubwa ya maendeleo ya mji ni shughuli za kiuchumi sio kuwepo kwa ofisi za Serikali. Kwa mfano soko la nafaka la Kibaigwa linaweza kuboreshwa na kuwa soko kubwa la kimataifa katika ukanda wa kusini mwa jangwa la Sahara.

Kwa upande wa miundombinu, reli ya kati ikiimarishwa na uwanja wa kimataifa wa ndege wa Msalato ukikamilika, shughuli za biashara ya uwekezaji zitashamiri. Tunaweza kuigeuza Dodoma kuwa kitovu cha elimu ya juu kwa kuongeza vyuo vikuu pamoja na taasisi za utafiti. Mpango huu utaongeza wakazi, mzunguko wa fedha na shughuli za kiuchumi katika kanda hii.

Kanda ya Kaskazini yenye mikoa ya Tanga, Arusha, Manyara na Kilimanjaro pia inaweza kuwa kanda ya kiuchumi.

Mikoa hii, hasa Tanga na Kilimanjaro, ilikuwa maarufu kwa viwanda siku za nyuma. Kazi ya kwanza ni kufufua viwanda hivyo. Mahitaji ya bidhaa zilizokuwa zinazalishwa kwenye viwanda hivyo bado yapo, ajira zilizokuwa zinatolewa na viwanda hivyo zinahitajika sasa zaidi kuliko hata ilivyokuwa huko nyuma.

Reli ya kutoka Tanga hadi Arusha ni kama imekufa. Kuna watu huko nyuma walipendekeza reli hii ing'olewe lakini Rais Kikwete aliingia kati na kutoa uamuzi wa busara wa kuzuia jambo hili. Kazi sasa ni kuifufua reli hii na kuirefusha hadi kufika Ziwa Victoria, katika mji wa Musoma. Inawezekana kabisa mizigo inayoagizwa kutoka nje ya nchi kwa ajili ya Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro na Kanda ya Ziwa ikapitia bandari ya Tanga ambayo haina msongamano kama ya Dar es Salaam. Vilevile, mizigo inayopelekwa Uganda inaweza pia kupitia Bandari ya Tanga na kusafirishwa kwa reli hadi Musoma na kuvushwa hadi

Uganda. Waganda walishakuwa na fikra ya hili jambo na Rais Museveni aliwahi kufanya safari ya Tanga kwa ajili ya kuangalia uwezekano huu. Lakini kwanza lazima kuboresha bandari ya Tanga irudi katika hadhi yake ya zamani na pia kuharakisha maendeleo ya bandari mpya ya Mwambani.

Kanda hii pia ni mahsusi kwa kilimo. Mikoa ya Manyara inaweza kujikita kwenye kilimo cha ngano, mikoa ya Tanga na Arusha kilimo cha mbogamboga na matunda na maua – ikiwemo kuwa na vituo maalum, kama ilivyo Mbeya, vya kufungasha kwa ajili ya kuongeza thamani na kuuza nje ya nchi.

Mikoa hii pia ina vivutio vikubwa cha utalii. Tunaweza kuimarisha sekta hii kwa kuongeza usalama, hasa katika mji wa Arusha lakini na kuweka mazingira kwa vijana wazawa kuwa na sehemu kubwa ya umiliki na manufaa katika sekta hii.

Lakini pia kipande cha ufukwe wa kuanzia Pangani hadi Saadani kinaweza kubeba shughuli kubwa za utalii kuliko ilivyo sasa.

Kwa upande wa Zanzibar, mawazo yangu ni kuifanya sio tu bandari huria, bali ukanda maalumu wa kiuchumi wa biashara huria, utalii, na kuwa kituo kikubwa cha kimataifa cha huduma za kifedha na kibenki. Lengo kubwa ni kutoa fursa kwa Wazanzibari kushiriki katika uchumi wa kimataifa kwa kuvutia makampuni makubwa ya kimataifa kuwekeza Zanzibar.



January Makamba akisalimiana na kufurahia jambo na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

Kanda ya mwisho ni kanda ya Dar es Salaam. Kanda hii inahusisha mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Hii ni kanda muhimu kwa sababu ya umuhimu ya jiji la Dar es Salaam kwa uchumi wa nchi yetu.

Kanda hii ni lango la uchumi na uwekezaji katika ukanda huu wa Afrika. Tukiwekeza katika miundombinu ya kisasa, tukarahisisha taratibu za kuanzisha na kuendesha biashara katika ukanda huu, tukidhibiti uhalifu, basi tunaweza kuongeza mchango wa ukanda huu katika uchumi wa nchi yetu. Katika ukanda huu, wanahamia na wanaishi watu wa aina mbili tofauti: wale waliosoma sana na wale ambao wanaotegemea misuli zaidi kujipatia kipato. Mazingira ya uchumi, na shughuli za uchumi katika ukanda huu, lazima yawezeshe watu wa aina hizi mbili kuwa na kipato. Tunaweza kabisa kupunguza idadi ya wachuuzi na kuongeza idadi ya wazalishaji mali. Kwa hiyo, juhudi za makusudi za kupanua shughuli za huduma za fedha, shughuli za tehamu, shughuli za uratibu wa usafirishaji, call centres, na uzalishaji viwandani.

Cha msingi ni kwamba maendeleo na uwekezaji katika ukanda huu yasiwe na yasionekane kuwa na athari kwa maendeleo na uwekezaji kwenye kanda nyingine za kiuchumi. Maendeleo na uwekezaji kwenye kanda hii yawe ni sapoti kwa maendeleo ya nchi nzima.

9

Baada ya kuingia Bungeni, ulipewa nafasi ya kuwa Mwenyekiti wa Kamati nyeti ya Nishati na Madini. Kwanza, tuambie uliwezaje kupata Uenyekiti wa Kamati nyeti katika wiki chache tu baada ya kuingia Bungeni. Tuelezee baadhi ya changamoto kwenye nafasi hii, lakini pia mlichukua hatua gani kulisaidia taifa kwenye sekta hizi nyeti? Ilikuwa je Kamati hii ikavunjwa mara tu baada ya wewe kuachia Uenyekiti? Nini kifanyike kumaliza tatizo la mgao wa umeme na bei kubwa za umeme?

Nilivyoingia Bungeni, nilipewa fomu za kuchagua Kamati ambayo ningependa kupangwa. Chaguo langu la kwanza lilikuwa ni Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Ilipotoka orodha ya Wajumbe wa Kamati nikaona jina langu kwenye Kamati ya Nishati na Madini. Kusema kweli, nikiwa kama mbunge wa mara ya kwanza, changamoto zilizokuwa zimezigubika sekta hizi miaka ile zilinitia hofu kidogo. Baada ya kutafakari na kushauriana na marafiki zangu bungeni, nikaona kuwa nikielekeza nguvu zangu na ari yangu katika Kamati hii, nitaweza kufanya mabadiliko makubwa katika sekta na kuwapunguzia kero wananchi wengi. Nikaamua kugombea Uenyekiti wa Kamati.

Hakukuwa na muda wa kampeni kwa sababu majina ya Kamati yametangazwa leo, uchaguzi kesho yake. Tukaingia ukumbini. Kwa nafasi ya Uenyekiti, nikaweka jina langu mbele, na Mheshimiwa Festus Limbu, Mbunge wa Magu, naye akaweka jina lake. Tukajieleza. Kura zikapigwa. Nikapata kura 19, Mheshimiwa Limbu kura 6. Baada ya siku chache tu kama mbunge, nikakabidhiwa dhamana hiyo nzito.

Kwa kutambua umuhimu wa dhamana tuliyokabidhiwa, tulijipanga kuwa wakali sana katika kuisimamia Serikali. Kama Mwenyekiti, nilijitahidi sana kuweka nidhamu na umakini katika utendaji wa kazi zetu. Tulikuwa tunapata taarifa kwamba Serikali na Taasisi zilizokuwa zinakuja mbele ya Kamati yetu zilikuwa zinajiandaa vyema kwa sababu walikuwa wanajua kwamba tulikuwa hatuna mchezo.

Kuhusu umeme, tulifanikiwa kuishauri Serikali mambo mengi ya msingi, ikiwemo kuachana na mitambo ghali ya kukodisha na kupanga fedha zaidi kwa ajili ya kupeleka umeme vijijini. Kuna nyakati katika kujadili Bajeti ya Wizara, tuliamisha fedha kutoka mafungu yasiyo na tija na kupeleka kwenye miradi ya umeme vijijini. Tulilazimisha ratiba ya uhakika ya kumalizika kwa mgao wa umeme, tuliibua maeneo yaliyokuwa na ufasidi ikiwemo kwenye suala la ununuzi wa mafuta ya mitambo ya dharura, tulihoji kuhusu gharama kubwa za kesi za Tanesco. Tulishirikisha wadau wote wa umeme, ikiwemo wenye viwanda, katika kazi zetu. Tulifanya mihadhara na midahalo mbalimbali katika kuisaidia nchi kupata suluhu ya tatizo hilo. Tuliwezesha kusimamisha bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini ili Serikali ilete Bungeni Mpango wa Dharura wa kulinusuru taifa na mgao wa umeme.



January Makamba akijibu maswali ya Wabunge ndani ya Bunge.

Kuhusu sekta ndogo ya mafuta, tuliingilia kati wakati nchi imeingia kwenye hatihati ya kusimama kabisa wakati wa mgogoro wa waagiza mafuta na Serikali kuhusu upangaji bei. Moja ya siku ninazojivunia katika muda wangu kwenye siasa ni pale nilipoleta hoja Bungeni ili Bunge lisimamishe shughuli zake zote na tujadili na kupata majawabu ya dharura ya mafuta nchini. Bunge lilikubali na Serikali ikalazimika kuchukua hatua za dharura kuokoa hali ile. Baadae tuliisimamia Serikali kuanzisha mfumo mpya wa ununuzi wa mafuta wa pamoja, yaani *Bulk Procurement System*. Vilevile, tulifanya vikao na Chama cha Wamiliki wa Magari ya Mizigo na kusikia kilio chao kuhusu tatizo la uchakachuaji wa mafuta na tukapendekeza njia muafaka zilizomaliza tatizo hilo kabisa.

Kuhusu gesi, kabla Kamati yetu haijaundwa, hapajawahi kuwa na mjadala Bungeni kuhusu masuala ya gesi. Niliunda Kamati Ndogo ya Kamati yangu ili kulichunguza kwa kina suala la gesi. Kamati ile ilifanya kazi nzuri na kwakweli napendekeza watu waitafute ile ripoti ya kizalendo na kuisoma. Ripoti ile ilijadiliwa Bungeni na maazimio yenye maslahi kwa nchi kupitishwa. Ripoti ile ilitikisa Bunge. Yapo baadhi ya masuala ya ulaghai wa wazi uliofanywa na baadhi ya makampuni ya gesi na tukapendekeza mikataba ivunjwe, watu hao wakamatwe, na warudishe pesa yetu. Vilevile mapendekezo ya ripoti hii kwa sehemu kubwa ndio yametengeneza rasimu ya Sera mpya ya gesi. Nakumbuka tulisimamisha ugawaji wa vitalu vipya vya gesi mpaka sheria mpya ya gesi ipitishwe. Bahati mbaya, sheria hiyo mpaka leo hii haijapitishwa. Natumaini itapitishwa karibuni.

Kama Kamati tulipata changamoto nyingi mara kwa mara. Sekta ya Nishati ni nyeti na kuna watu wengi wenye maslahi makubwa katika sekta hii. Sekta hii inahusisha fedha nyingi na kumekuwa na historia ya rushwa na ubadhirifu. Kazi kubwa tuliyofanya ni kuhakikisha wajumbe wote tunasimama pamoja na kuepuka ushawishi unaoweza kutupeleka pabaya. Katika kipindi changu tulifanikiwa kwa kiasi fulani.

Binafsi nilipata changamoto kubwa za kuchafuliwa. Kwakuwa nilikuwa mkali sana na niliharibia baadhi ya watu mianya yao ya kula na kwa sababu nilibainisha udhaifu katika utendaji na kwa sababu niliweza kuaminiwa sana na Watanzania, zikafanyika jitihada kubwa kunichafua. Nakumbuka mojawapo ni watu walitengeneza barua pepe ikidaiwa inatoka kwa dada yangu kwenda kwa mpenzi wake wa kufikirika eti akiomba pesa kwa ajili yangu na kisha hiyo barua pepe ikazungushwa dunia nzima. Barua pepe ile ilibainika kwamba ni ya kugushi. Wahusika wa ile barua pepe hadi leo tunasalimiana lakini wanaamini siwafahamu. Nashukuru kwamba nilimaliza kazi ya Kamati nikiwa msafi na nikiwa na heshima yangu. Kamati ile ilivunjwa baada ya mimi kuondoka kwa

tuhuma za rushwa dhidi ya wanakamati wachache, ingawa baadae tuhuma zikaonekana za kusingizia.



January Makamba akifafanua jambo bungeni kwa niaba ya Serikali.

Umeuliza pia nini kifanyike kumaliza tatizo la mgao wa umeme na bei kubwa za umeme. Ukirejea ripoti utaona mapendekezo yasiyopungua ishirini. Lakini haraka haraka niseme tu kwamba, kwanza, tuongeze vyanzo vya uzalishaji umeme: tunayo makaa ya mawe, ambayo ndiyo yaliyozalisha umeme ulioleta mapinduzi ya viwanda duniani. Bado hapa nchini hatuyatumii ipasavyo kuzalisha umeme. Vyanzo vya umeme kama upepo, jotoardhi na jua vinapatikana kwa wingi sana nchini mwetu. Gharama kubwa ya umeme inasababishwa na gharama kubwa ya chanzo cha nishati. Vyanzo hivi mbadala vitasaidia sana kupunguza bei na kutuhakikishia umeme wa uhakika kwa watu wote. Pili, kufanya mageuzi makubwa kwenye sekta ya nishati, ikiwemo muundo na utendaji wa Shirika la Umeme Tanzania. Hili ni muhimu sana kama tunataka kuona mapinduzi katika sekta hii nyeti kwa maendeleo ya taifa letu. Tatu, uwekezaji kwenye miundombinu ya usafirishaji na usambazaji umeme. Umeme mwingi unapotea njiani na kusababisha hasara kubwa. Nne, mfumo wa utaratibu wa upatikanaji wa vifaa vya usambazaji umeme urekebishwe ili vifaa hivyo vipatikane kwa haraka na kwa bei rahisi. Haipendezi Shirika ambalo uhai wake unategemea wateja wengi, linakosa nguzo za umeme, linakosa mita,

linakosa transfoma. Tano, kudhibiti hujuma na rushwa kwenye sekta ya nishati, ikiwemo mikataba mibovu isiyo na maslahi kwa taifa. Na mwisho tukamilishe haraka ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara ili tuzalishe umeme wa gesi na kuondokana na umeme wa kukodi wa kuzalishwa kwa mafuta.

Binafsi nafarijika, na naamini pia wenzangu tuliokuwa nao kwenye Kamati wanafarijika, kwamba udhibiti wa sekta hii na mapendekezo yetu ndio yalianzisha kwa uhalisia mapinduzi chanya katika sekta hii. Kamati yetu iliweka msukumo mkubwa kwa serikali kulishirikisha bunge katika mikataba yote, mikubwa na midogo, ya nishati na madini, hasa umeme na gesi, ili kupunguza mianya ya taifa letu kudhulumiwa na wawekezaji wa ndani na nje. Mpango-Mkakati Mpya wa Mageuzi kwenye Sekta ya Umeme kwa kiasi kikubwa umezingatia tuliyoyapendekeza. Pia, tulihakikisha walau tunayabainisha matatizo yaliyokuwepo kwenye sekta ndogo ya mafuta, ikiwemo suala nyeti la upangaji bei katika soko ambao hauakisi uhalisia wa bei ya dunia kupitia mdhibiti wetu, EWURA. Vilevile, tulisimama kidete kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo wa madini wanawezeshwa ipasavyo. Tuliilazimisha Serikali kupanga fedha nyingi zaidi kwa ajili hiyo. Nafarijika kwamba utaratibu huo umeeendelezwa hadi sasa.

10

Umeeleza kwamba ulikuwa sehemu ya kampeni ya Urais ya CCM mwaka 2005 na kwamba ulipata nafasi ya kuzunguka na Mheshimiwa Kikwete akiwa mgombea wa Urais wa CCM kwenye uchaguzi huo. Ulikuwa unafanya shughuli gani na ulijifunza nini katika shughuli ile?

Kwanza nilipata fursa ya kuijua nchi yangu kwa kina – tulisafiri kwa barabara katika kila kona ya nchi yetu isipokuwa nadhani Wilaya mbili au tatu. Na katika kila Wilaya Mheshimiwa Kikwete alizungumza na wananchi kwenye mikutano mingi ya nje na mikutano ya ndani ya viongozi. Kwakuwa kampeni yake ilijikita kwenye kujibu kero za Watanzania, na kwakuwa moja ya kazi zangu kwenye kampeni ile ilikuwa ni kusaidia kuandika dondoo za mazungumzo yake, nilipata fursa ya kuzifahamu kero za Watanzania na changamoto za nchi yetu katika kila Wilaya ya Tanzania. Nilipata pia fursa ya kufahamu majawabu ya baadhi ya hizo kero.

Nilienda mikoa ya Kanda ya Ziwa, mikoa ya Mwanza, Mara, Shinyanga, Kagera na maeneo ambayo sasa ni mikoa mipya ya Geita na Simiyu – nikashuhudia tatizo kubwa la maji, nikashuhudia na kuzifahamu changamoto za kilimo cha Pamba, nikakutana na wafugaji na kuzungumza nao. Nikafanikiwa kuyajua matatizo yao. Nilionana na wavuvi, hasa wavuvi wadogo wadogo. Tulikutana na wachimbaji wadogo wa madini na kuzungumza nao, kwahiyo nazijua kero zao – sio kwa kuhadithiwa bali kwa kuziona.

Nilienda mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, mikoa ya Mbeya, Iringa, Ruvuma, Rukwa na maeneo ambayo sasa ni mikoa mipya ya Njombe na Katavi nikaona matatizo ya pembejeo za kilimo, matatizo ya upatikanaji na bei ya mbolea na mbegu na nikaona jinsi wakulima wanavyolima kwa bidii lakini hawana pa kuhifadhi, pa kuuzia mahindi yao au wanapata bei ndogo.



January Makamba akiwa na Mheshimiwa Jakaya Kikwete, mjini Maswa kwenye harakati za kampeni za Urais za CCM mwaka 2005 wakati akiwa Msaidizi wa Mgomba Urais Mheshimiwa Kikwete.

Tulienda mkoa wa Morogoro na kuona fursa kubwa iliyopo ya kilimo cha kila aina, tukaona changamoto za matatizo ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima.

Nilienda mikoa ya Kusini, mikoa ya Lindi na Mtwara na nikaona matatizo ya barabara, maji na nikaona matatizo ya pembejeo na ununuzi zao wa korosho, nikaona jinsi ambavyo bandari za Mtwara, Lindi na Kilwa na viwanja vya ndege vya Lindi na Mtwara tunavyoweza kuviimarisha zaidi.

Nilienda mikoa ya Kanda ya Kaskazini, mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara nikaona matatizo ya ufinyu wa ardhi, matatizo ya viwanda vilivyokufa na haja ya kuvifufua, nikaona vijana wengi wanaohangaika na changamoto za ajira na kuona fursa kubwa kwenye utalii na madini.

Nimekaa na nilienda Kigoma na tukaenda Tabora na kuona haja ya kuimarisha na kuifufua reli ya kati, bandari ya Kigoma, haja ya kumaliza ujenzi wa barabara zinazounganisha Mkoa wa Kigoma na sehemu nyingine za nchi yetu. Nikaona fursa iliyopo kwenya biashara ya mpakani. Nikaona wakulima wa tumbaku ambao ukiona hali zao huwezi kuamini kwamba zao hili ndilo linaloingiza fedha za kigeni kuliko zao jingine lolote.

Nilienda mikoa ya Kanda ya Kati, mikoa ya Singida na Dodoma na kuona jinsi tunavyoweza kunyanyua uchumi wa maeneo haya kwa kuongeza chachu katika shughuli za uchumi zinazofanyika katika mikoa hii, ikiwemo kilimo cha alizeti na ufuta, na kusikia kilio cha wana-Dodoma juu ya haja ya kuharakisha maendeleo ya mji wa Dodoma.

Nilienda Zanzibar nikaona fursa iliyopo ya kuweza kujenga uchumi wa kisasa na kuifanya Zanzibar kuwa kituo cha kimataifa ya huduma za fedha na kibenki na kuendelea kuimarisha utalii. Nikaona jinsi siasa inavyozorotesha maendeleo. Nikaona fursa kwenye uvuvi bora unaoweza kuwakomboa watu kuliko uvuvi wa sasa.

Kwa hiyo, kwa maana ya kuijua nchi hii kwa sura, maumbile, changamoto na fursa katika kila eneo, naamini kwenye hilo nimefanikiwa. Na bahati sikuzunguka mara moja. Nimefanya mara mbili na baadhi ya maeneo mara tatu hadi nne.

Nilijifunza pia kwamba matumani wanayowekeza Watanzania kwa viongozi wao ni makubwa sana na pale tunapowaangusha kwa kweli tunatenda dhambi. Nilijifunza pia kutoka kwa Mheshimiwa Kikwete kwamba unaweza kuomba kura, kueleza dira yako, fikra zako na Sera na Ilani ya Chama chako bila kutumia matusi, kejeli, ulaghai na lugha kali na bado ukafanikiwa.

Nilijifunza pia mbinu na mikakati ya kufanya kampeni za kuomba nafasi hii kubwa ya uongozi wa nchi yetu. Nilijifunza mengi na kujua mengi kuhusu Chama chetu na uwezo wake katika ngazi za uongozi za chini kabisa. Katika kampeni nzima, tulihangaika na Ilani na Sera za CCM bila kuwasema wapinzani na bado tukashinda kwa kura nyingi. Nilifahamiana na kujenga udugu na urafiki na viongozi wengi wa Chama chetu katika kila kona ya Tanzania, jambo ambalo limekuwa na tija hata nilipoamua kuingia siasa.

Niseme tu kwamba namshukuru sana Rais Kikwete kwa kunipa fursa ya kuijua nchi yangu, kujua kero na changamoto za nchi yetu, kuona na kujua fursa zilizopo za kuweza kuiendeleza. Amenisaidia kuweza kuijua picha halisi ya nchi yetu. Nikipata nafasi ya kuzunguka tena nchi nzima, itakuwa ni kwa mara ya tatu.

11

Kwa miaka mitano na zaidi, ulipata nafasi ya pekee ya kuwa karibu na Rais wakati wote. Kutokana na nafasi hiyo ni mambo gani ya msingi uliyojifunza na yakakujenga kuwa kama ulivyo leo hii? Kwa nini uliamua kuacha kazi nzuri ya Ikulu na kwenda kugombea ubunge? Je, ilikuwa rahisi Rais kukuachia?

Kwanza kabisa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumsaidia Ikulu ni fursa adhimu sana na bado nitaendelea kumshukuru Rais kwa ajili hiyo. Uandishi wa hotuba za Rais ni moja tu ya shughuli nilizokuwa namsaidia Rais, ingawa ilikuwa ndio shughuli kuu, lakini yalikuwepo mambo mengine mengi. Nimejifunza mengi kwenye nafasi ile.

Kwanza, nimeifahamu Serikali na jinsi inavyoendeshwa. Nilikuwa nikipata nyaraka zote za Baraza la Mawaziri na kuhudhuria vikao vya Baraza la Mawaziri kwa miaka mitano na kujifunza jinsi sera zinavyotungwa, jinsi bajeti inavyotengenezwa, kujadiliwa na kupitishwa katika ngazi ya Serikali, jinsi Miswada ya Sheria inavyojadiliwa na kuidhinishwa ndani ya Baraza. Nimeshuhudia maamuzi makubwa na nyeti katika Serikali yakijadiliwa na kuamuliwa.

Nimejifunza kuhusu changamoto za utendaji na utekelezaji na usimamizi na ufuatiliaji ndani ya Serikali. Ni uzoefu ambao umekuwa na thamani kubwa sana kwangu na uzoefu mkubwa kuliko umri wangu.

Pili, nimejifunza kuhusu masuala ya nchi. Rais huzungumzia kuhusu masuala karibu yote kwenye nchi, ulinzi na usalama, afya, elimu, maji, barabara, mahusiano ya kimataifa, njaa, UKIMWI, mazingira, sayansi – kila kitu. Kama Mwandishi Hotuba, lazima ujitahidi uwe na uelewa mpana kuhusu masuala yote haya mbalimbali. Ndani ya wiki moja, Rais anaweza kuzungumza na Makamanda wa Polisi wa Mikoa, akazungumza na Maaskofu, akahutubia kwenye Mei Mosi, akazindua Program ya Mifugo na akahutubia mkutano

kwenye Umoja wa Afrika. Lazima uwe tayari na uwe na uelewa mpana wa kutosha kutambua ni maneno gani sahihi kwa kila shughuli. Kwa hiyo, lazima kusoma sana na lazima kujifunza haraka sana. Na kwakuwa mimi nilianza naye wakati anaanza Urais, ilikuwa ni lazima na kwa haraka sana kuipata sauti yake na staili yake. Kwa mfano, kutokana na kazi ile, nililazimika kwa haraka sana kujifunza kuhusu masuala ya uchumi kwa kusoma na kuongea na manguli wa uchumi, ili kuweza kumsaidia Rais kuwasiliana na wadau mbali mbali kuhusu malengo yake kwa uchumi wa nchi. Kwa hiyo uelewa wangu kwenye masuala ya uchumi na maendeleo kwa ujumla umepanuka kutokana na mazingira ya kazi ile. Na huo ni mfano wa uchumi tu, nimejifunza mambo mengi ya kisera na kimkakati kwenye sekta mbali mbali kama kilimo, afya, miundombinu, na mambo ya ulinzi na usalama.

Tatu, nimefanikiwa kujua nchi yetu kwa kina. Nchi yetu ni kubwa sana. Wakati wa kampeni nilizunguka na mgombea nchi nzima nikiwa msaidizi wake wakati anaomba kura. Alipofanikiwa kuingia Ikulu, Rais Kikwete alifanya ziara nchi nzima kukagua na kuhimiza maendeleo. Nami niliongozana naye tena katika ziara hizi. Akiwa Rais, kabla hajaanza ziara ya Mkoa au Wilaya sisi wasaidizi wake huomba taarifa za maendeleo za kila Wilaya, kisha huzisoma na kuandika dondoo za mazungumzo yake na wananchi kwenye kila wilaya. Kazi ya kuandika hizi dondoo nilikuwa naifanya mimi. Kwa hiyo, nilipata pia fursa ya kusoma taarifa za maendeleo za karibu wilaya zote katika nchi yetu. Hili lilinipa uelewa mpana sana kuhusu nchi yetu na changamoto zake kubwa na ndogo lakini pia na kazi zinazofanyika katika ngazi za chini kukabiliana na changamoto za Watanzania na kuwaletea maendeleo. Kwa mfano ukienda wilaya ya Masasi ni lazima kuelewa changamoto za zao la korosho, lakini ukienda Maswa basi lazima kuzifahamu changamoto za zao la Pamba, ukienda Geita lazima kujua masuala ya wachimbaji wadogowadogo wa madini. Hivyo, kupitia heshima hii ya kumsaidia Rais Kikwete nimeweza sana kujifunza na kuelewa matatizo yanayowakabili Watanzania na mbinu za kutatua kero zao.

Nne, nimefanikiwa kujua dunia na kujifunza kuhusu diplomasia ya kimataifa, na kuifahamu kwa kina nafasi ya Tanzania katika dunia ya sasa.

Nilipata fursa pia ya kuambatana na Rais na kuandika hotuba zake katika shughuli zake za kimataifa – kwenye mikutano ya kimataifa aliyohudhuria lakini pia kuandika dondoo au kwa kiingereza “talking notes” za mazungumzo yake na viongozi wenzake duniani. Licha ya kuandika hizi dondoo pia nilipata fursa ya kuhudhuria mikutano yake na viongozi wenzake na watu mashuhuri duniani

nikiwa kama muandika kumbukumbu za vikao hivyo. Kwa mfano nimehudhuria mazungumzo yake na Rais Bush, Gaddafi, Zuma, Kagame, Clinton, Mugabe, Mfalme wa Saudi Arabia, na wengine wengi pamoja na watu mashuhuri akiwemo Bill Gates na wengineo kwa ajili ya kusukuma ajenda za maendeleo ya Tanzania lakini pia ajenda za ustawi wa bara la Afrika na dunia kwa ujumla. Katika kuandika dondoo za mikutano hii na katika kuihudhuria nimejifunza namna diplomasia ya kimataifa inavyoendeshwa, namna maslahi ya nchi yanavyotafutwa na namna viongozi wakuu duniani wanavyopaswa kuhusiana. Pia katika nafasi ile moja ya majukumu yangu ilikuwa ni kuandika rasimu za barua za Rais kwa viongozi wenzake duniani. Hii pia ilinisaidia kujifunza kuhusu lugha na utaratibu na uzito wa maudhui katika mawasiliano kati ya viongozi wa nchi moja na nyingine. Ni elimu na uzoefu ambao huwezi kuupata darasani wala katika nafasi nyingine yoyote ile. Rais Kikwete alijidhihirisha kwamba ni mmoja wa wanadiplomasia mahiri duniani na nilipata bahati ya kushuhudia na kushiriki kwa karibu kabisa na kuona jitihada zake za kuing'arisha nchi yetu katika diplomasia ya kimataifa na kutengeneza mahusiano ya kiuchumi yenye manufaa kwa Watanzania.



January Makamba akimkabidhi Rais Kikwete hotuba atakayosoma katika moja ya mikutano ya kimataifa. Pembani ni Rais wa zamani wa Kenya Mwai Kibaki.

Tano, pia niliimarisha fikra zangu kwenye masuala ya maadili, siasa na uongozi. Nafasi ya Urais ni nafasi ya juu kabisa ya uongozi nchini. Ndicho kitovu cha siasa na uongozi.

Kama Msaidizi wa karibu wa Rais unapata fursa ya kujifunza kwa karibu jinsi siasa na uongozi wa nchi unavyoendeshwa. Kila kiongozi huwa anapitia vipindi vigumu katika uongozi wake. Na kwa Rais Kikwete ilikuwa hivyo hivyo. Zipo nyakati nyingi nilikosa usingizi.

Zipo nyakati tulipaswa kuandika hotuba ngumu kukabiliana na mazingira magumu na masuala mazito yaliyokuwepo kipindi hicho. Kwa mfano, wakati wa ukame na njaa kubwa iliyoikumba taifa mwaka 2007, kipindi cha kashfa za EPA na Richmond, na pia kipindi ambacho taifa lilikumbwa na wimbi kubwa na kutisha la ujambazi. Unapata fursa ya kujua siri nyingi za nchi na lazima uwe na ukomavu na uwezo wa kuzitunza. Yapo mambo mengine niliyoyaona na kujifunza ambayo nitakwenda nayo kaburini lakini yalinipa elimu tosha ya uongozi. Nilijifunza kwa Rais Kikwete umuhimu wa kutohamaki wala kutetereka kwani kama Rais akihamaki na kutetereka basi sisi sote na tulio chini yake na uongozi mzima wa nchi nao unatetereka na nchi inayumba. Nilijifunza kuhusu haja na umuhimu wa kusema mambo sahihi kwa wakati sahihi ili kupitisha ujumbe mahsusi au kukabiliana na changamoto mahsusi. Nilijifunza kwa Rais Kikwete kuhusu staha na uvumilivu, kwamba madaraka ya Rais ni makubwa sana na lazima mtu uwe na ukomavu, hekima na busara ya kutoyatumia vibaya hata kama watu wanakukosea namna gani.

Ni kweli, kama ambavyo nimemaliza kukueleza, kazi hii ya Ikulu ilikuwa ni kazi adhimu na ya heshima na hadhi kubwa. Kuwa na Rais karibu wakati wote na kusafiri naye kote nchini na duniani kumenipa uzoefu mkubwa. Hata hivyo, baada ya miaka mitano ya kazi hiyo, niliamini imefika wakati wa kutafuta changamoto nyingine mpya. Waswahili wanasema “msambaa mmoja havunji soko”. Sikuwa na shaka kabisa kwamba kazi niliyokuwa naifanya Ikulu itapata Mtanzania mwingine ambaye ataimudu vyema.

Niliamini kwamba nilijojifunza nikiwa Ikulu naweza kuyatumia kwa manufaa ya watu wa Bumbuli, ambako kuna changamoto nyingi na kubwa za maendeleo. Baada ya kuwa nyuma ya pazia la siasa kwa miaka mitano, niliamini sasa ni muhimu kujitokeza mbele ya pazia na kujaribu kuendesha siasa ya tofauti, siasa ambayo msingi wake ni utendaji zaidi kuliko maneno, siasa ambayo ubunifu unaelekezwa kwenye kukabiliana na changamoto za watu na sio kwenye mbinu za kupambana na wenzako, siasa ya kizalendo, siasa ya utetezi wa haki za watu, siasa ya ukweli na siasa ya utumishi zaidi, siasa ambayo sio

ya majukwaani ya kuamsha hamasa za watu tu na kuburudisha. Na hivyo ndivyo ambavyo nimejitahidi kufanya tangu nilipochaguliwa kuwa Mbunge. Sidhani kama umewahi kunisikia jukwaani namshambulia mwanasiasa au mtu mwingine yoyote kwa sababu naamini yapo mambo ya msingi zaidi ya kushambulia, ikiwemo shida za Watanzania.

Rais alitoa ridhaa yake ingawa kwangu ilikuwa ngumu kuanzisha mazungumzo ya uamuzi wangu wa kwenda kugombea Ubunge. Nilitumia muda mrefu sana kutafakari namna ya kuanzisha mazungumzo hayo. Kwa bahati nzuri, hatimaye tulipozungumza, Rais aliridhia na akanitia sana moyo kwa sababu siku zote anaamini kwamba kila wakati lazima upatikane uongozi wa kizazi kipya na alinitakia heri katika kampeni yangu.



January Makamba, kulia, akizungumza katika Mkutano wa Viongozi Barani Afrika uliofanyika Kigali, Rwanda.

12

Hivi karibuni wananchi wengi hasa wa kipato cha chini na cha kati wamekuwa wakilalamika kwamba maisha yamekuwa makali, na gharama za maisha zimekuwa zikipanda kila kukicha. Maarifa gani yanahitajika ili kuweza kupunguza ukali wa maisha kwa Watanzania?

Ni kweli hali ya maisha imekuwa kali sana siku za karibuni, chakula kimekuwa bei ghali, mafuta yamekuwa bei ghali, ada za shule ni kubwa, usafiri umekuwa bei ghali, watu wengi wanaishi kwa mikopo, kodi za nyumba zimekuwa kubwa, kodi za serikali zimekuwa nyingi, umeme umekuwa bei ghali, riba za mikopo zimekuwa juu, ajira zimekuwa adimu, thamani ya pesa yetu imeshuka, lakini upatikanaji wa pesa bado umekuwa mgumu. Vipato vya watu wetu havitoshi kuweza kuimarisha ustawi wao na familia zao. Watanzania wamekuwa wavumilivu sana kwa kipindi kirefu kukabiliana na ukali huu wa maisha lakini umefika muda sisi viongozi lazima tuje na mbinu, maarifa na mikakati mipya ya kuwapunguzia wananchi ukali wa maisha. Kwa zaidi ya miaka miwili sasa, serikali kwa kupitia Wizara ya Fedha na Benki Kuu wamejitahidi na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kudhibiti mfumuko wa bei lakini bado wananchi wengi hawajaona nafuu katika ukali wa maisha.

Mimi nashuhudia hali hii katika maisha yangu ya kila siku lakini vile vile ninapoongea na wapiga kura wangu. Wapo watu wengi ambao wana kipato kisicho cha uhakika ambao wanahangaika hata kupata mlo au nauli ya kwenda kutafuta riziki. Lakini pia lipo kundi la watu wenye kipato cha kati, yaani *middle class*, ambao wanapaswa kuwa injini ya uchumi, nao pia wanaishi maisha ya mashaka kutokana na ukali huu maisha, huku wakiumizwa na gharama mbalimbali ikiwemo mafuta na kodi. Kwa mfano, mfanyakazi wa Serikali au kampuni binafsi ambaye ana mshahara wa shilingi 800,000 kwa mwezi mwenye familia ya watoto wanne wanaosoma, anaishi kwenye nyumba ya kupanga ni lazima anakwazika na ukali huu wa maisha na mzigo mkubwa wa

kodi anazotozwa. Tanzania ndio inaongoza Afrika Mashariki kwa kutoza kodi kubwa ya mshahara (PAYE).

Haya mambo lazima tuyabadilishe na nina mapendekezo kadhaa ili kupunguza ukali wa maisha, kupunguza kodi ya mshahara (PAYE) ni mojawapo ya majawabu.

Katika kupunguza ukali wa maisha tunaweza kuanza na kuangalia namna ya kutoa nafuu kwenye gharama ya nishati muhimu kama mafuta, gesi, na umeme. Kwa sasa kila unapolipia lita moja ya mafuta, zaidi ya shilingi 600 ni malipo ya kodi tu. Ukubwa wa bei ya mafuta unakwenda sambamba na ukali wa bei za usafirishaji, uzalishaji mali, na inaongeza hadi bei za vyakula. Bei ya bidhaa kama saruji pia itashuka kama tukiweza kufanya jitihada kupunguza bei ya za mafuta, umeme, na gesi. Tukirekebisha mfumo mzima na utaratibu wa uagizaji mafuta, kama nilivyokwishasema awali, na kuondokana na baadhi ya gharama zisizo za lazima tutaweza kupunguza bei ya mafuta na ukali wa maisha. Mwisho kabisa, ili kushusha bei ya mafuta, ni lazima kuhakikisha kwamba sarafu yetu haipotezi thamani. Mafuta yanaagizwa nje kwa pesa za kigeni, ukakamavu wa shilingi yetu utatusaidia kuhakikisha kwamba tunaagiza mafuta kwa bei shindani.

Tukiweza kupunguza bei ya mafuta, tutafanikiwa kwa kiasi kikubwa kupunguza ugumu wa maisha kwa Watanzania.

Gharama za umeme na nishati ya kupikia pia inachangia ukali wa maisha, haya ni matumizi ambayo hayaepukiki. Ni lazima kuwasha taa usiku, na ni lazima kupika chakula. Hivyo gharama kubwa kwa huduma hizi zinaongeza moja kwa moja ukali wa maisha. Kama nilivyokwishasema mwanzoni, aina ya vyanzo vya uzalishaji umeme inachangia kwenye gharama ya umeme. Tutakapoweza kuondokana na umeme unaozalishwa kwa mafuta na kuweza kufikisha bomba letu la gesi na kuzalisha umeme wetu kwa gesi asilia kwa bei nafuu, na tukiweza kurekebisha gharama za uendeshaji wa Shirika letu la umeme, tunaweza kupata nafuu katika bei ya umeme. Lakini pia zipo mbinu mpya zinazoweza kutumika kumpunguzia mtu wa kipato cha chini gharama za umeme. Tukiweka mfumo mpya wa malipo ambapo watumiaji wakubwa wasiojali gharama wanachajiwa kwa aina tofauti ya mfumo na wale watumiaji wadogo tunaweza kuwasaidia watu wetu wa kipato cha chini.

Gharama za upangishaji wa nyumba za kuishi na biashara lazima tuzitazame upya, ila muhimu zaidi ni tabia ya wenye nyumba kudai kodi ya mwaka mzima.

Kikifika kipindi cha kulipa kodi wananchi wanaopanga wanakosa amani kabisa kutokana na idadi kubwa ya pesa inayotakiwa kwa mpigo. Hili nimelifanyia kazi siku za nyuma kama nilivyoeleza na ile Sheria ninayopendekeza ikipita basi tutapata nafuu.

Chakula kikiwa ni bei kubwa ni lazima maisha yatakuwa makali. Nchini kwetu kuna sababu nyingi sana zinachangia chakula kuwa bei ghali. Gharama za uzalishaji na usafirishaji ni vitu ambavyo tunaweza kuvimudu ili kupunguza bei ya chakula. Mbinu za kisasa za kilimo ili kuongeza mavuno, kuhakikisha miundombinu ya kufikisha chakula kwa mlaji kwa gharama nafuu iko vizuri, kusindika vyakula hapa nchini, na kudhibiti ulanguzi vitasaidia kushusha gharama za chakula. Kwa nchi kama yetu haipendezi kabisa kuagiza kutoka nje bidhaa za vyakula kama vile mafuta ya kula, ngano, sukari, maziwa, juisi, siagi, na mchele. Tutazame vizuri mfumo wa bei za chakula ikiwemo kudhibiti ulanguzi.

Mambo mengine yanayoongeza gharama za maisha ni ada za shule za watoto wetu na gharama za matibabu. Hapa Serikali inabidi tuboreshe shule zetu na hospitali zetu ziweze kutoa huduma sawa na za binafsi ili wazazi wasilazimike kuingia gharama kubwa kupata huduma hizi kutoka kwa watu binafsi. Utaratibu wa bima ya afya nilioupendekeza utasaidia kuwapunguzia makali wananchi wa kipato cha chini mara wanapopata ulazima wa kupata huduma ya afya.

Mwisho kabisa, Serikali ni muhimu tuangalie mfumo wa kodi. Watanzania wa kipato cha chini na cha kati ni lazima wawekewe mfumo wa kodi usiowapokonya kipato chao cha matumizi ya kujikimu na ziada. Serikali itambue kwamba Mtanzania akiwa na pesa mfukoni na kuzitumia kununua huduma na bidhaa, kuweka akiba, na kuwekeza anachangia kuinua uchumi pia.

Kama Serikali, inabidi tupunguze misamaha ya kodi isiyo na tija ili kuwapunguzia mzigo wa kodi Watanzania wa kipato cha kati na cha chini ambao ndio injini ya ukuaji wa uchumi nchini.

Tukiweza kuyafanya haya yote niliyoyapendekeza tunaweza kusaidia watu wetu kupunguza ukali wa maisha ambao kwa sasa umeongezeka maradufu.

13

Watanzania wengi wanajishughulisha na kilimo, ufugaji na uvuvi lakini wamekuwa hawanufaiki na shughuli hizi licha ya mipango mingi tangu wakati wa uhuru hadi sasa. Je, kizazi kipya cha uongozi wa nchi kinapaswa kuwa na maarifa gani mapya kuhusu mapinduzi ya kilimo na maendeleo ya uvuvi na ufugaji?

Ni kweli kwamba mapinduzi ya kilimo ambayo yamezungumziwa kwa miaka mingi bado hayajafikiwa. Kilimo ni uti wa mgongo wa taifa letu. Zaidi ya asilimia 70 ya kaya za Watanzania zinategemea kilimo kwa ajira na mapato. Ni dhahiri kilimo kina nafasi kubwa katika mikakati yetu ya kupunguza umaskini, na tusipofanya mapinduzi haraka Watanzania wengi tutabaki kwenye mzingo wa umaskini kwa miaka mingi ijayo.

Changamoto katika sekta ya kilimo ni nyingi, kuanzia za kisera, za kiutekelezaji, za pembejeo, za kiutaalamu, za kimasoko na za kifedha. Ni dhahiri mpaka leo hii tunaweza kusema kilimo chetu hakijatimiza lengo la kumkomboa mkulima. Wakulima wetu wanatumia nguvu nyingi na masaa mengi kazini na kuishia kuvuna mazao kidogo na kupata bei ndogo wanapoyauza. Na hapa naongelea kilimo katika tafsiri pana, kwa maana ya kilimo cha mazao ya chakula na biashara, uvuvi na ufugaji pia. Bado tunatumia teknolojia zilizopitwa na wakati katika shughuli za kilimo. Bado tunasuasua katika upatikanaji wa pembejeo halisi, kwa uhakika, kwa wakati, na kwa bei nafuu. Bado tunategemea mvua kwa kiasi kikubwa katika ukulima wetu. Mifumo yetu ya mauzo ya mazao ya kilimo, ufugaji na uvuvi bado yana mlolongo mrefu toka mzalishaji mpaka mlaji, hivyo kumwachia mzalishaji kiasi kidogo sana cha thamani ya mazao yake, huku mlaji naye bado akiumizwa na bei kubwa. Kwa mfano jimboni kwangu Bumbuli tunasifika kwa kilimo bora cha mbogamboga na matunda yanayopendwa kwenye masoko makubwa yote ya Nairobi, Mombasa, Dar es Salaam na Zanzibar. Bahati mbaya sifa hii haiakisi manufaa tunayopata kama wakulima ingawa mboga zetu zinauzwa kwa bei kubwa sana katika haya

masoko kuliko mboga kutoka maeneo mengine nchini. Na hali hii ni katika mazao yote katika sehemu zote za nchi yetu.

Jitihada nyingi zimefanyika tangu uhuru katika kilimo, lakini kutokana na ukubwa wa sekta hii, matokeo bado ni finyu. Serikali ya Rais Kikwete imeweka kipaumbele kwenye kilimo kupitia sera kubwa kuliko zote toka uhuru wa nchi yetu ya Kilimo Kwanza inayojumuisha miradi mikubwa kama vile mradi wa kisasa kabisa SAGCOT. Sera hii ya Kilimo Kwanza imeundwa kutatua matatizo yote katika sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi na kuongeza tija ya shughuli za kilimo kwa wakulima na uchumi wa taifa letu kwa ujumla. Pamoja na hayo, bado kunahitajika uwekezaji zaidi katika miundombinu ya vijijini, pembejeo, mashine na teknolojia za kisasa. Miundombinu kama barabara, umeme, maji, simu na masoko ni muhimu ili kuunganisha wazalishaji na masoko makuu ya mazao mijini na duniani kote. Mipango ipo lakini changamoto kubwa imekuwa ni rasilimali na usimamizi wa utekelezaji.

Kizazi kipya cha uongozi wa nchi kina jukumu kubwa la kuleta maarifa mapya katika kilimo yatakayotuondoa kwenye kauli ya mapinduzi ya kilimo na kutupeleka kwenye vitendo.

Bila kufuta mipango mizuri iliyopo sasa, napendekeza kuharakisha mambo makuu manne ili kuleta mapinduzi kwenye sekta hizi.

Kwanza, napendekeza kulishughulikia suala la ardhi. Ardhi, kwa maana ya umiliki na matumizi yake, ndio msingi wa yote. Hakuna maendeleo ya kilimo kama hakuna uhakika wa matumizi bora ya ardhi na kama hakuna uhakika wa mfumo wa umiliki wa ardhi. Lazima sasa kuondoa migogoro ya ardhi isiyoisha kati ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na Serikali na kuipa ardhi thamani halisi inayostahili. Ni wakati sasa inabidi tufanye maamuzi makini na ya busara kuhahakikisha kuwa tunatenga maeneo mahususi kwa ajili ya matumizi mahususi, yaani maeneo ya kilimo, ufugaji, vijiji na miji, yatakayolindwa kisheria. Katika nchi yetu, tumetenga eneo kubwa, takriban asilimia 40 ya eneo la nchi yetu kwa mbuga na hifadhi ya wanyama na misitu. Na maeneo haya yametengwa kisheria na mipaka yake inatambulika kisheria. Huwezi kulima au kuchunga ng'ombe kwenye hifadhi ya wanyama. Hata hivyo, maeneo ya shughuli muhimu za kilimo na mifugo maeneo yake hayajatengwa wala kulindwa kisheria.

Kama tunavyolinda hifadhi za misitu na mbuga za wanyama lazima maeneo ya kilimo na mifugo nayo yawe hivyo. Lazima wakulima wamiliki ardhi yao kisheria, na ni lazima kutenga maeneo maalumu ya wafugaji

yanayomilikiwa na wafugaji kisheria na bila kusahau korido mahususi za kupitisha mifugo kutoka upande mmoja wa nchi mpaka mwingine.

Siri ya maendeleo ya ufugaji ni kuwa na kuuza ng'ombe walionenepa. Hawa wanapatikana kwa namna mbili: aina ya mbegu ya ng'ombe wenyewe na uwepo wa malisho ya kutosha wakati wote. Huwezi kupata maendeleo ya mifugo kama huendelezi malisho. Kuswaga ng'ombe kwa kubahatisha hakuwezi kumuendeleza mfugaji. Hili lazima tulibadilishe na kumuwezesha mfugaji.

Ardhi ambayo haijapimwa ndio chanzo kikubwa cha migogoro. Tumejaribu kupima maeneo mengi nchini lakini kasi ni ndogo na bajeti haitoshelezi.

Napendekeza matumizi ya teknolojia ya satellite katika kupima na kupanga matumizi ya ardhi nchini. Kila kipande cha ardhi katika nchi yetu kiwe kimepimwa, kina hati na matumizi yake yanajulikana.

Kinachohitajika ni kufanya uamuzi na kusimamia utekelezaji. Tukifanikisha hili, tutarahisisha usimamizi wa kitaalamu katika kilimo na ufugaji wa kisasa, huku tukiondoa vizingiti kwa mabenki kutoa mikopo nafuu kwenye kilimo na ufugaji.

Pili, tunahitaji kurekebisha mifumo ya usambazaji wa pembejeo za kilimo na kuziba mianya ya ubadhirifu unaoendelea hivi sasa. Kilio kikuu cha wakulima ni upatikanaji wa pembejeo, hasa mbegu, mbolea na madawa, kwa wakati, bei nafuu na ubora. Kuna udanganyifu mkubwa unaofanyika kwenye suala la usambazaji wa pembejeo na kuwasababishia wakulima hasara kubwa kila mwaka. Kizazi kipya cha uongozi kinahitaji kwanza kuweka usimamizi wa hali ya juu kwenye hili, kwa kuwawezesha wakulima kuweza kuripoti udanganyifu unaofanyika na kutoa adhabu kali kwa watendaji na wasambazaji watacaoendeleza ubadhirifu. Lakini pia tunahitaji kuhakikisha kwamba pembejeo zote muhimu, hasa mbolea na mbegu, zinatengenezwa na kupatikana hapa nchini na karibu zaidi na wakulima.

Kote walikofanya mapinduzi ya kilimo, utafiti wa kilimo na matumizi ya utafiti huo ilikuwa sababu kubwa ya mapinduzi hayo. Ndio maana Mwalimu Nyerere alianzisha taasisi kadhaa za utafiti wa kilimo, mifugo na uvuvi. Wanasayansi wetu wamefanya tafiti nyingi sana na wamevumbua mbegu bora za mazao na mifugo, madawa sahihi kwa hali na tabia ya nchi yetu na mifumo ya usindikaji na uhifadhi wa mazao ya kilimo, uvuvi na mifugo. Kizazi kipya kinahitaji kuongeza uwezo wetu wa utafiti na kuchukua utaalamu huu na kuufanyia kazi. Lazima kuhamisha utaalamu kutoka kwa watafiti kwenda kwa wakulima.

Tatu, na muhimu zaidi, tunahitaji masoko ya uhakika ya mazao yetu ya kilimo, ufugaji na uvuvi.

Kulima na kuvuna ni jambo moja, uhakika wa kuuza na kupata bei nzuri ni jambo jingine. Tuweke mazingira ambapo mkulima wakati anapanda mazao yake tayari anajua pa kuuza na ikiwezekana hata bei.

Hata hivyo, pamoja na kilimo chetu kuwa na tija na uzalishaji mdogo, bado hata hayo mavuno madogo imekuwa kwa nyakati nyingi ni shida kununuliwa. Na hata pale yanaponunuliwa, mkulima hupunjwa. Kilio cha masoko kimekuwa sasa ni wimbo wa muda mrefu. Lazima tukubali kwamba hatuwezi tukafanya mabadiliko yoyote kwenye kilimo bila kuwa na masoko ya uhakika ya mazao yetu. Uongozi wa kizazi kipya ulete mbinu mpya kuhakikisha kwamba mazao ya kilimo, ufugaji na uvuvi yanaongeza kipato cha kaya za Watanzania. Ili kufanikisha hilo lazima tufanye yafuatayo: kwanza, ni lazima tuwaunganishe wazalishaji na walaji moja kwa moja kwa kupunguza walaghai wengi katikati. Hapa mfumo wa taarifa za bei halisi za sokoni ungesaidia wakulima kutodanganywa kuhusu bei ya mwisho ya sokoni. Pili miundombinu na urahisi na uwezo wao wa kumfikia mlaji wa mwisho ungeongeza nguvu yao katika kukubaliana bei na mtu wa kati. Si haki rumbesa la kabeji lenye kabeji zaidi 50 likauzwa shilingi 10,000 kijijini kwangu Mahezangulu, wakati kabeji moja jijini inauzwa shilingi 500 mpaka 1,000. Pili, tunahitaji kuwekeza kwenye uhifadhi wa mazao baada ya kuvuna ili kulinda ubora wa mazao, kusaidia kupata bei nzuri na kupata mikopo kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani. Wakulima wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wanaweka bidii kubwa katika kilimo na wanavuna mahindi mengi sana kila mwaka lakini wanakosa pa kuyahifadhi na kuyauza na mwishowe wanaishia kuyauza kwa bei ya chini au kuozea chini. Huko nyuma tuliamua kwamba Serikali itanunua mahindi ya wakulima kupitia Hifadhi ya Taifa ya Chakula, lakini mara nyingi fedha zimekuwa zinachelewa, au wakulima kukopwa, au maghala kujaa wakati mazao mengi hayajanunuliwa.

Uongozi wa kizazi kipya unahitaji kuhakikisha kuwekezaji kwenye maghala ya kisasa, makavu na ya jokofu pia, kwenye kila tarafa, kuendana na aina ya kilimo kwenye tarafa hiyo, nchini kote ili kukidhi mahitaji ya mavuno husika. Maghala haya makubwa yatakuwa pia vituo vya usambazaji wa pembejeo na mahitaji muhimu kwa wakulima ikiwemo magunia. Tatu, ni kuanzisha haraka sana Mfumosoko wa Mauzo ya Mazao, yaani Commodities Exchange. Soko hili litasaidia wakulima kuwa na nguvu ya ufahamu wa bei halisi katika masoko hivyo kuweza kudai bei inayolingana na jasho la kazi zao.

Hakuna nchi yoyote iliyoweza kuleta mapinduzi ya kilimo bila kuwa na soko kama hili. Mfumo huu unahitaji miundombinu kadhaa mahsusi, ikiwemo maghala na mifumo ya Tehama, na bahati nzuri mazingira hayo sisi tunayo. Mipango ya soko hili imefanyika kwa miaka mingi sasa. Ni wakati sasa uongozi wa kizazi kipya kuanzisha soko hili, au kuingia ubia au kuiachia sekta binafsi kuanzisha soko hili. Mwisho, ni kuhakikisha kwamba tunaanzisha taasisi moja itakayopewa jukumu ya kutangaza bidhaa za mazao ya Tanzania duniani kote. Wenzetu wanaotegemea kilimo kama nchi za Kenya, Afrika Kusini na Brazil wana taasisi zenye nguvu sana duniani ambazo kazi yao ni kuhakikisha mazao ya nchi zao yanauzwa kwenye masoko yote muhimu duniani katika kiwango cha kimataifa.

Kwa mazao ambayo yana wanunuzi wachache wanaojulikana kila mwaka, mazao kama pamba, tumbaku na korosho, ipo haja ya kwenda mbele zaidi kwenye kuweka udhibiti wa kuhakikisha kwamba kanuni za soko huria hazikiukwi, kwa maana kwamba wanunuzi, aidha wawe vyama vyao vya ushirika au watu binafsi, hawali njama za kupanga bei ya chini kwa mkulima. Hapa Serikali inabidi iwe kali.



January Makamba akikabidhiwa zawadi ya mbuzi na mmoja wa wazee wa kijiji cha Kwebamba, Bumbuli Mzee Akida, katikati ni Ndugu Hoza, diwani na Katibu wa Mbunge na kushoto ni Ndugu Moka, Afisa Tarafa Mgwashi.

Pendekeo langu la mwisho, ni kuwapa uwezo wakulima, wavuvi na wafugaji uwezo wa kuongeza thamani ya mazao yao kabla ya kuyauza.

Kama nilivyosema hapo mwanzo, ni aibu, na hasara kubwa, nchi yetu inaposafirisha mazao kama korosho, pamba, kahawa, ngozi na samaki bila kuyaongezea thamani. Tunapouza India korosho ambayo haijabanguliwa, dunia inatucheka kwa sababu ya mambo matatu: kwanza, kazi ya kubangua korosho ni kazi rahisi na mashine zake hata SIDO zinaweza kutengenezwa; pili, tunakuwa tumepeleka ajira India; na tatu, tunakuwa tumeuza korosho kwa bei ya chini. Hili lazima libadilike. Kuuza nyama ya ng'ombe bila kuhakikisha unalipwa pia na pesa ya ngozi ni kujikosesha mapato. Vilevile, masoko na bei ya mazao ghafi hayana uhakika na hukumbwa na misukosuko mara kwa mara, wakati masoko na bei za bidhaa zitokanazo na mazao ni za uhakika na nzuri kila kukicha. Tusipowekeza kwa nguvu zote katika usindikaji na viwanda vya kuongeza thamani kwenye mazao yetu, tutaishia kuwa maskini na manamba wa nchi zenye viwanda. Kama nilivyosema hapo awali kwenye haya mazungumzo, Serikali inaweza kuweka mpango mahsusi wa upendeleo wa kikodi au vinginevyo kwa wakulima wanaowekeza kwenye shughuli ya kuongeza thamani ya mazao yao.

Ardhi, maziwa na bahari tunavyo vya kutosha. Hali ya hewa ni nzuri kwa kilimo na ufugaji wa aina yoyote. Kijiografia, tumejaaliwa kuwa katika njia kuu ya kuyafikia masoko yote muhimu, ndani ya Afrika na dunia nzima. Wataalamu na utaalamu wa kilimo, ufuguji na uvuvi wa kisasa tunao. Nguvu kazi ni ya kutosha kwani sisi ni Taifa changa la vijana. Tunachohitaji ni uongozi imara, wenye kuona fursa tulizonazo, na nia thabiti ya kufanya mapinduzi ya kilimo kwa kuwa na fikra mpya zinazoendana na dunia ya sasa – uongozi ambao huko nyuma haujawa sehemu ya wimbo wa mapinduzi ya kilimo. Ni lazima tuangalie upya mpangilio wa kitaasisi wa uendeshaji wa sekta ya kilimo ukizingatia kwamba sekta hii inagusa karibu kila wizara na inagusa kila kona ya nchi yetu. Kama hakuna mpangilio, mgawanyo wa majukumu na uongozi thabiti tutaendelea kuwa na mipango inayoingiliana na inayojirudia na isiyokuwa na mwisho katika kilimo.

Ni lazima jamii za wafugaji wetu ziishi maisha mazuri kulingana na utajiri mkubwa wa mifugo walio nao. Ni lazima wavuvi wetu waongeze kipato chao marudufu kwa kuongeza ufanisi na kupata soko na bei la uhakika. Na mwisho, ni lazima turudishe heshima na utajiri kwa wakulima kama ambao unaendana na jasho la kazi zao.

14

Tanzania imekuwa ikisifika kwamba uchumi wake unakua kwa kasi kwa miaka kadhaa sasa. Lakini wananchi wengi bado hawajaona hayo manufaa. Nini kifanyike wananchi nao waone na wanufaike na uchumi kukua? Unaelezeaje uchumi wetu kwa ujumla?

Nimepata fursa ya kuujua vizuri uchumi wa nchi yetu kutokana na kazi nilizofanya huko nyuma na kusoma nyaraka za Baraza la Mawaziri na kuhudhuria vikao vya Baraza la Mawaziri kwa miaka mitano kama Msaidizi wa Rais ambapo mijadala na maamuzi kuhusu uchumi ilifanyika. Labda tuanze na tafsiri. Tunaposema uchumi unakua tunamaanisha Pato la Taifa linaongezeka mwaka hadi mwaka. Na Pato la Taifa ni thamani ya shughuli zote za uchumi – biashara, uzalishaji, huduma, na nyinginezo – katika kipindi cha miezi kumi na miwili. Kwa vipimo hivi, thamani ya shughuli za uchumi kwenye nchi imekuwa inaongezeka kwa kasi ya kuridhisha mwaka hadi mwaka. Kwa hiyo viongozi wetu wanaposema uchumi wetu unakua wako sahihi na ni jambo jema na la fahari kwamba uchumi unakua. Na uchumi haukui wenyewe tu bali kwa jitihada na sera sahihi. Zipo nchi ambazo thamani ya shughuli za uchumi haiongezeki au inashuka kabisa.

Lakini pia ni kweli kwamba wananchi wengi hawajaona manufaa ya ukuaji huu katika maisha yao ya kila siku. Na sababu zipo mbili:

Kwanza, shughuli za uchumi zilizokua kwa kasi katika miaka kumi na tano iliyopita ni zile ambazo hazijawagusa au haziwahusishi watu wengi – kwa maana ya ajira na kipato. Kwa mfano, mtaji uliowekezwa kwenye sekta ya madini ni mkubwa na mtaji huo umejumlishwa kwenye mchango wa Pato la Taifa, hivyo kuleta taswira ya ukuaji wa kasi wa uchumi, lakini ajira, kodi na manufaa mengine hayakuwa makubwa sana. Kwa kifupi ni kwamba uchumi wetu umepanuka katika sekta ambazo haziwagusi wananchi wengi moja kwa moja.

Shughuli ambazo zinawagusa au zinawahusisha watu wengi ni kilimo cha mazao, mifugo na uvuvi – shughuli ambazo zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania wanajihusisha nazo. Lakini ukitazama kasi ya ukuaji shughuli hizi, bado sio ya

kuridhisha. Kwa mfano kwa miaka kumi mfululizo sasa, mchango wa shughuli za uvuvi kwenye Pato la Taifa haujawahi kuvuka asilimia 1.5 kwa mwaka wakati tuna eneo kubwa la bahari, tuna maziwa makubwa na mito mingi na tuna watu wengi sana wanajishughulisha na uvuvi. Shughuli za mifugo nazo, mchango wake kwenye Pato la Taifa haujawahi kupita asilimia 5 kwa mwaka kwa miaka kumi mfululizo, licha ya Tanzania kuwa nchi ya tatu Afrika kwa kuwa na mifugo mingi. Shughuli za kilimo cha mazao, nazo ukuaji wake haujawahi kuvuka asilimia 6 kwa miaka kumi sasa licha ya eneo kubwa la kilimo na hali nzuri ya hewa na mabonde ya umwagiliaji tuliyo nayo yanayoruhusu kilimo cha mazao mengi kwa nyakati tofauti. Licha ya ukuaji huu mdogo, bado kilimo cha mazao kimechangia kwenye Pato la Taifa kwa wastani wa asilimia 19 kwa mwaka kwa miaka kumi sasa.

Naweza kusema hapa dhahiri kwamba kama shughuli za kilimo cha mazao, uvuvi na ufugaji na biashara ndogondogo vikikua kila moja kwa asilimia 10 tu kwa mwaka kwa miaka 10 mfululizo, basi tunaweza kumaliza umaskini katika nchi yetu. Na tukipanua sekta ya viwanda na kuongeza ajira na mauzo ya mazao yaliyosindikwa sisi hatuwezi kuwa nchi ya kutegemea misaada tena. Na haya yote yanawezekana.

Kwa hiyo kwa upande wangu suluhisho kubwa la watu kuona manufaa kwenye ukuaji wa uchumi ni kuwekeza kwenye ukuaji wa shughuli zinazowagusa au kuwahusisha watu wengi, kama vile kilimo cha mazao, biashara ndogo na za kati, uvuvi, ufugaji, utalii, uzalishaji viwandani, na ujenzi. Hapa ndipo ukuaji wa uchumi unaweza kuakisi ukuaji wa kipato cha Mtanzania wa kawaida.

Ninapendekeza kutengeneza chachu mpya ya uchumi, au economic stimulus, na kwa namna kubwa kuchochea ukuaji wa shughuli za uzalishaji mali zinazowagusa watu wengi zaidi.

Katika kipindi cha miaka karibu kumi na tano iliyopita, Serikali imefanya kazi kubwa na nzuri ya kuwekeza fedha nyingi kwenye sekta za huduma za umma, hasa afya, maji, na elimu. Uwekezaji huu umesaidia kuboresha huduma za jamii na kujenga rasilimali watu. Pia fedha nyingi zimewekezwa kwenye huduma kuu mbili za uchumi, barabara na umeme. Serikali ijayo ina wajibu, kwanza kuimarisha mafanikio hayo, lakini kubwa zaidi ni kuwekeza kwenye kujenga uwezo wa uzalishaji mali hasa kwenye kilimo, uvuvi, ufugaji na viwanda. Ukuaji wa uchumi hauwezi kuwa na tija kwa wananchi wa kawaida kama mfumo wa uchumi unawafanya wawe wachuuzi, vibarua au vijakazi. Lazima tuwe

wazalishaji mali, lazima tuumiliki uchumi wetu, ili tunufaike na ukuaji wa uchumi wetu.

Baadhi ya mipango hii ipo, wajibu wa serikali ijayo ni kuiboresha, kuipanua na kuitekeleza kwa uharaka mpya, maarifa mapya, na nidhamu mpya.

Fikra yangu mimi ni kwamba katika kila eneo la nchi yetu, tuanzishe programu kubwa za kukopesha au kutoa kwa ruzuku kwa mitaji na zana za uzalishaji mali kama vile nyavu, boti, matrekta, mbegu bora, pampu za kumwagilia, mitambo ya kuongeza thamani mazao ya kilimo, mitamba ya ng'ombe wa kisasa, mashine za kutotoa vifaranga, na mashine na mitambo mbalimbali moja kwa moja kwa wazalishaji mali.

Moja ya changamoto kubwa kwenye uzalishaji mali hasa wa kilimo ni upatikanaji wa masoko ya uhakika, kwamba wakulima wanalima kwa bidii kubwa lakini hawana pa kuuza kwa bei inayostahiki. Hivyo program za kuongeza uwezo wa uzalishaji mali lazima ziende sambamba na upatikani wa masoko na bei za uhakika. Uwekezaji ule ule tuliouweka kwenye upanuzi wa sekta ya elimu, kwa mfano, tukiuweka kwenye kujenga uwezo wa kuzalisha mali, tutapiga hatua kubwa kwenye kuwezesha Watanzania wengi kukuza kipato na kuumiliki uchumi wao.

Lakini jingine ni huduma kwa uchumi. Uchumi lazima uhudumiwe ili ukue na watu wanufaike. Zipo sekta kadhaa – ambazo zenyewe ni shughuli za uchumi lakini pia ni viwezeshi, yaani huduma, kwa shughuli nyingine za uchumi. Sekta hizo ni uchukuzi, kwa maana ya bandari, reli, barabara na usafiri wa anga; huduma za fedha, kwa maana ya upatikanaji rahisi na kwa unafuu wa mikopo ya biashara; nishati, kwa maana ya upatikanaji wa umeme wa uhakika na gesi viwandani kwa bei nzuri; mawasiliano, kwa maana ya huduma bora za simu na miundombinu ya TEHAMA; na huduma za utawala, kwa maana uwezo na weledi wa serikali kuwezesha biashara kuanzishwa na kuendeshwa bila vikwazo vya rushwa na urasimu, pamoja na usimamizi bora wa uchumi au sound economic management, ikiwemo sera wezeshi na rafiki kwa biashara na uwekezaji. Sekta hizi zinazohudumia uchumi ni muhimu sana ziwe bora na imara.

Kazi nzuri sana imefanywa na viongozi waliopita na wa sasa ya kuweka misingi mizuri ya uchumi, au *economic fundamentals*, misingi inayowezesha mazingira ya uchumi kukua. Kazi hii inabidi iendelezwe kwa nidhamu ya hali ya juu. Yapo mambo kadhaa katika kuhudumia uchumi ambayo tukiyaweka sawa, tunaweza kupiga hatua.

Jambo la kwanza ni lazima tulishughulikie ni usafirishaji, hasa bandari na reli. Haihitaji weledi wa hali ya juu kutambua kwamba, kwa jiografia ya nchi yetu, tukirekebisha bandari na reli zetu, vitachangia zaidi ya nusu ya mapato ya nchi yetu. Na ukitazama kwa kina takwimu zetu za uchumi, utaona kwamba mapato tunayopata kwa kupitisha bidhaa za nchi jirani katika miundo mbinu yetu yaani transit trade karibu yanalingana na mapato tunayopata kwa kuuza mazao yetu yote ya kilimo nje ya nchi. Hebu fikiria kama tungeongeza ufanisi wa bandari na reli kwa asilimia 50 tu, tungekuwa wapi?

Pili, katika kuhakikisha kwamba uchumi wetu unamilikiwa na kuwanufaisha Watanzania wote, hatuna budi kuikabili rushwa kwa nguvu zote. Rushwa ni adui wa haki. Lakini rushwa pia inaathiri shughuli za uwekezaji, biashara, na uchumi kwa ujumla. Moja ya vikwazo vikubwa vya maendeleo ya nchi yetu ni rushwa na wizi sio tu wa mali za umma pia na kwenye sekta binafsi. Uchumi wetu ungeweza kunawiri kuliko ilivyo sasa kama tungeweza kudhibiti rushwa na wizi. Wafanyabiashara wanaathirika sana na wizi unaofanywa kwenye biashara zao. Rushwa inapogusa maeneo yanayohusu uchumi ni tendo la uhujumu uchumi na lazima ichukuliwe kwa uzito huo.



January Makamba akihutubia ndani ya Bunge.

Bila kudhibiti rushwa na wizi hatuwezi kupata maendeleo. Kwa hiyo, kwa kiongozi yoyote, kama anataka kuacha rekodi nzuri ya maendeleo, kuitokomeza rushwa ni jambo la kufa na kupona.

Tatu, ni kutekeleza kwa kasi na kuanzisha miradi mikubwa ya ujenzi wa viwanda mama, yaani viwanda ambavyo vinawezesha maendeleo ya viwanda vingine au shughuli nyingine za uchumi. Viwanda hivi ni vya chuma, simenti, mbolea na ufuaji wa makaa ya mawe. Bahati nzuri malighafi zipo, mipango ipo na wawekezaji wapo. Cha msingi ni kuongeza kasi na nidhamu ya utekelezaji. Kwa upande wa viwanda vya mbolea, malighafi kubwa ni gesi asilia. Na ili viwanda hivi viwe na faida na mbolea ipatikane kwa bei nafuu, lazima bei ya gesi iwe chini ya ile inayouzwa sasa kwa ajili ya kuzalisha umeme. Suala la bei ya gesi kwa sasa limekwamisha kujengwa kwa viwanda vya mbolea kwa sababu pamoja na kwamba gesi ipo kwenye ardhi yetu lakini hatuna sauti katika kupanga bei yake. Haikubaliki nchi yetu kuendelea kuagiza mbolea wakati tuna malighafi za kutosha kuzalisha mbolea. Mapinduzi ya kilimo hayawezi kuletwa kama tunaagiza sehemu kubwa ya mbolea nje ya nchi na inamfikia mkulima kwa shida na kwa bei kubwa. Hili linaweza kumalizwa mapema kabisa.

Pia nizungumzie jambo jingine la jumla kuhusu uchumi. Majuzi nilikuwa natazama kitabu cha taarifa ya hali ya uchumi wa taifa na nikaona takwimu kwamba mwaka 2013, tumeuza nje huduma na bidhaa za thamani ya dola bilioni 6 na tumeagiza kutoka nje bidhaa na huduma za thamani ya dola bilioni 11. Hapa kuna nakisi ya dola bilioni 5. Hii ni kubwa sana. Kiasi cha akiba ya fedha za kigeni tulichonacho ni mojawapo ya viashiria muhimu vya uimara wa uchumi na sarafu yetu. Kwa hiyo, moja ya vipaumbele vikubwa kwenye uendeshaji uchumi ni kupunguza hii nakisi. Bidhaa zinazoongoza kwa kuagizwa kutoka nje ya nchi ni mafuta ya magari na mitambo, mashine na mitambo, lakini pia na mafuta ya kula. Ni changamoto kudhibiti kuagiza mafuta ya magari na mitambo kwa sababu hatuzalishi mafuta hapa nchini na kwa kadri uchumi wetu unavyopanuka ndivyo mahitaji ya mafuta yanaongezeka. Lakini tunaweza kupunguza kuagiza mafuta haya. Sehemu kubwa ya mafuta haya yanatumika kwenye kuzalisha umeme, kwa hiyo tukiharakisha kuzalisha umeme kwa kutumia gesi, makaa ya mawe na vyanzo vingine mbadala kama jua, upepo na joto-ardhi, tutapunguza kuagiza mafuta kutoka nje na hivyo kuwa na akiba kubwa zaidi ya fedha za kigeni na kuimarisha sarafu yetu. Lakini sio siri kwamba kuna udanganyifu mkubwa sana kwenye sekta ya mafuta. Nilipokuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini tuligundua changamoto nyingi na tulipendekeza majawabu. Yapo mafuta mengi hayalipiwi kodi, yapo mafuta mengi ambayo thamani iliyoandikwa kwenye makaratasi ya kuyaingiza nchini ni kubwa kuliko gharama halisi za mafuta yenyewe, yaani



January Makamba akiwafunda vijana wasomi wa CCM ikiwa ni moja kati ya majukumu yake aliyopewa na Kamati Kuu ya Chama kama Mlezi wa Shirikisho la CCM la Vyuo Vya Elimu ya Juu katika ukumbi wa Karimjee jijini Dar es Salaam.

over-invoicing na yapo mafuta mengi yanayoingizwa nchini kwa ajili ya kwenda nchi jirani lakini yanaingia kwenye soko letu. Ni dhahiri kabisa kwamba hii ni njia mojawapo ya kuiibia Serikali na kutorosha fedha za kigeni nje ya nchi.

Tukiidhibiti na kuisimamia vizuri sekta ndogo ya uagizaji mafuta tutaokoa fedha nyingi za kigeni na kuongeza mapato ya Serikali. Mafuta ni bidhaa muhimu sana kwa uchumi na usalama wa nchi. Sote tunakumbuka jinsi nchi ilivyosimama



mwaka 2011 kwa sababu ya tatizo kwenye uagizaji mafuta. Moja ya mambo tuliycopendekeza wakati ule kwenye Kamati ya Nishati na Madini ni kuwa na Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta Nchini, yaani National Strategic Petroleum Reserve, na kuna maarifa mengi mapya ya kuiendesha bila kuathiri biashara huria ya mafuta. Nchi haipaswi kuishiwa vitu viwili: chakula na mafuta. Mafuta yaliyopo nchini kwa wakati mmoja yanapaswa kutosheleza mahitaji ya zaidi ya miezi mitatu hata kama yasipoingizwa mengine.

Kwa upande wa uagizaji wa mafuta ya kula, haipendezi kabisa nchi kama yetu yenye uwezo wa kuwa na viwanda vya mafuta ya kula kutumia mabilioni, tena fedha za kigeni, kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi. Tunaweza kuzalisha mafuta haya hapa nchini na hata kuuza nje ndani ya miaka mitano. Kinachohitajika ni shamba la miti ya mawese la ekari 30,000 na kiwanda cha kuchakata mawese. Uwezekano wa kupata shamba hilo upo kwa sababu ardhi ipo na mawese yanastawi maeneo mengi ya nchi yetu. Na tukifanya hivyo, tutazalisha ajira maelfu, tutazalisha bidhaa nyingine za mawese kama vile sabuni, mafuta ya mitambo na umeme. Lakini pia tunaagiza sukari na ngano kutoka nje ya nchi kwa fedha nyingi za kigeni. Tunaweza kujitosheleza kwa ngano, sukari, na mchele na kuweza kudhibiti nakisi kubwa tuliyonayo na kujihakikishia usalama wa chakula. Lakini pia tunaweza kuuza nje bidhaa za viwandani na huduma zaidi. Pia tunaweza kupata zaidi fedha za kigeni kwenye utalii kuliko sasa kwa kutangaza zaidi vivutio vyetu na kuweka mazingira rahisi kwa wageni kuja na kutumia pesa zao za kigeni hapa nchini.

Hata hivyo, tunapaswa kuitazama upya dhana ya kutegemea uchumi wa kuuza bidhaa, hasa bidhaa ghafi, nje ya nchi. Tunaona nchi nyingi uchumi wake unadondoka ghafla kutokana na utegemezi huu – kwa sababu soko na bei za bidhaa hizi zinabadilika mara kwa mara. Tunao uwezo wa kuuza nje huduma na bidhaa zaidi ya bidhaa ghafi na pia tunalo soko kubwa la ndani la kukidhi mauzo ya kutosha kuwa na uchumi imara. Jawabu ni kuimarisha viwanda na ni jawabu la ajira pia. Pia tunaona jinsi uchumi wa baadhi ya nchi unavyotetereka kwa sababu wahisani wamesimamisha au kuchelewesha misaada. Kwa hiyo, naamini katika kujenga uchumi imara wa nchi yetu kujitegemea bado ni jambo la msingi sana. Yote haya tunayaweza.

Pia fikra yangu nyingine ya jumla kuhusu uchumi ni kwamba uchumi wa nchi unapaswa kuendeshwa na kusimamiwa kwa karibu zaidi na taasisi na watendaji waliowezeshwa kuwa na nguvu na mamlaka ya kufanya hivyo kwa weledi. Ni muhimu dira na mwelekeo wa jumla wa uchumi ikubalike na ijulikane wazi – na kwetu sisi Tanzania tunayo Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 ambayo inatuelekeza tuwe taifa la namna gani ifikapo 2025. Ni Dira nzuri na yenye malengo mazuri. Dira hii ilitengenezwa mwaka 1998 wakati kukiwa na mazingira tofauti kabisa ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Tangu mwaka 1998, dunia na nchi yetu imebadilika sana na darubini na maarifa au assumptions zilizotumika kutengeneza Dira hiyo zitakuwa zimepitwa na wakati. Ni wakati sasa wa kuitazama na kuipitia tena upya Dira ile na kutengeneza mpya inayoendana na mazingira ya sasa.

Katika kujenga uchumi imara na wa kisasa, taasisi za kusimamia uchumi zijue na zitimize wajibu – na ziwe na uwezo na umahiri wa kusimamia uchumi. Sisi tunazo taasisi muhimu tatu za usimamizi wa uchumi: Wizara ya Fedha, Tume ya Mipango, na Benki Kuu. Mahusiano na muingiliano baina ya taasisi hizi, nani anaamua nini na kwa wakati gani, na mahusiano na muingiliano kati ya taasisi hizi na nyingine za Serikali pia ni muhimu. Muhimu zaidi ni mahusiano kati ya sekta binafsi na taasisi hizi za menejimenti ya uchumi.

Uchumi ambao haupangwi na kusimamiwa vizuri ni uchumi ambao umepangwa kutostawi. Mwenendo wa uchumi ni jambo linalopaswa kufuatiliwa na viongozi wa umma kila siku.

Uendeshaji uchumi sio kama mapishi ya makande, kwamba ukishachanganya mahindi na maharage na maji ya kutosha, basi unasubiri tu yaive na huna haja ya kuchungulia chungu kila mara. Kwa hiyo, kwa viongozi wa nchi, ni muhimu sana kuweka mpangilio wa kitaasisi na utaratibu wa usimamiaji na uendeshaji wa uchumi ili kufanya maamuzi sahihi na ya wakati yanayozingatia picha halisi na ya jumla ya uchumi wa nchi.

Kama sasa tulivyo na Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa linalojumuisha viongozi wa taasisi, idara na wizara zinazosimamia ulinzi na usalama, napendekeza kuwe na Baraza la Uchumi la Taifa, kwa lugha nyingine National Economic Council, chini ya uenyekiti wa Rais, litakalojumuisha idara, taasisi na wizara zinazohusika na uchumi, pamoja na sekta binafsi.

Wajibu wa Baraza hili utakuwa ni kuratibu na kufuatilia maendeleo ya uchumi mpana wa nchi kuhakikisha kwamba juhudi za wadau wote zinaelekezwa kwenye lengo moja na changamoto katika mwenendo wa uchumi zinatambuliwa na kutafutiwa ufumbuzi haraka.

Uchumi wa Tanzania lazima umilikiwe na Watanzania wenyewe.

Zipo fikra kadhaa zinazoweza kufanikisha jambo hilo, kwa mfano biashara na uwekezaji inayoweza kufanywa na wafanyabiashara wa kitanzania, basi ufanywe na wafanyabiashara wa Wakitanzania lakini bila kuzuia au kuathiri uingizwaji wa mitaji ya wawekezaji au wafanyabiashara kutoka nje. Iwepo mipango na mikakati mahsusi ya uwezesaji wa wafanyabiashara wetu kushindana. Serikali inao wajibu wa kuona fahari ya kutengeneza mabilionea wa Wakitanzania ambao watawekeza fedha zao hapa, watatengeneza ajira, kulipa kodi, kuendeleza nchi yao.

Mwisho, katika yote ninayoyapendekeza kuhusiana na uchumi, azma yetu lazima iendelee kuwa ya kujenga uchumi imara utakaokidhi majukumu yetu ya msingi kama taifa, uchumi unaowashirikisha na unaotoa fursa kwa Watanzania wote, wa hali zote, wa kizazi cha sasa na kijacho na kuwawezesha kumudu maisha yao na kutimiza ndoto zao, na uchumi unaotupeleka kuwa taifa linalojitegemea.



January Makamba akisalimiana na mlemavu wa viungo katika moja za mikutano ya kuimarisha uhai wa CCM nchini.

15

Mwaka jana nilisoma kwenye vyombo vya habari kwamba ulipata tuzo ya taasisi ya National Democratic Institute ya Marekani, unaweza kutueleza ni tuzo ya nini na kwa nini ulipata? Pili, tulisoma kwamba uliteuliwa na taasisi ya *World Economic Forum* kuwa mmoja wa viongozi vijana mashuhuri duniani (*Young Global Leaders*). Pia tena majuzi tukasoma kwamba jarida mashuhuri duniani la *Forbes* limekutaja kuwa mmoja wa watu kumi wenye ushawishi Afrika kwa mwaka 2014. Ni kwanini unadhani wanakupa hizi tuzo? Na je, tuzo hizi zina maana gani kwa wapiga kura wako?

Nina tatizo kidogo na moja ya swali lako lakini ngoja nianze na hii tuzo ya *National Democratic Institute*. Hii ni taasisi mashuhuri duniani inayosimamia masuala ya uongozi na demokrasia. Kwa sasa inaongozwa na Waziri Mstaafu wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mama Madeline Albright. Katika kuadhimisha miaka ya 30 ya Taasisi hiyo, walitoa zawadi kwa watu mbalimbali duniani wanaofanya vizuri katika nyanja mbalimbali za demokrasia. Tuzo niliyopewa mimi inaitwa *Democracy Award* ambayo nilishinda kutokana na ubunifu wa kutengeneza mfumo wa kuwasiliana na wapiga kura wangu wa Bumbuli kwa kutumia SMS. Tuzo hii nilishinda pamoja na Rais wa nchi ya Estonia na mwanzishaji na mmiliki wa mtandao wa kijamii wa *Twitter*, Jack Dorsey. Nilipewa heshima ya kuzungumza katika halifa hiyo iliyokuwa na viongozi wakubwa katika Serikali ya Marekani. Ilikuwa heshima kubwa kwasababu huko nyuma waliopata kushinda tuzo hii ni pamoja na Kofi Annan na Desmond Tutu.

Kuhusu heshima ya Taasisi ya *World Economic Forum* ya kuwa mmoja wa viongozi vijana duniani, nadhani wao wana vigezo vyao lakini ninachofahamu ni kwamba kuna jopo ambalo linaongozwa na viongozi mashuhuri duniani ambao ndio wanapokea mapendekezo mbalimbali kutoka dunia nzima na mwishowe kuchagua vijana wachache. Ni heshima kubwa pia kwasababu wanaoshiriki kwenye shughuli za *World Economic Forum* ni watu wakubwa na mashuhuri sana duniani. Baadhi ya vijana mashuhuri waliowahi kupata heshima hii ni pamoja na Rais Joseph Kabila.



January Makamba akipokea Tuzo ya Ubunifu Katika Demokrasia kutoka kwa Waziri mstaafu wa Mambo ya Nje wa Marekani Bi. Madeleine Albright Jijini Washington DC Disemba 2013.

Kuhusu taasisi ya Askofu Tutu na yenyewe ni kama hiyo hiyo ya *World Economic Forum* isipokuwa hii ya Tutu inachukua vijana viongozi kutoka Afrika pekee.

Hii ya majuzi ya jarida la *Forbes* kwamba mimi ni mmoja wa Waafrika wenye ushawishi mkubwa, hata mimi sikuitegemea. Nao pia wanachukua kura ya maoni kutoka kwa watu mbalimbali duniani. Jarida hili linasomwa sana na kuheshimika duniani kwahiyo ni heshima kubwa kwangu, kwa watu wa Bumbuli.

Kwa kweli sababu zinazopelekea watu hawa kunipa heshima na tuzo hizi, wanazijua wenyewe. Mimi nafarijika kwamba kazi ninayofanya na jinsi mimi mwenyewe nilivyo na ninavyohusiana na watu wengine ni mambo yanayokubalika na kutambulika na watu wengi na taasisi nyingi kote duniani hata kama baadhi ya wenzangu hapa hawaoni hivyo.

Lakini kuna faida kubwa ya kiuongozi kuhusishwa na tuzo na heshima hizi. Heshima za Tutu na ya *World Economic Forum* zina programu za mwaka mzima ambazo zinatoa fursa na kujumuika na na kujifunza mengi kutoka kwa viongozi mashuhuri duniani katika kila nyanja za serikali na sekta binafsi. Ninaweza kusema kwamba, kwa kupata fursa hizi, nimejifunza mengi, kwanza nimefahamiana na kutengeneza urafiki na watu wengi mashuhuri wanaofanya mambo makubwa duniani, pili, nimepanuka fikra, upeo na weledi katika nyanja ya uongozi, tatu, nimeweza kuiweka Bumbuli katika nyoyo na fikra za watu wengi maarufu na taasisi mashuhuri duniani.

Hizi tuzo ni heshima na kutambulika tu na wala sio nyenzo ya kisiasa. Sidhani kama zina msaada wowote wa kisiasa. Huwezi kwenda kwa watu wa Manga, Funta kule Bumbuli ambao wana shida ya maji halafu ukawaeleza habari ya jarida la *Forbes*. Bado kazi ya kutafuta majawabu ya matatizo ya watu waliotuchagua iko pale pale. Hata hivyo, heshima hii inatokana na wao kuwa wa kwanza kuniona nafaa kuongoza.



Rais Kikwete akifurahia jambo na January Makamba wakati wa ziara ya Rais katika Jimbo la Bumbuli mwaka 2014. Kushoto ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tanga Ndugu Henry Shekifu. Katika ziara hiyo, Rais Kikwete alizungumzia kusikia habari za kugombea Urais kwa January na kusema kwamba anamtakia heri na kwamba Mungu ndio anaamua na kwamba kama wakati wake umefika, hata watu wapinge vipi, atafanikiwa. Na kama wakati wake haujafika, hatafanikiwa na asipofanikiwa asife moyo.

16

Kama kiongozi kijana uliyepata kufanya kazi katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ikulu, unazungumziaje nafasi ya Tanzania katika siasa za kimataifa?

Nianze kwa kusema kwamba Tanzania ni moja ya nchi zinazoheshimika duniani. Viongozi wetu wamefanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba heshima ya nchi yetu inabaki kuwa juu.

Mzee Mkapa, wakati akiwa Rais, na Rais Kikwete, wakati akiwa Waziri wa Mambo ya Nje, waliasisi Sera Mpya ya Mambo ya Nje, ambayo imejikita katika diplomasia ya kiuchumi. Sera hii imetusaidia sana katika kuongeza washirika wa maendeleo wa nchi yetu na kuongeza mitaji inayoingia nchini mwetu kwa uwekezaji. Hili ni jambo jema sana na lazima tuendelee nalo. Hata hivyo, imani yangu ni kwamba lazima pia tuendelee na msukumo wa diplomasia na siasa yetu kimataifa unaojikita katika kutafuta haki na usawa na heshima baina ya mataifa na watu wa mataifa, kushiriki katika jitihada za kutafuta na kulinda amani, ikiwemo msukumo mpya wa kutuma askari wetu wengi zaidi kwa kadri inavyowezekana kushiriki kwenye majeshi ya kimataifa ya kulinda amani ili kuyajenga majeshi yetu katika hali ya usasa na utayari lakini pia kama njia ya ziada ya kipato kwa askari wetu na Jeshi letu.

Vilevile, kuendelea na harakati za kuwezesha kuwepo mfumo wa uchumi na biashara duniani wa haki na usiokandamiza nchi changa; kuendelea na harakati za kujenga msingi wa nchi maskini kushirikiana zaidi ikiwemo kufanya biashara zaidi baina yetu; lazima tuendelee na harakati za kurekebisha taasisi za utawala wa siasa za kimataifa zizingatie matakwa na maslahi ya mataifa mengi zaidi; lazima kuendelea kupambana na ukoloni-mamboleo ambao kila kukicha unachukua sura mpya ikiwemo kuhusisha misaada kwa nchi yetu na maslahi ya kibiashara ya mashirika ya nchi zinatoa misaada hiyo, kupewa masharti ya kupata misaada isiyo na msingi, na mashinikizo ya kufuata sera na kuchukua misimamo isiyo na manufaa kwa nchi yetu.

Kipaumbele pia ni mahusiano mazuri na ya kidugu na majirani zetu. Hili ni la msingi sana. Usalama na ustawi wa nchi unategemea ni jinsi gani unaishi na majirani zako. Tunategemeana na majirani kwenye mambo mengi. Hawa ndio

tunafanya nao biashara zaidi. Watu wetu, hawa wa mipakani, wanatembeleana zaidi na wengine ni kabila au ndugu. Lazima kufanya jitihada za makusudi kuimarisha uhusiano mwema na jirani. Pia na ushiriki wetu wenye tija na manufaa kwetu kwenye taasisi za kikanda, kwa maana ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Umoja wa Nchi za Kusini mwa Afrika na Umoja wa Afrika.

Tanzania ni nchi kubwa kuliko nchi zote za Afrika Mashariki. Tuna historia adhimu ya ujenzi wa Umoja wa Afrika na tulikuwa tayari kuchelewesha uhuru wetu ili tuupate siku moja na nchi za Kenya na Uganda ili tuunde nchi moja. Tanzania ni taifa pekee Afrika inayotokana na muungano wa nchi mbili huru. Tanzania ni nchi pekee iliyokuwa na ukarimu wa kupokea wageni wengi wakimbizi na wapigania uhuru, ni nchi iliyowahi kutoa uraia kwa Waafrika wenzetu wengi zaidi kuliko nchi nyingine. Historia hii na uthubutu huu unatupa nafasi ya sio tu ya kushiriki kikamilifu bali kuchukua uongozi kwenye kwenye mtangamano wa ukanda huu, hasa kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki bila kusita wala kuwa na mashaka.

Madhumuni ya msingi ya siasa yetu ya kimataifa lazima yaendelee kubaki yaleyale ya siku zote: kwamba nchi yetu isiwe na uadui na nchi nyingine yoyote duniani; kwamba nchi yetu na watu wake wawe na uhuru wa kujiamulia mambo yao na waheshimike kote duniani na wanufaike na mahusiano kati ya nchi yetu na nchi na taasisi mbalimbali duniani



January Makamba akiwa na Mheshimiwa Paulo Gomez, Mgombea Urais wa Guinea Bissau, wakati wa mahojiano na kituo maarufu cha luninga Afrika Kusini.

17

Tunaona jinsi nchi jirani zetu wanavyopata changamoto za usalama. Je, sisi tufanyaje kuepukana nazo?

Nasikitishwa na hali tete ya usalama inayoendelea katika nchi jirani. Tunapenda majirani zetu waishi katika amani na tunapenda ukanda huu uwe na amani na usalama. Ndio maana kwa miaka mingi nchi yetu imeshiriki katika jitihada za kupatikana amani kwenye nchi jirani. Usalama na amani ya nchi ndio msingi wa mambo yote. Bila amani, utulivu na usalama ni vigumu kupata maendeleo ya haraka.

Jukumu la kwanza na la msingi la Serikali, ambalo viongozi wa Serikali wana wajibu wa kulitimiza, ni kulinda mali na maisha ya wananchi na kuhakikisha kwamba nchi ina usalama.

Yapo matishio kadhaa ya usalama wa nchi yetu. Kabla hatujaongelea nini tufanye kuepukana na changamoto za usalama ni muhimu tukayatambua matishio hayo.

Tishio la kwanza la usalama ni migawanyiko ndani ya jamii – baina ya waumini wa dini mbalimbali, baina ya wakulima na wafugaji, baina ya vyama vya siasa, baina ya Wabara na Wazanzibari.

Tishio la pili la usalama ni changamoto katika upatikanaji wa haki. Kuna msembo ambao ni kweli kabisa, kwamba amani ni tunda la haki. Kama watu hawaamini kwamba mfumo rasmi wa kutafuta, kutoa na kupata haki unafanya kazi, watatengeneza njia zao za kutafuta haki na hili linaweza kuwa tishio la usalama wa nchi.

Tishio la tatu la usalama wa nchi yetu ni ugaidi. Bahati mbaya tumeshakuwa wahanga wa ugaidi katika nchi yetu. Ipo hatari kubwa ya kuongezeka kwa matishio haya. Tunaona jinsi majirani zetu wanavyohangaika na kudhibiti ugaidi. Kwakuwa ugaidi ni changamoto ya kidunia, na kwa sababu tupo kwenye zama za utandawazi, magaidi wakishindwa kuwapata wanaowalenga katika nchi zao, wanaweza kuwashambulia raia wao, uwekezaji wao na majengo yao

ambayo yapo nchini mwetu. Pia tunaona magaidi wenye mrengo wa kidini ambao wanajikita kwenye kushambulia viongozi na nyumba za ibada za dini nyingine. Jambo hili linachangia kuchochea mgawanyiko katika jamii.

Tishio jingine la usalama wa nchi yetu ni kuongezeka kwa matukio ya uhalifu wa aina mbili, kwanza uhalifu wa kutumia silaha, ikiwemo ujambazi na pili uhalifu wa kutumia mitandao au cybercrimes, ikiwemo wizi wa fedha kwenye mitandao ya mabenki na uingiliaji wa mitandao na mawasiliano nyeti ya Serikali na sekta binafsi. Tunazidi kuona ongezeko la tishio hili.

Tishio jingine la usalama ni tofauti kubwa ya kipato na maisha kati ya matajiri na maskini. Katika hali ya kawaida, hili lisingekuwa tatizo sana lakini pale maskini wanapoamini kwamba utajiri wa matajiri ndio sababu ya umaskini wao, kuna hatari ya mpasuko na tishio la usalama.

Tishio la mwisho la usalama wa nchi yetu ni rushwa. Rushwa, licha ya kuwanyima haki watu, lakini pia inaweza kutumika kununua taarifa nyeti za Serikali na kununua maamuzi, kutoka kwa viongozi wasio waadilifu, yanayoenda kinyume na maslahi ya usalama wa nchi.

Ziko namna tatu za kukabiliana na changamoto za usalama wa nchi yetu. Kwanza ni kisiasa na kijamii. Viongozi wa kisiasa na kijamii wanao wajibu mkubwa, kwa kauli zao na matendo yao, kuhakikisha kwamba hawachochei migawanyiko. Lakini pia Serikali lazima iingilie kati na kuchukua hatua kali na za haraka kwa viongozi wa kisiasa na kijamii wanaochochea chuki na migawanyiko.

Namna nyingine ya kukabiliana na changamoto za usalama ni kwa kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama wa nchi kwa kuvijengea uwezo wa kiintelijensia na vifaa na mafunzo kuweza kukabiliana na matishio ya usalama wa nchi. Tuimarisha Jeshi la Polisi kwa kuwawezesha askari polisi kuishi katika mazingira mazuri na kuwa na vifaa na nyenzo muhimu za kufanya kazi zao.

Tuna bahati kwamba tunalo Jeshi la Wananchi wa Tanzania lenye askari wenye weledi na uzalendo mkubwa. Jukumu letu ni kuendelea kuliimarisha kwa vifaa na mafunzo lakini pia kwa motisha kwa askari. Tunaishi katika eneo lenye changamoto za kiusalama kwahiyo jukumu letu sisi viongozi ni kuhakikisha kwamba Jeshi letu linakuwa katika utayari wa hali ya juu wa kivita wakati wote. Mara nyingi, hali ya utayari wa kivita yenyewe tu inaweza kuzuia vita

kutokea. Askari wetu lazima watunzwe vizuri na wawe katika ari ma morali ya juu. Wamejitolea maisha yao kutulinda na hata kuwa tayari kupoteza maisha yao kwa ajili ya usalama wetu, ulinzi wa mipaka yetu na ulinzi wa uhuru wetu. Nchi yetu inao wajibu mahsusi wa kulipa fadhila hizo ipasavyo na kuliwezesha Jeshi letu na askari na makamanda wake wote kwa mahitaji yake yote. Hili lazima kulifanya. Vilevile, Idara ya Uhamiaji nayo pia haina budi kuimarishwa. Wapo wageni wengi wanaoingia na kuishi kinyemela wakiwa hawana nia njema na nchi yetu. Vilevile, weledi na uwezo wa mbinu za kisasa kwa Idara ya Usalama wa Taifa ni muhimu sana.

Namna ya mwisho ni ya kukabiliana na changamoto za usalama wa nchi ni kuwa na Serikali imara na taasisi imara za umma. Serikali itakayopambana na



January Makamba akihutubia katika mkutano wa vijana wa makanisa ya Pentekoste.

rushwa kwa nguvu zote. Serikali itakayoweka mazingira ya kupatikana kwa haki katika jamii, Serikali itakayoweka mazingira ya watu wote kuwa na fursa sawa za kujiendeleza kiuchumi ili tofauti ya kipato itokane na tofauti ya jitihada binafsi.

18

Kiwango cha elimu katika taifa letu kimeporomoka, ni kwa nini na unafikiri ni kitu gani kifanyike kuinua hali ya elimu katika taifa letu?

Ni lazima kukiri kwamba, pamoja na changamoto zilizopo, mafanikio makubwa yamepatikana kwenye nyanja ya elimu tangu uhuru, huku kasi kubwa ikiwa ni katika miaka nane iliyopita. Katika miaka 46, yaani tangu uhuru mwaka 1961 hadi mwaka 2004, tulikuwa tumejenga shule za sekondari takriban 1,200. Katika miaka nane tu, kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka 2013, tumejenda shule zaidi ya 3,500. Mwaka 2004, kulikuwa na wanafunzi wa sekondari kama 400,000 hivi leo hii wanakaribia milioni mbili. Nakumbuka wakati nikiwa Msaidizi wa Rais Ikulu, Rais Kikwete alipoingia madarakani mwaka Disemba 2005, moja ya vitu vya kwanza alivyoagiza ni kupewa taarifa ya wanafunzi walifaulu mtihani wa darasa la saba na ni wangapi wamepata nafasi za kwenda Sekondari. Taarifa iliyokuja ilionyesha kwamba karibu nusu ya wanafunzi waliofaulu hawakuwa wamepata nafasi na ilikuwa ndio basi wanabaki nyumbani. Hakuridhika na hali hiyo, kwamba wapo watoto wenye vipaji, waliofaulu, lakini kwa kuwa tu hakuna shule basi wanarudi nyumbani. Na hawa ni watoto wa miaka 13 na 14. Hakuna aliyekuwa na jawabu kwamba wakibaki nyumbani wanafanya nini. Ndipo akaagiza kwamba yajengwe madarasa na shule mpya haraka na kwa mtindo wa operesheni ili walau ifikapo mwezi Machi watoto hawa wawe wamepata nafasi. Nakumbuka huko miaka nyuma wakati nasoma shule ya msingi ilikuwa ni kawaida mwanafunzi kufaulu mtihani wa darasa la saba lakini kutochaguliwa kwenda Sekondari. Ilikuwa ni uonevu wa hali ya juu.

Operesheni hii ya kujenga shule iliendelea kwa miaka yote tangu mwaka 2006 hadi sasa. Ni dhahiri kwamba kazi ya kupata walimu wa kutosha kwa shule hizi nyingi mpya ingechukua muda mrefu kwa sababu kazi ya kusomesha walimu inachukua muda. Na ni dhahiri kwamba, kutokana na hilo, ubora wa elimu ungetetereka. Lakini ilikuwa ni lazima kuchagua: aidha kuacha kujenga shule ili kupata walimu kwanza au kujenga shule wakati huo huo kuongeza kasi ya kusomesha walimu ili wakishapatikana shule tayari ziwepo. Uamuzi uliochukuliwa ni huu wa pili. Kwa hiyo, ni kweli katika kipindi hiki cha mpito, kutokana na mazingira yaliyokuwepo, ubora wa elimu ya sekondari ulishuka. Hata hivyo, jitihada zilizofanyika, ikiwemo uamuzi wa kihistoria wa kujenga

Chuo Kikuu kipya cha Dodoma, kitakachokuwa na wanafunzi takriban 40,000, ambao nusu yake watasomea shahada ya ualimu ili kukabiliana na changamoto hii ya ubora wa elimu.

Sasa nini kifanyike kuboresha elimu, hasa ya Sekondari?

Kwanza, tumalize mjadala na tukubaliane kuhusu dira ya elimu – ni elimu gani na ya aina gani tunataka watoto wetu wapate? Ni nini maana na malengo ya elimu nchini mwetu? Tukimaliza mjadala huu na sote tukakubaliana kama taifa, tutaondokana na changamoto ya kubadilisha mtaala mara kwa mara kila anapokuja Waziri mpya wa elimu.

Pili, tumalize mjadala na tukubaliane kama taifa kuhusu lugha ya kufundishia watoto wetu. Kwa sasa, lugha ya kufundishia kuanzia Sekondari ni Kiingereza. Utafiti wa mwaka 2007 ulionyesha kwamba asilimia zaidi ya 60 ya wanafunzi wa sekondari walishindwa kusoma au kutafsiri aya rahisi ya lugha ya Kiingereza ya ngazi ya shule ya msingi. Na tunajua kwamba moja ya sababu kubwa ya kiwango kikubwa cha kufeli ni uelewa wa lugha hii ya kufundishia na kufanyia mitihani. Kama wanafunzi hawaelewi lugha ya kufundishia na kujifunza hawawezi kupokea maarifa na hawawezi kujieleza kwa ufasaha. Tunao uwezo wa kuwapa wanafunzi wetu uelewa wa lugha zote mbili, Kiingereza na Kiswahili.

Tatu, tumalize tatizo la uhaba wa walimu, hasa walimu wa masomo ya sayansi na hisabati. Masomo haya sio ya kusoma mwenyewe na kukariri, ni masomo ya kuelewa. Ni lazima kuwa na walimu, tena walimu mahiri. Na kwa bahati mbaya kufeli kwenye hisabati kunapelekea adhabu ya alama nyingine kwenye mtihani. Sababu kubwa ya kufeli kwa watoto wetu ni kutokana na kukosekana kwa walimu wa sayansi na hisabati.

Nne, tukabaliane na changamoto za walimu, ikiwemo mazingira yao ya kazi, motisha na hamasa yao ya kufundisha – ikiwemo mishahara yao, kupandishwa madaraja, mafunzo yao ya ziada ya kujiendeleza.

Tunasema ualimu ni wito lakini haipaswi kuwa adhabu. Mwalimu ndiye mjenzi wa kizazi cha taifa. Kama saikolojia ya mwalimu haijakaa sawa kutokana na changamoto nyingi, tusahau kuhusu ubora wa elimu. Walimu wanaofanya jitihada mahsusi katika ufundishaji na kupata mafanikio watambuliwe na watuzwe.

Napendekeza pia tuweke mfumo wa motisha kwa walimu wetu wa shule za Serikali kama unavyotolewa na shule za binafsi kwa walimu wao. Mfumo huu

wa malipo kwa kufanya vizuri ni utaratibu wa kutoa motisha ya fedha kwa walimu ili kuongeza juhudi za kufundisha na kufaulisha wanafunzi wao. Malipo ya motisha yatafanyika baada ya uthibitisho wa matokeo ya mtihamu wa darasa la saba na kidato cha nne. Hii itahusisha kuanzisha mahusiano mapya kati ya matokeo ya kujifunza na maendeleo ya sekta ya elimu ya msingi na sekondari. Ninaamini kabisa kuwa kwa kujielekeza zaidi kwenye matokeo ya kujifunza tutaleta maana halisi ya kujifunza katika shule zetu za serikali.



January Makamba alipotembelea shule Sekondari ya Mtakatifu Maria Mazinde Juu, Lushoto.

Tano, tutengeneze mitaala thabiti kabisa inayokidhi mahitaji ya mazingira na changamoto za sasa na mahitaji ya jamii na taifa. Ni muhimu pia mitaala isibadilishwe mara kwa mara kwani inaleta mkanganyiko kwa walimu na wanafunzi.

Sita, tumalize matatizo ya vifaa ya kujifunza na kufundishia, ikiwemo vitabu, vifaa vya maabara pamoja na miundombinu ya mashuleni kama madarasa ya kutosha na madawati.

Saba, lazima wazazi na walezi washiriki kwa ukamilifu na wafuatilie maendeleo ya elimu ya watoto wao. Kuna wajibu wa Serikali lakini pia kuna wajibu wa wazazi. Ni muhimu kila mzazi au mlezi akawa anachungulia madaftari ya watoto wao au walau anadadisi mara kwa mara kama watoto wanajifunza yale wanayopaswa kujifunza. Ni muhimu, katika ngazi ya shule, wakashiriki vikao

vinavyowahusu na wakarekebisha udhaifu katika ngazi ya shule ambao upo ndani ya uwezo wao kwa sababu mfumo wa uendeshaji wa shule zetu unatoa nafasi kwa wazazi kufanya hivyo.

Nane, utaratibu wa mitihani uwe thabiti kwa maana ya kupima uwezo halisi wa mwanafunzi ili kuondokana na hali ambapo mwanafunzi anafaulu mtihani lakini anakuwa hajapokea maarifa yaliyotarajiwa.

Tisa, tumalize changamoto za uendeshaji na utawala wa sekta ya elimu, ikiwemo masuala ya ukaguzi, usimamizi wa walimu, uidhinishaji na usambazaji vitabu kwenye mashule, upelekaji na matumizi ya fedha za uendeshaji wa shule na mambo mengineyo.

Kwa ujumla, mwamko wa Watanzania walio wengi kuhusu elimu ni wa kuridhisha.

Watanzania wengi wanathamini elimu na wanaamini kwamba elimu ni ukombozi na ni uwekezaji mzuri. Ndio maana wazazi wengi wanajitolea kwa hali na mali kwenye ujenzi wa mashule na kujitoa – hata kukopa au kuuza mali zao – ili watoto wao wasome. Ni muhimu sisi tulio kwenye uongozi tukaweka mazingira mazuri kama nilivyosema hapo awali ili imani hiyo na matumaini hayo yatimie.

Kabla sijasahau, pia umeniuliza kuhusu uchache wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, na ni wanafunzi wengi waliofaulu kusoma katika vyuo vyetu vikuu wanakosa ada ya kulipia elimu hii. Sasa nini kifanyike? Ni kweli kwa baadhi ya vijana wanaopata fursa ya kuingia vyuo vikuu huwa wanapata shida katika kulipa ada na gharama nyingine za masomo. Serikali ilianzisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kukabiliana na changamoto hii kwa sababu ni dhahiri kabisa wapo vijana wengi wanaotoka kwenye familia zisizo na kipato cha kutosheleza kulipia elimu hii ya juu. Hata hivyo, vijana wengi pamoja na wazazi wamekuwa wanalalamikia utendaji wa Bodi ya Mikopo. Kila ninapoongea na wanafunzi wa vyuo vikuu na taasisi nyingine za elimu ya juu, wamekuwa wananilalamikia kuhusu utaratibu wa mikopo. Kumekuwepo na tuhuma pia kwamba wapo wasiostahili kupata mikopo lakini bado wanapata mikopo.

La kwanza, naamini ni muhimu kufumua mfumo wa bodi nzima ili kuongeza ufanisi na uwazi katika utaratibu wa utoaji mikopo. Iliundwa Tume ya kutazama matatizo haya. Ni vyema mapendekezo mazuri yakatekelezwa haraka.

Ni muhimu kupanua wigo wa utendaji kazi wa bodi kwa kufungua ofisi za kanda na mikoa za Bodi ya Mikopo ili kupunguza mrundikano na urasimu wa kushughulikia matatizo ya wanafunzi hasa wanaoishi mikoani. Pili, kujenga uwezo wa kifedha kwa bodi yenyewe ikiwa ni pamoja na kuanzisha Mfuko wa Bodi ya Mikopo ili iweze kwa kiasi kikubwa kujiendesha bila kutegemea marejesho ya wakopaji.

Tatu, kuendelea kutegemea Bodi ya Mikopo pekee kugharamia elimu ya juu hakutatufikisha mbali. Ni muhimu kuanzisha vyanzo vingine vya kuwasaidia wanafunzi wa elimu ya juu – ikiwemo kuanzisha udamini wa serikali kupitia benki na mifuko mbalimbali ya jamii. Nne, wengi wa wanafunzi wanaoshindwa kulipa ni wale wanaotoka katika makundi maalum, kama vile walemavu, yatima na wale walio katika mazingira magumu. Kwa hiyo, ni vyema kukaanzishwa Mfuko wa Elimu ya Juu yaani *Higher Learning Foundation Fund*, ambao utakuwa ni msaada wala sio mkopo - kwa ajili ya wasiojiweza hasa walemavu, yatima na wale walio katika mazingira magumu.

Nne, zipo kada na taaluma muhimu sana kwa nchi yetu ambazo vijana wanaozisomea hawapati mikopo kwa sababu vyo wanavyosoma havimo kwenye utaratibu wa mikopo au ngazi ya elimu haipo kwenye utaratibu wa mikopo. Ni muhimu tukapanua wigo ili vijana hawa nao wapate mikopo.

Tano, ni muhimu kwa Bodi kuimarisha uwezo wake wa kukusanya malipo ya mikopo kwa wanafunzi waliomaliza shule, ili fedha hizo ziweze kutumika kuwakopesha wanafunzi wengine. Bodi ipange mikakati madhubuti ya kufuatilia wanafunzi waliomaliza vyo. Waajiri nao wanapaswa watoe taarifa za wanafunzi walioajiriwa au kubadilisha kazi katika wakati muafaka ili Bodi iweze kuwafuatilia. Hii inawezekana kwa njia mbili; Moja, Bodi ifanye kazi moja kwa moja na *Credit Reference Bureau* ili iweze kutoa taarifa na kuwabana wadaiwa sugu na kuhakikisha hawapati fursa yoyote ya kukopa sehemu nyingine. Mbili, Bodi ya Mikopo ishabihiane na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ili kuweza kuwafuatilia karibu wadaiwa sugu. Vilevile, mfumo wa sasa wa madeni yanayokusanywa na kurudishwa hazina sio sahihi, inashusha ufanisi wa mfuko kufanya kazi yake. Bodi ya Mikopo ipewe mamlaka ya kukusanya madeni yake na kuyatumia kutokana na bajeti yake iliyopitishwa.

Lakini kubwa na la msingi ni kujenga uchumi wa kati unaokua, ili kuwapa uwezo wazazi kumudu gharama za elimu na kutumia rasilimali za nchi kwa umakini ili ziweze kusaidia kutoa elimu iliyo nafuu kwa vijana wa Tanzania.

19

Walimu ni sehemu kubwa ya watumishi wa umma. Je, wewe unayajua matatizo yao? Una fikra na mawazo gani ya kuyashughulikia? Vipi kuhusu wahadhiri wa vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu?

Walimu ndio nguzo kuu ya elimu katika nchi yetu. Ustawi wao ni muhimu katika kufanikisha malengo ya elimu nchini mwetu. Lakini walimu pia ni sehemu muhimu sana katika utumishi wa umma na wanatumiwa katika kufanikisha malengo na shughuli muhimu za kitaifa kama vile sensa na chaguzi mbalimbali. Kwa hiyo hakuna ustawi wa taifa bila ustawi wa walimu.

Mimi nayafahamu matatizo ya walimu, na sio kwamba nayafahamu kwa kuyasoma tu kwenye taarifa bali kwa kuzungumza na walimu wenyewe, kwa kuwatembelea kwenye vituo vyao vya kazi na kwa kushirikiana nao kwenye kutatua baadhi ya changamoto zao jimboni mwangu na kwingineko nchini. Shangazi zangu wawili na ndugu zangu wengine chungu nzima ni walimu.

Baadhi ya matatizo hayo ni malimbikizo ya nyongeza za mishahara yao, kucheleweshwa kupandishwa madaraja, makato lukuki kwenye mishahara; malipo ya posho na mafao yao; urasimu katika kushughulikia matatizo yao; kupotea kwa hadhi na heshima ya kazi ya ualimu; mazingira magumu ya kazi, ikiwemo suala la makazi yao na kutotosheleza kwa vitendea kazi; mishahara isiyoendana na umuhimu wao wala kukidhi mahitaji yao; motisha kutokuwepo na mambo mengine mengi kwa kweli.

Kwa upande wa wahadhiri na wakufunzi wa vyuo vikuu, nako nina marafiki wengi ambao pamoja na kujadiliana nao kuhusu mustakabali wa taifa letu, tumekuwa pia tunazungumzia changamoto zinazowakabili katika kazi zao zikiwemo posho ndogo ya ufundishaji au kutokuwepo kabisa kwa posho hiyo, yaani *teaching allowance*, kwenye baadhi ya taasisi; malimbikizo ya nyongeza za mishahara; idadi kubwa ya wanafunzi isiyoendana na idadi ya walimu; mazingira magumu ya ufundishaji kama upungufu wa nyumba za kuishi pamoja na vitendea kazi; kutengwa kwa pesa ndogo kwa ajili ya tafiti na machapisho; kukatishwa tamaa kwa wanatafiti kutokana na tafiti zao kutozingatiwa; matatizo ya kimenejimenti

ya vyuo na utoaji wa taaluma isiyokidhi viwango; utunzaji hafifu wa kumbukumbu zinazohusu taaluma; baadhi ya vyuo kuajiri walimu wasio na sifa; kulazimishwa kuingia katika mifuko ya jamii kwa wanataaluma pindi wanapoanza kazi; na kufinyangwa kwa uhuru wa kitaaluma wa kutoa maoni.



January Makamba akizungumza na walimu wa Jimbo la Bumbuli.

Serikali imekuwa inachukua hatua kadhaa za kukabiliana na kero na changamoto za walimu, wahadhiri na wakufunzi. Bado ipo fursa ya kufanya vizuri zaidi. Ni vyema tukabadili mtizamo kwenye jamii, mtizamo ambao jamii pia imewaambukiza baadhi ya walimu, kwamba kazi ya ualimu ni kazi ya watu dhalili na wasiostahili maisha bora. Mtazamo huu lazima ubadilike. Wingi wa walimu usitumike kama kigezo cha kutotimiza matarajio yao na haki zao za msingi. Ichukuliwe kwamba wingi wao ni kutokana na kuhitajika kwao kama sehemu muhimu ya ujenzi wa taifa letu.

Ni muhimu kujenga jamii ya watu wanaothamini utaalum kuliko mazoea. Hili litapelekea walimu, wahadhiri na watafiti kuthaminiwa. Lazima kuondokana na kasumba kuwa makazi ya walimu ni yale yanayojengwa chini ya ubora. Suala la nyumba bora za walimu lazima lipate msukumo mpya wa kimtazamo na maarifa ya kisasa. Tunaweza kuanzisha miradi mikubwa ya ujenzi wa nyumba bora na za kudumu za waalimu – kupitia Shirika la Nyumba la Taifa au mifuko ya jamii. Miradi hii mikubwa, licha ya kuwapatia walimu nyumba, itaongeza ajira

na kuchochea mzunguko na matumizi ya pesa hasa maeneo ya vijijini ambapo ndipo walimu wengi wanaishi na ndipo nyumba nyingi zitajengwa.

Wahadhiri na wakufunzi kwenye vyuo vikuu ni hazina za kitaalam na kitaaluma kwa nchi. Maendeleo ya kitaaluma ya wahadhiri na wakufunzi lazima yachukuliwe kama ni sehemu ya mafanikio ya taasisi wanazofundisha lakini pia mafanikio kwa nchi. Wasiachwe tu wahangaika wenyewe kana kwamba utaalam na taaluma zao ni kwa ajili ya kupatia mishahara yao tu.



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Mtakatifu Agnes Mahenge Bi Tertula Tarimo akimshukuru January Makamba kwa kuwatembelea shuleni hapo na kutoa msaada wa kompyuta kumi kwa ajili ya wanafunzi. Nyuma ni Mkuu wa Wilaya ya Mahenge na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mahenge.

20

Kumekuwa na malalamiko kuhusu utendaji Serikalini, hasa juu ya urasimu; kwamba maamuzi hayafanyiki kwa wakati, lakini pia hakuna uwajibikaji. Je, nini kifanyike kurekebisha hali hii?

Serikali ni mifumo ya kitaasisi lakini pia na watumishi na watendaji wanaotumika ndani ya mifumo hiyo. Maendeleo ya nchi hayawezi kupatikana, na Serikali haiwezi kutimiza wajibu wake, kama mifumo ya kitaasisi haijakaa vizuri na kama hakuna watumishi wa kutosha, na kama watumishi waliopo hawana motisha, ari au weledi wa kutosha.

Kwa miaka kadhaa sasa kumekuwa na maboresho ya aina mbalimbali katika utumishi wa umma. Maboresho hayo yameweka mifumo mipya lakini bado matunda hayajaonekana.

Mimi naamini kwamba kuna ulazima wa kufumua upya mfumo wa utumishi na utendaji wa Serikali ili kukomesha urasimu uliokithiri Serikalini, ili kurudisha nidhamu ya kazi kwa watumishi wa umma, ili kuongeza uwezekano na uharaka wa uwajibishaji wa watumishi wa umma wanaokiuka maadili ya kazi zao lakini pia ili kurudisha ari, morali na fahari na heshima kwa watumishi wa umma.

Katika kufanya hili, tuongozwe na misingi ifuatayo: Kwanza, uwajibikaji. Kwa sasa, ni vigumu sana kuwawajibisha watumishi wa umma kwa uzembe, ubadhirifu au kutotimiza wajibu wao. Tubadilishe Sheria ya Utumishi wa Umma ili kupunguza mlolongo wa kufikia maamuzi ya kuwawajibisha watu. Kwenye sekta binafsi kuna ufanisi kwa sababu ya uharaka wa kuchukua hatua pale ambapo mtumishi anapaswa kuchukuliwa hatua. Ni lazima iwe vivyo hivyo kwenye utumishi wa umma. Cha msingi ni kwamba kusiwe na uonevu na kusiwe na matumizi mabaya ya madaraka katika kuwawajibisha watumishi wa umma.

Msingi wa pili wa mabadiliko katika mfumo wa utendaji Serikalini ni kuleta ufanisi na kuondoa urasimu. Serikalini tunaabudu zaidi taratibu na kanuni kuliko ufanisi. Tumeweka mlolongo mirefu ya kufanya maamuzi ili kujikinga

na mtu mmoja kuchukua dhamana na wajibu wa maamuzi, matokeo yake ni kwamba maamuzi yanachukua muda mrefu, kunakuwa na vikao vingi – kila mmoja anaogopa kufanya uamuzi. Matokeo yake tunaishia kufanya mambo bila ufanisi. Lazima kukomesha urasimu. Kuwe na kipimo cha uharaka wa kufanya maamuzi na kukamilisha jambo ndani ya Serikali kama kigezo cha kupanda cheo ndani ya utumishi wa umma.

Msingi wa tatu katika mabadiliko ninayoyazungumzia ni kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali. Sasa hivi tunaendesha Serikali kwa gharama kubwa sana. Asilimia zaidi ya 67 ya bajeti yetu ni mishahara na matumizi ya kawaida. Kuna semina, warsha, safari na mikutano mingi ambayo haina tija. Kuna manunuzi mengi na malipo mengi Serikalini ambayo hayana tija. Magari ya Serikali yapo mengi kuliko inavyopaswa. Bahati mbaya udhibiti wa malipo na manunuzi haya unafanyika baada ya kuwa yameshafanyika. Ukaguzi sio tiba ya matumizi mabaya ya fedha za umma. Ukaguzi ni kama *postmortem* tu ya kubaini kwamba marehemu alikufaje, lakini marehemu tayari ameshakufa. Kwa hiyo mfumo mpya wa utumishi wa umma lazima uwe kwa kiingereza wanasema *lean*, yaani sio mzigo.

Msingi wa nne wa mabadiliko ya mfumo wa utendaji Serikalini ni kuwezesha udhibiti wa rasilimali za umma. Wenzetu waliopo Serikalini ndio tumewakabidhi usimamizi wa mali zetu, ndio tumewakabidhi jukumu la kulinda maslahi ya nchi yetu. Mfumo mpya wa utumishi wa umma lazima uwawezeshe na uwawekee wajibu wa kufanya hivyo. Lazima tuzibe uchochoro wa wizi mkubwa unaofanyika hasa kupitia kwenye manunuzi ya umma.

Msingi wa tano wa mabadiliko ninayopendekeza ni namna ya upatikanaji wa watumishi wa umma. Imani yangu ni kwamba vijana mahiri na wenye weledi na uwezo mkubwa wanapaswa kupata fursa na ari na motisha ya kuingia Serikalini na kuitumikia nchi yao. Lakini kuna tatizo kubwa la namna tunavyoajiri watumishi wa umma. Tumeweka mchakato mrefu na mgumu ambao unasababisha Serikali kuchelewa kujaza nafasi zilizo wazi au nafasi zinazohitajika. Lakini pia mfumo uliopo hautoi uhakika wa kutokuwa na upendeleo kwenye kuajiri. Ni muhimu tukaondoa urasimu na kuwezesha mahitaji mahsusi ya watumishi katika kada na vituo husika wapatikane haraka.

Lakini pia ni muhimu tukaweka njia za wazi na za uwazi, ikiwemo mitihani ya wazi, kama wanavyofanya Brazil, kwa wanaotaka kazi Serikalini ili kuondoa dhana kwamba watu wanaajiriwa kwa upendeleo lakini pia kuhakikisha kwamba tunapata watu bora zaidi miongoni mwa Watanzania.

Msingi wa sita wa mabadiliko ni kuongeza uwezo wa utendaji wa Serikali katika ngazi za utawala za chini, vitongoji, vijiji, mitaa, Kata, Mamlaka za Miji na Halmashauri. Hizi ndizo ngazi ambapo wananchi wanaishi. Watumishi, watendaji na viongozi wa ngazi hizi ndio wanakutana na wananchi kila siku na ndio wako mstari wa mbele katika kutekeleza na kusimamia shughuli za kila siku za maendeleo. Ngazi hizi zinapaswa kuimarishwa kiutendaji, kiuongozi, na kirasilimali.

Upande wa pili katika mabadiliko ya utumishi na utendaji wa Serikali ni kuimarisha weledi, maadili na uwezo wa watumishi, watendaji na viongozi wa umma. Ili Serikali ifanye kazi vizuri lazima watu wanaofanya kazi Serikalini wawe na ari na motisha na uwezo wa kutimiza wajibu wao.

Zipo kada kadhaa muhimu za watumishi Serikalini ambazo ni muhimu tuziangalie kwa upendeleo na kuwawezesha na kuwalipa vizuri kwani wao ndio mhimili wa utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Serikali. Kada hizo ni walimu na wahadhiri; askari Polisi, wanajeshi, Magereza, Uhamiaji, na Zimamoto; watumishi wa sekta ya afya – madaktari, wauguzi, wafamasia, na wakunga; wataalam katika Halmashauri – maafisa mipango, wahasibu, wahandisi, mabwana shamba na mifugo, na maafisa ardhi; watumishi katika sekta ya utoaji haki – majaji, mahakimu, waendesha mashtaka na mawakili wa Serikali; na mwisho watendaji wa vijiji na kata na wenyevidi wa vitongoji, Serikali za vijiji na mitaa. Hawa wote ni muhimu sana katika kuhakikisha kwamba Serikali ipo imara na inatekeleza wajibu wake na inatoa huduma kwa wananchi katika ngazi za msingi.

Kama nilivyosema tangu mwanzo, bila mabadiliko katika mfumo wa uendeshaji wa Serikali, hakuna maendeleo wala mabadiliko yoyote yatakayotokea nchini. Cha msingi ni kuangalia kazi iliyopo mbele yetu na majukumu ya msingi ya Serikali na kuweka mkazo kwenye weledi na akidi ya watumishi wa umma, mifumo ya kufanya maamuzi na kuyatekeleza, mifumo ya kutathmini na kufuatilia, na mifumo ya kuwajibika kutokana na matokeo.

21

Wananchi wanalalamikia sana ufisadi. Mikakati ya sasa inaelekea haijafanikiwa kiasi cha kuridhisha wananchi. Je, wewe una mbinu zozote mpya za kupambana na tatizo hili? Je, unaongeleaje ufisadi wa Richmond, EPA na IPTL.

Rushwa ni kansa mbaya sana ambayo inaweza kuitafuna jamii. Moja ya dhambi kubwa unayoweza kufanya kama kiongozi ni kutumia dhamana uliyopewa na wananchi kujinufaisha mwenyewe na ndugu, jamaa na marafiki zako. Ni zaidi ya ujambazi.

Hakuna atakayeweza kubisha kwamba rushwa imeenea katika kila nyanja. Watu wananyimwa haki kutokana na rushwa, watu wanakosa huduma wanazostahili kutokana na rushwa, taifa linakosa mapato kutokana na rushwa, uchumi na maendeleo yanadorora kutokana na rushwa. Bila ya kukabiliana kwa dhati na tatizo hili, hatuwezi kupata maendeleo hata kidogo. Tatizo limekuwa kubwa sasa na watu wanakula mali ya umma waziwazi, bila woga – wanavimbiwa na kujitapikia kwenye viatu vyao. Na wadogo wanawaiga wakubwa.

Kulizungumzia na kulipigia kelele suala la rushwa pekee hakutoshi. Ziko namna mbili za kukabiliana na hili tatizo: njia ya kwanza ni kisheria, kimfumo na kitaasisi; njia ya pili ni kijamii.

Kwanza, ni lazima tusimike sheria, mifumo na taasisi za kudhibiti na kuadhibu vitendo vya rushwa. Hayo tumeyafanya. Ipo TAKUKURU, ipo Sheria ya Kudhibiti Rushwa, zipo sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza maadili ya viongozi na watumishi wa umma, ipo mifumo inayopaswa kuziba mianya ya rushwa na matumizi mabaya ya mali za umma. Pamoja na vyote hivi, bado tatizo lipo. Hatuwezi kuendelea hivi hivi halafu tukapata matokeo tofauti. Hatua za kimapinduzi zinahitajika. Kwa hiyo, tunapaswa kufumua na kujenga upya taasisi, mifumo na sheria za kudhibiti na kuadhibu vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma. Makosa ya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma yawe ni makosa ya uhujumu uchumi na uhujumu wa taifa, na adhabu

iongezwe. Pia, ikibidi, baadhi ya mambo yanayohusu watuhumiwa wa makosa ya aina hii, kama vile dhamana, yabanwe kwa kiasi fulani.

Napendekeza mabadiliko mawili ya kimfumo ya jinsi tunavyolishughulikia janga la ufisadi. Kwanza, ni kuiwezesha TAKUKURU kuwa na mamlaka kisheria ya kuwashitaki watuhumiwa wa rushwa moja kwa moja mahakamani. Pia, tuanzishe Mahakama Maalum ya Uhujumu Uchumi ambayo itahusika na makosa ya rushwa; ubadhirifu wa mali ya umma; ukwepaji kodi; kuiba, kunufaika au kutaka kuiba au kutaka kunufaika na mali ya umma; na makosa mengine ya aina hii – mahakama ambayo itakuwa na benchi au jopo maalum la majaji ambalo litafanya kazi mwaka mzima na kusikiliza na kuhukumu kesi hizi haraka. Haki ya dhamana kwa makosa ya aina hii iwe na masharti makubwa. Kesi za uhujumu uchumi ziendeshwe wazi na mfululizo na adhabu ziwe kali sana – ya chini iwe miaka 30 na ya juu iwe adhabu ya kifungo cha maisha. Kuwepo na magereza maalum, zenye mazingira mahsusi na kazi ngumu, kwa ajili ya wafungwa wa makosa haya. Pia napendekeza tuanzishe Kurugenzi ya Uchunguzi na Mashtaka ya Uhujumu Uchumi. Mahakama hii na Kurugenzi hii viwezeshe bila ukomo wa kirasilimali kuifanya kazi hii vizuri.

Namna ya pili ya kupambana na rushwa ni ya kijamii: kwamba, jamii nzima ijengwe kwenye misingi ya kuchukia rushwa, ulaghai na njia za mkato za kupata mali. Inapofika mahala jamii inasheherekea mali ambazo hazina maelezo, inapofika mahali ambapo jamii inawatukuza wachache ambao wametumia ujanja kufanikiwa, inapofika mahala ambapo jamii inakucheka ukiamua kulipa faini ya shilingi 30,000 polisi badala ya kutoa rushwa ya 5,000, hapo lipo tatizo ndani ya jamii. Lazima kujenga jamii tofauti, ambayo wala rushwa wanajiona kama wanatembea uchi, jamii ambayo inatoa adhabu za kijamii, yaani social sanctions, ikiwemo kutengwa, ambazo ni kali kuliko adhabu za kisheria. Mwalimu Nyerere alijaribu kujenga jamii ya aina hii: jamii ambayo kiongozi wa umma hapaswi kungoja mahakama itamke kwamba ni mla rushwa. Tunapaswa kuendelea kujenga jamii ya aina hii.

Na hapa sitaki kueleweka vibaya, kwamba mtu yoyote mwenye mafanikio kwenye biashara au shughuli zake basi watu wawe na shaka naye au aitwe mwizi. Hapana. Tusijenge jamii ambayo watu wanaficha pesa zao walizozipata kihalali. Jamii lazima iwatuze, iwathamini na kuwaonea fahari wale wanaofanya vizuri kutokana na jasho lao na kutokana na bidii yao ili wawe mfano wa wengine. Jamii lazima ipende mafanikio ya wanajamii wake. Tusiwe na jamii ambayo inataka kila mtu awe maskini, jamii ambayo ufukara ni sifa. Hapana.

Lakini pia tusiwe na jamii ambayo wajanja-wajanja na wale wanaotajirika kwa njia zisizo halali ndio wanaonekana mashujaa.

Umeuliza pia kuhusu masuala ya Richmond, EPA na IPTL.

Hizi skendo zimetudhihirishia kwamba bado tunayo safari ndefu na kazi kubwa ya kupambana na rushwa na matumizi mabaya ya madaraka. Zimetuonesha kwamba miongoni mwetu wapo ambao kwa tamaa binafsi wapo tayari kuhujumu uchumi wa taifa letu.

Lakini vilevile zimetufundisha kuhusu haja ya kuimarisha mifumo ya uwajibikaji kwa watendaji na viongozi wa umma. Inashangaza kwamba kiongozi amebainika kuhusika na ubadhirifu lakini bado anasubiri msukumo wa bunge au jamii kuwajibika.

Lazima tujenge utamaduni wa uwajibikaji lakini vilevile kwa viongozi waliobainika kutumia madaraka vibaya au kujihushisha na ubadhirifu, kujiuzulu au kuondolewa kwenye nafasi zao hakutoshi. Lazima jamii ishuhudie wakipewa adhabu kali ili kuzuia matukio ya namna hii kujirudia.

Ushauri wangu ni kwamba maswala ya uwajibikaji yasichanganywe na siasa. Kwamba pale kunapotokea wizi na ubadhirifu, wahasika ni watu binafsi, sio vyama na kwamba wabunge na viongozi wa vyama vyote wanapaswa kuungana kulaani na kuchukua hatua bila kuingiza siasa za vyama.

Skendo za EPA, IPTL na Richmond zimeandikwa sana kwenye magazeti lakini kila siku kuna wizi mkubwa zaidi unaoendelea katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambao hausikiki. Yapo madaraja yanayopaswa kujengwa lakini hayajengwi na pesa kuchukuliwa, pembejeo zinachakachuliwa, barabara zinajengwa chini ya kiwango na fedha zinaliwa, majengo hayakamiliki kwa ubora unaotakiwa. Malipo mengi hewa yanafanywa kwa ajili ya semina na warsha na mikutano na safari hewa. Haya yote ni mabilioni yanayopotea kila siku lakini huyasikii kwenye magazeti au bungeni. Ni lazima kusafisha mambo yote haya.

22

Kumekuwa na hii dhana ya kufanya maamuzi magumu kama sifa ya uongozi. Je, unalisemeaje hili? Je, wewe umeshawahi kufanya maamuzi yoyote magumu kwenye uongozi wako?

Watanzania karibu wote, hasa wa kipato cha chini, kila kukicha wanafanya maamuzi magumu kwenye kutengeneza maisha yao.

Hakuna uamuzi mgumu kama kuamua kati ya watoto wako wanne yupi umpeleke shule na yupi asiende shule kwa sababu huna uwezo wa kuwalipia wote ada na kuhimili michango mbalimbali ya shule. Hakuna uamuzi mgumu kama kuamua kulima shamba dogo na kupata kipato kidogo kwa sababu huna uwezo wa kupata pembejeo za kulima shamba kubwa. Hakuna uamuzi mgumu kama kuamua kufanya kibarua chochote tu kwa sababu hukufanikiwa kupata kazi uliyoisomea. Wananchi wangu wa Bumbuli nao walifanya uamuzi mgumu wa kuamua kufunga kiwanda cha Chai ambako walikuwa wanauza majani yao kutokana na dhuluma, kejeli na manyanyaso ya miaka mingi ya mwekezaji.

Wafanyabiashara nao kila siku wanafanya maamuzi magumu kukabiliana na changamoto na mazingira magumu ya biashara, ikiwemo rushwa na urasimu. Kwa hiyo, sifa ya kufanya maamuzi magumu ni sifa ya Watanzania wote kutokana na mazingira ya nchi yetu.

Kazi kubwa ya kiongozi ni kutenda kazi na kutimiza wajibu wako ili kuwaondolea wananchi ulazima wa kufanya maamuzi magumu.


Kwa upande wa uongozi, kila kiongozi, popote alipo na kwa nafasi yake, ikiwemo hadi viongozi wa Serikali za Wanafunzi Vyuoni, wanalazimika nao kufanya maamuzi ambayo kwa wakati huo yanaweza yasieleweke au kukubalika na wengi lakini yana manufaa kwa wanaowaongoza. Huu ndio wajibu wa uongozi. Kwa mantiki hii, binafsi, nimefanya maamuzi ya aina hii mara nyingi. Nitatoa mfano wa zamani na mfano wa hivi karibuni.

Nikiwa Msaidizi wa Meneja wa Kambi ya Wakimbizi ya Mtabila, moja ya majukumu yangu ilikuwa ni kusimamia ugawaji wa chakula kwa wakimbizi



January Makamba akiapishwa na Rais Kikwete kuwa Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

wapatao 120,000. Ni zoezi gumu linalochukua siku si chini ya tatu na chakula tulikuwa tunagawa cha wiki mbili mbili. Kazi ya kwanza ilikuwa ni kuhamisha chakula kutoka stoo na kukipeleka kwenye eneo la ugawaji, tulikuwa tunaita



prepositioning. Nilikuwa nasimamia watu wasiopungua 100 wa kufanya kazi hii, kuanzia wabebaji hadi wagawaji chakula. Mara nyingi, katika zoezi hili, huwa kuna wizi mkubwa wa chakula cha wakimbizi, hasa mafuta ya kupikia. Mara

nyingi wizi huu hufanywa na wafanyakazi wenyewe. Sasa siku moja, tukiwa katiwa ya kugawa, kambi nzima ikiwa imesimama kwenye foleni nikabaini kitendo cha wizi. Nilikasirika sana. Nikalazimika kufanya uamuzi wa aidha kuendelea tu kugawa chakula ili tumalize huku nikijua kuna watu wanaiba au kusimamisha zoezi ambako kuna gharama na usumbufu mkubwa. Nilichofanya nilienda kituo cha polisi kambini, nikatoa shitaka la wizi na nikaomba askari waje kwenye eneo na wakaja na gari lao pale kwenye uwanja wa kugawa chakula. Nikawatangazia wakimbizi kwamba tunasimamisha zoezi kwa muda kwa jambo lenye manufaa kwao na kwamba watulie. Nikawaambia askari kwamba naomba wafanyakazi wangu wote wakamatwe na kupelekwa ndani kwa tuhuma za wizi. Walijua ni mzaha. Na nikawaambia kwamba wana nusu saa wataje wezi miongoni mwao la sivyo kila mmoja anafukuzwa kazi papo hapo. Wakati huo huo nilikuwa natafuta vibarua wengine wa muda wa kuendelea kugawa. Chini ya nusu saa wakatajana. Waliohusika wakabaki polisi. Wasiohusika wakaja kuendelea kugawa chakula. Tangu siku hiyo tukakomesha wizi wa chakula cha wakimbizi. Hiyo ilikuwa mwaka 1997 na nilikuwa na miaka 23 tu.

Nilijifunza tangu zamani, tangu nikiwa kiongozi mdogo, kwamba, kuna baadhi ya mambo ya msingi, kama wizi au dhuluma, ambayo hakupaswi kuwa na suluhu.

Wengine wanaweza kusema huu ni uamuzi mgumu lakini mimi naamini ni katika kutekeleza wajibu.

Jambo jingine ambalo nililisimamia ambalo halikueleweka wakati tunalifanyia maamuzi, na ambalo tulilaumiwa nalo, ni suala la kupendekeza kuongeza kodi ya mafuta ya taa wakati nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini.

Miaka ya nyuma, kwa maelezo kwamba mafuta ya taa ni mafuta yanayotumika na wanyonge, uamuzi ulifanywa kuondoa kodi kwenye kuagiza mafuta haya. Kwa kuwa mafuta mengine yaliendelea kutozwa kodi kubwa, tofauti ya bei ya mafuta ya taa na dizeli ikawa ni kubwa, tofauti ya takriban kiasi cha shilingi 600 kwa lita mwaka 2011. Kukawa na malalamiko makubwa kwa wenye magari ya mizigo na watu wengineo kwamba, wafanyabiashara wengi wasio waaminifu wanaagiza mafuta ya taa na wanayachanganya na dizeli, yaani wanayachakachua, ili wapate faida kubwa. Na kwakweli hali ilikuwa mbaya. Vikazuka vituo vya mafuta vingi ambavyo vilikuwa na kazi ya kuchakachua tu. Mimi na wenzangu kwenye Kamati

tukaamua kulivalia njuga na kuita karibu kila mdau wa sekta ya mafuta nchini, tukatembelea bandari, kwenye hifadhi za mafuta na kufanya ziara za ghafla kwenye baadhi ya vituo. Tukachambua takwimu za kiwango cha mafuta ya taa kinachoingizwa nchini na kile kinachouzwa kwenye pampu na kwingineko na tukaona tofauti kubwa – kwamba kituo cha mafuta kinaweza kuagiza lori la lita 10,000 za mafuta ya taa kwa wiki lakini kwenye pampu yakauzwa lita 2,000 tu. Tukaangalia mafuta ya taa yanayoingizwa nchini yanaishia mikoa ipi, tukagundua kwamba asilimia 70 yanaishia kwenye mikoa sita ya barabara kuu, ambako kuna vituo vingi vya mafuta – na hayaendi vijijini kama inavyosemekana. Tukachambua hesabu za TRA na kubaini kwamba Serikali inapoteza shilingi bilioni 50 kwa mwezi kutokana na uchakachuaji. Tukaangalia hatua za Serikali za kuzuia hili jambo, tukabaini hazikuwa zinafanya kazi. Basi tukaamua tupendekeze kwamba kodi ya mafuta ya taa ipande na mafuta ya taa yauzwe bei sawa na dizeli ili kuondoa haja ya mtu kuchanganya hayo mafuta. Tuliambiwa kwamba Serikali ilikataa wazo hilo ili isionekane inawakandamiza wanyonge wanaotumia mafuta ya taa. Hata hivyo, waliokuwa wananufaika na bei ndogo ya mafuta ya taa wala sio wanyonge bali wahujumu uchumi wenye fedha nyingi. Tukalisukuma suala hilo Bungeni na kuwashawishi Wabunge wenzetu na likapitishwa kwenye Bajeti ya Serikali. Baadaye ikawa zahama kubwa. Nakumbuka kuna kikao kimoja cha Chama mimi nilikuwa Mjumbe nilichapwa maneno na Chama baadaye kikatoa tamko kutaka kodi hiyo iondolewe. Lakini sisi tulichopendekeza sio kutowajali wanyonge. Tulisema kwamba hatuwezi kuendelea kuchukua hatua za kuhimiza wanyonge waendeleo kutumia vibatari. Tulipendekeza kwamba tukirudisha kodi kwenye mafuta ya taa, fedha inayopatikana iende kwenye kupeleka umeme vijijini ili hao wanyonge tunaowatetea basi tusiwatetee kuendelea kutumia vibatari, tuwatetee kwa kuwapelekea umeme. Kabla ya kufikia kubatilisha uamuzi wetu, manufaa ya kodi ya mafuta ya taa yakaanza kuonekana, uchakachuaji ukakoma, na Serikali ikaamua kuendelea na uamuzi wa kodi kwa mafuta ya taa hadi leo. Matokeo yake, na kama ukiwa unasafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Chalinze ukihesabu idadi ya vituo vya mafuta aidha vilivyofungwa au vilivyoishia katikati kwenye ujenzi, utaona ni vingi mno kwa sababu vilikufa kutokana na shughuli ya uchakachuaji kukoma. Tulipendekeza na kusimamia uamuzi ambao haukuwa maarufu wakati ule lakini majuzi nimesikia watu ambao hawakuunga mkono suala hili wanapongezana kwa kumaliza tatizo la uchakachuaji.

Ipo mifano mingi ya maamuzi ya aina hii ambayo nimeyafanya, zamani na sasa, ambayo mimi siyaiti magumu kwa sababu ni maamuzi ya kutimiza wajibu kama kiongozi.

23

Hapa tupo Dar es Salaam. Inaelekea karibu kila mtu anataka kuhamia na kuishi Dar es Salaam. Una maoni gani kuhusu nafasi ya Jiji la Dar es Salaam katika maendeleo ya nchi yetu? Nini changamoto za jiji hili na nini kifanyike kuzirekebisha?

Kihistoria na kijiografia Dar es Salaam imekuwa na nafasi kubwa katika ustawi wa nchi yetu. Harakati za kutafuta uhuru ziliendeshwa kutokea hapa. Bandari ya Dar es Salaam ina historia ya kipekee. Kwa sasa, asilimia 11 ya Watanzania wanaishi kwenye Jiji la Dar es Salaam. Jiji la Dar es Salaam linachangia asilimia 18 ya Pato la Taifa. Jiji la Dar es Salaam linachangia asilimia zaidi ya 50 ya mapato ya Serikali. Jiji la Dar es Salaam likipata mafua, nchi nzima inapiga chafya. Na jiji la Dar es Salaam ndilo linaloongoza kwa kasi ya ukuaji hapa Afrika. Miaka 13 tu kuanzia sasa, Jiji la Dar es Salaam litakuwa na watu zaidi ya milioni 10. Na miaka 13 tu kuanzia sasa, kwa mara ya kwanza katika nchi yetu, watu wengi zaidi watakuwa wanaishi mijini kuliko vijijini. Kwa hiyo, kwa maendeleo ya nchi yetu, lazima miji yetu yote itengemae.

Kwa hiyo, kama viongozi, ni muhimu tuangalie suala la ukuaji wa Jiji la Dar es Salaam na miji mingine hapa nchini, na changamoto nyinginezo za nchi, kwa kuona mbali – miaka 20, 30, 40, 50 ijayo – ili kutengeneza majawabu ya kudumu na endelevu. Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam, ni muhimu kutambua kwamba miji ya Kibaha, Bagamoyo na Kisarawe, pamoja na kwamba ipo Mkoa wa Pwani, imeshakuwa sehemu ya Jiji la Dar es Salaam na watu wengi wanaofanya kazi Dar es Salaam wanaishi huko.

Zipo changamoto na mahitaji mahsusi ya jiji la Dar es Salaam na miji mingine mikubwa hapa nchini ambayo ni lazima tuyashughulikie kwa haraka. Mambo yenyewe ni haya:

Kwanza ni usafiri. Mfumo wa usafiri wa umma (public transport) na utaratibu wa kuendesha magari binafsi na miundombinu ya barabara lazima iwezeshe watu kutumia muda mfupi barabarani. Utafiti unaonyesha kwamba msongamano wa

magari katika Jiji la Dar es Salaam unaugharimu uchumi wa nchi yetu shilingi bilioni 4 kwa siku – au zaidi shilingi trilion 1.4 kwa mwaka – au zaidi ya bajeti za Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja. Gharama za kukaa barabarani masaa matatu au manne kunapunguza tija ya nguvu kazi na kuongeza gharama kwa Uchumi na kuchafua mazingira. Bahati nzuri kazi nzuri imeanza kufanywa kurekebisha hali hiyo, ikiwemo mradi wa DART na ujenzi wa flyovers na njia za mkato. Lakini kama sote tunavyojua, na kama historia kwenye miji mingine inavyoonyesha, barabara zinapopanuliwa tu punde hujaa tena magari na tatizo hurudi palepale. Kuna daladala karibu 8,000 katika Jiji la Dar es Salaam, ambazo zinatoshesheleza asilimia 43 tu ya watu wanaohitaji usafiri. Kuna magari madogo binafsi takriban 120,000 yanayosafirisha asilimia 6 tu ya watu na asilimia 51 aidha wanatembea au kutumia baiskeli, bodaboda na Bajaj.

Natambua kwamba mradi wa DART una awamu sita zinazokuja. Lakini kinachoweza kuongezwa kama jawabu la miaka 50 ijayo, kwa mtazamo wangu, ni usafiri wa reli nyepesi au light rail au trams, kwa lugha ya kigeni. Inawezekana kabisa kuwa na njia moja inayotoka Bagamoyo hadi Mikocheni, ambapo itakuwa na vituo vingi hapo katikati – Mbweni, Tegeta, Tangi-Bovu, Kawe na kwingine - na kuchukua watu wengi. Reli nyingine inaweza kutoka Kibaha hadi Magomeni na kuhudumia watu wote wa njia hiyo – Kimara, Mbezi na kwingine. Na njia ya tatu inaweza kutoka Kisarawe hadi Stesheni Kuu ya Dar es Salaam – na kuchukua na kuwarudisha watu wote wa Chanika, Pugu, Buguruni, Vingunguti na kwingineko. Reli nyingine inaweza kutokea Mkuranga na kuja kuunganika KAMATA na reli inayotokea Kisarawe. Njia hizi kuu zinaweza kuunganishwa katika miaka ijayo na kutengeneza mfumo mpana zaidi unaofika maeneo mengi. Wenzetu wa Ethiopia wako kwenye hatua za mwisho kumaliza mradi mkubwa wa reli katika jiji la Addis.

Swali linaweza kuja kwamba mradi huu ni wa gharama sana na fedha zinaweza zisiwepo. Jawabu lipo. Sio lazima kutumia fedha zote za Serikali. Maeneo ya vituo vya kuanzia na vituo vikubwa vya katikati vinaweza kujengwa maeneo salama ya kupaki magari hata kwa mwezi mzima, vituo vya mabasi, na majengo makubwa ya maofisi, nyumba za kuishi na maduka makubwa na huduma nyingine. Na ujenzi huu unaweza kufanywa na sekta binafsi, bila kutumia fedha za Serikali. Kitakachotokea hapa ni kwamba watu wengi watahamishia makazi yao na ofisi zao kwenye maeneo ya vituo vya treni ili kuongeza ufanisi katika shughuli zao. Fedha zitakazopatikana kutokana na biashara ya majumba, maofisi, maegesho, maduka ndizo zitakazotumika kuendesha mfumo huu wa usafiri. Ukiwa na vituo vikubwa 12 vya namna hii, pesa nyingi itapatikana. Miji yote mikubwa duniani huu ndio uzoefu. Treni hubeba watu wengi kwa wakati mmoja na haina msongamano. Utafiti na uzoefu sehemu nyingine duniani

unaonyesha kwamba upanuzi wa barabara na ujenzi wa fly-overs ni jawabu la msongamano, na lazima tufanye, lakini ni jawabu la muda mfupi. Kama tunatazama maendeleo ya Jiji la Dar es Salaam na maendeleo ya nchi yetu katika maono ya miaka 30, 40 ijayo, hakuna njia nyingine zaidi ya reli kwa uhakika wa usafiri. Tukifanya haya, na ukichanganya na mradi wa DART, jiji la Dar es Salaam litakuwa moja ya majiji bora hapa Afrika na mchango wake kwa uchumi wa taifa utakuwa mkubwa zaidi.

Tunaweza pia kujaribu kuangalia tozo za gari moja moja, hasa ikiwa na abiria mmoja, kuingia katikati ya mji ili kuwashawishi wanaokuja katikati ya mji watumie mabasi au wawe wanapeana lifti kwenye magari ili kupunguza msongamano.



January Makamba mara baada ya mkutano na wananchi katika Jimbo lake la Bumbuli.

Suala jingine ni usalama. Uhalifu unatishia ustawi na maendeleo ya miji yetu. Fursa za uwekezaji zinakimbia na gharama za biashara zinaongezeka kama miji imetawaliwa na uhalifu. Pia maisha ya watu saa zote yanakuwa na mashaka na watu badala ya kufurahia kuishi kwenye jiji wanakuwa saa zote wana wasiwasi. Ziko namna kuu za kukabiliana na uhalifu kwenye jiji. Moja ni kuhakikisha

kwamba vijana wengi wana ajira au njia halali za kipato. Pili, ni kuhakikisha kwamba katika kila mtaa wananchi wanajihusisha na kujua yanayoendelea mtaani na kujua watu wote wanaoishi au wageni wanaokuja pale wanajulikana na shughuli zao zinajulikana. Hapa ni muhimu Serikali za Mitaa zikawa zinatimiza wajibu wao kikamilifu. Na tatu, ni kuhakikisha kwamba vyombo vya ulinzi na usalama vina vitendeakazi na weledi wa kutosha kupambana na kuzuia uhalifu.

Jambo jingine muhimu kwa jiji ni miundombinu ya maji, majitaka na takataka. Jiji lenye hadhi haliwezi kupata mafuriko kila wakati mvua ndogo inaponyesha. Lazima kuwe na uwekezaji mkubwa wa kujenga mifereji na miundombinu ya kuzoa taka na majitaka. Jiji la Dar es Salaam linakua kwa kasi sana – kwa kasi kuliko majiji yote barani Afrika. Taka ngumu na taka-maji zitaongezeka maradufu kila mwaka na mahitaji ya maji yataongezeka maradufu kila mwaka. Kuna juhudi zinafanywa za kukabiliana na matatizo haya. Lakini majawabu yanayohitajika ni majawabu ya miaka 30 ijayo. Sekta binafsi ina nafasi katika hili suala. Takataka ni biashara.

Kwa upande wa maji, ongezeko la watu na makazi linaongeza ukubwa wa tatizo la maji katika jiji la Dar es Salaam. Chanzo kikubwa cha maji kwenye jiji la Dar es Salaam ni Mto Ruvu. Mto huu unapungua kwa kasi kubwa. Hata hivyo, kuna vyanzo vingine vikubwa vya maji ya chini ya ardhi vinavyoweza kuanza kutumika kusambaza maji katika kila kaya ya jiji.

Jambo jingine linalohitaji jawabu kwenye jiji ni suala la nyumba na makazi. Asilimia zaidi ya 60 ya wakazi wa Dar es Salaam wanaishi kwenye makazi yasiyo rasmi na wanalipa kodi kubwa kuliko hali ya nyumba wanazoishi. Jawabu ni kujenga nyumba zaidi. Jawabu la haraka ninalolifikiria ni kubadilisha kabisa maeneo yanayoonekana kama ni mabaya – Manzese, Tandale, Mbagala, Vingunguti na kwingineko – kuwa mazuri. Kwa mfano, ukienda Manzese ukaainisha eneo lenye nyumba duni la ukubwa wa uwanja wa mpira wa miguu, ambalo linaweza kuwa na familia kama 200, halafu ukazungumza na wakazi hao na kuwashawishi wakubali kuhama na kuwalipia makazi ya muda kwa miezi kumi na nane ili kuliendeleza. Wakihama, lile eneo unalivunja na kujenga nyumba za ghorofa tatu au nne zitakazochukua familia si chini ya 800, kuweka mifereji, bustani, maduka, na shule. Ukimaliza unazirudisha zile familia 200 katika nyumba hizi mpya bora zaidi na unakuwa umepata nafasi mpya kwa familia 600 zaidi katika eneo lile lile. Halafu unaendelea kwa kukata kipande kingine tena sawa na uwanja wa mpira wa miguu ambapo utapata familia nyingine 200 na safari hii huna haja tena ya kuzihamisha familia za eneo hili kwenye makazi ya muda kwa miezi kumi na nane, kama ulivyofanya mwanzo, kwa sababu tayari una nafasi za familia 600 – kwa hiyo utatoa nafasi 200

na kubakiwa na nafasi 400. Kwa hiyo utajenga kwenye eneo hilo na kupata nafasi nyingine mpya za familia 800 halafu ukijumlisha na zile 400 utakuwa na nafasi za familia 1,200. Familia 400 za kwanza zilizohamishwa zitalipa kodi sawa na waliyokuwa wanalipa zamani na nafasi mpya zilizobaki zitaunzwa au kukodishwa kwa gharama nafuu. Ukiendelea hivi na mpango huu katika maeneo yote tunayoyaita ya uswahilini katika miji yetu utapunguza sana tatizo la makazi, utapendeyesha mji na utawezesha watu wanaoishi kwenye miji kuishi kwenye nyumba zenye hadhi zinazohifadhi utu wao.

Suala jingine linalohusu ustawi wa jiji ni suala la ajira na fursa za uchumi. Jiji lolote ambalo sehemu kubwa ya wakazi wake hawana shughuli mahsusi ya kufanya, hawana fursa za kujiendeleza kiuchumi, na hawana kipato kinachoendana na gharama za maisha, jiji hilo ni hatari. Jiji la Dar es Salaam ni jiji la 16 Afrika kwa ukali wa gharama za maisha. Fursa ni muhimu zitengenezwe katika maeneo yanayozunguka Jiji hili. Juhudi za makusudi zinaweza kufanywa kuwa na viwanda vya nguo na viwanda vingine pembezoni mwa Dar es Salaam.

Biashara ni sehemu kubwa ya Jiji la Dar es Salaam.

Asilimia zaidi ya 80 ya biashara za jijini ni biashara ndogondogo zinazoajiri watu wasiozidi wawili. Kwa mujibu wa takwimu za Benki ya Dunia, asilimia 20 tu ya biashara hizi zikiongeza mfanyakazi mmoja tu, ajira zitakazopatikana ni 400,000 kwa mwaka. Kwa hiyo kuna haja kwa Serikali kuhakikisha kwamba biashara ndogo katika miji yetu zinapanuka na kuwa biashara kubwa na za kati na kiongeza watu wanaojishughulisha na biashara.

Miji mingi pia ni vivutio vya uchumi wa kisasa, ikiwemo huduma za benki, bima, mawasiliano na nyinginezo. Miji inavutia vijana wa aina mbili: wenye vipaji na elimu kubwa na wale ambao wanachokuja nacho mijini ni misuli yao tu na hamasa ya kujitengenezea maisha. Jiji bora ni lile linaloweka mazingira ya kunufaika na kuwanufaisha vijana wa aina zote hizi mbili.

Lakini mwisho ni jinsi jiji linavyoendeshwa. Utawala wa jiji una uhusiano mkubwa na ufanisi wa jiji. Ili tufanikiwe, lazima jiji la Dar es Salaam liendeshwe kwa mfumo tofauti na utaratibu wa kawaida wa TAMISEMI.

Moja ya njia hiyo ni kuanzisha Wizara mahsusi ya Maendeleo ya Jiji la Dar es Salaam (Ministry of Dar es Salaam Metropolitan Development) ili kuwezesha miradi mikubwa ya uwekezaji katika Jiji kutekelezwa kwa haraka.

Ipo changamoto ya kupata fedha kwa ajili ya uwekezaji kwenye miundombinu muhimu katika Jiji la Dar es Salaam. Ni dhahiri kabisa kwamba fedha za Serikali haziwezi kutosha kulingana na mahitaji. Kwa hiyo, ushiriki wa sekta binafsi hapa ni muhimu hasa kwa uwekezaji wa miundombinu inayoingiza mapato. Lakini pia, ukiondoa mapato ya Serikali Kuu yanayokusanywa Dar es Salaam, mapato yanayokusanywa na Manispaa tatu za Dar es Salaam yanafikia shilingi zaidi ya bilioni 100 kwa mwaka. Sote tunajua kwamba tukikusanya kama inavyopaswa hizi zinaweza kuongezeka hata mara tatu. Lakini pia, kwa sababu Jiji lina mapato ya uhakika, linaweza kutoa hati-fungani (*Municipal Bond*) na kupata fedha nyingi kwa ajili ya uwekezaji mkubwa.

Nimalizie kwa kusema, pamoja na kwamba umeniuliza kuhusu Dar es Salaam tu, lakini changamoto hizi na majawabu haya yanahusu pia miji mingine karibu yote katika nchi yetu.



January Makamba akiagana na vijana wa Bodaboda baada ya kukutana ili kuzungumzia shida na changamoto zinazowakabili katika shughuli zao.

24

Mwaka 2012 ulipeleka Bungeni Muswada Binafsi wa Sheria ya Kudhibiti shughuli za Upangishaji Nyumba. Tuelezee maudhui yake, nini kilikusukuma na muswada huo umefikia wapi.

Tangu nimekuwa Mbunge nimekuwa nafuatwa sana na vijana wengi wanaoishi mjini wengi wakiomba niwasaidie kwenye masuala ya aina tatu: ajira, masuala ya shule na matatizo katika upangaji wa nyumba. Nimekuwa najitahidi kwa kadri ya uwezo wangu kwa kila aliyekuja na tatizo. Hata hivyo, masaiibu waliyokuwa wananieleza vijana wenzangu hawa kuhusu adha za upangaji wanazopata yalikuwa yananisumbua sana akili yangu na nikaamua kulifanyia utafiti suala hili ili niweze kutoa msaada wa jumla kwa wapangaji wote nchini wanaohangaika lakini pia na kuisaidia Serikali kuweka udhibiti katika moja ya sekta muhimu kwa uchumi na ustawi wa watu. Katika kufanya utafiti na kuzungumza na wapangaji wengi, nilibaini yafuatayo:

Mosi, asilimia kubwa ya Watanzania, hasa waishio mijini, wanaishi kwenye nyumba za kupanga, na karibu asilimia hadi 40 ya kipato chao wanakitumia kwa ajili ya kulipia pango; Pili, kumekuwa na udhibiti mdogo wa biashara ya upangaji, na kupelekea kuongezeka kwa vitendo vya unyanyasaji dhidi ya wapangaji, ikiwemo kudaiwa pango la miezi sita hadi mwaka mzima, tena kwa fedha za kigeni; Tatu, ongezeko la tatizo la makazi mijini limewalazimisha wapangaji kukubali masharti ya upangaji yanayoenda kinyume na haki, na kwa kwamba vitendo hivi vimekuwa vinaendelea kwa muda mrefu bila udhibiti; Nne, hakuna Sheria mama inayodhibiti upangaji na inayolinda haki za mpangaji na haki za mwenye nyumba. Sheria zilizopo, yaani Sheria ya Ardhi ya 1999 na Sheria ya Mahakama ya Ardhi ya 2005 hazitoi udhibiti kamilifu wa sekta ya upangaji nyumba. Vilevile, hakuna udhibiti wa shughuli za madalali ambao, kutokana na tozo zao, wamechangia kwa kiwango kikubwa ongezeko la kodi za nyumba na kumekuwepo na ulaghai mwingi.

Kutokana na haya, nikataka Sheria ya Kudhibiti Shughuli za Upangaji wa Nyumba (*Rental Housing Act*) itungwe. Sheria hiyo, pamoja na mambo mengine, itaweka utaratibu na udhibiti wa sekta ya upangaji wa nyumba ikiwemo kuweka haki na wajibu wa wapangaji na wenye nyumba, kudhibiti kutoza kodi ya miezi

sita au mwaka mzima, kudhibiti kupandisha kodi ya nyumba kiholela, kuweka mazingira ya ukuaji wa sekta ya nyumba na makazi, kuhakikisha wenye nyumba nao wanalipa kodi kutokana na mapato yao ya upangishaji kama ambayo sisi wengine sote tunalipa kodi, na kuanzishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Sekta ya Nyumba (*Real Estate Regulatory Authority*), ambayo kama ilivyo EWURA kwa nishati na maji na TCRA kwa mawasiliano, na yenyewe itaweka udhibiti na nidhamu katika sekta hii muhimu kwa ustawi wa watu, taasisi ambayo pia itawalinda wapangaji kutokana unyanyasaji lakini pia kuhakikisha haki za wenye nyumba nazo zinalindwa.



January Makamba akiwasilisha hoja bungeni.

Nilipowasilisha Muswada huu ulipokelewa vizuri na Wabunge wote. Serikali pia iliupokea vizuri na ikaahidi kwamba kabla ya Sheria hii kutungwa basi lazima kuwe na Sera ya Nyumba kwanza. Hivyo ndivyo alivyoahidi Waziri, Mheshimiwa Profesa Tibajuka Bungeni. Mimi naamini swala hili litatekelezwa mapema.

Hata hivyo, suluhisho la tatizo hili ni ujenzi wa nyumba nyingi zaidi, hasa mijini. Kila Mtanzania anastahili heshima ya kumiliki nyumba yake. Watu wengi wanao uwezo wa kufanya hivyo lakini sio kwa utaratibu wetu hapa ambapo lazima uwe na pesa za mkupuo ndio ujenge nyumba. Ni vema kuweka mifumo kama ya wenzetu kwenye nchi zilizoendelea ambapo mtu ukiwa na kazi au shughuli ya kufanya ya kipato unaweza kupata mkopo wa muda mrefu – hadi miaka thelathini kujenga nyumba au kulipia ununuzi wa nyumba. Utaratibu huo umeanza hapa nchini lakini bado ni mikopo ya muda mfupi, riba ni kubwa na hauwafikii wananchi wote hasa wa kipato cha kati na chini. Kwa hili inabidi tuwape motisha na ahueni ya gharama wajenzi wa makazi mijini hasa Shirika la Nyumba la Taifa kuweza kujenga nyumba nyingi ambazo watanzania wengi watamudu kuzimiliki.

Natambua kwamba kuna changamoto katika urasimishaji wa uchumi kwa hiyo taarifa za historia ya fedha na ukopaji za Watanzania hazipatikani kwa sababu nyingi, ikiwemo kukosekana kwa vitambulisho vya taifa na watu wengi kufanya shughuli zao nje ya mfumo rasmi. Nimefarijika kuanza kuona kwamba kuna makampuni kadhaa yameanza shughuli za kuweka rekodi za ukopaji, yaani *Credit Reference*, kwa ajili ya matumizi ya mabanki na taasisi nyingine. Hili ni jambo jema.

Lakini mimi naamini kwamba kuna fursa ya ubunifu zaidi. Kwa mfano, karibu kila Mtanzania anatumia simu ya mkononi na kila siku anatumia airtime au anahifadhi pesa kwenye simu na kuhamisha na kufanya manunuzi mbalimbali. Simu ni kama akaunti ya benki siku hizi. Na kwenye simu kuna taarifa muhimu ya kujua nguvu ya kiuchumi ya kila mtumiaji simu. Makampuni ya simu, kwa ruhusa ya watumiaji, yanaweza kutumia taarifa hizi kama credit reference na kuwezesha watu wasio kwenye sekta rasmi lakini wenye nguvu ya kiuchumi kuweza kukopesheka na kupata mikopo nafuu ikiwemo ya ununuzi na ujenzi wa nyumba au mikopo ya biashara.

25

Inaelekea siku hizi kila mwanasiasa anajikita katika kundi la vijana na kuzungumzia masuala yanayowavutia vijana. Hakuna makundi mengine ya kuyasemea? Ni makundi gani na mahitaji yao ni yapi na ufumbuzi wa changamoto zao ni upi?

Ni kweli, labda kutokana na wingi wao na hamasa yao. Lakini yapo makundi mengine muhimu katika jamii ambayo yana changamoto mahsusi na mahitaji mahsusi. Labda nitaje makundi manne.

Kwanza ni wanawake. Wanawake ndio mhimili wa ustawi wa jamii yetu. Wanawake ndio walezi wa kwanza. Wanawake ndio wazalishaji mali wakubwa. Ustawi wa wanawake ni ustawi wa taifa.

Wanawake wana changamoto au mahitaji makubwa manne. Kwanza, fursa za kipato. Wanawake wa Tanzania wengi wanajishughulisha na shughuli za biashara na uzalishaji mali. Ni mara chache kukuta mwanamke hajishughulishi na biashara ya aina moja au nyingine. Lakini shughuli nyingi za kinamama zingeweza kuwa na tija kubwa kuliko ilivyo sasa. Tatizo ni mtaji mdogo, fursa finyu na ukosefu wa elimu ya ujasiriamali. Kwa hiyo, hitaji la kwanza ni mikopo, elimu ya ujasiriamali na fursa zaidi za kuongeza vipato. Nimepata bahati ya kujihusisha mara nyingi na ulezi au ufadhili wa vikundi vya ujasiriamali na uzalishaji mali vya kina mama. Nimeona jinsi ambavyo mtaji na elimu ya ujasiriamali na kupatikana kwa fursa kunavyoweza kubadilisha maisha ya wanawake. Benki ya Wanawake inaweza kupanuliwa na kutoa mikopo mingi zaidi na kufika kila kona ya nchi yetu. Mifuko mbalimbali, ikiwemo mifuko ya hifadhi ya jamii, inaweza kufika kila pahala na kutoa elimu na mikopo kwa wanawake. Hatuna budi kuanzisha mpango maalum wa viwanda vidogo-vidogo kwa kutumia mashine ndogo za uzalishaji mali au cottage industries kwa lugha ya kigeni, ambazo zitaendeshwa na kinamama.

Changamoto nyingine ya kina mama, hasa vijijini, ni huduma ya afya, hasa afya ya uzazi. Wanawake wengi wanafariki wakati wakijifungua, jambo ambalo

halikubaliki kabisa. Kama Mbunge ninayetoka jimbo la vijijini, hili naliona na nakabiliana nalo mara nyingi. Serikali imejitahidi kukabiliana na changamoto hii na vifo vimepungua. Lakini idadi bado ni kubwa. Wanawake wengi wanajifungulia majumbani bila msaada wala vifaa vya kitaalam. Jawabu la msingi ni kuhakikisha kwamba huduma ya afya inakuwepo kwenye kila kijiji na kuna watumishi wa kuwahudumia wanawake wajawazito. Jambo la faraja ni kwamba Serikali inaendelea na mpango wa kueneza huduma hii na Rais Kikwete amekuwa mstari wa mbele na anatambulika duniani kwa jitihada za kupunguza vifo vya uzazi.

Huduma duni za maji, hasa maeneo ya vijijini, ni changamoto kubwa kwa kinamama. Naamini hili nimeliongelea ufumbuzi wake hapo awali. Lakini kwa kifupi, tukimaliza changamoto ya maji basi tumepunguza kwa asilimia kubwa ya kero za kinamama vijijini.

Wanawake wanakabiliwa pia na changamoto za tamaduni, sheria na mifumo inayowakandamiza. Hapa ni lazima tuendelee na harakati za kuziondoa. Kuwe na adhabu kali kwa wanaonyanyasa wanawake. Tubadilishe sheria zinazohusu mirathi, watoto, ardhi na ndoa ili kutoa haki na usawa kwa wanawake. Lakini kubwa na la msingi ni kusaidia elimu ya wasichana kwa ngazi zote ili waweze kutimiza ndoto zao katika maisha na tuwe na viongozi wengi wanawake wenye weledi kwenye nyanja mbalimbali.



January Makamba akitaniana na bibi yake mzaa baba (mama yake Mzee Makamba) marehemu Bibi Masau.

Kundi jingine ni la wazee. Wazee, ingawa wako wachache, lakini ni kundi muhimu sana.

Wazee wetu wametoa mchango mkubwa hadi nchi yetu imefikia hapa ilipo.

Wengi wametumia jasho lao katika ujana wao kutoa mchango katika maendeleo ya nchi yetu. Katika uzee wao, ambapo nguvu za kufanya kazi na kupata kipato zimepungua, ni muhimu jamii sasa ikawatumikia wao. Kwa idadi yao, inawezekana kabisa, kama sehemu ya hifadhi ya jamii, kuwapa posho ya kujikimu kila mwezi. Wazee wakiwa ombaomba au wakiishi kwa adha ni fedheha kwa jamii. Hili la kuwafanya waishi maisha ya staha tunaweza kabisa kulifanya.

Kundi jingine ni la walemavu.

Ulemavu sio laana wala sio kukosa uwezo. Ulemavu ni kutokana na mazingira tuliyoyaweka kwenye jamii. Tunaweza kabisa kuyabadilisha haya mazingira na kuwapa uwezo wenzetu wenye ulemavu wa aina mbalimbali kuweza kuwa sehemu ya jamii na kutoa mchango wao kwa kadri uwezo na vipaji vyao vinavyoruhusu.

Walemavu lazima walindwe kisheria dhidi ya uonevu na unyanyasaji, ikiwemo kunyimwa haki na fursa kutokana na ulemavu wao. Muhimu kuwe na juhudi za makusudi, za kisera, kisheria na kiutendaji, hasa kwenye huduma za jamii, kama vile elimu, kwanza kutambua kwamba tunao watu wenye ulemavu ambao wana mahitaji maalum katika kunufaika na huduma za umma lakini pia kushiriki katika maisha ya taifa. Hili tunaliweza.

Tunao watoto wengi wenye mahitaji maalum lakini tuna changamoto ya shule zinazotoa elimu maalum zenye waalimu wenye uwezo wa kufundisha elimu hiyo na zenye miundombinu inayokidhi mahitaji ya watoto hawa.

Jamii iliyostaharibika ni ile yenye uwezo na utamaduni wa kutunza na kuwezesha watoto wenye mahitaji maalum.

Binafsi, naumia sana ninapotembelea watoto wenye mahitaji maalum na kuona jinsi akina mama wanavyobeba majukumu haya mazito. Serikali ni lazima ibebe jukumu la kuwasaidia hawa watoto na akina mama kwa nguvu zote.

Nataka pia nizungumzie kwa kipekee suala ya mauaji ya ndugu zetu wenye ulemavu wa ngozi, yaani albino. Huu ni ukatili usio na mfano. Serikali haipaswi kuwa na huruma katika kuwasaka na kuwaadhibu wanaofanya vitendo hivi. Ni

muhimu pia kuweka utaratibu wa kuwalinda wenye ulemavu wa ngozi dhidi ya tishio la kutekwa na kuuwawa.

Kundi la mwisho, ambalo ndio kubwa kabisa kuliko yote, ni kundi la watoto. Hawa wako wengi sana na wana mahitaji mahsusi.

Kama tunataka kujenga taifa imara, lenye wazalendo, wachapakazi, wenye uweledi, umahiri na uwezo wa kukabiliana na changamoto za ulimwengu wa sasa, basi lazima tuwekeze kwa watoto.

Mahitaji yao makubwa ni elimu, lishe bora na afya. Katika mazingira ya sasa, ambapo asilimia karibu 42 ya watoto wanakabiliwa na matatizo ya lishe, ni vigumu kutengeneza taifa imara. Mambo makubwa mawili ya kufanya: kwanza kuimarisha mfumo wa elimu na kuwawezesha watoto wote kupata elimu iliyo bora. Hili la elimu ulikwishaniuliza na tumelizungumza kwa kirefu. Jingine ni lishe bora. Watoto wanastahili kupata chakula shuleni. Kwa sasa, katika maeneo mengi, watoto wanashinda na njaa shuleni. Hili halikubaliki na tunao uwezo, kama Serikali na kama wazazi kulibadilisha. Lakini pia watoto wana haki zao za msingi, ikiwemo kutotumika kama wafanyakazi. Haki hizi lazima zisimamiwe na kutekelezwa.

Tafiti nyingi za hivi karibuni zimeonesha ongezeko la vitendo vya watoto wadogo kubakwa, kunajisiwa na kufanyiwa vitendo vingi vya udhalilishaji na ndugu, jamaa na marafiki wa karibu wa familia. Jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba hatua stahiki hazichukuliwi dhidi ya watu wanaofanya vitendo hivyo. Vitendo hivi vikitokea wanafamilia husisitiza kesi hizi kuamuliwa katika ngazi ya familia bila kujali madhara waathirika wa vitendo hivi watakayopata siku za mbeleni.

Napendekeza kila mmoja wetu, kuanzia ngazi ya familia, mtaa, kijiji na taifa tuwajibike kuwalinda na kuwalea watoto kwa pamoja kama hapo zamani wakati kila mtoto alikuwa wa jamii nzima na kila mtu aliwajibaka kuhakikisha kila mtoto wetu ni salama.

Tanzania imetia sahini mikataba mbalimbali ya kimataifa na kuna sheria kali za kuwalinda watoto, kwa hiyo ni muhimu sheria hizi zikatekelezwa ili kusaidia kulinda watoto wetu.

Nafarijika kwamba katika mjadala wa Katiba mpya na katika mapendekezo ya rasimu za katiba zote, ile ya Tume na hii inayopendekezwa, haki za makundi haya yote zimezingatiwa, kufafanuliwa vizuri na kulindwa.

26

Umekuwa mmoja ya viongozi ambao wanaliongelea sana suala la mabadiliko ya kasi ya kuongezeka kwa idadi ya watu nchini na taifa kuwa changa kiumri. Unaweza kutuelezea kwa upana nini maana ya mabadiliko haya kwenye mustakabali wa taifa letu la leo na la kesho?

Ni kweli nimekuwa naliongelea sana suala hili kwa kuwa ninaamini huwezi kuongelea mipango ya kesho ya Taifa letu bila kuelewa uhalisia wa idadi ya watu na mgawanyo wao kiumri. Hili ni jambo la muhimu tunapotaka kujenga Tanzania tuitakayo. Ni kweli idadi ya watu bado inaongezeka kwa kasi Tanzania.

Na ni kweli nchi yetu ni changa sana na inaendelea kuwa changa kwa spidi kali. Wakati Rais Mkapa anaapishwa Novemba 1995, nusu ya Watanzania waliopo sasa walikuwa hawajazaliwa. Vijana nchi hii chini ya umri wa miaka 35 ni asilimia 80 ya idadi ya watu, wakati watoto chini ya miaka 5 ni karibu asilimia 20 ya Watanzania wote. Vijana wa umri wa chini ya miaka 35 ni wengi kuliko idadi ya Watanzania wote miaka kumi tu iliyopita. Ninavyoongea hapa, watu wa umri wangu, yaani miaka 41, ni wakubwa kuliko asilimia 85 ya Watanzania. Na ambacho ni kigumu kusadikika, wazee wenye miaka 60 au zaidi kiumri ni asilimia 4 tu ya idadi nzima ya Watanzania.

Padre mimi na wewe kwa sasa tumeshakuwa kwenye kundi la wazee tukifananishwa na uhalisia wa uchanga wa nchi yetu.

Lakini naomba ieleweke kwamba hali hii ya idadi kubwa ya watu na uchanga wa Taifa sio janga kama wengi wanavyohubiri. Inategemeana na jinsi ambavyo tutajipanga kama taifa. Pamoja na hayo, naomba niongelee hali hii kwa kuangalia fursa na changamoto zinazokuja na uhalisia wa idadi ya watu na mgawanyo wa kiumri katika taifa letu.



January Makamba akisikiliza shida ya mwananchi katika mji wa Ifakara Novemba 2014.

Kwa upande wa changamoto, ni wazi uchanga wa taifa letu unaongeza changamoto katika kutoa huduma muhimu kama za elimu, afya na fursa za kazi. Kwa upande wa afya, inabidi tujipange vizuri kuweza kutoa huduma za afya kwa kina mama na watoto. Tunapoongea sasa hivi, kwa wastani kila mwanamke wa kitanzania anatarajiwa kuzaa watoto 5 katika maisha yake.

Mwaka jana tu, takriban watoto milioni 1.5 walizaliwa nchini. Hapa tunapoongea, kuna watoto zaidi ya milioni 10 walio na umri wa chini ya miaka 6. Hawa ni watoto wengi sana ambao inabidi tuwapatie huduma bora za kliniki na matibabu bure na lishe bora ili wakue vizuri kimwili na kiakili. Lakini watoto kama ni wengi kiasi hiki maana yake wazazi nao ni wengi mno. Na hawa wanahitaji huduma za afya ya uzazi vilevile.

Hii ni changamoto kubwa kwa nchi yenye bajeti finyu kutenga fedha za kutosha kuwahudumia vizuri watoto wetu na wazazi wetu hawa wapya.

Kwa upande wa elimu, hivi sasa tuna wanafunzi zaidi ya milioni 12 walioko shuleni, kuanzia shule za awali mpaka Chuo Kikuu. Mwaka huu tunao watoto zaidi ya milioni 1.5 ambao wako tayari kuanza darasa la kwanza. Hapa napo tunahitaji kuongeza uwezo wa shule zetu zote kuanzia za awali mpaka vyuo vikuu kuchukua wanafuzi wengi zaidi na kuwapatia elimu iliyo bora bila kuathiriwa na wingi huu. Hii ni changamoto kubwa ambayo lazima tuikabili.

Changamoto haziishii kwenye elimu tu. Mpaka sasa hivi tuna vijana zaidi ya milioni 22 kwenye soko la ajira, na kila mwaka wanaongezeka zaidi ya vijana 900,000 katika kutafuta ajira wakati ajira mpya kwenye sekta rasmi hazifiki 50,000. Mpaka mwaka 2030, tunatarajia kuwa na watu zaidi ya milioni 40 kwenye soko la ajira. Pia ni muhimu kufahamu kuwa zaidi ya asilimia 90 ya watafuta kazi hawa hawana elimu ya sekondari. Hii ni idadi kubwa sana ya nguvu kazi, na ni changamoto kwa Serikali kuweka mazingira mazuri yatakayotia chachu ya uwepo wa ajira za kuwachukua watu wote hawa.

Ingawa changamoto ni nyingi na nzito, mimi napenda kuangalia hali hii kama fursa nzuri kwa taifa letu.

Mgawanyo wa kiumri wa watu katika taifa letu unatoa fursa kubwa ya kuwa na nguvu kazi kubwa kuliko wategemezi ndani ya miaka michache ijayo. Kinachohitajika hapa ni uongozi wenye weledi wa kutambua fursa hii na kuiweka nchi tayari iweze kuvuna mafao ya mgawanyo huu wa kiumri, au kwa kiingereza *demographic dividend*.

Ni lazima tuwekeze sana kwenye elimu, hasa elimu ya wasichana, afya na muhimu zaidi, tuandae kazi sahihi zenye tija katika sekta zitakazosukuma gurudumu la maendeleo ya nchi yetu mbele. Nchi za Asia ya mashariki zijulikanazo kama *Asian Tigers* ziliweza kujipanga vizuri na kufanikiwa kuvuna mafao mengi yaliyopelekea ukuaji wa uchumi kufikia kipato cha juu. Naamini kabisa tukijipanga vizuri kisera na kiutekelezaji, na sisi tutafanikiwa kufikia uchumi wa kipato cha kati ndani ya miaka michache ijayo.

Lakini pia ni vyema tukatambua kuwa hali hii ya mfumo wa umri mdogo haikai nasi milele. Nchi kama Japan, miaka ya 1950 na 1960, ilikuwa na hali kama ya kwetu ya idadi ya kubwa ya vijana. Wakaitumia vizuri na kusomesha vijana wao katika nyanja za sayansi na teknolojia na kuifanya Japan ipae kwenye uchumi na uzalishaji mkubwa wa bidhaa za thamani kubwa ikiiga mifano ya nchi ya Marekani. Sasa hivi mfumo wa rika wa Japan umebadilika, wazee ndio wengi zaidi na Wajapan hawazai na hawaongezeki kabisa na nguvu-kazi imepungua. Lakini waliweka msingi wa uchumi imara. Japan sasa hivi suala kubwa la kisiasa ni pensheni, sio ajira tena. Sisi ni ajira. Lakini itakuja kufikia, labda miaka 50 ijayo, ambapo wazee watakuwa ni wengi zaidi ya vijana na watakuwa na nguvu kubwa ya kisiasa inayotokana na idadi yao na watataka kutunzwa na Serikali. Kama wengi hawakuwa na kazi ujanani na kuhifadhi pensheni basi litakuwa janga jingine. Hivyo ni lazima tuelewe kwamba hatuna muda wa kuuma vidole tukisubiri maajabu yatutokee, ni lazima kwa dhati kabisa tujipange na tupambane kuweza kuvuna mafao ya uchanga wa taifa letu.

27

Miaka ya hivi karibuni imejitokeza dalili kwamba mahusiano ya watanzania wenye dini tofauti si mazuri na kuna dalili kwamba hali hii inaweza kuleta kutoelewana siku za usoni. Wewe unalisemeaje suala hili? Nini nafasi ya imani ya kiroho katika kumwongoza Kiongozi wa nchi?

Moja ya sifa kubwa za nchi yetu ni umoja wetu – upendo, mshikamano, ushirikiano na uhusiano mzuri baina ya Watanzania wa dini, makabila na rangi mbalimbali.

Viongozi waliotangulia wamefanya kazi kubwa ya kuujenga umoja huu. Mwalimu Nyerere alionya tangu mwaka 1995, karibu miaka 20 iliyopita kuhusu nyufa zinazoanza kujitokeza na kuhatarisha umoja wetu – nyufa mojawapo ikiwemo ya udini.

Watanzania wengi wenye dini tofauti bado wanapendana, wanashirikiana na hata kuoana. Tatizo ni viongozi wachache, wa kisiasa na kijamii, ambao wanatumia dini kufanikisha malengo yao ya kisiasa na kijamii kwa kuchochea chuki baina ya watu wa dini tofauti. Watu hawa ni hatari sana ni lazima tuwabaini, tuwatenge, tuwadhibiti na tuwaadhibu haraka sana. Serikali yetu inao wajibu katika hili lakini pia jamii inao wajibu.

Matukio ya kuchomwa nyumba za ibada na kudhuriwa na kuuwawa kwa viongozi wa dini yanapaswa kukomeshwa mara moja na wahusika kutiwa mbaroni na kuhukumikiwa. Viongozi wa dini na madhehebu mbalimbali wamefanya kazi nzuri ya kuendelea kuhubiri upendo na uvumilivu licha ya maumivu haya, lakini na sisi viongozi wa siasa tutimize wajibu wetu.

Serikali haina dini lakini lazima iwalinde waumini wa dini wasidhuriwe kutokana na imani zao.



January Makamba akisalimiana na Msaidizi wa Askofu wa Jimbo la Katoliki la Mahenge Msinyori Callistus Mdai.

Kama kuna hujuma inafanyika ili kutugawa kwa misingi ya kidini vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vifanye kazi ya kubaini hujuma hizo na kuzidhibiti.

Na wale wanasiasa wanaoomba nafasi za kisiasa kwa misingi ya dini nao wanapaswa kuwekwa pembeni, kama ambavyo Mwalimu Nyerere alituasa. Nchi yetu hii ni moja, hatuna nchi nyingine ya kwenda, ni muhimu sote tukaendelea kupendana na kushirikiana. Kizazi kipya cha viongozi kinayo nafasi na wajibu wa kipekee ya kuendelea kuijenga Tanzania ya watu wanaopendana na kushirikiana.

Sasa umeniuliza swali lingine kwamba nini nafasi ya imani ya kiroho katika kumwongoza Kiongozi wa nchi?



January Makamba akifurahia jambo na Askofu wa Kanisa la Anglikana Jimbo la Tanga Mhashamu Maimbo Mndolwa katika harambee ya ujenzi wa shule ya kanisa Misozwe, Muheza.

Kwanza mimi naamini kama Mungu yupo na ndio muweza wa yote. Ndio mwenye kutoa neema kubwa kubwa na neema ndogo ndogo. Mfalme wa mbingu na ardhi. Mengi yaliyo mema tunafundishwa kutoka katika vitabu vya Mungu na mengi yaliyo mabaya tunakatazwa kutoka kwenye vitabu vya Mungu.

Nchi yetu ili istawi na kushamiri ni muhimu kwa viongozi wake na watu wake kumpenda Mungu na kufuata mafundisho yake. Dini ya kiongozi haipaswi kuongoza nchi lakini imani kwamba Mungu yupo ni muhimu kiongozi awe nayo. Mtu ambaye hamjui wala hamuogopi Mungu hafai kuwa kiongozi.

Lakini pia kiongozi hapaswi kuivaa dini yake kama tai au kofia kwa sababu anaongoza watu wa dini mbalimbali. Kiongozi hapaswi kupendelea au hata kuonekana ana chembechembe za kupendelea watu wa dini yake. Kiongozi anapaswa kuwalinda watu wa dini zote bila kutetereka. Kiongozi anapaswa kukemea na kuondosha sheria, kanuni, taratibu, taasisi, kauli au tamaduni zinazopendelea dini moja dhidi ya nyingine. Dini ya kiongozi haipaswi kuwa sababu ya yeye kuchaguliwa au kutochaguliwa.



January Makamba akiwa kwenye Maulidi jimboni Bumbuli.



January Makamba akiwa na Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Askofu Mkuu wa KKKT Dr. Alex Malasusa na Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini Mashariki Dr. Stephen Munga.



January Makamba akibadilishana mawazo na Mhashamu Baba Askofu Evaristo Marc Chengula wa Jimbo la Katoliki la Mbeya.

Kiongozi anaweza kuwa wa dini yoyote lakini cha muhimu asiwe mdini.

Watanzania wa dini yoyote wapo tayari kuchagua kiongozi wa dini yoyote. Ambacho hawataki ni kiongozi mdini.

Naomba nimalize kwa kusema, Tanzania ni nchi yenye waumini wa dini tofauti ila misingi ya upendo, heshima, amani, umoja, mshikamano, ujirani mwema ipo kwenye vitabu vyote vya Mungu lakini pia ipo kwenye katiba na sheria zetu. Hivyo sisi kama viongozi tutahakikisha kwamba misingi hii muhimu ya dini na katiba tunaisimamia.

28

Wewe kama kiongozi kijana, umewasaidiaje hawa vijana wenzenu wa *Bongo Movies* na vijana wa muziki wa kizazi kipa maana yake kila siku wanalalamika. Pia inaelekea tumetelekeza maendeleo ya sanaa kwa ujumla. Tufanyeje?

Ni kweli vijana wengi kwenye sanaa hizi za muziki na filamu ni wadogo zangu, wapo ambao wapo kwenye muziki wa injili ambao na rafiki zangu na walinichagua kuwa mlezi wa Chama cha Muziki wa Injili Tanzania, pia wapo wazee wangu kwenye muziki wa dansi. Kwa hiyo, ninao wajibu wa kusaidia kama kiongozi lakini pia kama mtu wa karibu na wasanii hawa. Nimejaribu kufanya hivyo kwa miaka 8 sasa, kwa msanii mmoja mmoja na kwa makundi. Kwa kifupi sana, nimefanya mambo kadhaa: kwanza, ingawa hili halijatangazwa sana, lakini watu wa TRA, BASATA, COSOTA na wengineo wanafahamu kwamba kuanzia mwaka 2008 nikiwa Msaidizi wa Rais, niliitisha vikao vya wadau wa muziki na filamu, ikiwemo wasambazaji wote wa filamu, ili kuangalia namna ya kuisaidia tasnia hizi. Katika kikao nilichoongoza, ndipo wazo la stika za TRA tulipolibuni kwa mara ya kwanza. Hata hivyo, suala hilo lilihitaji utafiti kidogo, na utafiti huo ulihitaji pesa. Nikaenda kumuomba Rais Kikwete pesa hizo, akakubali kutoa shilingi milioni 20, ambazo zilipelekwa TRA ambao ndio waliosimamia utafiti huo. Dhana nzima ya kuanzisha stika ilikuwa ni kwamba kazi za wasanii lazima zitambuliwe rasmi na kuwe na taasisi Serikalini inayosimamia uchakachaji wa kazi hizo kwakuwa huko nyuma ilikuwa ni holela tu na ilionekana kama halali kufanya uharamia kwenye kazi za wasanii. Tukaona kwamba, kwa kuwa, ukiwa na sigara feki, mvinyo feki au konyagi feki, unakamatwa na Serikali, basi tuweke utaratibu kwamba ukiwa na CD feki basi pia ukamatwe na Serikali. Na kwakuwa sigara, konyagi na mvinyo zinawekwa stika ili kuzitambua halali na feki, basi na kwenye kazi za wasanii na kwenyewe tuweke stika za TRA ili Serikali iwe na wajibu wa kusimamia kazi hizi. Bahati nzuri tukaanza utekelezaji. Imechukua muda na mwanzo tumeanza



January Makamba akiwa na wadau wa Tasnia ya Filamu Tanzania katika msiba wa mwigizaji wa filamu maarufu nchini marehemu Sajuki.

kwa kusuasua na kukiwa na changamoto za hapa na pale lakini naona sasa TRA wameamka na kuanza kukamata kazi feki. Kwa hiyo, naona fahari kwamba hili ni jambo nililianzisha, kwa maelekezo ya Rais, nikiwa Ikulu na likaingizwa kwenye mfumo wa Serikali na kupelekwa Bungeni na sasa ni utaratibu rasmi.

Jingine ambalo nimefanya kusaidia wasanii ni kufanya watambulike na waheshimike na washirikishwe kwenye shughuli rasmi za Serikali. Kabla ya mwaka 2005, wasanii hawa walikuwa wanaonekana kama wahuni tu na hawakuwa karibu na Serikali wala viongozi wa Serikali. Katika kampeni za uchaguzi za mwaka 2005, ambapo nilishiriki kama Msaidizi wa Mgombea Urais wa CCM, Mheshimiwa Kikwete, nilishauriana naye na tukaamua tuwashirikishe hawa wasanii kwenye mikutano yetu na shughuli zetu. Tukaanza na Bushoke. Akabadilisha wimbo wake wa Mume Bwege na kuweka maneno mapya na ukawa wimbo wa kampeni za CCM. Nakumbuka pesa ya kwenda kurekodi upya nilitoa mfukoni mwangu. Baada ya hapo, wasanii wengine karibu wote nao wakaingia. Rais akawapenda wote. Akawa anakula nao chakula, anapiga

nao picha. Alivyoingia madarakani, kwa mara ya kwanza kabisa, wanamuziki hawa tukawaalika lkulu. Mwanzo jambo hili lilistua wengi na kuzua mjadala lakini baadaye likaonekana ni jambo la kawaida. Na Serikali nzima ikaona ni sawa kuwashirikisha kwenye shughuli za kiserikali. Baadaye ikawa hivyo hivyo kwa wasanii wa filamu na wengineo. Kwahiyo, nilifungua mlango kwa wasanii vijana kuanza kutambuliwa na Serikali na viongozi wa Serikali. Lakini pia nilikuwa mfadhili wa mwanzo kabisa wa Tanzania House of Talent.

Lakini vilevile kwa nafasi yangu ya sasa, nimefanya vikao na wahusika, hasa makampuni ya simu, kuhusu utaratibu wa malipo kwenye miito ya simu. Bado hatujamaliza lakini mambo yamebadilika kidogo na yataendelea kubadilika. Lakini pia nimeshiriki katika kuweka presha ya mwanzo kwa vyombo vya habari, redio na televisheni, kuwalipa wasanii pale wanapopiga nyimbo zao. Nilitambulisha kwa Waziri wa Viwanda na Biashara Mheshimiwa Kigoda, vijana wenye teknolojia na utaratibu wa kuweza kubaini nyimbo zote zilizopigwa na redio na luninga zote, au filamu zote zilizoonyeshwa kwenye luninga, siku gani na kwa muda gani. Mazungumzo kati ya COSOTA, wenye redio na TV na wasanii yamefanyika mara kadhaa na mradi mpya umeanzishwa na Ndugu Rashid Shamte na unaosimamiwa na produsa mkongwe hapa nchini, P-Funk, kwa ajili ya kufanikisha jambo hilo.

Pia nimeendelea kuwasaidia wasanii hawa mmoja mmoja kwa shida zao mahsusi. Nisingependa kuwataja na kuzitaja hapa kwa sababu sio ustaarabu ila wasanii wengi wanajua kwamba mimi ni rafiki yao na mtu wao na nitaendelea kuwa hivyo. Yapo mengi nimeyafanya kimya kimya kusaidia tasnia hizi, ambayo siwezi kuyaorodhesha yote hapa.

Lakini pia nilishirikiana na wasanii wa filamu, bendi na Bongoflava kuhakikisha katiba pendekezi inawatambua wasanii hawa na kazi zao. Kutambuliwa huko kutawapa nguvu kisheria na kupelekea kutengenezwa kwa sera mpya itakayotambua sanaa kama sehemu ya utamaduni na biashara, tofauti na sera ya zamani inayotazama sanaa kama utamaduni tu.

Pia katika Wizara yetu, nilisimamia kikamilifu na sasa tuko mbioni kukamilisha kanuni zitakazoweza kuzibana kampuni za simu kuweka utaratibu utakaowanufaisha zaidi wasanii kwenye biashara ya miito na milio ya simu.

Kwa juhudi hizi zote, niliteuliwa kuwa mlezi wa Chama cha Muziki wa Injili Tanzania na kuna mambo makubwa zaidi tunayapanga kupitia chama chetu hicho.

Kuhusu maendeleo ya sanaa kwa ujumla, kama ulivyouliza, niseme kwa kifupi tu kwanza kazi za sanaa na ubunifu, na ninamaanisha sanaa za aina zote ni sehemu muhimu ya utambulisho wa taifa, utamaduni wake. Sanaa inaeleza sisi ni nani. Kwa msingi huo, sanaa za kwetu lazima zienziwe, zihifadhiwe, na ziendelezwe. Lakini kwa upande mwingine shughuli za sanaa na ubunifu ni shughuli za uchumi na biashara. Ni chanzo kikubwa cha ajira na sehemu ya mchango kwa uchumi wa taifa. Nchi nyingi, kama vile Nigeria, India, Marekani na kwingineko, tasnia za sanaa na ubunifu, au *creative industries* kwa Kiingereza, zinatoa mchango mkubwa kwa pato la taifa. Kuna kitabu kizuri kilichoandaliwa na Shirika la Haki Miliki Duniani alinipa zawadi mwanamuziki mkongwe nchini Bwana John Kitime kinaonyesha ukubwa na umuhimu na thamani kubwa ya kazi na sanaa na ubunifu katika uchumi wetu, hasa katika kutoa ajira na kuchangia pato la taifa.

Lakini bado mchango huu unaweza kuwa mkubwa zaidi na watu wanaojishughulisha na shughuli hizi wakanufaika zaidi kuliko ilivyo sasa na serikali ikapata mapato zaidi kuliko ilivyo sasa.

Muarubaini ni kurasimisha shughuli hizi – ni kutengeneza mifumo inayotambulika, iliyo wazi, ili kuondoa dhulma, na mifumo inayoendeshwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zinazoeleweka. Hali ya sasa sio nzuri. Tunatengeneza masikini wenye majina makubwa. Hata hivyo, yapo matumaini kwa sababu tunaanza kuona baadhi ya wasanii wanaishi vizuri, wanajenga majumba, wananunua magari ya kifahari, wanasomesha watoto na kuendesha maisha yao kwa kazi za sanaa. Lakini sio wa kutosha. Naamini upo uwezekano wa kufanya vizuri zaidi.

Kwanza, tukiweka sheria kali zaidi ya kudhibiti uharamia. Zaidi ya sheria, tukiweka taasisi za kusimamia utekelezaji wa sheria hizi. Kwa sasa adhabu inayotolewa kwa uharamia wa kazi za wasanii ni ndogo sana na hakuna taasisi wala mfumo mzuri wa kusimamia udhibiti wa uharamia. Katika kufanikisha hili, nilishirikiana na wasanii wa filamu, bendi na bongoflava kuhakikisha kazi zao zinatambuliwa na kulindwa kisheria kwenye katiba inayopendekezwa. Kutambuliwa kisheria kwa kazi hizi kutawapa wasanii nguvu za kisheria kutapelekea kutengenezwa kwa sera mpya ya utamaduni itakayotambua sanaa kama sehemu ya utamaduni na biashara, tofauti na sera ya sasa ambayo inatazama sanaa kama utamaduni tu.

Jambo la pili ni kubadilisha mfumo mzima wa kuzalisha, kusambaza na kununua kazi za sanaa. Mfumo uliopo sasa ni holela na hautoi manufaa makubwa kwa wabunifu, watunzi na wanasanaa kwa ujumla bali kwa wafanyabiashara. Mfumo

wa sasa unamdhalilisha mwenye kipaji na kumpa nguvu kubwa mwenye mtaji. Tukiwa na mfumo rasmi na ulio wazi wasanii na wabunifu wengi watapata manufaa zaidi.

Jambo la tatu, ni maendeleo ya sanaa kwa ujumla. Sanaa za aina zote zinapaswa kuendelezwa kama sehemu ya urithi na utambulisho wa taifa. Nchi nyingi zinawekeza katika maendeleo ya sanaa. Na sisi tunapaswa kufanya hivyo. Vipaji vinapaswa kuibuliwa na kuendelezwa. Elimu na mafunzo ya sanaa mbalimbali ni muhimu. Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TASUBA) na Idara ya Sanaa na Sanaa za Maonyesho (FPA) ya Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam havitoshi. Zipo aina mpya za taaluma, kama uendeshaji wa filamu, uhariri wa filamu, na kadhalika ambazo ni vyema kukawa na taasisi zenye weledi kuweza kuwafundisha vijana wetu. Kwenye hizi taaluma huwezi kuendelea kufanya kwa kubahatisha kwa muda mrefu.

Mwisho kabisa, ningependa sana kuona sanaa za maonyesho ya asili ya Mtanzania zinarudi na kupata heshima yake. Ningependa kuona utunzi na uandishi wa tamthiliya na riwaya za Kitanzania unarudi kwa kasi na vijana wanashiriki. Ningependa kuona ngoma zetu za asili zinapata heshima na kuthaminiwa na kutambuliwa na kuonyeshwa zaidi. Shaka yangu ni kwamba tusiwe tunajenga taifa la vijana ambao hawajui kabisa asili yao na wanapoteza kabisa utambulisho wao na fahari yao.

La msingi hapa ni fedha za kuendeleza sanaa. Lazima Serikali iwekeze kwenye kuendeleza sanaa mbalimbali.

Napendekeza tuanzishe Mfuko wa Sanaa wa Taifa ambao utapata fedha kwenye tozo dogo la viingilio kutoka kwenye shughuli zote za burudani nchini. Mfuko huu hautaendeshwa na Serikali pekee bali kwa kushirikiana na magwiji wa sanaa mbalimbali nchini na utaendeshwa kwa uwazi na uhuru. Moja ya majukumu yake itakuwa kutoa fedha kwa njia ya tuzo au ruzuku katika kuibua vipaji na kuendeleza kazi za sanaa. Pia unaweza kusaidia kutoa mtaji kwa wasanii katika tasnia mbalimbali ambao wameamua kuwekeza katika kazi zao wenyewe na kazi za wenzao.

29

Tanzania imekuwa ikijulikana kama kichwa cha mwendawazimu kwenye medani ya michezo ya kimataifa. Ni muda mrefu sasa tumeshindwa kupata medali zozote kwenye michezo ya Jumuiya ya Madola au Olimpiki. Mara ya mwisho kwa Taifa Stars kushiriki fainali za kombe la Mataifa ya Afrika ilikuwa ni miaka 36 iliyopita. Una fikra gani mpya katika kulirekebisha hili na kuwafanya Watanzania kujisikia fahari kutokana na mafanikio ya wanamichezo wake?

Kwanza nianze kwa kusema kuwa inafedhehesha sana kuona kwamba takriban asilimia 80 ya Watanzania walikuwa hawajazaliwa mara ya mwisho tumeshiriki katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika, kwa hiyo hawajapata faraja ya kuiona timu ya taifa ikipeperusha bendera huko. Vile vile nikukumbushe kwamba mwaka huo huo wa 1980 ndio mara ya kwanza na ya mwisho tuliweza kushinda medali za Olimpiki, rafiki yangu Mzee Suleiman Nyambui na Mzee wetu Filbert Bayi ndio walitutoa kimasomaso kipindi kile. Kwa taifa kubwa linaloheshimika dunia nzima kwa mambo mazuri hii ni aibu.

Tunapaswa kufanya mageuzi ya michezo katika nchi yetu. Watanzania wanastahili kupata fahari na kujivunia kuona vijana wao wakipeperusha bendera yao kwenye steji za kimataifa.

Ninayo mawazo ambayo tukiyaifanyia kazi nina uhakika tutapiga hatua kubwa na za haraka katika medani ya michezo.

Lazima tutambue kwamba maendeleo ya michezo yanatokana na vitu muhimu vinne. Kwanza, ni lazima kuwepo na vipaji, bahati nzuri nchi yetu ina vipaji vya kutosha katika aina zote za michezo. Pili, ni miundombinu na mifumo

ya kubaini na kuviendeleza vipaji hivyo, hii ni changamoto. Tatu, ni utawala, uongozi, na uendeshaji wa tasnia ya michezo, hii pia ni changamoto. Na nne, ni uwekezaji wa Serikali na sekta binafsi katika tasnia ya michezo, hii nayo pia ni changamoto. Hivi vitu vinne ni lazima viwepo ili tuweze kupata mafanikio kwenye medani ya michezo.

Baada ya kusema hayo, sasa nikueleze fikra zangu ambazo tukizitekeleza vizuri zitatusaidia kupata mafanikio katika michezo. Fikra hizi mzizi wake ni hayo mambo matatu niliyoyaelezea hapo awali.

Kwanza kabisa ni lazima tuanzishe vituo vikubwa vya michezo au sports academies kwenye kila kanda ya nchi yetu vyenye hadhi ya Kiolimpiki.

Kwa maana hiyo, tutakuwa na vituo vya aina hii sita katika nchi yetu ambavyo vitazungukwa na shule za boarding za msingi na Sekondari. Lengo kubwa ni kukusanya wanafunzi wote kwenye kanda husika ambao wameonekana kuonyesha vipaji ambavyo vinapaswa kuendelezwa. Hapa watapata fursa ya kusoma na kuendelezwa vipaji vyao vya michezo ya aina yote. Ukweli ni kwamba bila kuendeleza vipaji katika mazingira mazuri, basi tusahau kabisa kufanya vizuri kwenye michezo. Hili linaweza kufanywa kwa ushirikiano wa serikali na sekta binafsi.

Lazima kurudisha michezo mashuleni kwa nguvu kubwa zaidi kama ilivyokuwa zamani. Kuwe na masharti kwamba kila shule iwe na viwanja vya michezo na wakati wa kufanya shughuli za michezo. Tunaona siku hizi kwamba baadhi ya shule zimeachana kabisa na utaratibu huu. Vijapi vinatambulika kuanzia utotoni, kuanzia mashuleni.

Fikra nyingine ni kuhakikisha kila klabu iwekeze kwenye academies za watoto, na lazima kuwe na ligi za kitaifa za watoto. Tufikie wakati ambapo timu za taifa za miaka 10 ijayo ziwe zinaandaliwa kuanzia sasa. Na Serikali itenge bajeti kila mwaka kwa timu hizo ili kuziwezesha kukaa kambini, kufanya mechi za majaribio, na kuziwezesha kushiriki kikamilifu katika mashindano ya kimataifa. Mimi sio muumini wa hizi kamati za zimamoto kusaidia timu ishinde ghafla ghafla wakati siku zote watu hawafanyi maandalizi ya muda mrefu. Watoto wanaotoka kwenye academies za kanda wanahamia moja kwa moja kwenye academies za timu zao au kupata fursa ya kucheza kwa kulipwa nje ya nchi na kupata fursa ya kuendeleza vipaji vyao.

Vipo vilabu vingi vya daraja la kwanza au la pili lakini pia na timu nyingi nzuri za mpira za mitaani lakini zina shida kubwa za fedha za kushiriki

kwenye mashindano na kujiendesha. Serikali itoe motisha kwa sekta binafsi zitakazojitokeza kuzisaidia klabu hizi. Huko nyuma, taasisi na mashirika ya umma na binafsi yalikuwa na timu za michezo zilizokuwa zinafanya vizuri na kutoa michango kwenye maendeleo ya michezo. Kwa mfano, sote tunakumbuka timu nzuri za Pamba ya Mwanza, Sigara, Pilsner, Reli ya Morogoro. Ushiriki huu ulichangamsha sana michezo na ni lazima turudishe utamaduni huu.

Mwisho, ni lazima Baraza la Michezo la Taifa lipewe meno kuhakikisha kwamba viongozi wabovu, wala rushwa, na wababaishaji hawapewi nafasi kwenye vyama vya michezo na klabu. Hili ni tatizo kubwa, kila siku tunasoma kwenye magazeti jinsi malumbano baina ya viongozi wa michezo yanavyoleta migogoro mikubwa na kuzorotesha maendeleo ya michezo. Hapa ni lazima tubadilike, haiwezekani kila kipindi cha uchaguzi wa uongozi migogoro mikubwa inaibuka. Klabu na vyama vya michezo vinahangaika na migogoro kila wakati badala ya maendeleo yenyewe ya michezo.

Kwa kumalizia tu, michezo ni biashara kubwa inayoweza kulileta taifa kipato, kuitangaza nchi yetu na kutoa ajira safi kwa watu wetu. Tuendeshe michezo kibiashara. Umefika muda sasa tuheshimu kwamba uongozi wa michezo ni kama fani nyingine muhimu inayohitaji weledi.



January Makamba akiwa uwanja wa taifa katika mechi ya Simba na Yanga

30

Watu wengi wamekuwa wanalalamikia bandari na reli. Wengine wanasema kwamba kwa takribani miaka kumi sasa bandari na reli ziko vilevile, hakuna upanuzi wala ujenzi mpya. Una maoni gani kuhusu miundombinu ya usafirishaji? Nini kipya kinaweza kufanyika

Suala la miundombinu ya usafirishaji ni lazima tulipe umuhimu wa kipekee. Uchumi wa nchi unaendeshwa na miundombinu ya usafirishaji. Kihistoria hakuna nchi iliyoendelea duniani bila ya mapinduzi katika usafirishaji na uchukuzi. Reli na bandari zina uwezo mkubwa kuchangia Pato la Taifa na kuchochea shughuli za uchumi na biashara huko mikoani na hata nchi jirani.

Watu wengi hupenda kuongelea kuhusu reli ya kati na bandari ya Dar es Salaam. Na swali lako ni wazi limejikita hapo hapo. Hata hivyo, tukitaka maendeleo ya kasi na sawia na tukitaka biashara ishamiri katika maeneo yote nchini lazima tuitazame na tuishughulikie miundombinu ya usafirishaji nchini kama mfumo mmoja.

Kwa hiyo, kwa upande wa bandari, lazima tuziongelee bandari zote muhimu kwenye ufukwe wa Bahari ya Hindi, bandari kubwa za Mtwara, Tanga na Dar es Salaam, Unguja na Pemba na bandari ndogo za Lindi, Kilwa, Mafia, na Pangani. Lakini pia lazima tuziangalie na tuzizungumzie bandari katika maziwa yetu matatu makubwa: katika Ziwa Victoria, bandari kuu ya Mwanza, Nansio, Kemondo Bay, Bukoba na Musoma; katika Ziwa Nyasa, bandari za Itungi, Manda, Liuli na Mbamba Bay; na katika Ziwa Tanganyika, bandari za Kigoma na Kasanga. Mimi nimepata bahati ya kufika katika bandari zote hizi za maziwa yetu haya matatu.

Nafahamu kwamba kuna biashara kubwa sana inafanyika na watu wengi wanazitegemea bandari hizi lakini miundombinu na udhibiti katika bandari hizi si wa kuridhisha. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba, kama viongozi, tusijisahau tunapongelea bandari basi ni bandari ya Dar es Salaam tu. Kazi

ipo kubwa ya kuufanya mfumo mzima wa bandari zetu na muunganiko wa bandari hizi na reli zetu, barabara zetu na viwanja vyetu vya ndege kuwa mfumo thabiti na wa kutegemewa wa miundombinu ya usafirishaji nchini na katika ukanda wa maziwa makuu.

Vilevile, kutokana na jiografia ya nchi yetu, miundombinu ya usafirishaji, hasa bandari, reli na barabara, ni muhimu kuitazama kwa mtazamo wa kikanda. Tunao wajibu wa kuwaunganisha na kuwawezesha majirani zetu ambao hawana bahari kufanya biashara ya kimataifa kwa ufanisi kupitia bandari zetu. Kwa bahati nzuri, wajibu huu tunapoutimiza ipasavyo, sio tu majirani zetu wananufaika bali na sisi pia tunapata ongezeko la ajira, mapato na masoko ya bidhaa zetu.

Nchi yetu imebahatika kuzungukwa na nchi 8 zikiwa majirani zetu – na kati ya nchi hizo, ni nchi mbili pekee, yaani Kenya na Msumbiji, ndizo zenye ufukwe wa bahari. Hakuna nchi nyingine yoyote katika eneo la Maziwa Makuu au katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo imepata bahati kama hii. Hapa tuna fursa mbili. Fursa ya kwanza ni ya kufanya biashara na hawa majirani zetu wengi. Fursa ya pili ni hawa majirani kutumia bandari zetu, reli zetu na barabara zetu kufanya biashara na mataifa mengine duniani.

Hii ni biashara kubwa sana. Miaka mitatu tu iliyopita, biashara ya usafirishaji wa mizigo kupitia Tanzania (transit trade) ilikuwa inaingiza mapato kwa Serikali yanayokaribiana na mauzo ya nje ya mazao ya kilimo ambacho tunahangaika nacho kila siku.

Vilevile, kwa kuwa shughuli ya kupitisha bidhaa, yaani transit trade, yenyewe ni biashara kubwa, ni muhimu kuitazama miundombinu ya usafirishaji kwa mtazamo wa kiushindani. Kwa maana kwamba bandari zetu za Tanga na Dar es Salaam zinashindana na bandari nyingine katika ukanda huu. Kwa mfano, kwa sasa, majirani zetu wa upande wa kaskazini, wametengeneza Korido ya Usafirishaji ya Kaskazini (*Northern Infrastructure Corridor*) inayounganisha bandari za Mombasa na Lamu na nchi za Rwanda, Uganda na Burundi, Kongo, Ethiopia na Sudani ya Kusini kwa barabara, reli na bomba la mafuta. Ni dhahiri kwamba miradi hii, ambayo utekelezaji wake unaenda kwa kasi, itatoa ushindani kwa Korido ya Kati, inayotegemea kwa kiasi kikubwa Bandari ya Dar es Salaam na Reli ya Kati. Tusipokuwa makini, na tukaharakisha upanuzi na uboreshaji wa reli na bandari zetu, bandari yetu na reli yetu itakuwa ni kwa ajili ya mizigo ya Tanzania tu na tunaweza kukosa kiasi kikubwa cha fedha ambacho sasa tunapata kwa biashara ya kupitisha mizigo kwa ajili ya nchi za jirani.

Bandari ya Dar es Salaam, licha ya malalamiko yaliyopo, licha ya changamoto zilizopo, bado 2012 ilitengeneza faida ya takribani shilingi **bilioni 40**. Sidhani kama kuna kampuni yoyote hapa nchini, ya umma au ya binafsi, iliyotengeneza faida ya kiasi hiki. Na licha ya changamoto zilizopo, bado inapitisha mizigo ya thamani ya dola za Kimarekani bilioni 15 kwa mwaka, ambazo ni karibu ya nusu ya Pato la Taifa. Kwa mujibu wa utafiti wa Benki ya Dunia, tukiiboresha kidogo tu bandari ya Dar es Salaam, angalau ikafikia ufanisi wa bandari ya Mombasa, uchumi wetu utanufaika kwa kiasi cha dola za Kimarekani bilioni 1.8 au sawa na asilimia 7 ya Pato la Taifa. Jambo hili linawezekana bila gharama kubwa. Ufanisi unaweza kuongezwa kwa kuondoa ushuru usio na lazima, rushwa katika upitishaji wa mizigo, kupunguza milolongo ya usafirishaji mizigo na kutumia teknolojia za kisasa katika usafirishaji na upakuzi wa bidhaa. Baadhi ya haya mambo yameanza kufanyika na mabadiliko yameanza kuonekana ingawa kasi inahitajika.

Kimsingi tunayo fursa ya kunufaika zaidi kuliko ilivyo sasa. Lakini ni lazima kuimarisha miundombinu ya bandari na reli, sio tu katika Korido ya Kati, bali ni lazima pia kuitazama bandari ya Tanga na reli ya Tanga – Kilimanjaro. Miundombinu hii ambayo ni muhimu sana katika ustawi wa Kanda ya Kaskazini ina nafasi kubwa ya kushindana na bandari ya Mombasa na Lamu nchini Kenya. Lazima tuangalie namna ya kuifufua reli ya Tanga-Kilimanjaro na kuharakisha mpango wa kuifikisha kwenye bandari ya Musoma katika Ziwa Victoria inatekelezwa.

Bandari ya Mtwara inafaidika na upanuzi mkubwa na matumizi mapya ambayo yanatokana na uchumi wa gesi na viwanda vikubwa vinavyojengwa na vinavyotarajiwa kujengwa huko. Kuhusu Bandari ya Bagamoyo, hii ikikamilika itakuwa ni bandari kubwa kuliko zote mashariki mwa Afrika ikishindana na ile ya Durban ya Afrika Kusini. Itasaidia sana kupunguza msongamano katika bandari ya Dar es Salaam ambayo baada ya miaka michache ijayo itafikia ukomo kwa kukosa nafasi zaidi ya kupanuka. Kwa hiyo ni muhimu kujenga bandari hii kama tunafikiria kukidhi mahitaji ya Taifa miaka zaidi ya 50 ijayo.

Wananchi wa mikoa ya Pwani, Dodoma, Singida, Kigoma, Tabora, Mwanza, Shinyanga, Morogoro, Rukwa na Katavi wanategemea usafiri wa reli kwa uchumi wao. Tukiiacha reli yetu iwe goigoi maana yake tumewasahau hawa wenzetu katika mikoa 10. Treni ya reli ya kati ni muhimu irudishe safari zake za kila siku. Hata hivyo, reli hii inabidi ifumuliwe na kujengwa upya kulingana na kiwango cha kimataifa, yaani “standard gauge”.

Mkakati huu umeshaanza lakini kuna haja ya kuongeza kasi ya utekelezaji. Shirika la Reli linabidi lipate mtaji mkubwa wa kujiendesha kifanisi kabla ya kutazama ni jinsi gani ya kushirikisha sekta binafsi. Reli ya TAZARA nayo inahitaji maboresho makubwa na menejimenti imara ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Tanzania ni nchi ya nne Afrika katika soko la usafiri wa anga. Ufanisi wa sekta muhimu ya utalii unategemea sana kutengemaa kwa usafiri wa anga. Kuna mjadala wa haja ya Serikali kuendelea kumiliki Shirika la ndege la Taifa. Cha msingi sio umiliki, cha msingi ni uhakika wa usafiri wa anga. Biashara ya usafiri wa anga ni biashara ngumu yenye gharama kubwa za uendeshaji lakini faida ndogo. Uendeshaji wa shirika la ndege unahitaji nidhamu kubwa sana ya kibiashara na hasa matumizi ya fedha – nidhamu ambayo bado kama Serikali hatujaifikia. Tunahitaji wabia wa uhakika na wenye nguvu kubwa na uzoefu wa biashara hii ili tuweze kushirikiana nao kufufua na kuendesha Shirika letu la ndege – huku nasi tukiwa na umiliki. Pia, ni vyema kuyaunga mkono mashirika ya ndani na ya wazalendo, na hata ikiwezekana Serikali nayo iwe sehemu ya umiliki. Tumeona mafanikio ya kufungua anga kwa mfumo wa



January Makamba akishiriki ujenzi wa Ofisi ya CCM ya Kata ya Mbuzii Lushoto akiwa na Katibu Mkuu wa CCM Ndugu Kinana.

ushindani kwamba usafiri umeimarika zaidi na bei zimeendelea kushuka. Kwa hiyo tuendeleo kukaribisha ushindani katika sekta hii, na kujenga viwanja vya ndege vya kimataifa katika kanda zote katika nchi yetu, na kuimarisha viwanja vya ndege vya mikoa.

Serikali ya Awamu hii ya Nne, imepata mafanikio makubwa sana katika kujenga barabara kuliko awamu zilizopita. Barabara hizi zimefungua fursa zaidi, hasa katika mikoa ya pembezoni mwa nchi yetu na kuweza kuunganisha mikoa yote ndani ya mfumo wa barabara za kitaifa. Awamu inayofuata ni kuunganisha wilaya zote nchini kwa barabara za kiwango cha lami na kupanua barabara za taifa kuwa barabara mbili (dual carriageway).

Kwa ujumla, nchi yetu inahitaji uwekezaji wa takriban dola za Kimarekani bilioni 2.5 kwa mwaka katika miaka 10 ijayo ili kufikia malengo yetu kwenye miundombinu na kuendana na kasi ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Fedha hizi zote sio lazima zitoke kwenye bajeti ya Serikali. Ujenzi wa miundombinu ni shughuli inayovutia sekta binafsi na kote duniani miundombinu mikubwa inayohitaji fedha nyingi haikujengwa na bajeti za Serikali, ilhali hapa hapa



kwetu kwa sehemu kubwa inapata fedha kutokana na kodi tunazotoza watu kutoka kwenye mishahara yao na biashara zao ndogondogo. Tukiendelea hivi hivi tutachelewa sana. Tunahitaji falsafa mpya ya namna ya kugharamia ujenzi wa miundombinu hapa nchini ili kukidhi kasi ya ukuaji wa uchumi wetu.

Hatuwezi kuendelea kutegemea misaada ya wahisani kujenga miundombinu kwani misaada haina uhakika na imekuwa inapungua mwaka hadi mwaka. Mwaka 1973, katika misaada iliyokuwa inatolewa na wahisani, asilimia 50 ilikuwa inaenda kwenye ujenzi wa miundombinu, sasa hivi imeshuka na kufikia asilimia 10. Miaka ya nyuma, Rais Mkapa alifanya uamuzi mzuri wa kutumia fedha zetu za ndani kujenga miundombinu. Tumepata mafanikio makubwa, hasa kwa upande wa barabara. Lakini kwa kuwa tuna mahitaji makubwa ya huduma za kijamii, kama vile afya, maji, elimu, ulinzi na usalama – huduma ambazo sekta binafsi bado haina *interest* nazo – Serikali inabidi iongeze chachu ya kukaribisha uwekezaji wa sekta binafsi kwenye ujenzi wa miundombinu mikubwa, kama ilivyo kwenye nchi nyingine – ili fedha zetu chache za bajeti tuzielekeze kwenye mahitaji mengine muhimu ya watu wetu kama vile madawa, malipo ya walimu, madaktari, askari wetu na huduma nyinginezo. Dhana kwamba ni Serikali pekee ndio ina wajibu, uwezo na haki ya kujenga miundombinu ya usafirishaji imepitwa na wakati. Sekta binafsi ya ndani au nje ya nchi ikijenga bandari, bandari hiyo haitang’olewa bali itabaki nchini na kulinufaisha taifa. Mfano mzuri ni utekelezaji wa ujenzi wa Daraja la Kigamboni ambao umefanikishwa kwa haraka baada ya Serikali kuingia ubia na mbia (NSSF) ambaye amelea mtaji mkubwa na weledi katika utekelezaji. Kwa hiyo, sekta binafsi inapotaka kushirikiana na Serikali kujenga au kugharamia ujenzi wa miundombinu isikatishwe tamaa au kuwekewa vikwazo bali iwezeshe tukizingatia tija na maslahi ya Taifa ya sasa na baadae.

Fursa nyingine muhimu sana ni kutumia maendeleo katika masoko ya kifedha duniani katika kugharamia miundombinu mikubwa. Serikali inabidi kuharakisha utekelezaji wa mipango ya kuuza hati fungani ya taifa, yaani Sovereign Bond, katika masoko ya kimataifa na hati fungani za Halmashauri, yaani Municipal Bonds, ili kutoa fursa ya kupata mikopo ya muda mrefu kugharamia ujenzi wa reli zetu, barabara zetu, madaraja yetu, viwanja vyetu vya ndege, na bandari zetu kwa uharaka zaidi kuliko kutegemea makusanyo ya kodi huku tukiipunguzia Serikali mzigo wa riba unaotokana na mikopo midogomidogo ya muda mfupi kutoka soko la ndani.

Kwa ujumla uongozi wa sasa wa Wizara ya Uchukuzi ukishirikiana na Hazina unafanya kazi nzuri katika kuleta marekebisho kwenye sekta ya uchukuzi. Lazima watiwe moyo ili waongeze kasi na ufanisi.

31

Nimetembea sana vijijini na nimeona kuwa vijiji vingi havina huduma yoyote ya afya. Hata kule ambapo zipo watumishi hawatoshi, vifaa hakuna, hakuna umeme, na wakati wote hakuna dawa. Ukienda hospitali, iwe ndogo au kubwa, una hatari ya kupata ugonjwa kuliko nyumbani. Haya matatizo wewe unayaonaje? Kwa kweli watu hawamudu gharama za matibabu na wanakufa bila sababu za msingi. Nini kifanyike?

Ni kweli hili ni tatizo. Hata kule ninakotoka Bumbuli, nimekuta changamoto hii. Kati ya vijiji 83 tuna zahanati 14 tu, na nusu ya hizo tumezijinga katika kipindi hiki cha miaka minne tangu niwe Mbunge. Kwa hiyo ni kweli tatizo ni kubwa vijijini. Sasa hivi tunaongeza kasi na tumeanza ujenzi wa zahanati nyingine zaidi ya 20.

Hili sio eneo langu sana lakini nitasema mambo ambayo ni dhahiri, ambayo nayaamini kama kiongozi ambaye pia huhangaika na afya za watu wake, kama mtu aliyewahi kuugua na kuuguza na kufiwa na ndugu na jamaa wakiwa hospitalini ambao niliona kabisa wangeweza kupona kama huduma zingekuwa bora.

Changamoto kubwa inayosababisha changamoto nyinginezo katika sekta ya afya ni ile ya mfumo mzima wa huduma ya afya, yaani health system.

Kutatua matatizo ya afya nchini ni lazima kuulewa kwa undani mfumo wa afya na kuzielewa changamoto zake. Katika kufanya kwangu kazi Serikalini, katika nafasi yangu ya Ubunge lakini pia kama Mtanzania ambaye huenda hospitali, nimebaini kwamba kwa kiongozi yoyote mwenye nia thabiti ya kutatua changamoto za afya nchini, ni lazima kuweka mfumo thabiti na imara wa afya. Mfumo imara wa afya utasaidia katika jitihada za kupambana na

magonjwa, utasaidia wasio na kipato wasikose huduma ya afya kwa ajili hiyo na wale wenye kipato basi wasifilisike kwa kulipia tiba mara wauguapo.

Kikubwa cha kwanza kwenye huduma ya afya ni kwamba lazima kuwe na access, yaani miundombinu ya huduma iwepo. Kwa maana ya zahanati, vituo vya afya, hospitali ziwepo na tena ziwepo kwa usawa katika kila eneo la nchi yetu, na miundombinu hii iwe bora, sio ili mradi jengo tu. Kazi kubwa imefanyika katika awamu zote za uongozi wa nchi yetu kusogeza huduma hizi karibu na watu. Kasi imeongezeka katika awamu ya nne, na kama Mbunge nashuhudia na nafarijika na mwamko wa wananchi kujenga zahanati na vituo vya afya. Tumeshuhudia kwamba sasa karibu Wilaya zote, isipokuwa zile mpya, sasa zina hospitali za wilaya. Tunashuhudia hospitali za mikoa zinaimarishwa. Tunaona mipango ya kujenga hospitali nyingine kubwa za kusomesha madaktari. Tumeona pia sekta binafsi imeongeza uwekezaji kwenye huduma za afya kwa kasi ya kuridhisha. Lakini changamoto bado ipo kwenye miundombinu ya afya ya msingi, zahanati na vituo vya afya. Hapa lazima tuongeze kasi na tuwasaidie wananchi.

Lakini jengo zuri la zahanati au kituo cha afya au hospitali sio huduma ya afya. Lazima kuwe na watumishi wa kutosha na weledi, lazima kuwe na vifaa-tiba na lazima kuwe na madawa.



January Makamba akihutubia moja ya mikutano yake ya kuimarisha CCM.

Hakuna mjadala kwamba watumishi kwenye sekta ya afya hawatoshi. Na hii ni changamoto ya dunia nzima. Katika mfumo mzima wa afya, rasilimali-watu ndio kipengele chenye gharama kubwa kuliko zote. Hapa tunawaongelea Watabibu, Wauguzi, Wafamasia, hadi walinzi wa vituo vyetu vya afya. Bila watumishi wa kutosha na wenye weledi unaohitajika basi hakuna huduma ya afya. Kupitia Mpango Maalum wa Afya ya Msingi, na kwa msaada wa wafadhili mbalimbali, Serikali imefanya jitihada kubwa katika miaka ya hivi karibuni kuongeza watumishi wa kada mbalimbali katika sekta ya afya. Kwakuwa tulianza chini sana, na kwa kuwa tunaendelea kupanua huduma hii nchi nzima, inawezekana ongezeko hili lisionekane dhahiri. Ili watu wetu wahakikishiwe huduma bora ya afya, lazima tuendeleo na kasi ya kuongeza watumishi wa afya, tuhakikishe wale walioajiriwa wanapangwa katika vituo kwa haki na usawa na kuzingatia mahitaji, na wanabaki vituoni; kwa wale waliopangwa kwenye maeneo yenye mazingira magumu, tuwape motisha ili kuongeza ari na morali. Lakini jingine la msingi ambalo tunaweza kulifanya bila gharama ni kuhakikisha mchakato wa kuajiri watumishi wa afya unafanyika kwa haraka, vibali vinatoka kwa haraka, na mishahara inatoka kwa haraka. Bila kuwekeza kwenye haya, tutaendelea kupata shida kutoa huduma za afya kwa watu wetu.

Kama nilivyosema, jambo jingine linalolalamikiwa na wananchi, na linafanya huduma yetu iwe duni, ni upungufu wa madawa, vifaa-tiba na teknolojia duni ya tiba. Hapa lengo ni kuhakikisha kwamba madawa, chanjo, vifaa-tiba, huduma za maabara, na teknolojia nyingine za afya zinapatikana kwa muda sahihi na kwa ubora wa hali ya juu. Kama hakuna vifaa wala uwezo wa kubaini mtu anaumwa nini, na kama hakuna dawa, basi ni sawa na kama huduma ya afya hakuna. Kuwepo kwa zahanati pale kijijini kwetu Mahezangulu Bumbuli kumetoa matumaini makubwa kwa wananchi lakini kama wanaenda pale na wanaondoka bila huduma, kama ambavyo imetokea mara nyingi, ni kana kwamba zahanati ile haipo kabisa. Hatuwezi kuwa na mfumo wa afya ambao madawa na vifaa vinapatikana kwa mashaka mashaka au havipatikani kabisa. Tunao wajibu wa kuhakikisha kwamba madawa na vifaa tiba vinapatikana katika vituo na hospitali zote nchini.

Kwa mfumo wa sasa, Bohari Kuu ya Madawa, yaani MSD, ndio muuzaji pekee wa madawa na vifaa kwenye vituo vya Serikali. Sote tumeona jinsi mfumo huu unavyokabiliwa na changamoto nyingi. Wote tumesoma kwenye vyombo vya habari kwamba serikali imechelewa kulipa madeni yake kwa MSD, hivyo kusababisha usumbufu mkubwa wa ukosekanaji wa madawa. Pia nimeambiwa, sina hakika itabidi kucheki, kwamba katika mikoa yote 31 ya Tanzania, Bohari za MSD zilizopo hazifiki 10. Maana yake hapa ni kwamba dawa na vifaa huchelewa kufika katika mikoa yote ya Tanzania kwa wakati.

Ili kuweza kurekebisha hali hili, ninapendekeza kuwe na utaratibu wa malipo ambao hautasababisha kusimamishwa kwa utoaji wa madawa na vifaa kutoka MSD. Vilevile, imefika wakati sasa tutazame upya utaratibu wa ukiritimba wa MSD kama ndio muuzaji na msambazaji pekee wa vifaa vya huduma ya afya kwenye vituo vya Serikali.

Vilevile kuna janga kubwa linaloendelea nchini ambalo watu wengi hawalizungumzii lakini mimi nimekutana na wahanga wake. Janga hilo ni kuingizwa nchini kwa dawa na vifaa-tiba feki. Watu wengi wanapoteza maisha kimyakimya kutokana na jambo hili. Mamlaka husika, hasa TFDA, zina wajibu wa kuwalinda wananchi na janga hili.

Suala jingine muhimu, ambalo limekuwa na mjadala wa muda mrefu Serikalini na miongoni mwa wananchi kwa ujumla, ni suala la fedha za uendeshaji wa sekta na huduma za afya, yaani health financing. Hili ni jambo la msingi sana. Huduma za afya ni haki ya kila mtu, lakini huduma ya afya vilevile ina gharama, wakati mwingine gharama kubwa sana kutegemea na ugonjwa. Kwa bahati mbaya serikali yetu inategemea kwa kiasi kikubwa misaada ya wahisani katika kuendesha huduma za afya. Kwa hiyo ni muhimu tukabuni mbinu bora za kuwezesha uchangiaji wa huduma za afya.

Jambo la msingi ni kwamba uchangiaji huu uendane na uwezo wa mtu na kwamba mtu yoyote asinyimwe huduma ya afya kutokana na kutokuwa na uwezo. Namna pekee ya kuhakikisha hili ni kwa kila Mtanzania kuwa na bima ya afya. Serikali imeanzisha Mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa ambayo unatoa huduma hizo kwa wafanyakazi wa sekta rasmi, na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) kwa wananchi walioajiriwa katika sekta isiyo rasmi. Ni lazima kuiwezesha CHF pamoja na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuweza kutoa bima kwa Watanzania wengi zaidi.

Kero za afya nchini zitatatuliwa pale tu ambapo asilimia kubwa ya Watanzania watakuwa uwezo wa kulipia huduma ya afya kupitia bima zao. Baadhi ya nchi za Kiafrika zimeweza kufanya hili. Michango ya bima itasaidia kuboresha mifumo ya afya hususan upatikanaji wa wataalam na vifaa tiba sehemu zote. Lakini ni muhimu pia kuhakikisha kwamba taasisi hizi zinatumia michango ipasavyo ili kuinua ubora wa huduma ya afya inayotolewa. Tufikirie kuiwezesha mifuko hii ya Bima kuwa mlipaji pekee, yaani single payer, wa huduma za afya nchini. Hii itainua ufanisi katika matumizi ya fedha za bima za wananchi. Lakini pia tuweke mfumo wa soko huria la Bima ili kutoa fursa kwa wale wanaochagua huduma binafsi kama wanaona ni bora na gharama nafuu zaidi.

Jambo jingine muhimu ni mpango wa taarifa za afya. Sera za afya, mipango ya bajeti, na mipango mingine kwenye huduma ya afya inategemea sana taarifa sahihi na za uhakika za masuala ya afya. Takwimu muhimu kama vile idadi ya zahanati, idadi ya wakina mama wanaohudhuria kliniki, idadi ya watumishi wa afya, asilimia ya watoto wanaopata chanjo, idadi ya wakinamama waliojifungua kwenye vituo vya afya, umbali katika kufikia huduma za afya, aina ya magonjwa kwa maeneo mahsusi, na kadhalika ni muhimu zikapatikana kwa haraka na kuhuishwa katika mipango yetu. Tunaweza kabisa kutumia mifumo ya Tehama katika kukusanya na kuchambua taarifa hizi.

Vilevile usimamizi na uongozi wa sekta ya afya ni muhimu. Bila uongozi na usimamizi madhubuti wa sekta ya afya, hatuwezi kuimarisha huduma za afya nchini. Ni muhimu kuwe na uongozi madhubuti utakaosimamia rasilimali-watu na rasilimali-fedha kubwa inayoenda kwenye sekta ya afya. Hili linahitaji viongozi wenye uwezo lakini pia waadilifu kwani kuna dhana kwamba kwenye sekta ya afya kuna ulaji mkubwa wa fedha za miradi lakini pia wizi wa madawa na vifaa, lakini pia na semina, warsha, makongamano na sherehe nyingi zisizo na tija. Lazima kuwa na uongozi wa kijasiri unaoweza kukomesha haya.

Kuna msemu kwamba kinga ni bora kuliko tiba. Kwa kuzingatia hali halisi na mazingira na changamoto za nchi zetu hizi maskini, tufanye jitihada kubwa zaidi kuzuia baadhi ya magonjwa kabla ya kutumia gharama kubwa kwa tiba. Ni lazima sisi katika uongozi wa kisiasa na viongozi wengine wa kijamii na wadau mbalimbali tushirikiane kutokomeza magonjwa ambayo yanaweza kuepukika kwa kutumia chanjo, usafi wa mazingira, elimu ya jamii au vyandarua. Gharama kubwa za afya zinakwenda kwenye magonjwa ya kuambukiza ambayo yanaweza kuzuilika kama vile malaria, homa ya mapafu na UKIMWI. Pia, ajali za barabarani, hasa za pikipiki, zinaongeza mzigo wa matumizi ya rasilimali katika vituo vyetu vya tiba. Ajali hizi zinaweza kuzuilika.

Mwisho kabisa ni kuendelea kuwekeza katika utafiti katika sekta ya afya. Utafiti usiwe tu kwa faida ya wahisani ambao kwa sasa ndio wawekezaji wakubwa kwenye utafiti wa afya nchini, bali utafiti ufanyike katika magonjwa yanayowaathiri watu wetu zaidi. Lakini pia utafiti sio kwenye magonjwa tu bali kwenye sera na mipango ya huduma za afya. Kuwekeza kwenye utafiti pekee haitoshi, bali tunapaswa kuyakubali, kuyaheshimu na kuyafanyia kazi matokeo ya utafiti ili tuweze kuwekeza kwenye mipango iliyodhibitishwa na inayotekelezeka, yaani *evidence-based*.

32

Umesema kwamba Rais Kikwete amejitahidi kuboresha huduma. Unadhani ni huduma gani ya jamii bado ni kero kwa Watanzania na unadhani kuna maarifa gani mapya ya kuitatua?

Ni kweli kabisa Rais Kikwete amefanya kazi kubwa sana kwa upande wa kusambaza huduma za jamii nchini. Umeme unasambazwa kote vijijini, barabara zinajengwa, zahanati zinajengwa vijijini, na watumishi wa huduma ya afya wengi zaidi wanapangiwa vituo; shule nyingi za Sekondari zimejengwa na sasa walimu wengi wa shahada wanaajiriwa kila mwaka. Kwa kweli kazi kubwa sana kwa upande wa huduma za kijamii imefanyika.

Hata hivyo, kwa nianavyo mimi, kwa kutembea maeneo mengi ya nchi yetu, bado huduma ya maji ni changamoto kubwa. Wakati Rais Kikwete anaingia madarakani alitaja kuwa hii ni kero namba moja ya Watanzania walio wengi. Ukienda maeneo mengi katika nchi yetu, mijini na vijijini, bado wananchi wengi hawapati maji salama na ya uhakika.

Kuhusu maji, ziko changamoto za aina mbili: kwanza ya ukosefu wa vyanzo vya maji; na pili ukosefu wa miundombinu ya usafishaji na usambazaji wa maji. Baadhi ya maeneo hayana maji kabisa, hasa wakati wa kiangazi. Baadhi ya maeneo, kwa mafano jimboni kwangu Bumbuli, vyanzo vipo na maji yapo lakini hayajawafikia watu pale walipo.

Katika nchi yetu, tuna bahati kwamba tunayo maji ya kutosha na maji haya yanapatikana sehemu tatu: angani, kwa maana ya mvua zinazonyesha; juu ya ardhi, kwa maana ya maji ya kwenye mito, maziwa na mabwawa ya asili; na chini ya ardhi, kwa maana ya maji yaliyo chini ya miamba. Tatizo kubwa ni maji haya kuwafikia watu pale wanapoishi yakiwa safi na salama wakati wote.

Kama tukiwa wabunifu wa kutosha hatuwezi kushindwa kumaliza tatizo hili.

Kwa hiyo majawabu ni nini?

Kwanza, pale kote kwenye majengo ya umma kama vile shule, hospitali na mengineyo inabidi tukinge maji na kuyahifadhi. Nilishawahi kwenda pahala kwenye shule ya sekondari nikapewa kero ya maji, kwamba yapo mbali na sio masafi. Lakini nikaangalia ile shule ina majengo makubwa zaidi ya 9. Nikauliza hali ya mvua huwa ikoje. Nikaambiwa huwa zinanyesha sana, hasa wakati wa masika na vuli. Tukaanzisha harambee ya kujenga kata za kukinga maji na matenki ya kuhifadhi maji. Siku hizi naambiwa kwamba mvua zinakuta bado maji ya msimu uliopita yapo na wanakijiji pia wanayatumia. Kwa hiyo, kwanza, katika masharti ya kutoa vibali vya ujenzi, kuwepo na kanuni mahsusi za kulazimisha uwepo wa miundombinu ya kukinga maji katika majengo na kuyahifadhi.

Yapo maeneo hapa nchini ambayo yanajulikana kuwa ni makavu – maeneo mengi ya usukumani, hasa katika maeneo ya wafugaji katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Geita na baadhi ya maeneo ya mikoa ya Mara, Dodoma, Tabora na Singida na mikoa ya Arusha na Manyara. Hata hivyo, ukienda nyakati za mvua katika maeneo haya utashangaa na hutaamini kwamba huwa panakuwa pakavu, kwani mito hujaa maji na hata mafuriko hutokea.

Katika maeneo haya makavu, hasa maeneo ya Usukumani, napendekeza, kama hatua ya dharura, kwamba tujenge mabwawa au malambo makubwa matatu kila kata – moja kwa ajili ya matumizi ya watu, jingine kwa ajili ya matumizi ya mifugo, na jingine kwa ajili ya hifadhi. Malambo au mabwawa haya, tukiyajenga vizuri, yatakuwa na maji mwaka mzima kwa ajili ya watu na mifugo. Malambo au mabwawa haya ni hatua ya muda mfupi tu wakati tunajenga uwezo wa kupeleka maji ya bomba kwenye kila kijiji, kitongoji na kaya.

Lakini malambo haya tukiyanua na kuwa makubwa zaidi na imara tunaweza kuweka mitambo ya kusafisha maji na kuyasambaza kwenye vijiji na vitongoji yakiwa safi na salama.

Kwa sasa, sehemu kubwa ya miradi ya maji vijijini inatekelezwa kupitia mkopo kutoka Benki ya Dunia na wafadhili wengine. Tunahitaji kuwekeza fedha zetu wenyewe ili kuharakisha upatikanaji wa maji. Sababu kubwa ya mafanikio katika ujenzi wa miradi ya umeme na barabara ni fedha. Miradi ya barabara na umeme inajengwa na wakandarasi. Serikali inachofanya ni kutoa fedha. Fedha zikiwepo kazi inafanyika. Kwenye maji hivyo hivyo, fedha ikipatikana maji yatafika vijijini.

Tuanzishe Mfuko wa Maji Vijijini pamoja na Wakala wa Maji Vijijini. Tumeona jinsi Mfuko wa Barabara na Wakala wa Barabara wa Taifa unavyofanya kazi nzuri kwenye ujenzi wa barabara. Tumeona jinsi ambavyo Mfuko wa Umeme Vijijini na Wakala wa Umeme Vijijini ulivyofanya kazi nzuri kusambaza umeme vijijini. Utaratibu mpya na msukumo mpya wa kupeleka maji vijijini utasaidia. Chanzo cha fedha kwa Mfuko wa Maji kinaweza kuwa tozo maalum kwenye matumizi ya maji mijini na maji ya kunywa kwenye chupa.

Ukosefu wa fedha ni changamoto katika utekelezaji wa miradi ya maji, lakini hakuna changamoto kubwa kama ubadhirifu na ubabaishaji unaosababisha miradi mingi ya maji kila mahali kujengwa chini ya kiwango, au hata kutojengwa kabisa. Serikali kwa ushirikiano na wafadhili imewekeza mabilioni ya fedha katika kuwasogezea wananchi wote maji safi na salama lakini hatuoni matokeo yake kutokana na ukosefu wa uaminifu kuanzia kwa wafanyakazi wa umma, wahandisi washauri, wasanifu na wasimamizi wa miradi ya maji, wakandarasi na viongozi wa kisiasa wanaotakiwa kusimamia miradi hii inayotugharimu fedha nyingi sana. Mimi kule jimboni kwangu hii imekuwa ni changamoto kubwa sana na ilibidi tuukatae mradi wa maji baada ya mkandarasi kutaka kukabidhi mradi ambao ulikuwa na kiwango cha chini sana kuanzia usanifu, ujenzi na ufanisi wa miundombinu ambayo haikuweza kutoa huduma iliyotegemewa.

Usimamizi madhubuti katika miradi hii ya maji ni muhimu sana kama tunataka kusogeza maji karibu na kaya zetu nchini kote. Napendekeza kuwe na utaratibu wa kuwamilikisha wananchi katika vijiji vyao miradi ya maji na miundombinu yake na kuwawezesha kitaalamu kusimamia mchakato mzima wa kusanifu, kujenga, kukabidhiwa na kuitunza kwa ajili ya faida zao na vizazi vijavyo. Sisi wanasiasa, hasa wabunge, hatuna budi kuwa wakali na kuifuatilia kwa ukaribu kabisa miradi hii ya maji ili iweze kuleta tija kwa wananchi wetu. Natumaini kabisa kuwa kwa spidi ya uwekezeji katika miundombinu ya maji, tukiweza kuwasimamia wakandarasi vizuri, tutamaliza tatizo la maji ndani ya muda mfupi.

Nina uhakika kabisa kuwa ndani ya miaka kumi tunaweza kusogeza maji safi, salama na ya uhakika karibu kabisa na kaya zote nchini kote.

33

Ukiwa kama kiongozi kijana wa CCM, uliyepata fursa ya kuwa kiongozi wa juu wa Chama chenu, huoni kama Chama chenu kimepoteza mwelekeo na kinapata ushindani mkubwa sasa? Kuna sababu za Chama chenu kuendelea kuaminiwa na Watanzania? Ukichaguliwa Rais, pia unakuwa Mwenyekiti wa CCM, je kijana anaweza kukiongoza Chama kikongwe kama CCM?

Ni kweli kwamba ushindani wa siasa umeongezeka na kwa kweli hali hii sio ya ajabu. Baada ya miaka 22 ya mfumo wa vyama vingi ni dhahiri kwamba ushindani utaongezeka na hili ni jambo jema kwa demokrasia ya nchi yetu. Lakini niseme pia kwamba si kweli kwamba CCM imepoteza mwelekeo. CCM bado ndio chama bora, Chama pekee chenye uwezo wa kubeba dhamana ya uongozi wa nchi.

Mambo kadhaa yanadhihirisha ubora wa CCM ukilinganisha na vyama vingine: kwanza, muundo wa Chama chetu ni thabiti, kuanzia kwenye nyumba-kumi hadi ngazi ya taifa tuna uongozi, tuna vikao na tuna kanuni na taratibu za kuendesha mambo yetu. Pili, tuna Katiba na Kanuni zinazotuongoza katika kuendesha mambo yetu. Tatu, ni chama cha kidemokrasia kwani tuna chaguzi kwa ngazi zote, na tunazifanya kila baada ya miaka mitano bila kukosa na viongozi hawabaki walewale miaka yote kama vyama vingine. Nne, tunazo sera za msingi zinazotuongoza lakini pia kila baada ya miaka mitano tunatengeneza Ilani za Uchaguzi ambazo zinajibu kero na changamoto za Watanzania. Tano, tunayo historia adhimu ya kuongoza ukombozi wa bara la Afrika na heshima ya CCM inatambulika duniani kote. Sita, sisi ndio tumeongoza ujenzi wa taifa hili. Amani na umoja uliopo sasa ni matunda ya kazi ya CCM. Saba, tunao uzoefu wa kuongoza nchi. Tumeiongoza Tanzania vizuri, na licha ya changamoto kadhaa, maendeleo yanaonekana. Nane, bado tunao viongozi wengi wazuri, wazalendo, waadilifu na wenye uwezo na wenye busara. Tisa,

tunao wanachama, washabiki na wapenzi nchi nzima, tena wengi kuliko wa vyama vingine, ambao wako tayari kukipigania Chama chetu kwa maslahi ya taifa letu.



January Makamba akihutubia Mkutano Mkuu wa CCM Kizota Novemba 2012.

Ni dhahiri kwamba zipo changamoto kadhaa kama ambavyo ni kawaida kwa taasisi yoyote kubwa. Ni kweli kwamba Chama kimeingiliwa na wajanja wachache ambao wanataka kununua uongozi kwa ajili ya kujinufaisha. Ni kweli kwamba harakati za kutafuta uongozi zinaonyesha dalili ya kutugawa. Lakini la msingi ni kwamba tunao utaratibu, tunayo Katiba na Kanuni na kikubwa tunao utamaduni ambao siku zote vimetuongoza katika kukabiliana na changamoto hizi. Bado tuko imara, na bado tunayo nafasi kubwa ya kuendelea kuiongoza nchi yetu.

Lakini ili tufanikiwe lazima tuendelee kusimama kidete kuwasemea na kuwatetea Watanzania, hasa wanyonge wa hali ya chini.

Kazi hiyo inaendelea kufanyika. Lazima tuendeleo kutengeneza Sera na Ilani zinazotoa majawabu ya mahitaji ya Watanzania. Hili nalo linafanyika. Lazima tuendeleo kuwaunganisha Watanzania kuendelea kuwa kitu kimoja. Hili nalo linaendelea kufanyika. CCM ndio Chama pekee kinachobeba sura ya kitaifa bila kujali kanda, dini, kabila, upande wa Muungano na jinsia. Vyama vingine vyote havina sifa hii. Lazima tuendeleo kuimarisha muundo wa Chama chetu na kujenga uwezo wa watendaji na viongozi wa CCM kwa ngazi zote, ikiwemo


kuangalia maslahi yao na kuwapatia vitendea kazi, ikiwemo rasilimali za kuweza kufanya kazi za siasa katika ngazi zao.

Kazi nzuri inayofanywa na Sekretarieti ya Chama chetu chini ya uongozi madhubuti wa Katibu Mkuu, Ndugu Abdulrahman Kinana, umesaidia kuchochea utekelekezaji wa Ilani yetu, kurudisha imani kwa baadhi ya wanachama wetu waliokuwa na fikra kuwa chama kinapoteza nguvu, hasa katika maeneo ya vijijini na kujenga umoja baina ya wanachama wetu. Juhudi hizo zimepelekea yeye pamoja na wasaidizi wake kuvuka mito na mabonde, kutembea usiku na mchana, kuhimili jua ya mvua katika harakati zake za kufufua na kujenga uhai wa Chama. Yeye na wenzake wanastahili pongezi kubwa. Vilevile, viongozi na makada wa Chama na Jumuiya zake katika ngazi za matawi, Kata, Wilaya na Mikoa nao wanafanya kazi kubwa, tena wengi kazi ya kujitolea kukiimarisha Chama.



January Makamba akifurahia jambo na Katibu Mkuu wa CCM, Ndugu Abdulrahman Kinana.

Hata hivyo, Chama chetu ni lazima kiendelee kupambana na kukemea vitendo vya rushwa na maovu kwa nguvu zote. Vitendo vya rushwa na ubadhirifu vinavyofanywa na wachache vinakiharibia sifa Chama chetu. Tusikubali hata kidogo wanachama na viongozi wetu ambao sio waadilifu wachafue sifa, heshima na imani waliyonayo wananchi kwa chama chetu.



January Makamba akibadilishana mawazo na Mzee Job Lusinde na Mzee Kingunge Ngombale Mwiru ambao aliwaalika katika Mkutano wa Viongozi Vijana wa CCM alioandaa Mwaka 2008.

Imani ya wananchi kwa CCM ndio msingi wa yote na lazima iendeleo kuimarishwa. Na imani hiyo itaimarishwa kwa mambo matatu, ambayo nimekwishayasema kwa namna moja au nyingine: kwanza, kuwasemea na kuwatetea wanyonge; pili, kukemea rushwa na maovu katika Chama chenyewe, Serikali na jamii nzima; na tatu, kutekeleza ilani na ahadi za CCM kwa wananchi. Haya yote lazima yafanyike kwa pamoja. Moja peke yake halitoshi. Tumeona jinsi ambavyo unaweza kutekeleza ilani kwa asilimia 100 lakini bado ukanyimwa kura kama watu hawawaamini, hawaoni mnaowatetea, wanaona mnaendekeza rushwa, mnagombana kwa ajili ya vyeo kila siku.

Kwa hiyo sioni mbadala wa CCM kwa sasa kwa utayari wa uongozi wa taifa letu. Amani, utulivu, umoja na maendeleo ya nchi yetu, salama yake iko mikononi mwa CCM. Lakini kwa uimara wa demokrasia hapa nchini, tunahitaji vyama vya upinzani imara lakini sio wajibu wa CCM kuimarisha vyama vya upinzani.

Na sidhani kama navyo vimefanya kazi nzuri kujiimarisha kwani kila kukicha tunasikia migogoro ya kufukuzana na kugawanyika vipande ambako hakutoi taswira ya utayari wa kupewa uongozi wa nchi. Pale ambapo tumeshindwa na upinzani kwenye chaguzi mbalimbali, mara zote huwa ni kutokana na makosa yetu aidha migawanyiko au kuchagua wagombea wasiokubalika au kutotimiza ahadi au kutochukua hatua kwenye masuala ya rushwa, lakini sio kwa sababu kwa kukubalika kwa upinzani. Kwa hiyo makosa yetu yanarekebisha. Na tunayarekebisha.

Kuhusu uwezo wa kijana kukiongoza Chama kikongwe, uzuri wa Chama chetu ni kwamba Mwenyekiti wa CCM ni Mwenyekiti wa vikao vya ngazi ya juu ya Chama. Rais wa nchi huwa ana maamuzi yake ya kimamlaka kama Rais lakini Mwenyekiti wa CCM hana maamuzi binafsi. Mambo yote yanaamuliwa katika vikao ambavyo yeye anaviongoza. Kwa mfano, Wakuu wa Mikoa anateua Rais mwenyewe lakini Makatibu wa CCM wa Mikoa wanateuliwa na Halmashauri Kuu ya Taifa. Chama chetu hakiendeshwi na mtu mmoja. Kinaendeshwa na Katiba, Kanuni na maamuzi ya vikao. Kinachohitajika ni busara na hekima ya kupata Sekretarieti nzuri, Kamati Kuu nzuri na watendaji wazuri. Inahitajika ubunifu



January Makamba akizungumza na wananchi wa Mponde, Bumbuli wakati wa kutangaza utatuzi wa mgogoro wa kiwanda cha chai.



Rais Kikwete akimsikiliza kwa makini January Makamba akihutubia katika moja ya mikutano ya wananchi.

wa kusimamia upatikanaji wa rasilimali za kutosha za kuendesha siasa na shughuli za Chama na Jumuiya zake. Ubunifu huo vijana wengi tunao. Vilevile, Chama chetu kinahitaji mabadiliko makubwa ya kiutendaji na kiuendeshaji ili



kikabiliana na zama mpya za ushindani mkali wa kisiasa na mazingira mapya na changamoto mpya za ndani ya jamii. Ufahamu na uwezo wa kuleta hayo mabadiliko vijana wengi tuliotelewa na kukulia na kupata uongozi wa juu wa

CCM tunao. Naweza kuelewa kwamba, bila hata kujali umri, mtu ambaye hajawahi kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu au Halmashauri Kuu ya Taifa anaweza kupata changamoto ya uelewa wa namna ya kukiongoza Chama chetu. Lakini kama umeshakuwa Mjumbe wa Sekretarieti, Mjumbe wa Kamati Kuu, Mjumbe wa Halmashauri Kuu, kama ambavyo nimeshawahi kushika nafasi zote hizo, utakuwa umepata uelewa madhubuti wa uendeshaji na uongozi wa Chama.



January Makamba akiwa katika nafasi yake ya Mjumbe wa Sekretarieti ya CCM akipokea maelekezo kutoka kwa Mwenyekiti wa CCM Ndugu Kikwete kwenye Mkutano Mkuu wa CCM Kizota, pembeni ni ndugu Pius Msekwa, Novemba 2012.

34

Hapa Tanzania karibu kila mtu, hata ambao ni watumishi wa Serikali na hata wananchi wa vijijini ni wajasiriamali. Lakini ujasiriamali unakwamishwa na ukosefu wa mikopo. Benki ziko nyingi lakini hazikopeshi watu maskini ambao hawana dhamana. Taasisi za ukopeshaji, *microfinance*, zimejaa lakini riba ni kubwa na watu wanashindwa. Kulikuwa na Mabilioni ya JK lakini hayakufika mbali. Kuna jambo gani kubwa na jipya la kumaliza tatizo hili?

Ni wazi kwamba taratibu za sasa za ukopeshaji katika huduma ya fedha bado zinawaacha wajasiriamali na wananchi wengi kwa ujumla nje ya mfumo wa huduma ya fedha.

Tunayo nafasi ya kipekee kabisa ya kumaliza umaskini wa Watanzania kwa kuwawezesha kupata mikopo wanayoihitaji na wanayoweza kuimudu.

Nawaza tuanzishe Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Ujasiriamali Vijijini ambao utafanya kazi kwa karibu na Mamlaka mpya tuliyoiongelea, Mamlaka ya Ujasiriamali Mdogo na wa Kati. Mfuko huu, kwa miaka miwili ya kwanza, utagharamiwa na Serikali. Napendekeza utaratibu ufuatao wa uendeshaji wa Mfuko huu:

Kwanza, kila kijiji katika nchi yetu kiwe na mfuko mdogo au taasisi ndogo ya fedha, kwenye mfumo wa VICOBA pamoja na Village Savings and Loans Groups (VSLs), ambayo itasimamiwa na Kamati Ndogo ya watu watano – wanawake watatu na wanaume wawili, ambao wamepitia na kufuzu uendeshaji wa vikundi vya kuweka na kukopa. Watu hawa watano watachaguliwa katika mkutano mkuu wa kijiji.

Serikali itatenga kiasi cha shilingi milioni 50 kwa kila kijiji kwa mwaka kwa miaka miwili kwa ajili ya kukopesha wananchi wanaohitaji mikopo kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali kama vile kununua pembejeo za kilimo, mashine za kusindika mazao, na kadhalika. Kila mwananchi pale kijijini anayehitaji mkopo atapeleka maombi yake kwenye Kamati ya Kijiji. Maombi yatakatopokelewa yatakuwa ya thamani kati ya shilingi 50,000 hadi milioni moja.

Fedha zitakazotengwa kwa kila kijiji zitawekwa kwenye akaunti maalum katika Benki ambayo itakuwa mshirika katika mpango huu. Kamati haitakuwa na fedha mkononi. Atakayeidhinishiwa mkopo atapewa hundi kwenda kuchukua pesa aliyoidhinishiwa benki. Wanakijiji, katika mkutano wao, watakuwa na uhuru wa kuamua kuhusu riba na utaratibu wa urejeshaji wa mikopo. Mikopo hii itatumika kwa shughuli za ujasiriliamali na uzalishaji mali, sio matumizi ya kawaida au kutatua matatizo ya kila siku. Wanakijiji wote watakuwa na wajibu wa kuhakikisha aliyepewa mkopo anarudisha kwa wakati ili wengine nao wapate. Wanakijiji katika umoja wao ndio watakaokuwa dhamana na hakika ya mkopo kurudi na fedha hizi kuzunguka.

Imani yangu ni kwamba tukiongeza mzunguko wa shilingi milioni 100 ndani ya miaka miwili katika kila kijiji tutaona mzunguko mkubwa wa fedha, tutaona matunda ya uzalishaji mali na tutaona maendeleo ya watu.

Mpango kama huu umefanyika nchini Thailand kwa miaka kumi sasa. Serikali kule ilitoa fedha kwa kila kijiji, takriban dola 30,000 kwa mwaka, kwa miaka miwili tu na haikutoa tena lakini Mfuko ule umepanuka na kuwa na jumla ya dola za Kimarekani bilioni 6 na umepunguza umaskini wa watu kwa kiasi kikubwa. Na ni mfuko unaoongoza duniani kwa kuwawezesha wajasiriamali wengi zaidi. Na sisi tunaweza kufanya hivi. Pesa zinazohitajika Serikali inaweza kuzipata. Na matumizi ya pesa hizi sio matumizi potevu ni pesa zinazozunguka ndani ya uchumi wetu, ndani ya vijiji vyetu, na kutumika kuzalisha mali na kutengeneza ajira.

Natambua kuna mifuko kadhaa ya ukopeshaji na uwezeshaji wajasiriamali lakini mifuko hii ni midogo midogo, na inatoa fedha ndogo ndogo na katika maeneo machache. Kama tunataka kupata matokeo makubwa na ya haraka, tulifanye jambo hili kwa ukubwa unaostahili. Fedha iwe nyingi na ifike nchi nzima na utaratibu wa mikopo uwe wa uwazi.

35

Nini nafasi ya uhuru wa vyombo vya habari katika kuchochea maendeleo ya taifa letu. Unaongeleaje suala la kuwa na vyombo vya habari vingi ambavyo vinaandika habari za uchochezi.

Vyombo vya habari vina nafasi kubwa kwa maendeleo ya nchi yetu. Kukomaa kwa demokrasia kunategemea uhuru wa vyombo vya habari. Kuwepo kwa wananchi walioamka na wanaojua haki zao na namna ya kuzipata kunategemea uwepo wa uhuru wa vyombo vya habari. Uwajibikaji wa viongozi wa umma unategemea uwepo wa uhuru wa vyombo vya habari.

Siamini katika kufungia magazeti au kukamata na kufunga waandishi wa habari. Naamini kwamba Serikali ambayo haina cha kuficha haiwezi kuwaogopa au kuwa na uadui na vyombo vya habari. Naamini katika haki ya kikatiba na kisheria ya wananchi kupata habari. Naamini katika uwezeshaji wa waandishi wa habari kuandika habari za kiuchunguzi. Karibu kila mtu anaweza kuripoti matukio na siku hizi kuna fursa nyingi za watu kupata habari za matukio moja kwa moja bila hata kungoja yaandikwe. Mchango mkubwa wa vyombo vya habari unaweza kupatikana katika habari za kiuchunguzi ambazo zinaweza kuisaidia Serikali na jamii kwa ujumla.

Weledi, uwezo na maadili ya waandishi wa habari pia yana nafasi kubwa katika kuifanya tasnia ya habari itoe mchango unaohitajika kwenye maendeleo ya nchi. Kwa hiyo kujenga uwezo wa waandishi wa habari ni nyenzo muhimu katika kuiwezesha tasnia ya habari kutimiza wajibu wake kwa jamii. Hata hivyo, vyombo vya habari vina haki lakini pia vina wajibu.

Wajibu wa kwanza ni ukweli. Kwakuwa watu wengi wanaamini taarifa za vyombo vya habari, wajibu wa kuwa wakweli una maana na umuhimu mkubwa. Mtu anaposingiziwa uongo na kuchafuliwa kwenye vyombo vya habari maisha yake yote yanaweza kuharibika kabisa. Kuna namna mbili za kukabiliana na jambo hili. Moja ni kutumia taratibu za ndani ya tasnia yenyewe kujiadabisha, yaani *self-policing*. Ni muhimu taratibu hizi zikatoa fursa za uwajibikaji wa vyombo vya habari kwa kukiuka misingi na maadili ya tasnia. Ni muhimu taratibu hizi

za ndani ya tasnia zikaaminiwa na watu kwamba zinatoa haki na uwajibikaji. Namna nyingine ni kutumia mifumo ya udhibiti wa maadili ya upashanaji habari itakayokuwa imewekwa na sheria za nchi. Cha msingi ni kwamba sheria hizi na mifumo hii isionekane kuminya uhuru wa vyombo vya habari. Lakini pia hatupendi kuwa na jamii ambapo mtu anaonewa na anachafuliwa makusudi kwenye vyombo vya habari lakini hana namna ya kurejesha heshima yake kwenye jamii.

Vilevile, katika sheria mpya ya vyombo vya habari inayofikiriwa, naona fursa ya ushirikiano wa karibu kati ya Serikali na vyombo vya habari katika kudhibiti masuala yanayohusu tasnia ya habari.

Wajibu mwingine wa vyombo vya habari ni uzalendo. Tunaruhusiwa kuanika maovu kwenye jamii lakini katika kuandika habari za taifa tuongozwe na uzalendo. Kote duniani, vyombo vya habari vinafanya hivyo kwa nchi zao. Hata katika nchi zenye uhuru mkubwa wa vyombo vya habari, baadhi ya vyombo vimekuwa tayari kutochapisha habari ambazo zinazoweza kuhatarisha usalama wa nchi. Vilevile, kwa mfano kwenye nchi kama Marekani, vyombo vya habari vya kule vinasema kwamba sisi Wamarekani ndio tuna haki ya kumsema Rais wetu na kweli vinafanya kazi hiyo lakini pale tu vyombo vya habari vya nje vinapomsema Rais wa Marekani, vyombo hivyo vinakuja juu na kuungana. Hapa nimeona kuna baadhi, sio vyote, baadhi ya vyombo vya habari vinashabikia na kurudia udhalilishaji wa nchi yetu unaofanywa na vyombo vya nje. Lazima tuongozwe na uzalendo. Nakubali pia kwamba kufichua maovu ni kielelezo cha uzalendo na kwamba kazi hiyo lazima iendeleo kufanywa.

Kuhusu wingi wa magazeti, mimi sina tatizo na jambo hili. Wingi wa magazeti unatoa fursa kwa watu kupata mitazamo tofauti na vionjo tofauti. Kama soko la magazeti 30 lipo, na kama mahitaji yapo, sioni kwanini ni tatizo. Magazeti ambayo hayana habari zenye mvuto au ambayo hayaaminiwi na wasomaji yataondolewa yenyewe na soko.

Uimara wa vyombo vya habari na uwezo wa vyombo hivyo kutimiza wajibu wake pia utategemea ari na motisha ya waandishi wa habari na maripota. Hawa ndio askari wa mstari wa mbele wanaoenda kutafuta stori na ambao wanashuhudia matukio. Lazima wawezeshwe kitaaluma na kimaslahi kuifanya kazi hii. Uandishi wa habari ni kazi ya heshima na wajibu mkubwa. Hakupaswi kuwa na mwandishi wa habari kibarua.

Vilevile tunaona jinsi maendeleo ya TEHAMA yanavyobadilisha tasnia ya habari kwa kutoa changamoto lakini zaidi fursa kwa wanahabari kuwafikia watu wengi kwa haraka zaidi. Kwa mfano, gazeti lolote makini haliwezi kumudu kutokuwepo kwenye mitandao ya kijamii. Vilevile, kwa kuwa kutokana na TEHAMA, matukio yanaripotiwa kwa kadri yanavyotokea na watu wengi wanapata habari mapema bila hata kungoja gazeti kesho yake, tasnia ya habari ina changamoto ya kuwa na ubunifu katika kuripoti taarifa ambazo tayari sio habari tena.



January Makamba akiongoza mkutano alioitisha kwa ajili ya kutafuta utatuzi wa matatizo katika Kampuni ya Simu ya TTCL. Mkutano huo ulipelekea kusimamishwa kazi kwa baadhi ya maofisa wakuu wa kampuni hiyo. Mafanikio ya mageuzi katika TTCL yameanza kuonekana.

36

Baada ya uvumbuzi wa gesi nchini, kumekuwa na mjadala kuhusu Watanzania kunufaika na rasilimali za taifa hili. Una maoni gani kuhusu huu mjadala? Nini kifanyike ili watu wa hali ya chini wanufaike? Kama kiongozi umeshiriki vipi kuhakikisha Watanzania wananufaika na rasilimali zao?

Watanzania wanayo haki na wajibu wa kuhoji na kujadili kuhusu manufaa wanayopata kutokana na uvunaji wa rasilimali asili za nchi yao. Kwa hiyo mjadala huu ni mjadala mzuri. Cha msingi ni kwamba mjadala huu usitekwe na wanasiasa au wanaharakati wachache ambao hawana taarifa wala uelewa wa kina kiasi cha kupotosha watu. Ni muhimu wananchi wote wapewe uelewa ili washiriki katika mjadala huu.

Mambo manne yanahitajika ili Watanzania wanufaike na rasilimali-asili zilizopo nchini.

Kwanza, ni muhimu kuwa na taarifa sahihi kuhusu kiwango cha rasilimali asili iliyopo kama sehemu ya mkakati wa uvunaji. Kwa mfano ipo tofauti kubwa kama kabla ya kutoa leseni ya uchimbaji gesi au madini, wewe mwenyewe kama Serikali ukawa unajua kiwango na ubora wa madini au gesi iliyopo. Mara kadhaa nyingi kampuni za kigeni zinapoomba leseni za utafutaji wa rasilimali kama vile gesi au madini yenyewe huwa tayari zina taarifa sahihi za rasilimali zilizopo ardhini. Taarifa hizi ni mali kubwa kwani zipo kampuni za kigeni ambazo hazikuwa na mtaji wa kuvuna hizi rasilimali lakini zimetumia taarifa hizi kwenda kutafuta mitaji kwenye masoko ya fedha. Kwa hiyo kama nchi, ni muhimu tukajenga uwezo wa kuwa na hizi taarifa.

Pili, ili kujua kiasi au kiwango cha rasilimali-asili zilizopo, hasa gesi, mafuta au madini, pamoja na mchakato wa kuzivuna rasilimali asili hizo, kunahitaji matumizi ya teknolojia na mtaji mkubwa. Kama hatutajenga mtaji wa ndani na uwezo wa kiteknolojia wa ndani ya nchi, basi siku zote tutatafuta mitaji

na teknolojia kutoka nje ya nchi kuja kusaidia kuvuna rasilimali-asili. Kujenga uwezo wetu kunaweza kuchukua muda mrefu lakini pa kuanzia ni kwenye ukweli kwamba rasilimali uliyonayo ni sehemu ya mtaji.

Tatu, ni suala la uwazi kwenye gharama za uvunaji rasilimali na mapato kwa washiriki wote wa uvunaji wa rasilimali-asili. Lazima sheria, kanuni na taratibu za uvunaji rasilimali zilazimishe washirika wote kuonyesha gharama za uvunaji, mapato yanayopatikana katika mauzo, gawio la kila mshirika na kodi au mirahaba inayolipwa Serikalini. Uwazi utawezesha kupunguza mianya ya wachache kujinufaisha lakini pia utatoa fursa kwa wananchi kujua na kuhoji kuhusu matumizi ya fedha zinazotokana na uvunaji wa rasilimali. Hapa la kuanza nalo ni uwazi kwenye mikataba na kwenye mchakato wa kujadiliana na kukubaliana juu ya mikataba hii.

Nne, ni muhimu kukawepo mpangilio wa kitaasisi na mifumo na sheria imara za kudhibiti shughuli za uvunaji pamoja na maamuzi ya matumizi ya fedha zinazotokana na rasilimali-asili. Mfumo wa maamuzi muhimu kuhusu rasilimali zetu yasitegemee tu aina na busara ya viongozi waliopo kwa wakati huo bali yawe na nguvu za kisheria na utaratibu wa kitaasisi.

Tano, mapato yatokanayo na uvunaji wa rasilimali asili, hasa gesi, yasiingie moja kwa moja kwenye matumizi ya kawaida ya Serikali kama kununua magari au kugharimia vikao au kulipa mishahara bali yatumike kwenye mambo makubwa na ya msingi ambayo yataonekana na wananchi na wananchi wanaweza kuyatambua kama matunda ya uvunaji wa rasilimali zao – kwa mfano ujenzi wa vyuo vikuu vipya na vyuo vya ufundi kote nchini, ujenzi wa mahospitali na zahanati, ufundishaji wa madaktari na manesi, utekelezaji wa miradi mikubwa ya maji, ujenzi wa miradi mikubwa ya miundombinu, uanzishaji wa mifuko mikubwa ya kutoa mitaji ya biashara kwa shughuli za uzalishaji mali. Mapato ya rasilimali-asili yatumike kujenga rasilimali-watu ya nchi na kujenga uwezo wa uzalishaji mali katika sekta nyingine, kama vile kilimo na viwanda, ili kuondokana na utegemezi wa rasilimali-asili kwa ustawi wa taifa.

Mwisho, ni muhimu pia sisi tunaoishi sasa kutambua kwamba kuna vizazi vingine vya Watanzania vinavyokuja. Kwa hiyo, kwanza, tusigawe na kuvuna rasilimali asili zote sasa hivi kana kwamba ndio mwisho wa dunia na kana kwamba sisi ndio Watanzania wa mwisho kuwepo. Hakuna sababu ya kugawa vitalu vyote vya gesi na maeneo yote yenye dhahabu au kutoa vibali vya kuwinda kila pahala au kuvuna misitu yote – kana kwamba sisi ndio wa mwisho kuishi kwenye nchi hii. Nchi ya Norway iligundua mafuta miaka ya 1960 na wakati huo walikuwa hawana uwezo wa kimtaji na kiteknolojia kuvuna mafuta hayo. Kwa

hiyo wakawakaribisha Wamarekani kufanya hiyo kazi, lakini waligawa vitalu kidogo kidogo, na hadi sasa wana vitalu havijagawiwa, na kutokana na busara hivyo walijenga maarifa mapya na uwezo wao wenyewe na kunufaika zaidi kwa kadri muda ulivyoenda. Rasilimali-asili huwa zinaisha. Tubakize baadhi kwa vizazi vijavyo vinavyoweza kuwa na maarifa tofauti na uwezo tofauti wa kuvuna na kunufaika na rasilimali hizi. Pili, matumizi ya pesa tunazopata kwa uvunaji wa rasilimali yalenge kwenye uwekezaji utakaosaidia pia vizazi vinavyokuja.

Nafahamu kwamba kuna mpango wa kuanzisha Mfuko wa Mapato ya Gesi au *Sovereign Wealth Fund*. Hili ni jambo jema. Fikra yangu mimi ni kwamba jambo muhimu zaidi ni kujenga uwezo wa uwekezaji wa Serikali, yaani *public investments*, wenye tija. Hapa namaanisha kwamba, kwa mfano, kama tumewekeza kiasi kikubwa cha fedha kwenye elimu lakini hatukupata matokeo ya elimu yanayoendana na uwekezaji huo, kuweka fedha zaidi za gesi kwenye elimu hakutakuwa na maana kama hatutajua kwanza ni kwanini hatupati thamani ya fedha kwenye uwekezaji unaofanywa na Serikali. Kwa hiyo kabla ya kuongeza fedha kwenye jambo lolote lazima kujifunza na kurekebisha kasoro zinazofanya fedha za umma zipotee na zisitupe tija na matokeo tunayotarajia.

Jingine la mwisho ni kwamba ni muhimu sheria, kanuni na taratibu zikawekwa ili mchakato wa mavuno ya rasilimali asili, hasa gesi na madini, ambayo karibu mara zote unafanywa na kampuni za nje, ukawezesha biashara na shughuli nyingine za uchumi, hasa zinazomilikiwa na Watanzania, zikashamiri. Makampuni haya yanafanya manunuzi ya thamani kubwa sana. Ni muhimu manunuzi haya yakafanyika hapa nchini. Uchumi wa gesi sio mapato ya gesi peke yake. Uchumi wa gesi lazima uingiliane na ushamirishe uchumi mpana.

Pia kumekuwa na mjadala kuhusu manufaa wanayopata wananchi wanaoishi kwenye maeneo ambapo rasilimali-asili hizi zinavunwa. Baadhi ya maeneo wanasema hizi ni rasilimali zao na wao ndio wana maamuzi ya aidha rasilimali hizi zivunwe au la. Mimi sikubaliani na msimamo huu.

Rasilimali-asili, popote zilipo, ni mali ya Watanzania wote. Ila nakubaliana kwamba walinzi na watunzaji wa kwanza wa rasilimali hizi ni wananchi wanaoishi kwenye maeneo hayo. Kwahiyo ni muhimu wao waone manufaa ya haraka na ya moja kwa moja ya uvunaji huo. Na lazima juhudi za makusudi zifanyike kuwezesha hili suala.

37

Wakati wa Bajeti, kila tunapozungumzia kutotekelezwa kwa miradi ya maendeleo, kutolipwa kwa wazabuni, kutolipwa kwa walimu na askari, tunasikia sana msembo wa “kasungura kadogo”. Je, kutokana na hali hii, kuna matumaini ya kupata maendeleo kama kila wakati Serikali inasema haina fedha ya kutekeleza majukumu yake ya msingi? Je, kuna maarifa gani mapya, ambayo wewe kama kiongozi wa kizazi kipya, ambayo unayo kuhusu namna ya kupata fedha za maendeleo?

Ni kweli kwamba kiasi cha fedha ambacho Serikali inakikusanya ni kidogo ukilinganisha na mahitaji yetu. Kwa sasa, kwa upande wa kodi, Serikali inakusanya wastani wa shilingi bilioni 800 kwa mwezi. Kati ya hizo, bilioni 400 zinaenda kulipa mishahara, bilioni 200 kwenye matumizi ya lazima, na zinabaki bilioni 200 kwa ajili ya kuendesha Serikali na shughuli za maendeleo. Hizi ni kidogo ukilinganisha na majukumu tuliyonayo. Kwa hiyo lazima tubadilishe hali hii. Kwanza, kama taifa ni muhimu tukayabainisha mahitaji na majukumu yetu ya msingi, yaani mambo gani muhimu tunayopaswa kuyafanya na ambayo inabidi kuyatafutia fedha. Hata kwenye familia, tunatafuta fedha kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya msingi ambayo tayari tunakuwa tumekwishayabainisha – kodi ya nyumba, chakula, ada ya shule kwa watoto, nauli na kadhalika. Kama taifa, kuyatambua na kuyabainisha majukumu ya msingi lazima iwe kazi ya kwanza kama tunataka kutumia pesa ya umma vizuri. Inawezekana ikaonekana kwamba hapa nazungumza jambo ambalo ni dhahiri. Hapana. Hili ni muhimu kwa sababu tusipofanya hivi, tutakuwa tunatafuta na kutumia rasilimali katika mambo ambayo sio ya msingi.

Sasa mambo gani ambayo mimi naamini ni majukumu ya msingi?

Naweza kuyagawa majukumu yetu ya msingi kwa aina nne.

Aina ya kwanza ni yale majukumu ya msingi yanayotoa uhalali wa uwepo wa dola. Haya yapo ya aina tatu.

Kwanza, ni ulinzi wa mipaka yetu. Hapa maana yake tunalinda uhuru na usalama wetu. Hapa hatuwezi kusema “tuna kasungura kadogo”. Kazi hii hatuwezi kuifanya nusunusu.

Pili, ni usimamizi wa amani na utulivu na ulinzi wa uhai na usalama wa Watanzania na mali zao. Hili ni jukumu la msingi la dola. Kazi hii hatuwezi kuifanya nusunusu kwa sababu ya msemu wa “kasungura kadogo.”

Tatu, ni usimamizi wa upatikanaji wa haki za watu pamoja na usimamizi wa utawala wa sheria. Hili pia ni jukumu la msingi ambalo lazima litekelezwe kwa ukamilifu, bila kuathiriwa na ufinyu wa bajeti.

Aina ya pili ya majukumu ya msingi yanahusu ustawi wa watu, kwa maana ya huduma za jamii na kipato chao.

Kuhusu huduma za kijamii, tunalo jukumu la msingi na wajibu wa kuhakikisha watoto wetu wanapata elimu, tena elimu iliyo bora kabisa inayoendana na mazingira ya dunia ya sasa. Tunalo jukumu la msingi la kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora ya afya, wanapata umeme huko walipo, wanapata maji safi na salama, wana huduma ya mawasiliano, wanafikiwa na barabara nzuri.

Serikali inao wajibu, kwa kushirikiana na wadau wengine, kuwekeza katika kuhakikisha Watanzania wote – wa vijijini na mijini wanapata huduma hizi kwa usawa. Hili ni jukumu la msingi sana – na hatuwezi kuendelea kusema kwamba hatuna fedha za kulitekeleza. Tusipotekeleza wajibu huu, kutajengeka hali ya kutokuwepo kwa usawa kwenye jamii kwa sababu watakuwepo watu wenye uwezo kwa kupata huduma hizi wakati wengine wakibaki hohehahe.

Kuhusu kipato cha Watanzania, ni dhahiri Serikali haiwezi kuwawekea fedha mifukoni Watanzania lakini tunao wajibu wa msingi wa kuweka mazingira mazuri ya Watanzania kupata fursa za kutumia nguvu zao na maarifa yao kujitengenezea kipato. Tunalo jukumu la msingi kuhakikisha kwamba shughuli za uchumi zinaendeshwa kwa uhuru na zinapanuka na kila Mtanzania ana fursa ya kushiriki na kunufaika na uchumi unaokua. Tunalo jukumu la kuhakikisha



January Makamba ni kipenzi cha watoto, pichani anaonekana akifanya mazungumzo nao.

kwamba wazalishaji mali wanaotumia ardhi na maji, yaani wakulima, wavuvi, na wafugaji wananufaika na jasho lao na shughuli zao zina tija. Tunalo jukumu la msingi la kuhakikisha kwamba wazalishaji mali kwa kutumia mitaji nao wanayo mazingira mazuri ya kunufaika na mitaji yao. Tunao wajibu wa msingi wa kuhakikisha hakuna vikwazo vya kisera, kikodi au kiutendaji kwenye kuwawezesha Watanzania kutafuta riziki ili kuendesha familia zao na kujitengenezea utajiri.

Lakini mwisho tunalo jukumu la msingi la kuwalipa mishahara na stahili zao watumishi wa umma kama vile askari wa vyombo vya ulinzi na usalama, walimu, madaktari na manesi, na wengineo - ambao wanaiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya msingi.

Haya ndiyo majukumu ya msingi nionavyo mimi. Sasa tunajenga vipi uwezo wa kirasilimali ili kuyatekeleza haya?

Kwanza, kuna suala la kimtuzamo. Tuondokane na mtuzamo wa kimaskini na mtuzamo wa kuyatazama haya majukumu ya msingi kama ni mzigo mkubwa ambao hauwezekani kuubeba. Tanzania ni nchi kubwa, yenye changamoto nyingi lakini kuna msembo kwamba tembo hashindwi kubeba mkonga wake. Haya majukumu hayapaswi kutushinda. Kwa hiyo kwanza ni lazima tubadilishe mtazamo na lugha ya kasungura kadogo. Tukibaki na fikra na mtazamo huo, kila siku tutakuwa tunatengeneza maarifa na ubunifu wa kugawana kasungura kadogo badala ya kutengeneza maarifa na ubunifu wa kuwinda nyati mkubwa.

Pili, na muhimu zaidi ni kwamba lazima tujenge uchumi unaoweza kubeba majukumu haya yote. Majukumu haya hayawezi kubebwa kwa misaada ya wahisani au kukopa fedha pekee. Waswahili wanasema “nunua kiatu kwa saizi ya mguu wako”. Sasa ukubwa wa majukumu yetu tunaufahamu kwa hiyo hatuna budi kujenga uchumi ambao utatupa uwezo wa kutekeleza haya majukumu. Lazima shughuli za uchumi zipanuke, wananchi wengi washiriki kwenye uzalishaji mali wenye tija na kuingia kwenye uchumi rasmi, uwekezaji wa ndani na kutoka nje ukue, ajira ziongezeke, watu wengi zaidi walipe kodi. Kipato cha mtu mmoja mmoja kiongezeke ili watu waweze kumudu maisha na Pato la Taifa nalo liongezeke ili taifa liweze kumudu mahitaji ya nchi. Kwa ujumla, vipato vya watu na mapato ya Serikali yapanuke ili tumalize kabisa na tuache kuendelea kuzungumzia vitu kama madawati, vitabu mashuleni, malipo ya walimu, wauguzi, na askari; masuala kama pembejeo; maji safi na salama, na mambo mengineyo yasiwe tena masuala ya kujadili, kama ilivyo katika baadhi ya nchi duniani ambazo mambo haya walishayamaliza na leo hawajadili tena kuhusu madawati au ujenzi wa vyoo au pembejeo kuwafikia wakulima. Hili linawezekana kabisa hapa kwetu Tanzania.

Wakati tunaelekea kwenye uchumi mkubwa unaoweza kubeba majukumu yetu ya msingi, tunaweza kuchukua hatua za muda mfupi, ili kupata rasilimali za kutosha kutekeleza majukumu hayo, kuna mambo ambayo ni lazima tuyafanye.

Kwanza, tubuni vyanzo vipya ya mapato ya Serikali. Kuongeza kodi kwenye vyanzo pekee vya sasa hakutoshi. Baadhi ya vyanzo vipya vya mapato kwa Serikali vimebainishwa kwa kina kwenye ripoti ya Bunge kuhusu mapato ya Serikali. Tukifanikiwa kukusanya fedha kwenye vyanzo hivi, tutaongeza uwezo mkubwa wa kutimiza majukumu yetu ya msingi kama nilivyoyaeleza hapo awali.

Pili, kila Mtanzania anayestahili kulipa kodi anapaswa kulipa kodi stahiki. Kwa sasa wengi wa Watanzania wanaolipa kodi ni watumishi wa umma na wafanyakazi walio kwenye sekta binafsi rasmi na wenye biashara walioamua

kuzirasimisha. Hatuwezi kuwa na majukumu haya yote lakini wapo wenzetu wanaokwepa kulipa kodi. Kila Mtanzania awe na namba na kadi ya mlipakodi, hata kama hana kipato chochote basi ajaze fomu kusema hana kipato. Sasa hivi unaweza kupata TIN pale TRA lakini ni mpaka wewe mwenyewe ukiomba, na tena mpaka uipate ni shida kweli kana kwamba sio nyenzo ya mapato ya Serikali.

Vilevile, tubadilishe sheria ili kosa la ukwepaji kodi liwe ni kosa la uhujumu uchumi na adhabu yake iwe ni kufilisiwa na kifungo kirefu. Tujenge utamaduni kwamba kosa la kukwepa kulipa kodi iwe ni dhambi kubwa na usaliti kwa taifa.

TRA ipewe mamlaka kubwa zaidi iweze kukamata watu, kuwashtaki na kuwafilisi bila kupitia hatua ndefu za kimashtaka. Hili linawezekana. Nchi kama Marekani, Mamlaka ya Mapato ya nchi hiyo, yaani IRS, inaogopwa kuliko hata Polisi au Mahakama. Na sisi iwe hivyo hivyo. Na mtu yoyote ambaye amepatikana na hatia ya kukwepa kodi basi akose baadhi ya haki, kwa mfano haki ya kugombea uongozi, kwa kipindi fulani. Lakini nguvu hiyo mpya ya TRA lazima iendane na weledi na uadilifu wa hali ya juu wa watumishi wa TRA. Kwa sasa, tunakusanya kiasi kidogo cha kodi – takriban asilimia 30 ya kiwango tunachoweza kukusanya. Tukikusanya kodi ambayo haikusanywi sasa, tutaweza kuongeza kwa kiasi kikubwa rasilimali ya kutekeleza baadhi ya majukumu haya ya msingi.

Jambo jingine ni la misamaha ya kodi. Ni kweli kwamba ipo misamaha ya kodi ambayo inachochea uchumi, kuongeza uzalishaji na kusaidia ufanikishaji wa baadhi ya majukumu ya msingi ya Serikali. Lakini pia ipo misamaha ambayo haina tija yoyote na ambayo inatumiwa vibaya na kuwanufaisha zaidi watu binafsi kwa manufaa binafsi. Hii nayo ni muhimu kuitazama upya na kuifuta. Lakini pia ipo misamaha ambayo ni sahihi lakini inatumiwa vibaya. Kwa mfano unatoa msamaha wa mafuta kwa ajili ya mitambo ya uchimbaji madini lakini nusu ya mafuta hayo yanauzwa mitaani. Misamaha ya kodi imeongezeka kutoka shilingi bilioni 680 mwaka 2010, mpaka kufikia Trilioni 1.8 mwaka 2012, hili ni tatizo kubwa. Kuna tafiti mbalimbali zinazosema kwamba misamaha ya kodi sio kivutio cha uwekezaji pekee, bali ubora wa miundombinu, utawala bora, na urahisi wa kufanya biashara pia vinachangia kwa kiasi kikubwa kuvutia wawekezaji. Ukipunguza misamaha iliyopo sasa, na kubaki na misamaha ya lazima tu kama ya taasisi za kidini, unapata pesa ambazo zinatoshia kuboresha miundombinu, kutoa ruzuku ya pembejeo na kununua matrekta hivyo kuchochea uzalishaji wa kilimo na kukuza sekta ya kilimo inayojiri Watanzania asilimia zaidi ya 70.

Jambo jingine ni kudhibiti wizi wa fedha za umma na kuongeza nidhamu ya matumizi ya fedha za umma. Hapa pia kuna tatizo kubwa. Wapo Watanzania wenzetu ambao hawaoni haya kuiba fedha za umma. Upo pia uzembe katika usimamizi ambapo Serikali inapoteza fedha nyingi tu. Kichocho kikubwa ni kwenye manunuzi ya umma, ambapo Serikali inapoteza kiasi kikubwa cha pesa kila mwaka, fedha ambazo zingesaidia kutekeleza majukumu yetu ya msingi. Kwa mfano mwaka wa fedha 2012, mashirika ya umma 315 yalitumia Trilioni 4.32 kufanya manunuzi tu, na kiasi kikubwa cha pesa kinapotea kutokana na mianya kwenye mchakato wa manunuzi na utamaduni wa “10 percent”. Zimewekwa taratibu ndefu za manunuzi ya umma kwa ajili ya udhibiti lakini wezi wa mali za umma wanatumia urefu huohuo wa taratibu hizohizo kujinufaisha. Hapa tunaweza kufanya mambo mawili: kwanza, kurahisisha taratibu za manunuzi na kuziweka wazi. Serikali ikitaka kununua kitu inatangaza wazi na washindani nao wanaweka bei zao wazi, tunafanya mnada wa wazi, ikiwemo kwenye tovuti mahsusi itakayowekwa na Serikali kwa ajili hiyo. Anayetoa kwa bei ya chini na ubora unaohitajika anashinda, basi kazi imekwisha.

Pili, tubadilishe sheria na kuweka utaratibu madhubuti wa kubaini rushwa na ubadhirifu kwenye manunuzi; na tuweke adhabu kali sana, siyo kufukuzwa kazi tu bali kufilisiwa na kifungo kirefu ukibainika umeiibia Serikali.

Haiwezekani kabisa sisi sote tuwe tunajua mshahara wako, na tunajua huna shughuli nyingine ya kipato lakini umejilimbikizia mali ambazo hazina maelezo halafu tunakutazama tu wakati kuna zahanati hazina hata bandeji, kuna shule hazina madawati, kuna walimu hawajalipwa stahili zao. Hapana kabisa! Huu ni usaliti wa hali ya juu. Watu wa namna hii hawapaswi kabisa kupona. Tukiweka vizuri nidhamu ya matumizi ya fedha, tutaweza kuelekeza fedha nyingi kwenye majukumu yetu ya msingi niliyoyaelezea.

Jambo jingine la muhimu la kutambua kwamba maendeleo hayaletwi na kodi inayotozwa na Serikali. Maendeleo, na uwezo wa taifa kutimiza majukumu yake, unatokana na ujumla wa shughuli za uchumi zinazoendelea ndani ya nchi. Kwa hiyo ni muhimu kukawa na mazingira wezeshi ya kila mtu kushiriki kwenye shughuli za uchumi na kujipatia kipato. Kila Mtanzania akiwa na kipato na uwezo wa kukabiliana na changamoto zake katika maisha na kutimiza majukumu yake ya msingi basi taifa nalo linakuwa katika nafasi nzuri ya kutekeleza majukumu yake ya msingi.

Vilevile, badala ya kusubiri watu watozwe kodi ndipo pesa ya maendeleo ipatikane na kutekeleza miradi ya maendeleo, ukweli ni kwamba ipo miradi ya

maendeleo ambayo ina mapato ya kibiashara na inaweza kufanywa na sekta binafsi kwa kushirikiana na Serikali. Kwa mfano ujenzi wa masoko, stendi na minada kwenye Halmashauri zetu, ujenzi wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji, na mambo mengineyo yanaweza kufanyika, kwa ushiriki wa sekta binafsi, bila kusubiri tugawane kasungura. Ni vema hapa tukarahisisha taratibu za Serikali kuingia ubia na sekta binafsi kwani kwa sasa ni taratibu ndefu na zinakatisha tamaa na kuchelewesha utekelezaji wa miradi muhimu.



January Makamba akifurahi na wananchi katika viwanja wa Karimjee.

Jambo jingine ni kwamba siku zote vyanzo vya fedha za maendeleo vimekuwa ni vilevile, yaani kodi, mikopo, na misaada ya wahisani. Siku hizi kuna mbinu na maarifa mengi mapya ambayo ni lazima tuyatumie. Imefika wakati sasa tutoe hati-fungani ya taifa, yaani Sovereign Bond, kama ilivyo Kenya, Rwanda, Ghana na nchi nyingine ambazo zimefanya hivyo na kupata fedha nyingi za maendeleo na kutekeleza miradi mikubwa. Kenya majuzi walikuwa wanatafuta dola za kimarekani bilioni 2 lakini wakajitokeza watu kununua hati-fungani ya Kenya kwa dola bilioni 8. Na sisi tumekuwa na mpango huo, ingawa kiasi tunachokitafuta cha dola milioni 700 ni kidogo kuliko mahitaji yetu na ni kidogo kuliko tunavyoweza kupata. Tutafute na sisi dola za kimarekani bilioni 3 ili

tumalize mambo makubwa na ya msingi yatakayoongeza chachu ya ukuaji wa uchumi wetu.

Vilevile, Halmashauri nazo ziruhusiwe kutoa hati-fungani, yaani Municipal Bonds, ili ziweze kutekeleza miradi mikubwa ya kuchochea uchumi kwenye Halmashauri hizo. Sheria inaruhusu. Serikali Kuu tunaweza kuzijengea uwezo Halmashauri na kuzidhamini kufanya hili. Tukifanikiwa kwenye hili, na kuwekeza kiasi kikubwa cha fedha kwenye ngazi ya Halmashauri kwenye miradi kama vile ya umwagiliaji na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, maendeleo ya haraka yataonekana.

Kuna tatizo kubwa la usimamizi wa miradi ya Serikali. Hapa tunapoteza fedha nyingi sana kwa wajanja wachache. Kwa mfano, daraja ambalo linapaswa kujengwa kwa shilingi milioni 100, linatengenezewa BOQ, yaani mahitaji, ya shilingi milioni 300 na hatimaye linajengwa kwa shilingi milioni 30 na linavunjika baada ya miaka miwili na zinatafutwa fedha nyingine za ujenzi.

Au kwenye mradi wa maji, panapostahili bomba la inchi 6 linawekwa bomba la inchi 2 na baada ya muda linapasuka na maji hayatoki tena. Haya nimeyashuhudia kama Mbunge ambapo niliwahimiza watu wa Bumbuli kukataa kupokea mradi uliojengwa chini ya kiwango. Cha ajabu kulikuwa na presha kubwa sana kutoka kila pahala kwamba tuupokee. Cha ajabu zaidi hakukuwa na adhabu yoyote kwa waliohusika. Cha ajabu zaidi mkandarasi huyo huyo akaendelea kupewa kazi nyingine zaidi za ujenzi. Haya yanatokea kila siku, kila mahali kwenye maeneo yetu.

Fedha za Serikali zimekuwa kama shamba la bibi, kila mtu anazila kwa nafasi yake, na pale alipo. Sasa hili lazima likome.


Fedha hizo zinazopotea zingeweza kutumika kutimiza majukumu yetu mengine ya msingi. Kuna haja kubwa ya kuweka utaratibu wa ukaguzi wa miradi ya Serikali, ikiwezekana hata kwa kutumia taasisi zenye weledi mkubwa kutoka sekta binafsi au nje ya nchi kwa kipindi kifupi ambapo tunajenga utamaduni mpya.

Lakini kubwa zaidi ni kuyabadilisha makosa ya wizi wa mali ya umma kuwa makosa ya uhujumu uchumi ambapo adhabu yake ni kali na ya wazi kama kufilisiwa na kifungo kirefu.

Serikali ina mali, tena mali nyingi sana. Serikali inamiliki moja kwa moja na ina hisa kwenye mashirika ya kibiashara zaidi ya 100. Mtaji wa Serikali kwenye haya mashirika ni zaidi ya shilingi trilioni 10 au asilimia karibu 30 ya Pato la Taifa. Tuchukue mashirika matano tu: Shirika la Mafuta Tanzania, yaani TPDC, yenye hisa kwenye visima vyote vya gesi nchini; Shirika la Umeme, yaani TANESCO, yenye mitambo na miundombinu ya kuzalisha na kusafirisha umeme kila kona ya Tanzania; Mamlaka ya Bandari, TPA, yenye bandari zote nchini; Shirika la Nyumba la Taifa, NHC, yenye maelfu ya majumba katika miji yote Tanzania; Shirika la Reli, TRL, lenye mtandao wa reli na injini na mabehewa mamia nchini. Haya mashirika matano tu, yakiendeshwa vizuri yanaweza kuendesha uchumi wa nchi yetu na kuwa vyanzo vikubwa vya mapato ya Serikali. Hapa sijataja mashirika na kampuni nyingine nyingi ambazo zinafanya biashara ambazo Serikali ina hisa. Ingekuwa watu binafsi wanamiliki mashirika haya wangekuwa matajiri wa kutupwa. Ukiwa unamiliki mashirika haya haupaswi kushindwa kununua vitabu vya watoto mashuleni, haupaswi kukosa madawa kwenye zahanati na hospitali. Lakini ili tufanikiwe lazima tubadili mfumo wa umiliki na usimamizi wa mali za Serikali. Kwa sasa mwenye mali ni Msajili wa Hazina lakini anayesimamia uendeshaji wa mashirika ni Wizara za Kisekta. Huu ni mkanganyiko wa kwanza. Shirika moja lina mabwana wawili. Suala hili aliwahi kulizungumzia kwa ufasaha zaidi rafiki yangu Ndugu Zitto Kabwe, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma.

Ni vyema basi tukaanzisha Kampuni kubwa tanzu, kwa Kiingereza wanaita *a Holding Company*, itakayomiliki na kusimamia uendeshaji wa Mashirika ya kibiashara ya Serikali kwa weledi, maarifa ya kisasa na kanuni ya kibiashara bila kuingiliwa na siasa.

Singapore wamefanya hivyo na wamefanikiwa sana. Msajili wa Hazina ameelemewa na majukumu mengi, ikiwemo kushiriki kwenye bodi za mashirika zaidi ya 100. Pia baadhi ya Wizara za kisekta zimeishia kuwa waendeshaji na wasemaji wa mashirika yaliyo chini ya Wizara hizo badala ya kutoa uongozi wa ujumla wa kisera na kimkakati wa maendeleo ya sekta husika.



January Makamba akielezea mikakati ya maendeleo jimboni Bumbuli.

Kwa kifupi, kama una mali, na mali hiyo ina uwezo wa kuzalisha na kukupa mapato, lazima uhakikishe mali hiyo inafanya hivyo ili utimize majukumu yako ya msingi. Hivyo hivyo kwa Serikali. Tunazo mali nyingi. Lazima zitusaidie kutupa rasilimali za kutekeleza majukumu yetu ya msingi kama nilivyoyaelezea hapo awali.

Jambo jingine la kutambua ni kwamba wananchi pia wanao wajibu binafsi wa kuchangia kwenye ustawi wao na hivyo ustawi wa nchi. Wananchi sio watwana tu wa kusubiri maendeleo kutoka Serikalini. Wananchi ni sababu ya maendeleo lakini pia ni wakala wa maendeleo. Ili tufikie jamii tunayoitaka, ili tutimize majukumu yetu ya msingi, haitoshi tu kwa Serikali kukusanya na kutumia kodi vizuri. Lazima Watanzania nao washiriki kwenye shughuli za uzalishaji mali zenye tija. Nasema zenye tija kwa makusudi kwa sababu Watanzania wanafanya kazi sana, Watanzania sio wavivu, lakini matunda ya kazi zao hayalingani na jasho wanalotumia. Hata hivyo, lazima Serikali iweke mazingira mazuri ya wananchi kunufaika na jasho lao. Kwanza, iwe rahisi kuingia kwenye ujasiriamali. Ziwepo fursa za mikopo kwa ajili ya shughuli

hiyo. Pili, kuwepo na mfumo mzuri wa masoko ya mazao ya wakulima. Kwa sasa mfumo wa ununuzi wa mazao karibu yote una matatizo na unamdhulumu mkulima. Shughuli za wafugaji na wavuvi nazo lazima ziwe na tija. Tatu, lazima tuwaingize Watanzania wengi zaidi kwenye mfumo wa hifadhi ya jamii, hata kama hawamo kwenye sekta rasmi. Huu ni moja ya muarubaini wa umaskini na unyonge.

Mwisho, ni dhahiri kabisa kwamba hatuwezi kumaliza matatizo yote kwenye jamii kwa wakati mmoja. Hakuna jamii iliyoweza kufanya hivyo hadi sasa. Lakini tunaweza kabisa kumaliza matatizo ya msingi – kama vile upatikanaji wa maji au vitabu vya wanafunzi au malipo na stahiki za walimu na wauguzi na wengineo – ambayo wenzetu kwenye nchi zilizoendelea hawayazungumzii tena. Tunaweza kabisa, na tunapaswa, kuondokana na mtizamo na lugha ya kasungura kadogo kama maelezo ya kushindwa kutekeleza majukumu ya msingi.

38

Mwaka jana niliona picha yako kwenye gazeti ukiwa Butiama na Mama Maria Nyerere mkiomba pembeni ya kaburi la Mwalimu Nyerere. Ulifikaje huko? Mama Maria alikupa usia gani? Unazungumziaje nafasi ya Mwalimu Nyerere kwenye siasa za sasa za nchi yetu?

Nilialikwa Butiama kwenye siku ya Mwalimu Nyerere yaani tarehe 14 Oktoba mwaka 2013. Ilikuwa heshima kubwa kwangu.

Nilipata fursa ya kuhudhuria misa ya kumbukumbu ya Mwalimu pale kijijini na pia nafasi ya kuzungumza na Mama Maria na Kaka Madaraka Nyerere na wengineo na tukapata chakula cha mchana na kuzuru kaburi la Mwalimu na kuweka mashada na kuomba. Sidhani ni sahihi kuelezea mazungumzo binafsi tuliyokuwa nayo kwa hiyo utanisamehe.

Kuhusu nafasi ya Mwalimu Nyerere kwenye siasa za nchi yetu, hakuna mjadala kabisa kwamba bado ana nafasi kubwa kama mfano wa uzalendo, uadilifu, uchapakazi na uongozi bora sio tu hapa Tanzania bali Afrika nzima na duniani kote. Mimi ni muumini wa falsafa za Mwalimu Nyerere na kama kiongozi kijana najitahidi niwezavyo niige mfano wake, mfano wa maisha yake, mfano wa msimamo wake, mfano wa uadilifu na uchapakazi wake.

Yeye, pamoja na Sheikh Amani Abeid Karume, ndio waasisi wa taifa letu. Mwalimu Nyerere ndiye aliyejenga misingi ya taifa letu na yeye bado ndiye anabaki kuwa reference pale tunapoyumba na kutetereka kama taifa.

Watanzania wote, hata wale ambao walikuwa hawajazaliwa wakati anatutoka, bado wanakubali kwamba yeye ndio mhimili wa ustawi wa taifa letu. Mwalimu anatuunganisha Watanzania wote, na ni jambo jema kwa taifa kuwa na jambo au mtu ambaye ndiye Waingereza wanasema "*the conscience of the nation*".

Jambo la msingi ni kwamba viongozi kuishi kwa namna alivyotufundisha na kutuasa.

Mwalimu hapaswi kuenziwa kwa maneno tu bali kwa vitendo.

Mwalimu ameacha kumbukumbu ambayo haitafutika katika uhai wa taifa hili, ameacha maandiko mengi na ameacha hotuba nyingi. Lakini pia Mwalimu ameacha taasisi: *Mwalimu Nyerere Foundation*. Taasisi hii alianzisha mwenyewe mwaka 1996 kwa malengo mema. Lakini ukweli ni kwamba taasisi hiyo inasuasua.

Kwa jinsi ilivyo sasa hailingani na hadhi na jina la Mwalimu Nyerere. Mapendekezo yangu ni kwamba Serikali ijayo iwe inatenga bajeti ya kuiendesha taasisi ya Mwalimu Nyerere Foundation. Hili linawezekana.

Sidhani kuna atakayepinga. Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ni sehemu ya hifadhi ya kumbukumbu ya taifa letu. Taasisi hii ikishamiri ni fahari kwa nchi yetu ni heshima kwa jina la Mwalimu Nyerere.



January akiwa na mazungumzo ya faragha na Mama Maria Nyerere alipokaribishwa nyumbani kwa Mwalimu Nyerere Butiama, Oktoba 2013.

39

Je, kati ya marais wanne waliowahi kuliongoza taifa letu, unafikiri ni rais gani ameacha historia kubwa kama Rais aliyefanya mambo makubwa kuliko wote katika taifa letu?

Maendeleo ya nchi yetu mpaka hapa ilipofikia yametokana na mchango wa uongozi wa marais wote waliopitia. Kwa ujumla, Marais wetu wote wamefanya kazi nzuri. Kila Rais aliyeongoza nchi hii alianzia pale mwenzake alipoishia, na kila mmoja wao alikabiliwa na changamoto na majukumu mahsusi katika wakati wake ambayo yalikuwa tofauti na wengine. Na kila mtu alitekeleza wajibu wake kadiri ya changamoto za wakati huo na kulingana na mazingira aliyokabiliana nayo. Mwalimu Nyerere alipigania ukombozi wa nchi yetu kabla ya kuwa Rais kwa hiyo kazi yake ni ni ya kihistoria na vigumu kulinganishwa na hakuna mtu yoyote anayeweza kufuta heshima aliyojipatia yeye ya kututoa katika makucha ya ukoloni na aliyoliletea taifa letu.

Pia, aliweka misingi bora ya ujenzi wa taifa letu. Kazi ya kujenga taifa moja katika misingi ya haki na usawa haikuwa ndogo. Taifa lilikuwa na makabila 120, yote yakiwa na mfumo wa uongozi wa jadi, na lugha zao tofauti. Vilevile, kulikuwa na mgawanyo wa kidini hasa katika fursa ya elimu. Mwalimu Nyerere kwa busara zake alifanya kazi kubwa na muhimu ya kujenga taifa moja ambalo linasifika dunia nzima kuwa na amani na utulivu mpaka leo hii. Hii haikuwa kazi rahisi kwake kufanikisha mambo yote aliyofanikiwa kutekeleza kwa kuzingatia kwamba kuna changamoto nyingi zilizokuwepo wakati huo, ikiwemo ukosefu wa rasilimali-watu na rasilimali-fedha. Yeye pamoja na viongozi wenzake walijenga kila kitu upya na changamoto za wakati huo zilizhitaji usahihi wa dira au kuchukua risk kubwa kufanya mambo mapya bila kuwa na reference point.

Mwalimu alichukua uongozi wa nchi wakati dunia imegawanyika katika makundi ya vita baridi ambayo ilikuwa imepamba moto kati ya mataifa ya Magharibi na Mashariki. Vita baridi ilileta changamoto hata katika utawala wa ndani na hivyo kuchangia mwelekeo wa siasa na dira za ndani ya nchi za wakati huo. Uongozi wa Mwalimu ulikumbwa na changamoto nyingi ambazo zilikuwa nje ya uwezo wake, uchumi wa dunia kufifia kutokana na changamoto

za bei ya mafuta miaka ya 1970 ambako kulileta hali ngumu sana ya uchumi nchini. Vilevile uvamizi wa Nduli Iddi Amin mwaka 1978 ulileta changamoto ya kipekee kwenye uongozi wake na kuzidi kuzorotesha uchumi wetu.

Ukombozi wa Afrika nao ulihitaji mrengo na falsafa mahsusi lakini pia na matumizi ya rasilimali zetu za ndani. Sifa kubwa ya nchi yetu ni kwamba ilijengwa kutokana na msimamo wa Mwalimu Nyerere wa kutaka kumkomboa Mwafrika, kusimamia na kutetea haki za watu. Lakini jambo la msingi ambalo Watanzania watamkumbuka Mwalimu Nyerere ni juhudi zake kujenga umoja na usawa miongoni mwa Watanzania, na atabaki kuwa Baba wa Taifa letu na jabali la siasa za ukombozi na usawa dunia nzima.

Kwa upande wa Rais Mwinyi, naye alitimiza wajibu wake vizuri katika mazingira magumu na changamoto mahsusi alizokabiliana nazo. Aliingia madarakani wakati hali ya kiuchumi ikiwa mbaya na viwanda vingi vilikuwa havizalishi na uchumi ulikuwa haukui, hali ya maisha ilikuwa ngumu sana kipindi kile na uchumi wa nchi ulikuwa umefungwa. Alikuwa na ujasiri, busara na hekima ya kufungua milango ya Tanzania hata pale Mwalimu Nyerere alipopingana nae hadharani. Raisi Mwinyi alibadilisha kabisa mfumo wa uchumi, siasa, na jamii. Aliongoza katika kipindi kigumu cha mabadiliko makubwa katika nchi yetu na aliyaongoza mabadiliko hayo kwa ujasiri mkubwa. Tulikuwa tunaingia katika zama mpya ambazo hatukuwahi kuzijua lakini alishika usukani vyema kabisa. Alipata ujasiri wa kuanzisha mfumo wa siasa za ushindani, yaani vyama vingi, alikuwa na ujasiri na hekima ya kuruhusu uhuru wa vyombo vya habari, alikuwa na ujasiri kwa kuanzisha mfumo wa uchumi wa soko huria na kuanza mazungumzo na taasisi za fedha za kimataifa kuhusu mikopo na urekebishaji wa uchumi wetu. Hata hivyo utaratibu mpya wa soko huria ulitumika vibaya na baadhi ya watu, likawa soko holela, na nidhamu katika usimamizi wa uchumi ikapungua. Ilikuwa ni kama kufungua madirisha ya nyumba ili hewa iingie lakini pia ikaruhusu vumbi na nzi kuingia pia.

Kwa hiyo kazi kubwa ya Rais Mkapu ilikuwa ni kusafisha hali hiyo na kuleta nidhamu ya uchumi, kurasimisha uchumi na kurekebisha nidhamu ya hesabu za serikali ili Tanzania iweze kukopesheka na kuaminiwa kwenye jamii ya kimataifa. Taasisi nyingi za udhibiti uchumi zilianzishwa wakati wake, hata Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilianzishwa katika kipindi chake. Aliweka mikakati ya kulipa madeni nchi yetu iliyokuwa inadaiwa na jumuiya ya kimataifa na kupelekea kutengemaa kwa uchumi mkuu, yaani macroeconomic stability, na kujenga mahusiano mazuri na wafadhili na kuvutia wawekezaji wengi. Uchumi ulianza kukua, uwekezaji ukaingia kwa kasi. Biashara zikapanuka



Rais wa Kwanza wa Tanzania Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika shughuli za kuupokea uhuru Tanganyika mwaka 1961, akiwa na umri wa miaka 39 tu.

na hali ya uchumi ikatengemaa. Alifanya kazi nzuri sana ambayo hadi leo inaipa heshima kubwa nchi yetu duniani. Na Rais Mkapu ni mmoja wa viongozi wanaoheshimika duniani kwa weledi wake na maarifa yake na uongozi wake madhubuti. Naye alitimiza wajibu wake vizuri.



Kwa upande wa Rais wa sasa Ndugu Jakaya Kikwete, kazi kubwa aliyoifanya ni kutumia misingi bora aliyoiacha Rais Mkapa kwa kutoa huduma za kijamii nchi nzima na kuboresha zile zilizokuwepo. Rais Kikwete ametumia nguvu kubwa kujenga miundombinu ya kuunganisha mikoa yote ya Tanzania, amejenga shule nyingi za Sekondari, vyuo vikuu na kuboresha utoaji wa elimu. Idadi ya

walimu na wafanyakazi wa afya walioajiriwa imeongezeka maradufu kwenye kipindi chake. Rais Kikwete amejenga rasilimali-watu kubwa ya Watanzania kwa ajili ya maendeleo ya miaka 30 ijayo ya nchi yetu. Kazi ya Rais Kikwete imewarahisishia viongozi watakaokuja kwani ameweka misingi na kufanya mambo ya kihistoria ambayo yalibakizwa huko nyuma. Lakini pia amejenga misingi ya uwazi na uhuru iliyopelekea Watanzania wote kwa ujumla na vyombo vya habari kuwa huru. Ameimarisha demokrasia kwa kiasi kikubwa katika nchi yetu. Silka yake ya uvumilivu imeifanya nchi yetu kuendelea kuwa ya amani na utulivu katika kipindi ambacho matishio ya umoja na amani na usalama yalikuwa makubwa zaidi. Lakini pia ameipaisha kwa kiasi kikubwa diplomasia ya nchi yetu na kujengea heshima kubwa nchi yetu duniani. Ameifungua nchi yetu upya kwenye safu ya kimataifa.

Rais Kikwete pia atakumbukwa kwa kuwashirikisha vijana katika mustakabali wa nchi yetu. Tumeona vijana wakipata nafasi za uongozi wakati alipoingia madarakani na vijana wengi wakijiona kwamba wana wajibu na nafasi katika ujenzi wa nchi yao. Rais Kikwete ametengeneza fursa na kutoa uwezeshaji kwa kila Mtanzania kujitengenezea maisha yake. Wajibu umebaki wa Watanzania wenyewe.

Kwa hiyo, jambo la msingi hapa ni kwamba kila Rais aliyeingia madarakani alisimamia kwenye mabega ya Rais aliyepita, kuendeleza pale alipoachia kwa kuzingatia misingi ya usawa, amani, umoja, na mshikamano iliyoasisiwa na waasisi wa Taifa letu. Hakuna Rais anayeanza upya kabisa. Tumepata bahati katika nchi yetu kuwa na viongozi walioumbwa kwa nyakati zao na waliokuwa na uwezo na maarifa ya kukabiliana na changamoto mahsusi katika nyakati zao.

40

Kuna mambo yoyote unayodhani hatukuyazungumzia ambayo unadhani yana umuhimu katika ustawi wa nchi yetu?

Sina hakina maana yake tumezungumzia mambo mengi na maswali yako yalikuwa mengi, ila naamini yapo mengi sana muhimu hatujayagusia. Labda kwa haraka haraka nizungumzie mambo mawili ambayo sikumbuki kama tumeyajadili. Jambo la kwanza ni mazingira na jingine ni suala la mfumo wa utoaji haki nchini au *justice sytem*.

Kuhusu mazingira, nataka niseme tu kwamba tusipobadilisha mwelekeo wa hali inayoendelea sasa, nchi yetu inaelekea kwenye janga kubwa la mazingira katika miaka 30 au 40 ijayo.

Shughuli kuu za uchumi wa taifa na kipato cha Watanzania, hasa kilimo, ufugaji, uvuvi na utalii, zinategemea uimara na hifadhi ya mazingira.

Kila mwaka, kuanzia 1990, hekta milioni moja, au ekari milioni mbili na nusu za misitu, zinapotea. Ubora wa udongo kwa kilimo unapungua, mvua zinapungua, mito inapungua maji na mingine inakauka kabisa, na maji yaliyo chini ya ardhi yanapungua. Kilimo, ambacho kinaajiri asilimia zaidi ya 70 ya Watanzania, kinategemea uwepo wa mvua na ardhi yenye rutuba. Kupukutika kwa miti na misitu kunapunguza ubora wa ardhi na kunapunguza mvua na kunapunguza hifadhi ya maji. Kilimo kisicho cha kitaalamu kinapunguza thamani ya rutuba ya ardhi na kuwafanya wakulima waendeleo kukata misitu zaidi kutafuta maeneo mapya ya kulima. Wakati tunapata uhuru tulikuwa watu milioni 9. Leo tunakaribia milioni 50, lakini ardhi haiongezeki. Kwa hiyo matumizi bora ya ardhi ndilo jambo la msingi kama tunataka kuendelea kupata maendeleo na kuondokana na umaskini.

Utalii unatuingizia fedha nyingi za kigeni, lakini asilimia 70 ya utalii wetu ni utalii wa kutazama wanyamapori. Ustawi wa wanyama pori unategemea malisho yao – ambayo yanategemea mvua na kuendelea kuwepo wa uoto wa asili. Sehemu iliyobaki ya utalii ni utalii wa fukwe za bahari, na utalii huu unategemea fukwe zilizo bora na safi. Lakini uvuvi haramu, hasa wa kutumia baruti na

mabomu, unaharibu kinga za asili, *coral reef*, za fukwe zetu na sasa fukwe nyingi zinaharibika na zinamomonyoka na kuchafuka hivyo kutofaa tena kwa utalii au hata ujenzi.

Vilevile, ufugaji usio na tija, yaani wa kuwa na makundi makubwa ya ng'ombe bila utaratibu bora wa malisho, pia unachangia katika kupunguza ubora wa ardhi.

Cha kufanya hapa ni kuwa wakali zaidi kwenye sheria za hifadhi za mazingira. Kulingana na hali halisi ya maisha ya watu wetu, hasa wanaoishi vijijini, ni dhahiri kwamba wataendelea kutegemea kukata miti kwa ajili ya mahitaji yao muhimu, ikiwemo ujenzi wa nyumba, nishati na kupanua mashamba yao. Hakuna shaka kabisa kwamba watu wetu wanastahili kuzitumia maliasili zetu kwa ajili ya maisha yao. Cha msingi ni matumizi endelevu ya rasilimali ili tuendeleo kuhifadhi mazingira yetu. Hili linawezekana kulifanikisha.

Ni dhahiri kwamba biashara ya mkaa inachangia kwa kiasi kikubwa kwenye uharibifu wa mazingira. Pia ni dhahiri kwamba mkaa ni nishati inayotumiwa na kutegemewa na watu wengi, zaidi ya asilimia 90, hasa wenye kipato cha chini. Vilevile, ni dhahiri kwamba hii ni biashara kubwa sana na inayoajiri na kuwapatia kipato watu wengi. Mwaka 2009, biashara ya mkaa ilikuwa na thamani ya dola za Kimarekani milioni 600, zaidi ya mauzo ya mazao yetu ya kilimo nje ya nchi. Hata hivyo lazima tuanze safari ya kuachana na matumizi ya mkaa. Tulijaribu kupiga marufuku mkaa mwaka 2006 lakini hatukuwa tumefanya maandalizi ya kuwezesha watu wetu kupata nishati mbadala. Tunaweza kubuni sera, mipango, mikakati na motisha ya kikodi kwa matumizi ya nishati mbadala zaidi ya mkaa, ikiwemo gesi. Kule ambako majaribio yamefanyika tumeona manufaa. Tunaweza kuokoa mazingira bila kuwaumiza watu wa kipato cha chini. Tusiufanye mkaa ghali bali tufanye matumizi ya nishati mbadala nafuu zaidi.

Vilevile, kwenye uvuvi haramu, ambao sio tu unaharibu fukwe bali unaondoa kabisa uwezekano wa samaki kuendelea kuwepo tena, hapa ni lazima kuwe na sheria kali na zitekelezwe kikamilifu.

Kwa upande wa ufugaji, kama nilivyosema mapema, ni vyema wafugaji wakatengewa maeneo mahsusi ya malisho, wapakewa mafunzo ya ufugaji endelevu, ikiwemo namna ya kuendeleza malisho kwa ajili ya kunenepesha mifugo yao. Zipo nchi hapa Afrika, kama Botswana na Namibia, ambazo zina maeneo madogo sana kuliko sisi, lakini wananufaika zaidi na mifugo kwa sababu wamegundua siri ya malisho ya kunenepesha ng'ombe. Nasi tunaweza.



January Makamba akibadilishana mawazo na Ndugu Zitto Kabwe, Mbunge wa Kigoma Kaskazini.

Nimalizie tu kwa kusema kwamba kuna vipengele vingi tu vya hifadhi ya mazingira ambavyo sijavizungumzia lakini nataka niseme kwamba hifadhi ya mazingira ina uhusiano wa moja kwa moja na maendeleo yetu.

Tunaweza kufanya mambo mengi mazuri kwenye kujenga barabara, kujenga shule, kwenye huduma za afya na mengineyo, lakini kama hatutakuwa wakali na makini kwenye hifadhi ya mazingira basi tusahau habari ya maendeleo.

Jingine ambalo nilisema nitaliongelea ni suala la mfumo wa kutoa haki hapa nchini.

Mambo yote katika nchi yanaweza kwenda kombo, lakini mfumo wa utoaji haki ukiharibika, nchi inaingia hatarini. Watu hustahili na hupenda kupata haki zao. Tumeweka Mahakama na taasisi nyingine za umma kwa ajili hiyo. Ikiwa hazifanyi kazi vizuri, ikiwa hazitoi haki kwa wakati na kwa usahihi, siyo kwamba watu wataacha kutafuta haki zao, bali watazitafula kwa namna wanayojua wao, na tukifika huko nchi inaweza kuvurugika.

Kwa hiyo taasisi kama Polisi na Mahakama lazima ziwe zinafanya kazi vizuri na tena kwa uadilifu wa hali ya juu sana. Sasa hivi hali siyo nzuri. Kila mtu anaona. Masuala ya kubambikiwa kesi yamekithiri. Masuala ya kuoneana yapo mengi.

Haki ni suala la msingi wala halipaswi kuonekana kama ni la upendeleo. Msingi mkuu kwenye mfumo wa utoaji haki ni kwamba sote tuko sawa mbele ya sheria, au kwa Kiingereza wanasema *equality before the law*. Kwa sasa siyo hivyo. Ukiwa ni mkubwa au una pesa unapata haki zaidi, unapata dhamana kwa urahisi, kesi yako inaenda haraka, na wakati mwingine inaamuliwa kwa namna unavyotaka. Hii siyo sawa na ni lazima ibadilike.

Kesi za watu zinazopelekwa mahakamani lazima zimalizwe haraka. Na lazima watu wawe na uhakika wa kesi zao kuamuliwa kwa haki. Mahakama zimepewa nguvu kubwa na nguvu hiyo ni vema itumike vizuri. Mfumo wa jinai na dhamana unahitaji marekebisho makubwa. Takriban nusu ya watu waliopo katika magereza yetu hapa nchini leo hii sio wafungwa bali ni mahabusu. Wakati mwingine, mahabusu inaonekana ndio njia ya mkato ya kukomesha mtu. Lakini mara nyingi mfumo wa dhamana unapelekea kuwa na mahabusu wengi zaidi. Lakini kubwa zaidi ni ucheleweshaji wa kusikilizwa kesi za jinai. Kesi nyingi za jinai kwenye Mahakamu Kuu zinachelewa kusikilizwa kutokana na ukosefu wa fedha. Na wakati mwingine mahabusu anakaa ndani miaka 7 au 8 halafu anaonekana hana hatia au Mkurugenzi wa Mashtaka anaondoa mashtaka na mtuhumiwa anakuwa amepoteza kila kitu bila fidia yoyote. Ni vema sasa kukawa na *a criminal bench*, yaani Mahakama ya Jinai, kama ilivyo Mahakama ya Ardhi, Mahakama ya Kazi, na Mahakama ya Biashara, ambayo inafanya kazi kila siku, ili haki za watu zipatikane haraka. Kupatikana kwa haki za watu kusitegemee uwezo wa kifedha wa Serikali.

Labda la mwisho dogo, lakini naamini ni muhimu, ni kwamba ukiangalia kwenye kesi za madai utaona zimewekewa viwango, kwamba kesi ikiwa ni ya zaidi ya milioni 100 kwa fidia au milioni 50 kwa mali zisizohamishika, yaani *fixed assets*, inasikilizwa na Jaji, kwenye Mahakama Kuu. Msingi hapa ni kwamba kuna kesi kubwa na kesi ndogo. Lakini ukienda kwenye jinai unakuta kwamba Hakimu ana uwezo wa kumfunga mtu hadi miaka 30. Mimi nadhani kwamba kesi ambazo zinaweza kupelekea vifungo virefu kama miaka 30 nazo pia zisikilizwe na Jaji wa Mahakama Kuu kwa sababu tunashuhudia mara nyingi huko Wilayani watu wanafungwa miaka mingi, tena kirahisi sana. Kifungo chochote inabidi kiwe na uhakika kabisa kwamba kesi ilikuwa ya uhakika na haki halisi imetolewa.

Mimi naamini kwamba mfumo wa utoaji haki nchini lazima uwe imara zaidi. Majaji, mahakimu, mawakili wa Serikali, waendesha mashkata na watumishi wote wa mfumo wa utoaji wa haki ni muhimu wathaminiwe na wapate nyenzo zote muhimu za kuwawezesha kutimiza majukumu yao vizuri na kwa ufanisi.